# SHUHUDA KWA KANISA

2026 Edition

1 • 2 • 3 • 4 • 5 • 6 • 7 • 8 • 9



Uhamisho Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

MaarifaMtandaoni.com

RohoYaUnabii.Org

ISAIAH 52:7

SAMARITAN LAYMEN MINISTRIES

*Enendeni mtandaoni kote*



SHUHUDA KWA KANISA
Gombo la 9
2026 Edition
New Jersey, Marekani
RohoYaUnabii. Org / RohoYaUnabii.Africa
MaarifaMtandaoni.Com
Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

**KARIBUNI katika safari ya KUSIKILIZA NA KUSOMA SHUHUDA PAMOJA**

**MaarifaMtandaoni.Com     ROHOyaUNABII.Org     RohoYaUnabii.Africa**

**SHUHUDA KATIKA SAUTI- SIKILIZA SHUHUDA**
**Shuhuda ni magombo tisa, yenye kurasa 4738 yaliyoanza kuandikwa mwaka 1855**
**Madhumuni, ushauri wa kiroho na ushauri wa kivitendo katika nyanja mbali mbali kama vile (Soma kurasa za 5TShuhuda 663-667)**

**2025 EDITION-Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo.**

**Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4Tsw 472)**

**Madhumuni, ushauri wa kiroho na ushauri wa kivitendo katika nyanja mbali mbali kama vile (Soma kurasa za 5TShuhuda 663-667)**

Miaka 10 iliyopita tulikutana na watu wanaosoma Shuhuda kwa Kingereza kule Dallas, Texas, Marekani, kwenye mkutano wa Vijana wa Marekani uitwao Generation of Youth for Christ -GYC (Testimonies for the Church-Revivalplan.com). Walitueleza umuhimu wa kuyasoma magombo haya na kutuhamasisha kuyasoma, hapo ndipo tulipoanza kuyasoma, tulikuwa tumesikia sura zake chache ila siyo sura zote. Tuling'amua kuwa hayakuwa na tafsiri ya Kiswahili. Nasi Tunashauri kila mtu asome magombo yote haya tisa, na Kila kiongozi wa Kanisa na hata mshiriki afanye jitihada ya kuyasoma kwa

mpango. Wengi wamechukua wiki 16 kwa kusoma Kurasa 10 kila siku (Revivalplan.com). Ukisoma au kusikiliza nusu saa kwa siku, itakuchukua miezi mine kumaliza magombo yote tisa. Tulianza kuyatafsiri kama marafiki  miaka sita iliyopita, na ilituchukua muda wa mwaka, kisha tukaingia uhariri, na uhakiki.
Magombo ya Shuhuda tisa, ni kurasa 4738, ambazo zimetafsiriwa  kwa ajili ya kila mwanadamu, na hasa wale watu wanaompenda Mungu na kutamani mabadiliko ya tabia. Habari hizi ni muhimu sana hivyo wewe uko huru kunakili na kusambaza kwa wengine kama zilivyo. Kwa nakala ya kidijitali ya vitabu hivi, tafadhali tembelea R***ohoYaUnabii.Org, RohoYaUnabii.Africa MaarifaMtandaoni.Com, MaarifaMtandaoni.Africa*** au kwa Kingereza ***WhiteEstate.org***. Kugushi Maandishi ya namna hii au kuyakaba koo yasinene, ni kujiletea taabu kubwa. Yeremia 36:27 na Ufunuo 22:18,19 na Kumbukumbu la Torati 4:9.Enendeni Mtandaoni Kote duniani.

**Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo na kufanya tabia zetu zifae.**

Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu...."

Maombi yetu makuu yawe matatu. Nayo ni ROHO MTAKATIFU, kujisalimisha kwa MUNGU  na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu, na kuishi mtindo wa maisha anayotaka Bwana. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma Hizi shuhuda. Haya ni mausia ambayo yanatubidisha sote wenye mwili kuzisoma hizi shuhuda. Mambo mengine kwa kuelewa zaidi unaweza kupakua ‘Google App’ ya Roho ya Unabii kwa Kingereza.

-Mkakati wa uamsho au Tumaini linalotiririka ni msaada mkubwa kwetu leo ambao hatuelewi vyema tufanye nini ili Maisha yetu yampendeze MUNGU na watu, katika muda ambao maadili yanayomomonyoka na ulimwengu hauna mafundisho mema au haufundishi kabisa. Mafundisho haya ni mazuri kwa kila binadamu anayeelewa Kiswahili! Mpango huu kwa Kingereza utaupata katika Revivalplan.Com

Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4T 472)

‘Maelfu ya watu wataoongoka kwenye ile Kweli, katika saa ya kumi na moja, AMBAO wataupata na kuukubali Ukweli wa injili na Neno la Mungu na KUHUISHWA KWA harakati za Roho wa Mungu.—EGW’88 755 (1890). – {LDE 212.2}.’ Unabii huu unatimia, Maelfu ya watu duniani kote  wanamwamini Mwenyezi Mungu na kubatizwa kwa siku moja, kwa wazi au kwa faragha. Tafsiri zetu ni kama Wikipedia, ukitaka kuongeza ladha bila kupoteza maana, wewe boresha tu, ila usipoteze kabisa ujumbe na maana iliyokusudiwa. Kila Shuhuda imehaririwa mara tano, binafsi nimepitia mara tatu. Tumeweka Pointers (2Tsw 45.5) na kadhalika ili ujihakikishie mwenyewe na kutafsiri kwa ubora zaidi unapotaka. Sw inawakilisha, Kiswahili ambacho kinazidi kupanuka na kuwa moja za lugha za Wakristo wengi duniani. Niliona Machapisho ya Nuru kwa

Kanisa ambayo sasa tukiyaona tunashangaa, ila enzi hizo yalikuwa yenyewe kabisa kwa uzuri, japo yalichuja kurasa 4738 na kuwa 80 tu!

Asante kwa Wasomaji, Watafsiri, Wahariri, Washauri, Wahakiki, Waombezi, Wanaufundi na wote ambao wanasaidia hii kazi ya Machapisho duniani kote. Tuna idadi ya vitabu 130 sasa. Kama umeshiriki hii kazi na jina lako halikuweka, tafadhali tujulishe, Asante

## MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI…

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni ROHO MTAKATIFU, ushauri, na Maombi yako msomaji. Wako watu wanaoishi nje ya Afrika Mashariki wanahitaji pia kusoma Maandishi ya kalamu iliyovuviwa, kwa Lugha ya asili. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la MUNGU limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi karibu 7000 kati ya 14,000, ambayo bado kufikiwa, angalia Joshuaproject.org na habari za ‘1040 window’

‘Sambaza Biblia kote,’ ndiyo kauli mbiu ya muumini; sambaza Neno la MUNGU kote.

Jiunge nasi katika kuandika vitabu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ikiwa kuna kosa lolote la kiuandishi au kiutafsiri, tafadhali wasiliana nasi na endapo ukiamua kuchapa, usibadilishe chochote labda typos tu.

Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Kwa hapa Kwetu Afrika Mashariki, tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu; mada za afya, lishe, mahusiano kama ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga ufalme wa Mungu, nyimbo zetu na noti zake; haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandao ya magharibi na ni mema tu, lakini kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu Afrika, basi tunabidishwa pia kuwa waandishi, Watunzi wa nyimbo, na watu wa kuhifadhi kumbukumbu zetu kwa miaka mingi, kwa sababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya Ya jamii kuliko mtu mwingine.

Kwa nini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa umakini, nyimbo zilizoimbwa miaka kama 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu vya tenzi na kisha watu waimbe? Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila hata wao wanaendelea kuziongeza vitabuni, nasi hapa tuna nyimbo nzuri, ambazo zinaendana na utamaduni wetu na mtindo wetu wa kuchukua mafungu ya Biblia takatifu, na kuelezea kisa fulani. Kwa nini basi tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu vitu vizuri, ikiwemo

nyimbo za watoto? Tuna wataalamu wengi wa nyimbo. Pia umefika wakati wa ‘Reverse Mission’-misheni iliyogeuka na kuwa kinyume cha kawaida. Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Waumini wengi kuliko Amerika ya kusini, na tunajua lugha nyingi kubwa kama Kifaransa, Kireno, Kihispania na Kingereza, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu. Watoto wetu na sisi mara zingine tunaona pengine tuwe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au tuwe na mwenendo kama ule.

Mfano mdogo sana ni ule waandishi wengi wa nje huandika vitu vingine visivyoendana na muktadha wetu, mfano vyakula kama Pizza, Tambi, Kimchi, Taco, Panzit, Empanada, Manicotti, Tortellini, Sushi, au Falafel. Je, viwanda vyetu hutengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila maandalizi hupishana. Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk.

Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! tunaelewa kwamba sio utamaduni wetu kuandika, ila sio utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya!

Sio kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii; wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii, kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu. Kitabu cha Jando na Unyago kwa muktadha wa Maandiko kwa Waamini ni vizuri tupatie watu wa kutusaidia kuandika, kwani jamii inaishi sehemu tofauti na asili ya kabila la mtu, na hii inafanya kusiwe na Mafundisho au kujifunza kwa mambo fulani muhimu toka kwa Kabila la mtu kama ilivyokuwa, na wakati huo huo pengine serikali haiwezi kukidhi hitaji hili kwa urahisi.

Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio umma. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili, kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake. Tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwenye ujasiliamali, nk. Ukiwa na chochote, hata ikiwa ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani, tafadhali usisite kuutoa na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, fundisha wengine, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa Maandishi yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku.

## UTANGULIZI

Wapendwa vitabu hivi ni vyetu sote! Maana kila mtu anahitaji Mashauri. Shuhuda ni vitabu vya mashauri na maonyo. Kwenye wingi wa Ushauri hapaanguki jambo, na kuna usalama. Masihi Yu karibu kuja kuchukua bibi harusi asiye na waa wala kunyanzi. Maneno haya na yatuchome sana, na kutuvutia tusiwe waongofu tu bali wanafunzi na watu wanaoishi kwa uamsho na matengenezo kila siku, tukiendelea kuwezeshwa na ROHO MTAKATIFU kubadilisha mitindo yetu ya maisha ili tumpende na kumpendeza Mwenyezi MUNGU, na kuwapenda watu. Hivi ndivyo vitu pekee ambavyo tutaenda navyo mbinguni.

Shuhuda zimejaa mashauri, Makaripio na maonyo ya maisha ya kila siku kwa undani zaidi. Tumeambiwa kwenye maagizo kwamba shuhuda zina kila namna ya kukamilisha tabia zetu. Tulisikia kuhusu kuwepo kwa Shuhuda kwa Kanisa ila hatukujua sana kwamba zinahusiana na nini! Ila baada ya kuanza kusoma kila siku katika mpango wa kusoma Shuhuda Revivalplan.com kwa lugha ya Kiingereza tuliona kuna haja kubwa ya kuzitafsiri katika lugha ya Kiswahili maana waamini wengu wanaishi chini ya Sahara, ambao kuna wengi wanaozungumza Kiswahili. Kwa sasa, takwimu zinaonesha kuwa Afrika ina asilimia 50% ya waamini wanaotarajia marejeo ya YESU (Waadventista). Miaka kama 10 iliyopita, ni asilimia 3% tu ya Maandishi ya Roho ya Unabii ilikuwa imetafsiriwa Kiswahili.

Wana Marejeo wanaozungumza Kiswahili duniani sasa ni 11%. Kutokana na Google wale wanaozungumza Kingereza ‘fluently’ katika nchi za Kiswahilii ni asilimia ndogo sana kuliko tunavyofikiria! Tumepewa ulimwengu wa Kiswahili tuufikie. Hivyo Kutafsiri mambo haya ni jambo la dharura. Katika kutafsiri, Mambo manne ndiyo yalikuwa kwenye mawazo yetu kuliko mengine

1. Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu...."
2. Kubeba ujumbe kama ulivyo ili watu wapate kilichonuiwa, bila kupotosha Neno la MUNGU
3. Lugha rahisi itakayoweza kusomeka Kenya, Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Tanzania
4. Sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu iwe imezingatiwa.

Maombi yetu makuu yawe matatu. Nayo ni ROHO MTAKATIFU, kujisalimisha kwa MUNGU na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma Hizi shuhuda. Haya ni mausia ambayo yanatubidisha sote wenye mwili kuzisoma hizi shuhuda. Mambo mengine kwa kuelewa zaidi unaweza kupakua ‘Google App’ ya Roho ya Unabii kwa Kingereza.

Google imesaidia mambo kadhaa mfano Kujua zama hizo kulikuwa na mambo gani,

mfano mitindo na mavazi ya sketi za hoops miaka ya 1800BK zilizozungumziwa; zitakupa maoni waliyokuwa nayo wakati ule utakapoingia katika tovuti. Japo hekima haiongezeki kwa urahisi, maarifa yameongezeka, hivyo angalia mambo haya kwa kichujio cha Biblia zaidi ya teknolojia. Usiogope kurejelea kamusi, ndio kujifunza. Muumini daima ni mwanafunzi na anasaidiwa zaidi kukumbuka mambo mengi anapotumia machapisho zaidi ya njia zingine. Mengine ya Kingereza imebidi tuweke maana tunayatumia na hivyo utapata utambuzi wa jambo haraka, mfano mara nyingi hatusemi Jimbo, ila Konferensi/conference, majina ya magonjwa au mitindo n.k Tunashauri kila mtu magombo yote haya tisa, na Kila kiongozi wa Kanisa na hata mshiriki afanye jitihada ya kuyasoma kwa mpango. Wengi wamechukua miezi 16 kwa kusoma Kurasa 10 kila siku (Revivalplan.com)

Wenu wadhamini, watafsiri, wahariri, washauri, wahakiki, marafiki, wajoli na ndugu katika safari ya kwenda mbinguni.

Zifuatazo ni sentensi za Kalamu ya matumain, kalamu iliyovuviwa kwa wamaani, ya Ellen White kuhus u umuhimu wa kuzisoma Shuhuda.

*1."Niliichukua Biblia ya thamani na kuizingira kwa Shuhuda kadhaa kwa ajili ya Kanisa, zilizotolewa kwa ajili ya watu wa MUNGU. Hapa, nilisema, kesi za karibu zote zinapatikana. Dhambi wanazopaswa kuacha zimeianishwa. Shauri wanalotaka linaweza kupatikana hapa, likitolewa kwa kesi zingine zinazofanana na Zao wenyewe. MUNGU ameridhika kuwapatia kanuni juu ya kanuni na amri juu ya amri. Lakini si wengi wenu ambao wanajua kwa hakika kile kilichomo katika Shuhuda. Hamyafahamu Maandiko. Laiti mngelifanya Neno la MUNGU kuwa funzo kwenu, kwa shauku ya kufikia kiwango cha Biblia na kufikia ukamilifu wa Kikristo, msingehitaji Shuhuda. Ni kwa sababu mmepuuza kujifunza Kitabu cha MUNGU kilichovuviwa ndio maana Yeye ametaka kuwafikia kwa shuhuda rahisi na za moja kwa moja, akiita usikivu wenu kwenye maneno ya uvuvio ambayo mlikuwa mmepuuza kuyatii, na kuwahimiza kuyatengeneza/kuyaumba maisha yenu kulingana na mafundisho Yake safi na yaliyotukuka. {5T 664.3}*

2.“Mashaka na hata kutokuamini shuhuda za ROHO WA MUNGU, kunayachachua makanisa yetu kila mahali. Shetani angependa iwe hivi. Wachungaji wanaohubiri ubinafsi badala ya Kristo wangependa iwe hivi. Shuhuda hazisomwi na wala hazithaminiwi. MUNGU amezungumza na wewe. Nuru imekuwa ikiangaza kutoka kwa Neno Lake na Kutoka kwa Shuhuda, na haya yote yamechukuliwa kwa urahisi na kupuuzwa”. 5T 217.2

3.“Mwokozi wangu alinitangazia kwa mjumbe WAKE. "Kazi yako," Alinielekeza “Ni kubeba Neno Langu... kuchukua Neno Langu mbele ya wale wasioamini, na kwa kalamu na sauti kemea kutokana na Neno, matendo ambayo sio sawa ……. Kwa ushawishi thabiti wa unyenyekevu, kwa sauti na kalamu, ujumbe nitakaoutoa utasikika kutoka kwa mtu ambaye hajawahi kujifunza shuleni… “Usimwogope mwanadamu, Sio wewe unayezungumza: ni Bwana Anayetoa jumbe kwa siku hizi za mwisho; nazo

zitaandikwa katika vitabu, na zitasimama milele zote, ili kushuhudia dhidi ya wale ambao wameongozwa kuziacha kwa sababu ya ushawishi wa udanganyifu wa uovu.” RH, Julai 26, 1906

4.Niliona kwamba wote wanapaswa kuchunguza mioyo na Maisha yao kwa ukaribu na kuona ikiwa hawakuwa wamefanya makosa yaleyale ambayo wengine walisahihishwa, na ikiwa maonyo yaliyotolewa kwa wengine hayakuhusu kesi zao wenyewe. Ikiwa ndivyo, wanapaswa kuhisi kwamba ushauri na maonyo yalitolewa haswa kwao na wanapaswa kufanya matumizi hayo kwao, kana kwamba walikuwa wanaambiwa wao wenyewe. {2T 687.2}

5.“Zamani MUNGU alinena na wanadamu kwa kinywa cha manabii na mitume. Katika siku hizi Anazungumza na wanadamu kUPITIA Shuhuda za Roho WAKE. Hakukuwa na wakati ambapo MUNGU aliwafundisha watu WAKE kwa bidii zaidi ya vile anavyowafundisha sasa juu ya mapenzi Yake na njia ambayo angewataka wafuate…… Acha shuhuda Ipimwe kwa matunda yake .... kwamba kazi hii ni ya MUNGU, au sio ya MUNGU. MUNGU hafanyi chochote kwa kushirikiana na Shetani…… Hakuna kazi ambayo ni nusu ya Shetani au nusu ya MUNGU katika jambo hilo. Ushuhuda ni wa ROHO WA MUNGU, au wa Shetani. Udanganyifu wa mwisho kabisa wa Shetani utakuwa ni kuzifanya Shuhuda za ROHO WA MUNGU zisiwe na ushawishi. "Mahali ambapo hakuna maono, watu huangamia." Mithali 29:18. Shetani atafanya kazi kwa ustadi na kwa njia tofauti na kupitia wakala tofauti kutia mashaka imani ya watu wa MUNGU wa masalio katika Ushuhuda wa Kweli…. FLB: 296 "Jambo moja ni hakika: Wale Waadventista Wa Sabato ambao wanachukua msimamo wao chini ya bendera ya Shetani kwanza wataacha imani yao katika maonyo na makaripio yaliyomo katika Shuhuda za ROHO WA MUNGU. Lt156-1903

6.“Ukikosa Imani katika Shuhuda utaondoka kwenye Ukweli wa Biblia. 5T: 674

7.“Nimejawa na huzuni ninapofikiria hali ya watu wetu. BWANA hajatufungia mbingu, lakini njia yetu wenyewe ya kurudi nyuma imetutenga na MUNGU … Na bado cha kushangaza ni kuwa maoni ya jumla ya wengi ni kwamba wanafikiri kanisa linastawi na kwamba amani na ustawi wa kiroho uko katika mipaka yake yote. "Kanisa limeacha kumfuata Kristo Kiongozi Wake na linarudi nyuma kuelekea Misri. Walakini ni wachache wanaochukua tahadhari dhidi ya uhitaji wao wa nguvu za kiroho… 5T: 217

8.“Nimeonyeshwa kuwa kutokuamini Shuhuda kumekuwa kukiongezeka kadiri watu wanavyorudi nyuma kutoka kwa MUNGU. Hali hii ipo katika safu zetu zote, na katika nyanja zote. Lakini ni wachache wanaojua ni uzoefu gani kanisa linaenda kupitia. Niliona kwamba kwa sasa tuko chini ya uvumilivu wa BWANA; lakini hakuna anayejua ukubwa wa rehema ambayo imetolewa kwetu. Lakini ni wachache waliojitoa kwa MUNGU kwa moyo wote. Kuna wachache tu ambao, ni kama nyota katika usiku wenye dhoruba kali, ambazo, huangaza hapa na pale kati ya wingu… RH, Agosti 30,1906

9.“Wakati Shuhuda, ambazo ziliaminiwa wakati mmoja, zinapotiliwa shaka na kuachwa, Shetani anajua waliodanganywa hawataachia hapo; na huongeza juhudi zake maradufu hadi atakapowaingiza kwenye uasi wa wazi, uasi ambao huwa hauwezi kupona na huishia katika uharibifu. "Shuhuda haipaswi kuhafifisha Neno la MUNGU, bali kuliinua na kuzivutia akili Kwake, ili Ukweli mzuri wa kunyenyekesha uweze kuwavutia wote... Ikiwa ungefanya Neno la MUNGU kuwa Somo lako, na hamu ya kufikia Kiwango cha Biblia na kufikia kwa ukamilifu wa Kikristo, usingehitaji Shuhuda….. Ukweli wa ziada haujatolewa: lakini MUNGU kupitia shuhuda amerahisisha Kweli kuu ambazo tayari zimetolewa, na kwa njia Yake Mwenyewe aliyochagua amezileta mbele ya watu ili zituamshe na kuvutia akili zetu. Ili sote tusiwe na udhuru FLB: 295

10.“Wengi sasa wanadharau maonyo ya uaminifu yaliyotolewa na MUNGU katika Shuhuda…. Lakini Upinzani dhidi ya vitisho vya MUNGU hautazuia utekelezaji wake. Kukataa Maneno ya Bwana, yaliyonenwa kupitia chombo CHAKE alichokichagua, itasababisha hasira Yake tu na mwishowe italeta uharibifu kwa mkosaji. 5T: 678

11."Uelewa wa wale wanaodharau Shuhuda zilizo wazi za Neno la MUNGU, na kukataa kuamini kwa sababu ni jambo linalowabugudhi au lisilovutia wengi kufanya, utatiwa giza; Ukweli utaonekana kwao kama uongo, na uongo utakubaliwa kama Ukweli…. Lakini upendo kwa Kristo na kwa roho ambazo alizifia kwa ajili Yake, zitamwongoza mtumishi wa MUNGU kutoa maonyo na wito kwa uaminifu. SW, Juni 23, 1908

12."Kupuuza Nuru ni Kuikataa." 13 Agizo nilipewa na Mwokozi, "Sio wewe ambaye wamekukataa, lakini Mimi, Mwokozi wao …… Wale ambao wamepuuza Jumbe ambazo nimempa mjumbe wangu kubeba wamemtukana YULE aliyetoa jumbe hizo. …….Watunze Watu, HAO kundi la malisho Yangu, wasifundishwe na matabibu au walimu wanaokataa maonyo ambayo nimetoa kupitia mjumbe wangu.’ SpM: 384

13."Wengi wanaenda kinyume kabisa na nuru ambayo MUNGU amewapa watu WAKE, kwa sababu hawasomi vitabu ambavyo vina nuru na maarifa yenye kutoa tahadhari, makaripio, na maonyo……. Nuru ya thamani sana, inayotoka kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, imefichwa chini ya pishi. MUNGU atawafanya watu WAKE wawajibike kwa uzembe huu. Hesabu lazima itolewe KWAKE kwa kila mwale wa nuru ambao umeangazia njia yetu, ikiwa nuru hii imeboreshwa kwa maendeleo yetu katika mambo ya mbingu au imekataliwa kwa sababu ilikubalika kwao kufuata mwelekeo wa mambo.” 5T: 681

14.“Ushuhuda huu, ukipokelewa utaamsha utendaji, na kusababisha kujishusha, na kukiri dhambi. Shahidi wa Kweli anasema, "Nazijua kazi zako, ya kuwa hu baridi wala hu moto." Na tena, " Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu." Halafu inakuja ahadi, “Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja

naye, na yeye pamoja Nami..... “Makosa na dhambi hizi, ambazo zimewaleta watu wa MUNGU katika hali yao ya unyonge, upofu, na umasikini, lazima yaonekane, na kuamsha toba ya bidii, na kuondoa dhambi hizi ambazo zimewaleta watu katika hali mbaya sana, hali ya upofu na udanganyifu wa kutisha. Ushuhuda ulio wazi lazima uishi kanisani. Na hii peke yake itajibu ujumbe kwa Watu Wa laodikia.... RH, Septemba 16, 1873

15."Hatupaswi kuogopa na kuuomba msamaha ulimwengu kwasababu ya kuwaambia Ukweli: Tunapaswa kudharau kuficha mambo. Dhihirisha rangi zako halisi ili kukidhi mahitaji ya wanadamu na malaika (1Wakor 4:9) kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu). Wacha ieleweke kwamba Waadventista Wa Sabato hawawezi kufanya mapatano yoyote udunia. Kwa maoni yako na imani yako lazima kusiwe na kuonekana kidogo kwa kutetereka: ulimwengu una haki ya kujua nini cha kutarajia kutoka kwetu. - Sisi ni wamoja katika imani katika Kweli za msingi za Neno la MUNGU … Tuna ujumbe kwaajili ya ulimwengu wote, Amri za MUNGU na Shuhuda za YESU KRISTO ni mzigo wa kazi yetu Ev: 16 na 179

16."Bwana anakusudia kuwaonya, kuwakaripia, kuwashauri wanadamu, kupitia shuhuda zinazotolewa, na kuzivutia akili zenu kwa umuhimu wa Ukweli wa Neno Lake. Shuhuda zilizoandikwa siyo za kutoa nuru mpya, bali kusisitiza kwa uwazi kwenye moyo, Ukweli wa uvuvio ambao tayari umefunuliwa. Wajibu wa mwanadamu kwa MUNGU na kwa wanadamu wenzake umebainishwa waziwazi katika Neno la MUNGU, lakini ni wachache miongoni mwenu wanaotii nuru iliyotolewa. Ukweli wa ziada haujatolewa; bali MUNGU kupitia Shuhuda amerahisisha zile Kweli kuu zilizokwisha kutolewa, na kwa njia Yake aliyoichagua Mwenyewe kuzileta mbele ya watu ili kuziamsha na kuzivutia akili, ili wote waachwe bila kisingizio. {5T 665.1}

17. “Kiburi, kujipenda, ubinafsi, uchoyo, chuki, husuda na wivu vimefunika kwa ukungu, nguvu za ufahamu, na ile Kweli, ambayo ingewafanya muwe na hekima ili kufikia wokovu. Ile Kweli Imepoteza uwezo Wake-Bwana wa kuchangamsha moyo, na kudhibiti akili. Kanuni muhimu sana za ucha Mungu na ibada, hazieleweki kwa sababu hakuna njaa na kiu ya ujuzi wa Biblia, usafi wa moyo, na utakatifu wa maisha. Shuhuda hazijaletwa ili kulipuuzia Neno la MUNGU, bali kuliinua juu na kuvutia akili, kwamba usahili mzuri wa Ukweli unaweza kugusa mioyo ya watu wote. {5T 665.2}

18,"Nilisema zaidi: Kama vile Neno la MUNGU linavyozingirwa ndani ya vitabu hivi na vipeperushi, ndivyo ambavyo MUNGU amewawekea hizi kuta kwa ajili ya maonyo, mashauri, makemeo na kutia moyo. Hapa mlipo mnalia mbele za MUNGU, katika uchungu wa nafsi zenu, kwa ajili ya nuru zaidi. Nimeidhinishwa kutoka kwa MUNGU kuwaambia kwamba hakuna mwale mwingine wa nuru kupitia Shuhuda utakaoangaza katika njia yenu mpaka muitumie kwa vitendo ile nuru ambayo imekwishakutolewa. Bwana amewazingira kwa nuru; lakini ninyi hamjaithamini, mmeikanyaga, na wengine

wameidharau nuru, wengine wameipuuza au kuifuata lakini kwa kutojali, ni wachache wameweka mioyo yao kuitii nuru ambayo MUNGU ameridhika kuwapatia. {5T 666.1}

Shuhuda zina Kila HALI NA mazingira ya kutusaidia Tabia zetu, Na Tabia za binadamu wenzetu. Hivi ndivyo vitu pekee yake, tutakavyopaa navyo kwenda mbinguni kutoka hapa duniani! Na kuziona uso kwa Uso, Kovu za Mikono, miguu, na ubavu wa Yesu!

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Amina

1. Alex Ngamije -PreciousPresentTruth.org Rwanda
2. Stephen Letta-Masasi, Tanzania
3. Samuel Mhololo -Kigoma, Tanzania
4. Musa Budodi -Shinyanga Tanzania
5 Isack Msusu-Kigoma, Tanzania
6. Mr and Mrs Kumbuka Mlazi Misibo -Kigoma, Tanzania
7. Aimo Abayo –Morogoro, Tanzania
8. Zablon Mgonja -Arusha, Tanzania
9. Mwalimu Peter Marwa -Mwanza, Tanzania
10. Faustine Momadi Mkama -Dar Es Salaam,Tanzania
11. Paul Masaka -Oklahoma, Marekani
12. Ibrahimu Makamba-Tarime, Tanzania
13. Geoffrey Herman -Manyara, Tanzania
14. Pendo Makori -Visiga,Tanzania
15. Judi Mmari Mugane -Siha, Tanzania
16. Kikundi cha Mbaki/Ngulu Maombi -TAUS—USA
17. Women Prayer Warriors WPM -California, Marekani
18. Ezekiel Ojwang -Kiterere,Tanzania
19. John Mugane -Nakuru, Kenya
20. Sandra Barron -Kentucky, Marekani
21. Eliphas Sambeke -Arusha, Tanzania
22. Stefano Kasiri -Kibaha, Tanzania
23.Gideon Christian - Ukerewe, Tanzania
24.Musa Muneja -Bariadi, Tanzania
25. Victoria Swai Mhololo -Arusha, Tanzania
26. Julius Letta -Morogoro, Tanzania
27. John Chilala Momadi -Dar Es Salaam, Tanzania
28. Milinje Bariki Momadi -Dar Es Salaam, Tanzania
29. Mbaraka Hamisi -Kilimanjaro, Tanzania

30. Rachel Akinyi Atandi-Nairobi, Kenya
32. Mbusi Mpagalushu -Bariadi, Tanzania
33. James Ongoro- Mara, Tanzania
34. Basanthi Thavamani-Lazar -Madras, India
35. Ndege Aruya-Rorya, Tanzania
36. Kwandu Kasiri -Pwani,Tanzania
37. Elinath Elisante Kukome -Kilimanjaro, Tanzania
38. Sharifa Athuman Seleman -Dar-es-Salaam, Tanzania
39. Jackson Musa Singano -Dar-es-Salaam, Tanzania
40. Daniel Masaka -Kisii, Kenya
41. Ellen Nyangoye- Nyagori-Rorya, Tanzania
42.Fares Ogilo-Rorya, Tanzania
43. Walter Nehemia -Dar Es Salaam, Tanzania
44. Gerard Nyafanga -Mara, Tanzania
45. Bilionea Wayoga-Rorya, Tanzania
46. Bettie Magesa Muasya-Machakos, Kenya
47. Kilango Makala -Kilimanjaro, Tanzania
48. Loyce Pima -Bunda, Tanzania
49. Niwaeli Mburuja -Hedaru, Tanzania
50. Cindy Tustch -Washington, Marekani
51. Elias Luwela-Rukwa, Tanzania
52. Sandra Barron -Kentucky, Marekani
53. John Ngasa -Mwanza, Tanzania
54. Methusela Mahumbi-Bariadi, Tanzania
55. Elmad Daudi Ndonga-Mombasa, Kenya
56. Luck Rahim Datoo -Arusha, Tanzania
57. Ruth Lilian Bango -Arusha, Tanzania
58. Mohammed Mboi -Kisii, Kenya
59. William Kalokaza-Rukwa, Tanzania
60. Eline Mrema-Kilimanjaro, Tanzania
61.Obed Lissi-Baraton, Kenya
62. Elias Luwela-Rukwa, Tanzania
63. Emmanuel Oola-Rorya, Tanzania
64.Nhandi Masunga-Bariadi, Tanzania
65. Mr and Mrs Weber- Alaska, Marekani
66. Eliakim Mabula-Bariadi, Tanzania
67. Ngusa Mayunga-Rukwa, Tanzania
68. Evans Mobegi-Kisii, Kenya
69. Debbie Bisheli-Nairobi, Kenya
70. Yunus Tiras-Tarime, Tanzania
71.Sharon Ondieki-Nairobi, Kenya
72. Ibrahimu Ibare-Tarime, Tanzania
73. Ghati Matiko-Tarime, Tanzania

74. Haron Wamboa-Machakos, Kenya
75. Timothy Misungwi-Michigan, Marekani
76. Enoc Omosa-North Carolina, Tanzania
77. Filipo Lubua-Pittsburg, Marekani
78. Gibson Mujuni-Kagera, Tanzania
79. Mickey Marr-Scranton, Marekani
80. Lisa Lothian-New York, Marekani
81. Azizi Jacob-Niassa, Mozambique
82. Robert Ndinayo-Goma, Congo
83. Eduardo Punda-Beira, Mozambique
84. Kasereka Mbilika-Goma, Congo
85. Mmaliro Congo-Goma, Congo
86. Yunus Tiras Magira-Tarime, Tanzania
87. Nasra Idrissa Oola-Lushoto, Tanzania
88. Daudi Jabez Masaka-Pennslvyania, Marekani

Wenu katika huduma ya ***MaarifaMtandaoni.Com***, ***MaarifaMtandaoni.Africa RohoYaUnabii.Org***, ***RohoYaUnabii.Net***, ***RevivalPlan.Com*** na ***Tumaini Ughaibuni Youtube***

Shuhuda zina Kila hali au mazingira ya kutusaidia Tabia zetu, Na Tabia za binadamu wenzetu. Hivi ndivyo vitu pekee yake tutakavyopaa navyo kwenda mbinguni kutoka hapa duniani! Na kumwona Mwokozi uso kwa Uso, na kuziona Kovu za Mikono, miguu, na ubavu wa Yesu!

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Amina
Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

Waanzilishi wa Huduma Grace Momadi Masaka, Daniel Masaka, Paul Masaka na Daudi Masaka-New Jersey, Marekani

Uhamishoni.Ughaibuni.Mtandaoni.Majumbani

**2025 EDITION-Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo.**

Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4T 472)

Wenu katika huduma ya ***MaarifaMtandaoni.Com***, ***MaarifaMtandaoni.Africa*** ***RohoYaUnabii.Org*** ***RohoYaUnabii.Net***, ***RevivalPlan.Com*** na ***Tumaini Ughaibuni Youtube***
Daniel Masaka and Grace Momadi Masaka -New Jersey, Marekani

# YALIYOMO


MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI... 1
Utangulizi 4
Nyakati Za Gombo La 9 10
SEHEMU YA 1—KUJA KWA MFALME 16
**SURA YA 1**
**PAMBANO LA MWISHO** 17
**SURA YA 2**
**KUITWA KUWA MASHAHIDI** 22
**SURA YA 3**
**KAZI YA UMISHONARI NYUMBANI** 29
**SURA YA 4**
**HAJA YA JUHUDI ZA DHATI** 38
**SURA YA 5**
**"MMEPOKEA BURE, TOENI BURE"** 42
SEHEMU YA 2—MACHAPISHO KATIKA HUDUMA 50
**SURA YA 6**
**MACHAPISHO YETU** 51
**SURA YA 7**
**SAMBAZA MAJARIDA** 54
**SURA YA 8**
**MTAZAMO MPANA** 62
**SURA YA 9**
**MIKUTANO YA MAKAMBI NA MACHAPISHO YETU** 66

SEHEMU YA 3—KAZI KATIKA MIJI 72
**SURA YA 10**
**HALI KATIKA MIJI** 73
**SURA YA 11**
**KAZI YA SASA HIVI** 78
**SURA YA 12**
**MBINU ZA KAZI** 86
**SURA YA 13**
**WITO KWA WALEI** 97
**SURA YA 14**
**MANENO YA USHAURI KWA WATUMISHI.** 105
SEHEMU YA 4—KAZI YA AFYA 116
**SURA YA 15**
**UAMINIFU KATIKA MATENGENEZO YA AFYA** 117
**SURA YA 16**
**WITO KWA WAINJILISTI WAMISHENARI WA KITABIBU** 126
**SURA YA 17**
**CHUO CHA WAINJILISTI CHA LOMA LINDA** 130
SEHEMU YA 5—ROHO YA UMOJA 134
**SURA YA 18**
**UMOJA MIONGONI MWA WATU WA MATAIFA TOFAUTI** 135
**SURA YA 19**
**UMOJA KATIKA YESU KRISTO** 138
**SURA YA 20**
**KAZI YA UCHAPISHAJI KATIKA CHUO CHA COLLEGE VIEW,** 142
**SURA YA 21**
**KONFERENSI ZA UJERUMANI NA SCANDINAVIA** 146
SEHEMU YA 6—MIONGONI MWA WATU WEUSI (WASIO WAZUNGU) 149
**SURA YA 22**
**WITO KWA WATENDAKAZI WEUSI** 150
**SURA YA 23**
**KUUTANGAZA UKWELI MAHALI PALIPO NA UBAGUZI WA RANGI** 153
**SURA YA 24**
**SWALA LA UTOFAUTI WA RANGI** 159
**SURA YA 25**
**KUWAZINGATIA WATENDAKAZI WEUSI** 166
**SURA YA 26**

MAHITAJI YA ENEO LA KIUTUME 168
SEHEMU YA 7—KAZI YA UHURU WA DINI 170
SURA YA 27
WAKATI WA KUJARIBIWA U MBELE YETU 171
SURA YA 28
KUFANYA KAZI SIKU YA JUMAPILI 174
SURA YA 29
MANENO YA TAHADHARI 178
SEHEMU YA 8—MASHAURI KWA WAKATI 182
SURA YA 30
UWAKILI MWAMINIFU 183
SURA YA 31
FAIDA 188
SURA YA 32
ROHO YA KUJITEGEMEA 191
SURA YA 33
MGAWANYIKO WA MAJUKUMU 194
SURA YA 34
KATIKA UNYENYEKEVU NA IMANI 199
SURA YA 35
KWA WAFANYAKAZI WA KUSINI MWA CALIFORNIA 204
SURA YA 36
"MIMI NI MTOTO MDOGO TU" 207
SURA YA 37
THAWABU YA JUHUDI ZA DHATI 210

# NYAKATI ZA GOMBO LA 9

Tunapotazama Nyakati Za Gombo La 9 Tunatazama Kipindi Cha Miaka 5 Ambayo Inaenda Hadi Kufikia Kipindi Kilichopita Cha Majira ya Joto Cha Mwaka 1909 (Juni -Agosti). Kwa Uzoefu Wa Bi White Kipindi Hiki Ni Kipindi Kilichofunguliwa Na Kufungwa Na Safari Za Kutoka Nyumbani Kwake St. Helena, Califonia, Kuelekea Mashariki Kuhudhuria Mikutano Muhimu. Kwa Dhehebu, Hiki Ni Kipindi Chenye Wingi Wa Kujengwa Upya Kutokana Na Zahama Ya Mwaka 1902-03 Na Ya Kusogeza Mbele Kazi, Ya Kufungua Makampuni Mapya, Na Kuanzisha Taasisi Mpya. **(9T 3.1)**

Kufuatia Mikutano Muhimu Huko Michigan Kipindi Cha Majira Ya Kuchipua Ya 1904 (Machi-Mei), Mama White Alitembelea Kusini Na Baadaye Alishika Njia Kuelekea Washington D.C, Ambapo Hatua Zilikuwa Zikichukuliwa Kupata Majengo Kwa Ajili Ya Kazi Ambayo Ilikuwa Imeanzishwa Katika Makao Makuu Ya Nchi Ya Marekani. Kulikuwa Na Jengo Jipya La Makao Makuu Ya Kanisa Kuweza Kujengwa Pale Takoma Park Maryland (General Conference), Gazeti la Review And Herald Lazima Lipewe Makazi Karibu na General Conference Mahali Panapoitwa Hagerstown, Maryland, Nyumba Ya Uponyaji-Tiba Rahisi Kwa Jina Maarufu la Takoma Park Sanitarium na Baadaye Hospitali, Ilikuwa Lazima Ijengwe, Na Chuo Washington Adventist University Kuanzishwa hapo Takoma Park. Ukweli Kwamba Mama White Aliweka Makazi Washington DC Kwa Miezi Kadhaa, Ambapo Aliweza Kutoa Ushauri Juu Ya Kazi, Kwani Taasisi Hizi Nne Zilikuwa Zimeanzishwa, Ilikuwa Ni Tukio Kubwa La Kutiwa Moyo Kwa Watenda Kazi. Pia Ilichochea Shinikizo La Kusonga Mbele Katika Kuwafikia Waumini Na Kuwajengea Ujasiri Kwa Dhehebu Lote Kwamba Mungu Ameongoza Katika Kuhamishia Nyumba Ya Uchapaji Na Utawala Katika Makao Makuu Ya Taifa Washington DC, Makao Makuu Haya Kabla Yalikuwa Battle Creek, Michigan. (Mwaka 1980 Makao Makuu ya Kanisa GC, Yalihamishwa Old Columbia Pike Maryland, Karibu na Makao Makuu ya Zamani). **(9T 3.2)**

Hiki Ni Kipindi Cha Maendeleo Makubwa Katika Maendeleo Ya Kazi Za Afya Katika Pwani Ya Pasifiki. Nyumba Za Tiba Rahisi (Sanitarium) Zilifunguliwa Katika Jiji La Taifa, Glendale, Na Loma Linda, Califonia. Kuanzia Mwanzo Loma Linda Ilikuwa Imejiweka Kuwa Kituo Cha Kutoa Elimu Kwa Watendakazi Katika Huduma Za Afya Na Kwa Siku Za Baadae Kufanya Kazi Za Dhehebu Hili Zilizoanza Battle Creek. Katika Vipindi Hivi Vigumu Vya Kuanzisha Chuo Cha Tiba/Utabibu, Mama White Alifanya Ziara Nyingi Kusini Mwa Califonia Ambapo Angetoa Mashauri Yake

Binafsi Na Kuwatia Moyo Watu, Na Kusaidia Kuweka Mipango Kwa Kazi, Kwa Kadri Ilivyosonga Mbele. Na Kuwapatia Mafunuo Ambayo Bwana Alimpatia, Ambayo Yalitusogeza Hatua Kwa Hatua Hatimaye Kuanzisha Rasmi Chuo Kilichotambuliwa Kwa Afya (Loma Linda Medical University). Hivyo Vizuizi Visivyoweza Kushindwa Havikuwepo Kwa Sababu Ya Imani Na Usadikisho Kutoka Kwenye Maneno Na Mashauri Ya Mara Kwa Mara Ya Roho Ya Unabii, Vinginevyo Taasisi Kamwe Zisingeweza Kudumu. **(9T 3.3)**

Haya Maslahi Muhimu Ndiyo Yaliyomfanya Mama White Kuhamisha Makazi Na Maandishi Yake, Matokeo Yake Ilikuwa Ni Kuchelewa Sana Kwa Kutoka Kwa Vitabu Ambavyo Karibuni Vingekuwa Shambani Kufanya Kazi. Huduma Ya Uponyaji Ni Kitabu Pekee Cha Mama White Kilichotoka Katika Kipindi Cha Miaka Mitano.***(9T 4.1)***

Kazi Ya Kanisa Katika Kipindi Hiki, Ilikuwa Imekua Kwa Upana Sana Kwa Sisi Kutaja Kwa Upana Hatua Mbalimbali Za Ukuaji. Ujumbe Ulikuwa Ukisambaa Ulimwengu Wote, Wamishenari Walitumwa Mahala Pengi Duniani Kwa Wingi. Taasisi Nyingi Zilijitoa Katika Nyanja Za Elimu, Uchapaji Na Tiba/Afya Vilianzishwa. Ujumbe Kwa Hakika Ulikuwa Unafika Mwisho Wa Nchi. **(9T 4.2)**

Ilileta Furaha Kuu Katika Moyo Wa Mama Ellen White Kukutana Na Wawakilishi Kutoka Kote Ulimwenguni Walipokutana Washington, D.C Kipindi Cha Majira Ya Kuchipua Ya Mwaka 1909 Kwa Ajili Ya Uchaguzi Wa Konferensi Kuu (General Conference Session). Hii Ilikuwa Safari Yake Ya Mwisho Mashariki—Hiki Kilikuwa Kikao Chake Cha Mwisho Kuhudhuria Katika Konferensi Kuu. Mama White Alikuwa Sasa Na Umri Wa Miaka Themanini Na Moja, Na Alikuwa Ametoa Kipindi Kirefu Cha Huduma Katika Kazi Ya Bwana. Alishuhudia Kazi Ikikua Kutoka Katika Changamoto Ambapo Kulikuwa Na Watunza Sabato Wachache Waliotazamia Marejeo Ya Haraka Ya Bwana. Sasa Walikuwa 85,000, Na Walikuwepo Wachungaji 1,200 Waliowekewa Mikono Na Kupewa Vibali Vya Kazi. Wakati Ellen White Anasimama Mbele Ya Konferensi Kuu Aliongozwa Kuongea Juu Ya Masomo Kadhaa Ya Umuhimu Ambayo Lazima Yapitiwe Upya. Miongoni Mwayo Ni Matengenezo Ya Afya. Kwa Miaka 45 Alikuwa Amefundisha Juu Ya Kanuni Kuu Za Kuishi Kwa Afya Ambazo Ziliwasilishwa Kwake Kwa Maono. Alishuhudia Matunda Ya Mafundisho Yake. Hata Hivyo, Kulikuwa Na Baadhi Ya Watu Waliokuwa Wapinzani na Walirudi Nyuma, Kuna Wengine Ambao Walikuwa Wamelemewa Na Misimamo Yenye Kupitiliza, Hivyo Alipitia Vipengele Vya Msimamo Wetu Na Mafundisho Pointi Kwa Pointi. Tamko Hili Lilitolewa Mbele Ya Konferensi Kuu Linaunda Sura Muhimu ya Gombo La 9. **(9T 4.3)**

Mada Nyingine Aliyochagua Kuzungumzia Ilikuwa Ya Chuo Cha Afya/Tiba Cha

Lomalinda. Aliweka Malengo Ya Taasisi Hiyo Na Kuwasihi Watenda Kazi Na Walei Kuwa Sehemu Ya Mafanikio. Ujumbe Huu Muhimu Pia Upo Katika Gombo La 9. ***(9T 5.1)***

Bi White Alikuwa Ameona Kazi Ya Utawala Ya Maendeleo Ya Kanisa Kutoka Kuwa Kamati Ya Watu Watatu, Iliyoteuliwa Mwaka 1863 Kuchukua Uongozi Wa Konferensi Kuu Kwa Ujumla Na Kuwa Taasisi Yenye Hadhi Na Idara Na Divisheni Na Union Ikigawa Majukumu Miongoni Mwa Mamia Waliobeba Mzigo Wa Kazi Katika Sehemu Mbalimbali Za Fildi Za Ulimwengu. Kwa Maneno Yake Akimalizia Hotuba Yake Alitoa Wito Kwa Umoja Na Kujitoa Wakfu. Katika Maneno Yake Aliyoandika Alijikita Sana Kwa Mamlaka Iliyopo Katika Konferensi Kuu Na Umuhimu Wa Maamuzi Yanayochukuliwa Na Konferensi Kuu- GC- Wakati Wajumbe Wote Wakiwepo na Wanapopiga Kura Wakiwa Pamoja (Full Session). Aliandika Na Kusema Juu Ya Mgawanyo Wa Majukumu Na Umuhimu Wa Unyenyekevu Na Imani. Mashauri Haya Yanafanya Sehemu Muhimu Ya Kufungia Gombo La Tisa. **(9T 5.2)**

Karne Ilipokua Inaanza (1900) Bi White Alianza Kutoa Wito Wa Kuwa Na Shauku Mpya Ya Kufanya Uinjilisti Kwa Mamilioni Ya Watu Katika Miji Na Majiji Makuu Ya Ulimwenguni Pote (metropolitan). Mahitaji Haya Yametiliwa Mkazo Tena Na Tena Katika Mashauri Yaliyotumwa Kwa Watendakazi Viongozi. Katika Kujibu Hii Hoja, Shauku Pekee Yenye Nguvu Kubwa Kwa Uamsho Wa Majiji Ilianzishwa. Maslahi ya Kazi katika Miji Mikubwa Ilizinduliwa. Miji Mikubwa Ilifikiwa. Mikutano Mingi ya Hadhara Iitwayo Efoti ilifanywa, Makanisa Ya Siku Nyingi Yalihuishwa Na Makanisa Mapya Yalianzishwa. Kuutunza Wito Kwa Ajili Ya Kazi Hii Na Mashauri Ya Jinsi Ya Kuifanyia Kazi Hii Iwe Ya Kudumu, Sehemu Kubwa Ya Gombo La Tisa Imetolewa Kwa Ajili Ya Somo Hili Muhimu. **(9T 5.3)**

Tulikuwa Pia Katika Siku Ambazo, Taasisi MbaliMbali Zilipokuja, Nazo Zilitoa Wito Na Nguvu Mpya KwaAjili Ya Talanta/Vipawa Na Nguvu Ya Washiriki Wetu Ambao Ni Walei. Ilianza Kuwa Wazi Kuwa Kazi Hii Kamwe Isingeweza Kuisha Isipokuwa Walei Waungane Na Wahudumu Katika Kusukuma Mbele Ujumbe Kwa Ulimwengu. Kazi Ya Walei Ilikuwa Na Umuhimu Wake Tena. Magombo Mawili Ya Mwisho Ya Shuhuda Yanaongeza Msisistizo Juu Ya Kazi Ya Walei, Na Hapa Ilifikia Kilele Cha Gombo La Tisa. Picha Inayofuata Ya Dhahama Za Mwisho Na Matukio Ya Kufungwa Kwa Historia Ya Ulimwengu, Kurasa Kadhaa Zimetolewa Kuwaita Waadventista Wasabato Kushiriki Kikamilifu Katika Uinjilisti, Katika Huduma Ya Nyumbani, Na Katika Kugawa Na Kusambaza vitabu Na Machapisho.**(9T 6.1)**

Ipo Pia Mistari Mingine Miwili Yenye Mashauri Ambayo Imewasiliswa Katika Gombo Hili Kwa Mara Ya Kwanza Kwa Wakati Huu, Katika Shuhuda, Ingawa

Maelekezo Ya Kujitosheleza Yamekwisha Kutolewa Kwa Miaka Yote Ambayo Yanafanana. La Kwanza Ilikuwa Juu Ya Kazi Ya Watu Wanaobaguliwa (Wasio Wazungu, Hasa Weusi). Ya Pili Ilikuwa Juu Ya Kazi Ya Uhuru Wa Dini. Kwa Kiasi Kikubwa Ilikuwa Ni Kujibu Wito Wa Mama White Alioutoa Kwenye Gazeti La Review Katikati Ya Miaka 1900 Kwamba Watendakazi Na Walei Waende Huko, Katika Ardhi Ya Kusini Na Kuanza Huduma Yao, Wengine Katika Elimu, Afya, Wengine Katika Kuhubiri Ujumbe Na Wengine Katika Kuuishi Ujumbe Halisi Kimya Kimya Katika Mtindo Wa Maisha, Pale Ambapo Nyumba Zilianza Kujengwa Katika Maeneo Ambako Ujumbe Ulikuwa Haujapokelewa Kama Nuru. Wengine Bado Walijiunga Na Kazi Hii Kwa Kutii Wito Wa Gombo La Saba. Watenda Kazi Walikabiliwa Na Matatizo Mbalimbali. Mipango Lazima Ilikuwa Iwekwe Kwa Ajili Ya Kusonga Mbele. Mambo Mbalimbali Mapya Lazima Kukutana Nayo Hasa Yale Yanayoendana Na Kazi Ambapo Kulikuwa Na Ubaguzi Mkubwa Wa Rangi. Kupitia Miaka Ya Changamoto Kubwa Mashauri Yalitolewa Ambayo Ilifanyika Kama Ngao Ya Usalama Kwa Ajili Ya Kazi, Na Kufanya Mashauri Haya Kuwa Alama Ya Kudumu Kuhudumia Kanisa, Iliongezwa Katika Gombo La 9. **(9T 6.2)**

Uhuru Wa Dini Ni Msitari Wa Jitihada Ambao Tumeufanyia Kazi Kwa Miaka Mingi. Wengine Walikuwa Na Msimamo Wa Kupitiliza (Ushabiki) Kwa Kusema Kuwa Katika Kutunza Sabato Mtu Lazima Aifanye Kuwa Maarufu Kwa Wale Wasioitunza Na Wanaotunza Jumapili. Kwa Baadhi Ya Maeneo Mengine Hili Lilipelekea Kuwepo Kwa Mateso. Mungu Kwa Wema Wake Alituma Ujumbe Kwa Watu Hao Kutupatia Mizania Ya Mawazo Ya Maswala Kama Haya. Hayo Pia, Yanaonekana Katika Gombo Hili la 9, Katika Sehemu Isemayo Kazi Ya Uhuru Wa Dini Ikianza na Sura Isemayo, "Muda Wa Majaribu Kwetu", Na Inafunga sa Sura Yenye "Maneno Ya Tahadhari." Hivyo Gombo La 9, Linaleta Pamoja Mashauri Mapya Na Ya Zamani, Ikitafakarisha/Ikikumbusha Juu Ya Mistari Ya Maelekezo, Ikitoa Maelekezo Ya Kina Na Mashauri Katika Mistari Mingine, Ikitia Moyo Kufanya Kazi, Kutoa Huduma, Na Kuonesha Hatari Ya Imani Ya Kupitiliza/Ushabiki na Ikileta Ujasiri/Imani Katika Taasisi Na Kuonesha Thawabu Ya Bidii Isiyokoma, Basi Hicho Ndiyo Kikawa Kilele na Kumbukizi Ya Gombo Hili la Shuhuda Kwa Kanisa. **(9T 7.1)**

Kazi Ya Ellen White Haikufungwa Baada Ya Kutoa Shuhuda Kwa Kanisa, Gombo La 9. Wakati Huu Alijitoa Kwa Karibu Kabisa Na Kazi Yake Ya Kuandaa Kitabu, Katika Miaka Mitano Iliyofuatana, Alileta Kitabu Cha Matendo Ya Mitume/*Acts Of Apostles* Mwaka 1911 Na Mashauri Kwa Wazazi, Waalimu, Na Wanafunzi/*Counsels for Parents, Teachers And Student*s Mwaka 1913. Pia Alifanya Kazi Yake Ya Mwisho Kwenye Machapisho Ya Muswada/Manuscript, Na Kwenye Toleo Jipya La Kitabu Kipya Cha Watenda Wa Injili/*Gospel Workers*, Na Mistari Ya Maisha*/Life Sketches* Kilichochapwa Mwaka 1915 Na Manabii Na

Wafalme/*Prophets and Kings* Ambacho Kilitoka Kwenye Kiwanda Cha Uchapaji Mwaka 1916. **(9T 7.2)**

Alifurahi Kuweka Juhudi Kwa Namna ya Kipekee Kupeleka Ujumbe Kuionya Majiji Makubwa, Na Kwa Nyakati Tofauti Ujumbe Umekuja Kutoka Katika Kalamu Na Maandishi Yake Ukiwa Na Jumbe Za Mashauri Na Maelekezo Juu Ya Umuhimu Wa Hatua Hii Ya Kazi. Maendeleo Yenye Uhakika na Thabiti Yaonekanayo Ulimwenguni Yalionyeshwa Na Huyu Mjumbe Huyu Wa Mungu Ambaye Sasa Akiishi Katika Milima Mitulivu, Kaskazini Mwa Califonia. Ingawa Alijua Kazi Yake Ilikuwa Inakaribia Mwisho, Hakuogopa Juu Ya Kazi Ya Mungu Katika Siku Za Usoni, Na Aliandika'' Haijalishi Kama Maisha Yangu Yatanusuriwa Au Yasiweze Kunusuriwa, Maandiko Yangu Yataendelea Kuongea Daima, Na Kazi Zake Zitasonga Mbele Maadamu Muda Utataendelea Kuwapo''- Kuandika Na Kutuma Shuhuda Kwa Kanisa, Kurasa Za 13,14. **(9T 7.3)**

Wakati Mipango Inawekwa Kwa Ajili Ya Mkutano wa General Konferensi Wa Mwaka 1913, Mama White, Angefurahi Kama Angehudhuria, Lakini Kutokana Na Kuwa Na Umri Mkubwa Ilikuwa Siyo Hekima Kuhudhuria. Kwa Kuwa Hakuwa Na Uwezo wa Kuzungumza Kwenye Mkutano, Aliandika Mawasilisho Mawili Ili Yasomwe Kwa Wajumbe Na Washiriki Wa Kanisa Waliokusanyika. Katika Ujumbe Wake Wa Pili Uliosomwa Na Mwenyekiti Wa Konferensi Kuu Katika Mkutano Huu Wa Uchaguzi, Muda Wa Asubuhi Mei 27, Alipitia Uzoefu Wa Miaka Ya Nyuma Na Kufurahia Alama Za Ushahidi Za Wazi Zilizoonekana, Ambazo Mungu Alitenda Katika Kuwaongoza Watu Wake. Kisha Kwa Kuangalia Mbele, Kisha Alikumbusha Wajumbe Kwa Upya Tena Kufanya Jitihada Tena Ajili Ya Kazi Ya Kuokoa Roho Na Kutoa Wito Wa Pekee Juu Ya Miji Ambayo Haikuwa Imeonywa. Akiangalia Mbele Aliona Ushindi Wa Kanisa Na Kutoa Maneno Ya Kutia Moyo. **(9T 8.1)**

"Nina Maneno Ya Kutia Moyo Kwenu Wajoli. Tusonge Mbele Katika Imani Na Kwa Matumaini Tukitegemea Vitu Vikubwa Kutoka Kwa Mungu. Adui Atatafuta Kila Njia Kukwamisha Juhudi Zilizowekwa Ili Kuendeleza Ukweli Lakini Katika Nguvu Za Mungu Mnaweza Kupokea Ushindi. Hebu Kusiwepo Na Kukatishana Tamaa Kwa Maneno Yanayozungumzwa, Lakini Tu Maneno Yatakayowafanya Kuwa Imara, Kuwatia Moyo, Kuwategemeza Na Kuwaimarisha Watendakazi Wenzako…… **(9T 8.2)**

Matamanio na Maslahi Ya Kazi Kwangu Kwa Jumla Ni Ya Kina Bado Kama Zamani Na Mimi Ninatamani Kusudi La Ukweli Wa Leo Litasonga kwa Uhakika na Kasi Katika Pande Zote Za Ulimwengu….. **(9T 8.3)**

"Ninaomba Kwa Dhati Kuwa Kazi Tuifanyayo Sasa, Itagusa Mioyo Kwa Kina Ndani

Ya Moyo, Roho Na Akili. Changamoto Zitaongezeka, Lakini Sisi Kama Waaminio Katika Mungu Tutiane Moyo, Kwa Kila Mmoja Wetu. Hebu Tusishushe Viwango Vyetu, Lakini Tuvipandishe Juu, Tukimtazama Yeye, Ambaye Ndiye Mwandishi Na Mmalizaji Wa Imani Yetu. Ninapokuwa Siwezi Kulala Usiku, Ninainua Moyo Wangu Katika Maombi Kwa Mungu Naye Ananitia Nguvu Na Kunipa Hakikisho Kwamba Yeye Yuko Pamoja Na Wahudumu Wake, Katika Filidi Hapa Marekani Na Mahali Pengine Nje ya Nchi. Ninatiwa Moyo Na Kubarikiwa Kwa Kujua Bwana Wa Israel Yuko Pamoja Na Watu Wake, Naye Ataendelea Kuwa Nasi Hata Mwisho Wa Wakati…… **(9T 8.4)**

"Bwana Anatamani Kuona Kazi Ya Kuutangaza Ujumbe Wa Malaika Watatu Ikienda Kila Mahala Na Ufanisi Unazidi Kuongezeka. Kama Alipokuwa Akifanya Katika Zama/Vizazi Vyote Kutoa Ushindi Kwa Watu Wake, Maana Alikwisha Kufanya Katika Vizazi Vyote Kutoa Ushindi Kwa Watu Wake, Ndivyo Katika Kizazi Hiki Anataka Kuchukua Ujumbe Wa Ushindi Na Kukamilisha Kusudi La Kanisa Lake. Yeye Anawasihi Watakatifu Wake Kusonga Mbele Kwa Umoja, Kwa Nguvu na Nguvu Zaidi, Kutoka Kwenye Imani Na Ongezeko La Uhakika Katika Ujasiri Katika Kweli Na Haki Katika Kusudi Lake. **(9T 9.1)**

"Hatuna Budi Kusimama Imara Kama Mwamba Katika Kanuni Ya Msingi Wa Neno La Mungu, Tukumbuke Kwamba Mungu Yuko Pamoja Nasi Kutupatia Nguvu Kukabiliana Na Uzoefu Mpya Kila Siku. Hebu Tuendeleze Kanuni Za Haki, Daima Katika Maisha Yetu, Ili Tuweze Kusonga Mbele Kutoka Ushindi Hadi Ushindi Kaika Jina La Bwana. Tushikilie Kwa Utakatifu Sana Imani Ambayo Tumepewa Kwa Majaliwa Ya Mungu Na Ushahidi Kwa Maagizo na Kibali Cha Roho Wa Mungu Kutoka Kwenye Uzoefu Wa Kwanza Hadi Wakati Huu. Tufurahie Kazi Ya Thamani Ambayo Mungu Ameibeba Na Kuindeleza Mbele, Kupitia Watu Wake Wazitunzao Amri Zake, Na Ambao Kupitia Nguvu Za Neema Yake, Watakuwa Imara Na Wenye Nguvu Na Ufanisi Zaidi Na Zaidi. Adui Anatafuta Kutia Wingu Hekima na Utambuzi, Ili Kuwadhoofisha Watu Wa Mungu, Na Kudhoofisha Ufanisi Wao, Lakini Watakapofanya Kazi Kama Vile Roho Wa Bwana Anavyoongoza, Yeye Atafungua Milango Ya Fursa Kwa Watu Wake Ili Kujenga Mahala Pa Zamani Palipobomoka na Kuachwa Ukiwa. Uzoefu Wao Utaendelea Kukua Daima Mpaka Bwana Atakapokuja Kutoka Mbinguni Kwa Nguvu Na Utuufu Mwingi Kusimika Muhuri Wake Wa Ushindi Wa Mwisho Kwa Waaminifu. **(9T 9.2)**

"Kazi Iliyo Mbele Yetu Ni Ile Itakayonyumbulisha Kila Nguvu Ya Mwanadamu. Itahimiza Kuizoeza Imani Imara Na Uaminifu Wa Kukesha Bila Kuyumba daima. Kwa Nyakati Fulani, Magumu Tutakayokutana Nayo Yatatuvunja Mioyo Yetu. Ukuu Wa Hii Kazi Utatushtua. Hata Hivyo, Kwa Msaada Wa Mungu, Watumishi Wake Hatimaye Watashinda."-Imeripotiwa Katika Kitini Cha Konferensi Kuu, May 28, 1913, kurasa Za 164,165. **(9T 9.3)**

Katika Nyakati Za Gombo La Tisa La Shuhuda Kwa Kanisa Lililoandikwa Katika Kipindi Cha Miaka Hamsini Na Mitano, Kanisa Lilikua Kwa Kasi Na Kuendelea Na Kuimarika. Mashauri Yaliyotolewa Yalikidhi Kulinda Usalama, Kuonya, Kukaripia Na Yaliongoza Miguu Mingi Iliyoacha Njia Kurudi Kwenye Njia Ya Haki na Kujisahihisha Na Maneno Ya Kuchangamsha Na Kutia Moyo Yaliamsha Mioyo Mingi Iliyozimia, Na Picha Hii Ya Thawabu Kwa Waaminifu Imechochea Maelfu Kuamua Kufikia Malengo Yaliyowekwa Mbele Yetu. **(9T 10.1)**

Tunapotazamia Mbele Yetu, Lazima Tukumbuke Maneno Katika Kitabu Cha Michoro Ya Maisha, Ukurasa Wa 196:**(9T 10.2)**

"Hatuna Chochote Cha Kuogopa Kwa Ajili Ya Siku Zijazo, Isipokuwa Tu Kama Tutasahau Njia Ambayo Bwana Ametuongoza, Na Mafundisho Yake Katika Historia Yetu Iliyopita." **(9T 10.3)**

Wadhamini Wa Maandishi Ya Ellen White.

# UJIO WA MFALME

37 Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia.
38 Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; Naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye.
39 Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu. Waebrania 10

# SEHEMU YA 1—KUJA KWA MFALME

"Bado kitambo kidogo sana, Yeye ajaye atakuja, na wala hatakawia." Waebrania 10:37.

## SURA YA 1
## PAMBANO LA MWISHO

Tunaishi katika wakati wa mwisho. Utimizwaji wa haraka wa ishara za nyakati hutangaza kuwa kuja kwa Kristo kuko karibu. Siku tunazoishi ni nyeti, adhimu na muhimu. Roho wa Mungu anaondolewa taratibu duniani, hatua kwa hatua lakini kwa uhakika. Mapigo na hukumu za Mungu tayari zinawaangukia watu wanaodharau neema ya Mungu. Majanga juu ya nchi kavu na bahari, hali ya jamii kukosa utulivu, tahadhari na tetesi za vita, na matukio ya kutisha, yanatoa onyo na kushangaza. Huonesha zahama ya matukio makuu yanayokaribia na yenye kutisha. {9T 11.1}

Mawakala wa uovu wanaunganisha nguvu zao na kujizatiti. Wanajiimarisha kwa zahama kuu ya mwisho. Mabadiliko makubwa hivi karibuni yatatokea katika ulimwengu wetu, na harakati za mijongeo ya mwisho zitakuwa za kasi sana. {9T 11.2}

Hali ya vitu ulimwenguni inaonyesha kuwa nyakati za taabu ziko juu yetu. Kurasa za magazeti ya kila siku zimejaa dalili za pambano baya linalokaribia muda si mrefu. Ujambazi wa wazi hutokea mara kwa mara. Migomo ni ya kawaida. Wizi na mauaji hufanywa kila upande. Watu wanaomilikiwa na mapepo huutoa uhai wa wanaume, wanawake, na watoto wadogo. Watu wamerubuniwa kuupenda uovu kwenye mawazo yao ya kufikirika na hivyo kila aina za uovu hutawala. {9T 11.3}

Adui amefanikiwa kupotosha haki na kujaza mioyo ya watu na misukumo ya faida

za ubinafsi "Haki imesimama mbali sana; maana Kweli imeanguka katika njia kuu, na unyofu hauwezi kuingia." Isaya 59:14. Ndani ya miji mikubwa kuna umati wa watu wanaoishi katika umaskini, uharibifu, huzuni na unyonge, karibu sana wanakosa chakula, malazi,na mavazi; wakati katika miji hiyo hiyo kuna wale ambao wana zaidi ya matamanio ya mioyo yao, ambao wanaishi kwa anasa/lakshari, hutumia pesa zao kwa nyumba za fahari/ukwasi zilizo na samani/vifaa vingi, kwa mapambo ya kibinafsi, au mambo mabaya zaidi, ya kuridhisha hamu na tamaa za kimwili, kama pombe, tumbaku, na vitu vingine vinavyoharibu nguvu ya ubongo, kuondoa usawa wa akili, na kushusha roho. Vilio vya watu wanaotaabika kwa njaa huja mbele za Mungu, wakati kwa kila aina ya ukandamizaji na ulafi watu wanajirundikia utajiri mkubwa. {9T 11.4}

Katika tukio moja, nilipokuwa katika Jiji la New York, katika majira ya usiku nilielekezwa kutazama majengo yaliyoinuka ghorofa baada ya ghorofa kuelekea angani. Majengo haya yalithibitishwa kutowaka moto (fireproof), na yalikuwa yameinuliwa ili kuwatukuza wamiliki na wajenzi wake. Juu na juu zaidi Majengo haya yaliinuliwa na kuongezeka, na ndani yake vifaa vyenye gharama kubwa vilitumika. Wamiliki wa majengo haya hawakujiuliza: "Je! Tunawezaje kumtukuza Mungu?" Bwana hakuwa katika fikra zao. {9T 12.1}

Nilifikiri: “Laiti, wale ambao wanawekeza katika mali zao wangeweza kuona mwenendo wao kama vile Mungu anavyouona! Wanarundika majengo mazuri, lakini ni upumbavu gani mbele za Mtawala wa ulimwengu hawa wenye kupanga na kubuni. Hawajifunzi kwa nguvu zote za moyo na akili jinsi wanavyoweza kumtukuza Mungu. Wamepoteza ufahamu wa hili, ambalo ndilo jukumu la kwanza la mwanadamu.” {9T 12.2}

Wakati majengo haya yakipanda juu, wamiliki walifurahi kwa kiburi kikubwa, na matamanio ya ukuu, kwamba walikuwa na pesa za kutumia katika kujifurahisha nafsi na kuchochea wivu wa majirani zao. Pesa nyingi ambazo wao walikuwa wamewekeza zilikuwa zimepatikana kupitia shughuli za kupora, ubahili na kupitia kuwatafuna maskini. Walisahau kuwa mbinguni hesabu ya kila shughuli ya biashara/shuguli huhifadhiwa; kila jambo lisilo la haki, kila tendo la ulaghai, limeandikwa. Wakati unakuja ambapo katika ulaghai, wizi na jeuri watu hawa watafikia hatua ambayo Bwana hataruhusu waivuke, na watajifunza kwamba uvumilivu wa Bwana una kikomo. {9T 12.3}

Baadaye maono yaliyopita mbele yangu yalikuwa mlio wa king’ora cha moto. Watu walitazama juu ya majengo yaliyoinuka na ya kudhaniwa kutoshika moto na kusema: "Yako salama kabisa." Lakini majengo haya yaliungua kana kwamba yametengenezwa kwa lami/petroli. Magari ya Zimamoto na mashine visingeweza kufanya chochote kuzuia moto na uharibifu. Watu wa kuzima moto hawakuweza

kufanikiwa kutumia mashine zao kuizima mioto. {9T 13.1}

Nimeelekezwa kwamba wakati wa Bwana utakapofika, na kusiwe na mabadiliko yoyote yaliyofanyika mioyoni mwa wanadamu wenye kiburi, wenye tamaa ya ukuu, ndipo watu watafahamu kwamba mkono ambao ulikuwa una nguvu ya kuokoa na tayari kufanya hivyo, sasa utakuwa wenye nguvu kuharibu. Hakuna nguvu ya kidunia inayoweza kuzuia mkono wa Mungu. Hakuna nyenzo zinazoweza kutumika katika ujenzi wa majengo ambazo zitayahifadhi dhidi ya uharibifu wakati wa Mungu ulioamriwa utakapofika kulipiza kisasi kwa wanadamu kwa kupuuza kwao sheria Yake na kwa tamaa yao ya ubinafsi. {9T 13.2}

Sio wengi, hata kati ya waelimishaji na viongozi wa serikali, ambao wanaelewa sababu za hali ya sasa ya jamii. Wale ambao wanashika hatamu za serikali hawawezi kutatua shida ya kuharibika kwa maadili, ufukara, umaskini, na kuongezeka kwa uhalifu. Wanajitahidi na kupambana bure kuweka shughuli za biashara katika misingi salama zaidi. Ikiwa watu wangezingatia na kuweka umakini zaidi kwenye mafundisho ya Neno la Mungu, wangepata suluhisho la shida ambazo zinawasumbua, zinawafadhaisha na kuwachanganya. {9T 13.3}

Maandiko yanaelezea hali ya ulimwengu kabla tu ya kuja Kwake Kristo mara ya pili. Kuhusu watu ambao kwa ujambazi na ulafi wanajikusanyia utajiri mwingi, imeandikwa: "Mmejiwekea akiba katika siku za mwisho. Angalieni, ujira wa wafanya kazi ambao wamevuna mashamba yenu, mliozuia kwa hila, unapiga kelele, na vilio vyao waliovuna vimeingia masikioni mwa Bwana wa Majeshi/Sabaoth. Mmeishi kwa anasa duniani, na kujifurahisha kwa tamaa; mmejilisha mioyo yenu, kama siku ya machinjo. Mmemhukumu na kumwua mwenye haki; wala hashindani nanyi (Yakobo 5: 3-6). {9T13.4}

Lakini ni nani anayesoma maonyo yaliyotolewa ya ishara na nyakati zinazotimia kwa haraka? Ni hisia gani hufanywa juu ya walimwengu? Ni badiliko gani linaonekana katika mitazamo yao? Hakuna zaidi ya ilivyoonekana katika mtazamo wa wakazi wa ulimwengu wa Nuhu. Walimezwa katika mambo ya kiulimwengu na raha, watu wa zamani walioishi kabla ya gharika "hawakutambua, hata gharika ikaja, ikawazoa wote. "Mathayo 24:39. Walikuwa na maonyo yaliyotoka mbinguni, lakini walikataa kutii. Na leo ulimwengu, bila kujali sauti ya onyo ya Mungu, unafanya haraka kuelekea katika wa upotevu wa milele. {9T 14.1}

Ulimwengu unachochewa na roho ya vita. Unabii wa Danieli sura ya kumi na moja karibu unafikia utimilifu wake kamili. Hivi karibuni matukio ya taabu yaliyotabiriwa katika unabii yatatokea. {9T 14.2}

"Tazama, Bwana ameifanya dunia kuwa tupu, aifanya ukiwa, aipindua, na kuwatawanya wakaao ndani yake. . . . Kwa maana wameziasi sheria, wameibadili

amri, wamelivunja agano la milele. Ndiyo sababu laana imeila dunia, na hao wanaoishi humu wameonakana kuwa na hatia . . . . Sauti ya furaha ya matowazi imekoma, kelele yao wafurahio imekwisha; furaha ya kinubi inakoma. "Isaya 24: 1-8. {9T 14.3}

“Ole wake siku hii! Kwa maana siku ya Bwana inakaribia, nayo itakuja kama uangamivu utokao kwake aliye Mwenyezi……. Mbegu zinaoza chini ya udongo wake, ghala zimeachwa ukiwa, mabanda yamevunjika;kwa maana nafaka imekauka. Jinsi wanyama wanavyougua! makundi ya ng'ombe yanafadhaika, kwa sababu hawana malisho; naam, makundi ya kondoo yamepata mateso. “Mzabibu umesinyaa, mtini nao umevia; nao mkomamanga, na mtende, na mtofaa, Naam, miti yote ya mashamba imekauka; Maana furaha imekauka katika wanadamu.” Yoeli 1: 15-18, 12. {9T 15.1}

"Moyo wangu umefadhaika ndani yangu; ... siwezi kunyamaza, kwa sababu umesikia, Ee nafasi yangu,sauti ya tarumbeta, mshindo wa vita. Ungamivu baada ya uangamivu umetangazwa; maana nchi yote imeharibika. "Yeremia 4:19, 20. {9T 15.2}

"Naliingalia nchi, na, tazama, ilikuwa ukiwa, haina watu; naliziangalia mbingu, nazo zilikuwa hazina hazina nuru. Naliiangalia milima,na tazama, ilitetemeka, na milima yote ilisogea huko na huko . Nikatazama, na tazama, hapakuwa na mtu hata mmoja, na ndege wote wa angani wamekwenda zao. Nikangalia, na tazama, shamba lilizozaa sana limekuwa ukiwa;na miji yote ilikuwa imebomoka. "Mstari wa 23-26. {9T 15.3}

"Ole! Maana siku ile ni kuu, hakuna inayofanana nayo; maana ni wakati wa taabu yake Yakobo; lakini ataokolewa nayo.” Yeremia 30: 7. {9T 15.4}

Sio wote katika ulimwengu huu waliochukua upande wa adui, kinyume na Mungu. Sio wote wamekuwa wasio waadilifu. Kuna wachache waaminifu ambao ni wa Kweli kwa Mungu; Maana Yohana anaandika: "Hawa ndio wazishakao amri za Mungu, na imani ya Yesu. "Ufunuo 14: 12. Hivi karibuni pambano kali litainuka dhidi ya wale wanaomtumikia Mungu na wale wasiomtumikia. Hivi karibuni kila kitu kinachoweza kupepetwa kitapepetwa, ili yale yasiyoweza kuchujwa yabaki. {9T 15.5}

Shetani ni mwanafunzi wa Biblia mwenye bidii. Anajua kuwa wakati wake ni mfupi, na anatafuta kila namna kuipinga/kuipiku kazi ya Bwana juu ya dunia hii. Haiwezekani kutoa wazo lolote la uzoefu wa watu wa Mungu ambao watakuwa hai duniani wakati utukufu wa mbinguni na kurudiwa kwa mateso ya zamani vitakapochanganywa. Watatembea katika nuru itokayo kwenye kiti cha enzi cha Mungu. Kwa njia za malaika kutakuwa na mawasiliano ya kila wakati kati ya mbingu na dunia. Na Shetani, akiwa amezungukwa na malaika waovu, na akidai

kuwa ni Mungu, atafanya miujiza ya kila aina, ili kudanganya, yumkini, walio wateule. Watu wa Mungu hawatapata usalama wao katika kutenda miujiza, kwa maana Shetani ataigiza miujiza ile watayoitenda, kwa kazi zake bandia. Watu wa Mungu waliothibitishwa na kuimarishwa watapata nguvu zao katika ishara iliyozungumziwa katika Kutoka 31: 12-18. Wanapaswa kuweka msimamo wao juu ya neno lililo hai: "Imeandikwa." Huu pekee ndio msingi ambao kwake wanaweza kuwa salama. Wale waliovunja Agano lao na Mungu katika siku hiyo watakuwa bila Mungu na bila matumaini. {9T 16.1}.

Wale wamwabuduo Mungu watatofautishwa hasa kwa utii wa amri ya nne, kwa kuwa ni ishara ya nguvu ya uumbaji wa Mungu na ni ushuhuda wa madai Yake ya heshima/kicho na ibada kwa mwanadamu. Waovu watatofautishwa na juhudi zao za kubomoa kumbukizi ya Muumbaji na kuinua taasisi ya Rumi. Katika suala la pambano, Jumuiya yote ya Wakristo, itagawanywa katika makundi mawili makubwa, wale wanaozishika amri za Mungu na imani ya Yesu, na wale wanaomwabudu mnyama na sanamu yake, na kupokea alama yake. Ingawa kanisa na serikali vitaunganisha nguvu zao kulazimisha watu wote, "wadogo kwa wakubwa, matajiri na maskini, huru na watumwa," kupokea alama ya mnyama, bado watu wa Mungu hawataipokea. Ufunuo 13:16. Nabii wa Patmo aangalia "wale wenye kushinda,watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na alama yake, na kwa hesabu ya jina lake, walikuwa wamesimama kando kando ya hiyo bahari ya kioo, wakiwa na vinubi vya Mungu, nao wauimba wimbo wa Musa na Mwana-Kondoo. Ufunuo 15: 2. {9T 16.2}

Majaribu ya kutisha yanawangoja watu wa Mungu. Roho ya vita inachochea mataifa kutoka upande mmoja wa dunia hadi mwingine. Lakini katikati ya wakati wa taabu unaokuja, - wakati wa taabu ambayo haukuwahi kuwepo tangu kuwepo kwa taifa, - wateule wa Mungu watasimama bila kutikiswa au kusogea. Shetani na mawakala wake hawawezi kuwaangamiza, kwani malaika wenye nguvu zaidi watawalinda.- {9T 17.1}

Neno la Mungu kwa watu Wake ni: "Tokeni kati yao, mkatengwe nao, ...Msiguse kitu kilicho kichafu; Nami nitawakaribisha, nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa Kwangu Wanangu, wa kiume na wa kike” “Ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa kipekee; mpate kuzitangaza sifa Zake aliyewaita mtoke gizani na kuingia katika nuru Yake ya ajabu. "2Wakorintho 6:17, 18; 1 Petro 2:9. Watu wa Mungu wanapaswa kutambuliwa kama watu wanaomtumikia kikamilifu. kwa moyo wote, bila kujitwalia heshima, na kukumbuka kuwa kwa agano kuu la thamani wamejifunga kumtumikia Bwana peke Yake. {9T 17.2}

"Bwana akasema na Musa, na kumwambia, Kisha Nena wewe na wana wa Israeli, na kuwaambia, Hakika mtazishika Sabato Zangu; kwa kuwa ni ishara kati Yangu na ninyi katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua ya kuwa Mimi Ndimi Bwana niwatakasaye ninyi. Basi mtaishika hiyo Sabato; kwa kuwa ni takatifu kwenu. Kila

mtu anayeitia unajisi hakika yake atauawa; kwa kuwa kila mtu afanyaye kazi katika siku hiyo, huyo mtu atakatiliwa mbali na watu wake. Kazi itafanywa siku sita; lakini ya saba ni Sabato ya kustarehe kabisa, takatifu kwa Bwana; kila mtu atakayefanya kazi yo yote katika siku ya Sabato, hakika yake atauawa. Kwaajili ya hayo wana wa Israeli wataishika Sabato, kuiangalia sana hiyo Sabato katika vizazi vyao vyote, ni agano la milele. Ni ishara kati Yangu Mimi na wana wa Israeli milele; kwani kwa siku sita Bwana alifanya mbingu na nchi, akastarehe kwa siku ya saba na kupumzika." Kutoka 31: 12-17. {9T 17.3}

Je! Maneno haya hayatuoneshi kama sisi ni watu wa kanisa la Mungu? na je, hayatutangazii kuwa kadri muda upitavyo, tunapaswa kuonesha utakatifu, na tofauti/upekee wa kanisa iliyowekwa juu yetu? Wana wa Israeli walipaswa kushika Sabato katika vizazi vyao vyote "kuwa agano la milele." Sabato haijapoteza maana yake yoyote. Bado ni ishara kati ya Mungu na watu Wake, na itakuwa hivyo milele. {9T 18.1}

## SURA YA 2
## KUITWA KUWA MASHAHIDI

Kwa namna ya pekee Waadventista wa Sabato wamesetiwa/wamewekwa ulimwenguni kama walinzi na wabeba nuru. Kwao limekabidhiwa onyo la mwisho kwa ulimwengu unaopotea. Kwao inang'aa nuru nzuri ya ajabu kutoka katika Neno la Mungu. Wamepewa kazi ya adhima kubwa sana na ya thamani zaidi - kutangaza ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Hakuna kazi nyingine yenye umuhimu mkubwa kama hiyo. Hawapaswi kuruhuhusu jambo lingine lolote kuingilia kati na kuteka akili zao na kuwatenga kutoka kwenye jukumu hili. {9T 19.1}

Ukweli wa wenye kicho/adhima kabisa kuwahi kukabidhiwa wanadamu umekabidhiwa kwetu kuutangaza kwa ulimwengu. Kazi ya kutangaza Kweli hizi ni jukumu letu. Ulimwengu unapaswa kuonywa, na watu wa Mungu wanapaswa kuwa wa kweli na waaminifu kwa imani iliyowekwa kwao. Hawapaswi kujihusisha na uvumi, wala hawapaswi kuingia katika mapatano ya biashara na wasioamini; kwani hili litawazuia katika kazi yao waliyokabidhiwa na Mungu. {9T19.2}

Kristo anasema juu ya watu Wake: "Ninyi ni nuru ya ulimwengu." Mathayo 5:14. Sio jambo dogo kwamba mashauri na mipango ya Mungu imefunuliwa waziwazi kwetu. Ni upendeleo wa pekee kuweza kuyaelewa mapenzi ya Mungu kama

yanavyofunuliwa katika Neno la hakika la unabii. Hili linatupa wajibu mzito. Mungu anatarajia sisi kuwapa wengine Maarifa na ujuzi ambao ametupatia. Ni kusudi Lake kwamba mawakala wa mbingu na wa kibinadamu kuungana katika kutangaza ujumbe wa onyo. {9T19.3}

Kadiri fursa zinavyoendelea kuwepo, kila mtu ambaye amepokea nuru ya Ukweli yuko chini ya wajibu huo huo kama ilivyokuwa kwa nabii wa Israeli ambaye Neno lilimjia: "Mwanadamu, nimekuweka kuwa mlinzi kwa nyumba ya Israeli; basi ulisikie Neno hili kinywani Mwangu, na uwape maonyo Yangu. Ninamwambiapo mtu mtu mwovu, Ee mtu mbaya, hakika utakufa; nawe husemi Neno la kumwonya mtu huyo aiache njia yake, mtu mbaya huyo atakufa katika uovu wake; lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Walakini, ukimwonya mwovu juu ya njia yake kusudi aiache; wala yeye asipoiacha njia yake, atakufa kwa uovu wake; lakini wewe umejiokoa nafsi yako." Ezekieli 33:7-9. {9T 19.4}

Je! Tunangoja hadi utimilifu wa unabii wa mwisho kabla ya kusema chochote kuuhusu? Maneno yetu yatakuwa ya thamani gani wakati huo tena basi? Je! Tutangoja mpaka hukumu za Mungu zimwangukie mkosaji kabla hatujamwambia jinsi ya kuziepuka? Je, Imani yetu iko wapi katika Neno la Mungu? Lazima tuone mambo yaliyotabiriwa yakitokea kabla hatujaamini yale aliyosema? Kwa uwazi miale ya nuru imekuja kwetu, ikituonyesha kwamba siku kuu ya Bwana iko karibu, "iko mlangoni kabisa." Hebu na tusome na tuelewe kabla hatujachelewa. {9T 20.1}

Tunapaswa kuwa mifereji iliyowekwa wakfu, ambamo maisha ya mbinguni hutiririka kwenda kwa wengine. Roho Mtakatifu anapaswa kuhuisha na kujaza kanisa lote, akitakasa na kuimarisha mioyo. Wale ambao wamezikwa pamoja na Kristo katika ubatizo wanapaswa kuinuka katika maisha mapya, wakitoa ushuhuda hai wa maisha ya Kristo. Juu yetu kumewekwa wajibu mtakatifu. Tumepewa agizo la utume: "Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu: na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi: na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari."Mathayo 28:19, 20. Umejitoa kwa kazi ya kuitangaza injili ya wokovu. Ukamilifu wa Mbingu unapaswa kuwa nguvu yako. {9T 20.2}

## Maisha Matakatifu

Sio tu kwa kuuhubiri Ukweli, sio tu kwa kuyasambaza machapisho, kwamba tunamshuhudia Mungu. Tukumbuke kuwa maisha kama ya Kristo ndiyo hoja yenye nguvu zaidi ambayo inaweza kuendelezwa ili kuuthamini Ukristo, na kwamba tabia isiyokamili ya Kikristo ina madhara mabaya ulimwenguni kuliko

tabia ya udunia/kiulimwengu. Sio vitabu vyote vilivyoandikwa vinaweza kutumika katika kusudi la maisha matakatifu. Watu wataamini, sio kile mchungaji anachohuhubiri, bali kile kanisa kinachoishi. Mara nyingi sana ushawishi wa mahubiri yanayohubiriwa kutoka kwenye mimbari hupingwa/huhafifishwa na mahubiri yanayohubiriwa katika mtindo wa maisha ya wale wanaodai kuwa watetezi wa Kweli. {9T 21.1}

Ni kusudi la Mungu kujitukuza kupitia watu Wake kwa ulimwengu. Anatarajia wale wanaolibeba Jina la Kristo kumwakilisha Yeye kwa mawazo, neno, na tendo. Mawazo yao yanapaswa kuwa safi na maneno mazuri yenye kuinua, na kuwavuta wale wanaowazunguka karibu sana na Mwokozi. Dini ya Kristo inapaswa kuunganishwa na kufumwa katika yote wanayoyatenda na kusema. Kila shughuli yao ya kibiashara inapaswa kuwa na harufu nzuri ya uwepo wa Mungu. {9T 21.2}

Dhambi ni kitu cha kuchukiza. Iliharibu uzuri wa maadili ya idadi kubwa ya malaika. Iliingia katika ulimwengu wetu na kuharibu kabisa sura ya maadili ya Mungu ndani ya mwanadamu kwa kiasi kikubwa na cha kutisha. Lakini kwa upendo Wake mkuu, Mungu alitoa njia ambayo kwayo mwanadamu anaweza kupata tena nafasi ambayo alianguka kwa kujitoa kwa mjaribu. Kristo alikuja kusimama kama kichwa cha ubinadamu, kutenda matendo ya ukamilifu kwa niaba yetu. Wale wanaompokea Yeye huzaliwa mara ya pili. {9T 21.3}

Kristo aliuona ubinadamu, kupitia kwa kazi ya ukuaji mkubwa wa dhambi, uliokuwa chini ya mkuu wa nguvu ya anga na kutoa nguvu kubwa katika kukabiliana na uovu. Pia aliona kuwa nguvu kuu ilikuwa ni ya kumshinda Shetani. "Sasa ni hukumu ya ulimwengu huu," Alisema, "sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje. "Yohana 12: 31. Aliona kwamba ikiwa wanadamu watamwamini, watapewa nguvu dhidi ya malaika walioanguka, ambao jina lao ni jeshi/legioni. Kristo aliimarisha roho Yake na fikra kwamba, kwa dhabihu ya ajabu ambayo alikuwa karibu kutoa, mkuu wa ulimwengu huu angetupwa nje na wanaume na wanawake kuwekwa mahali ambapo, kupitia neema ya Mungu, wangeweza kupata tena kile walichokuwa wamekipoteza. {9T 21.4}

Maisha ambayo Kristo aliyaishi katika ulimwengu huu, wanaume na wanawake wanaweza kuyaishi kupitia nguvu Zake na chini ya maelekezo Yake. Katika pambano Lake na Shetani wanadamu wanaweza kupata msaada wote aliokuwa nao. Wanaweza kuwa zaidi ya washindi kupitia Yeye aliyewapenda na kujitoa Mwenyewe kwa ajili yao. {9T 22.1}

Maisha ya watu wanaojiita Wakristo ambao hawaishi maisha ya Kristo ni dhihaka kwa dini. Kila ambaye jina lake limeandikwa kwenye orodha ya kanisa yuko chini yuko chini ya wajibu wa kumwakilisha Kristo kwa kufunua mapambo ya ndani ya roho ya upole na utulivu. Wanapaswa kuwa mashahidi Wake, wakionesha faida ya kutembea na kutenda kazi kama Kristo alivyowapa kielelezo. Ukweli katika wakati

huu unapaswa kuonekana katika nguvu Yake kupitia maisha ya wale wanaouamini, na unapaswa kutolewa kwa ulimwengu. Waumini wanapaswa kuonesha katika maisha yao nguvu Yake ya kukuza na kutakasa. {9T 22.2}.

## Wawakilishi wa Kristo.

Wakazi wa mbinguni wanatarajia wafuasi wa Kristo kuangaza kama nuru ulimwenguni. Wanapaswa kuonyesha nguvu ya neema ambayo Kristo alikufa kuwapa wanadamu. Mungu anatarajia wale wanaokiri kuwa Wakristo kufunua katika maisha yao maendeleo na ukuaji  mkubwa wa Ukristo. Wanatambuliwa kuwa wawakilishi wa Kristo, na wanapaswa kuonyesha kwamba Ukristo ni uhalisia. Wanapaswa kuwa watu wa imani, watu hodari, watu jasiri, watu wa kiroho, ambao, bila kutilia shaka, wanamtumaini Mungu na ahadi Zake. {9T 22.3}

Wote ambao wataingia katika jiji la Mungu lazima wakati wa maisha yao duniani wamwonyeshe Kristo katika mwenendo na shuguli zao. Hii ndio huwafanya kuwa wajumbe wa Kristo, mashahidi Wake. Wanapaswa kubeba Ukweli wazi, ushuhuda uliokusudiwa dhidi ya vitendo vyote viovu, ukiwaelekeza wenye dhambi kwa Mwana-Kondoo wa Mungu, ambaye huiondoa dhambi ya ulimwengu. Huwapa wote wanaompokea, nguvu ya kufanyika kuwa wana wa Mungu. Kuzaliwa upya ni njia pekee ambayo kwayo tunaweza kuingia katika jiji la Mungu. Njia ni nyembamba na nyofu, na mlango tunaoupitia umesonga; lakini kando yake tunapaswa kuwaongoza wanaume na wanawake na watoto, tukiwafundisha kwamba, ili kuokolewa, lazima wawe na moyo mpya na roho mpya. Tabia za kale, na za kurithi lazima zishindwe na zipingwe kabisa. Nia ya asili ya nafsi lazima ibadilishwe. Udanganyifu wote, uwongo wote, kusema mabaya kote, lazima kutupiliwe mbali. Wanapaswa kuishi maisha mapya, ambayo yanawafanya wanaume na wanawake, kuwa kama Kristo. {9T 23.1}

## Kuufata Ukweli kwa uthabiti

Hakupaswi kuwa na maisha ya kuigiza au kujifanya (feki au bandia) kwa wale wenye ujumbe wa thamani na mtakatifu walioitiwa kuubeba. Ulimwengu unawaangalia Waadventista Wasabato kwa sababu unajua kitu kuhusu ushuhuda wao wa imani na ubora wao wa hali ya juu, na unapowaona wale ambao hawaishi kulingana na ushuhuda/Kukiri kwao, huwatazama kwa kuwadharau. {9T 23.2}

Wale wanaompenda Yesu wataleta yote yaliyo katika maisha yao kupatana na mapenzi Yake. Wamechagua kuwa upande wa Bwana, na maisha yao yanapaswa kuwatofautishwa kabisa na maisha ya walimwengu. Mjaribu atawajia kwa pongezi  kwa kuwabembeleza, na kujikomba kwao kwa kuwasifia na hata kutoa rushwa, akisema: Nitakupa haya yote ukiniabudu mimi. "Lakini wanajua kwamba adui hana anachostahili kupokea (ibada yao nk), na wanakataa kujitoa kwa majaribu yake. Kupitia neema ya Mungu wanawezeshwa kushikilia usafi wa kanuni bila kuchafuliwa. Malaika watakatifu wapo kando yao, na Kristo

anadhihirishwa kwa uthabiti wa utii wao, katika kushikama na ile Kweli. Wao ni askari wenye utayari na kasi kwa Kristo, wakiubeba, kama mashahidi wa Kweli, ushuhuda imara unaoithamini Kweli. Wakionesha kwamba kuna nguvu ya kiroho inayoweza kuwawezesha wanaume na wanawake kutopindisha hata nukta kutoka katika haki na Kweli kwa zawadi zote ambazo wanadamu wanaweza kutoa. Watu kama hao, popote wawezapo kuwa, wataheshimishwa na mbingu kwa sababu wamepatanisha maisha yao na mapenzi ya Mungu, bila kujali ni dhabihu gani wameitwa kuitoa. {9T 23.3}

## Ujumbe kwa Ulimwengu wote

Nuru ambayo Mungu amewapa Watu wake si ya kufungiwa ndani ya makanisa ambayo tayari yanaujua Ukweli. Nuru hii inapaswa kutawanywa nje katika maeneo yenye giza duniani. Wale wanaotembea katika nuru kama Kristo alivyo katika nuru watashirikiana na Mwokozi kwa kuwafunulia wengine yale ambayo Kristo amewafunulia. Ni kusudi la Mungu kwamba Ukweli wa wakati huu utajulishwa kwa kila taifa, na lugha, na jamaa za watu. Katika ulimwengu wa leo wanaume na wanawake wamevutwa katika kutafuta faida za kidunia na anasa na furaha za kidunia. Kuna maelfu-elfu ambao hawatoi muda au hata kufikiria juu ya wokovu wa roho. Wakati umefika ambapo ujumbe wa kuja kwa Kristo hivi karibuni usikike ulimwenguni kote. {9T 24.1}

Ushahidi usio na mashaka unaonyesha mwisho umekaribia. Onyo linapaswa kutolewa kwa sauti fulani. Lazima njia iandaliwe na kuwa tayari kwa kuja kwa Mfalme wa Amani katika mawingu ya mbinguni. Kuna mengi ya kufanywa katika miji ambayo bado haijausikia Ukweli wa wakati huu. Hatupaswi kuanzisha taasisi kwaajili ya kushindania ukubwa na utukufu na taasisi za kiulimwengu; lakini kwa Jina la Bwana, na uvumilivu usiochoka na bidii isiyokoma ambayo Kristo alileta ndani ya watumishi Wake, tunapaswa kuipeleka mbele kazi ya Bwana. {9T 25.1}

Kama watu tunahitaji sana kunyenyekeza mioyo yetu mbele za Mungu, tukiomba msamaha Wake kwa ajili yetu kwa kupuuza kulitimiza agizo la injili. Tumeweka vituo vikubwa katika maeneo machache, na kuacha bila kufanya kazi katika miji mingi muhimu. Hebu sasa na tuichukue kazi tuliyoitiwa na kuutangaza ujumbe ambao utawaamsha wanaume na wanawake kuhisi hatari yao. Ikiwa kila Mwaadventista Msabato angefanya kazi liyowekwa juu yake, idadi ya waumini ingekuwa kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa. Katika miji yote ya [Marekani] kutakuwa na wale ambao wangekuwa wameongozwa kutii ujumbe wa kuitii Sheria ya Mungu. {9T 25.2}

Katika maeneo mengine ujumbe kuhusu utunzaji wa Sabato umepelekwa kwa uwazi na kwa nguvu, wakati maeneo mengine yameachwa bila onyo. Je! haiwapasi wale wanaoujua Ukweli kuamka kwa wajibu ulioweka juu yao? Ndugu zangu, hamwezi kujizika/kujifukia wenyewe katika mambo au maslahi ya kidunia.

Hamwewezi kumudu kupuuza agizo la utume mliopewa na Mwokozi. {9T 25.3}

Kila kitu katika Sayari zote kinawataka wale wanaoijua Kweli kujitakasa wao wenyewe bila kusita kwa ajili kuutangaza Ukweli kama ilivyojulishwa kwao katika ujumbe wa Malaika wa tatu. Kile tunachokiona na kukisikia hutuita kwenye wajibu wetu. Utendaji kazi wa mawakala wa Shetani hutoa mwito kwa kila Mkristo kusimama katika nafasi yake. {9T 25.4}

### Aina ya Watenda-kazi Wanaohitajika

Kazi tuliyopewa ni kubwa na muhimu, na ndani yake wanahitajika watu wenye hekima, wasio na ubinafsi, watu ambao huelewa ni nini humaanisha kujitoa kwa juhudi isiyo na ubinafsi ya kuokoa roho. Lakini hakuna haja ya huduma ya watu ambao ni vuguvugu, maana watu kama hao Kristo hawezi kuwatumia. Wanahitajika wanaume na wanawake ambao mioyo yao imeguswa na mateso/huzuni ya wanadamu na ambao maisha yao yanatoa ushahidi kuwa wanapokea na kuangaza nuru, uzima na neema. {9T 26.1}

Watu wa Mungu wanapaswa kumkaribia Kristo kwa kujikana na kujitoa dhabihu, lengo lao moja likiwa ni kutoa ujumbe wa rehema kwa ulimwengu wote. Wengine watafanya kazi kwa njia moja na wengine kwa njia nyingine, kama Bwana atakavyowaita na kuwaongoza. Lakini wote wanapaswa kujitahidi pamoja, wakitafuta kuifanya kazi hiyo yote kuwa kamili. Kwa kalamu na sauti wanapaswa kumfanyia kazi. Neno lililochapishwa la Ukweli linapaswa kutafsiriwa katika lugha tofauti-tofauti na kulipeleka hadi miisho ya dunia. {9T 26.2}

Moyo wangu mara nyingi umelemewa kwa sababu watu wengi ambao wangeweza kuwa wanafanya kazi hawafanyi chochote. Wao ni mchezo wa majaribu ya Shetani. Kila mshiriki wa kanisa ambaye ana ujuzi wa Ukweli anatarajiwa kufanya kazi wakati kungali mchana; kwa maana usiku waja, asipoweza mtu kuifanya kazi. Sio muda mrefu, sisi tutaelewa nini usiku huo unamaanisha. Roho wa Mungu anahuzunishwa na kufukuzwa duniani. Mataifa yanakasiriana. Maandalizi yanaenea tayari kwa vita. Usiku umekaribia. Kanisa sasa na liamke na kwenda kufanya kazi yake iliyoamriwa. Kila muumini, aliye na elimu ama asiye na elimu, anaweza kuubeba ujumbe. {9T 26.3}

Umilele unasimama mbele yetu. Pazia linakaribia kuinuliwa. Je, tunafikiria nini, kwamba tutang'ang'ania upendo wetu wa ubinafsi wa urahisi, wakati roho zinazotuzunguka pande zote zinaangamia? Je, mioyo yetu imekuwa migumu kabisa? Je, hatuwezi kuona na kuelewa kwamba tuna kazi ya kufanya kwa ajili ya wengine? Ndugu zangu, nyinyi ni miongoni mwa wale ambao, wana macho, lakini hawaoni, na wana masikio, lakini hawasikii? Je, ni bure kwamba Mungu amekupa ujuzi wa mapenzi Yake? Je, ni kwamba haina maana yoyote Yeye kukutumia onyo baada ya onyo juu ya kukaribia kwa wakati wa mwisho? Je! unaamini matamko ya

Neno Lake juu ya mambo yanayoujia  ulimwengu? Je, unaamini kwamba hukumu za Mungu zinaning'inia juu ya wakazi wa dunia? Sasa kwa vipi basi, wewe unaweza kukaa na kutulia, kutojali na kuwa mzembe? {9T 26.4}

Kila siku ipitayo hutuleta karibu kabisa na mwisho. Je, inatuleta pia karibu na Mungu? Je, tunakesha katika maombi? Wale tunaohusiana nao siku baada ya siku wanahitaji mwongozo wetu na msaada wetu.Wanaweza kuwa katika hali ya akili ambayo Neno kwa wakati litatumwa nyumbani na Roho Mtakatifu kama msumari mahali pa uhakika. Kesho baadhi ya roho hizi zinaweza kuwa mahali ambako hatuwezi kuzifikia tena. Mvuto wetu ni upi kwa hawa wasafiri wenzetu? Tunafanya juhudi gani ili kuwaleta kwa Kristo? {9T 27.1}

Muda ni mfupi, na nguvu zetu lazima zipangwe kufanya kazi kubwa zaidi. Watendakazi wanahitajika ambao wanafahamu ukubwa wa kazi hiyo na wawe tayari kuifanya, si kwa ajili ya mishahara wanayopokea, bali kutokana na kutambua mwisho ulivyo karibu. Muda unadai ufanisi mkubwa na kujiweka wakfu wa kina. Aah!, mada hii imesheheni kichwani mwangu, hata ninamlilia Mungu: "Bwana Uondoke, na Uinue watu, na uwatume haraka wajumbe waliojazwa kwa ufahamu wa wajibu wao, wajumbe ambao mioyoni mwao ibada ya sanamu ya nafsi, ambayo ndio msingi wa dhambi zote, imesulubishwa. {9T 27.2}

## Tukio la Kushangaza. Onyesho la Kushangaza

Katika maono ya usiku, tukio la kuvutia sana lilipita mbele yangu. Niliona mpira mkubwa wa moto ukianguka miongoni mwa baadhi ya majumba mazuri, na kusababisha uharibifu wa ghafla. Nilimsikia mtu akisema: "Tulijua kuwa hukumu za Mungu zilikuwa zikija juu ya dunia, lakini hatukujua kwamba zingekuja mapema kiasi hiki." Wengine, kwa sauti za uchungu, walisema: "Hivi kumbe mlijua! Kwa nini basi hamkutuambia? Sisi hatukujua."Kila upande nilisikia maneno kama hayo ya kulalamika yakisemwa. {9T 28.1}

Kwa huzuni kubwa nikaamka. Nikalala tena, na nilionekana kuwa kwenye kusanyiko kubwa. Mmoja Mwenye mamlaka ilikuwa Akihutubia kusanyiko, ambaye mbele Yake ilitandazwa ramani ya dunia. Alisema kwamba ramani ilifananishwa na shamba la mizabibu la Mungu, ambalo ni lazima lilimwe. Kama vile nuru kutoka mbinguni imulikavyo kila mtu, hiyo ilipaswa kuakisi nuru kwa wengine. Taa zilipaswa kuwashwa mahali pengi, na kutoka kwenye hizi taa bado taa zingine zilipaswa kuwashwa. {9T 28.2}

Maneno hayo yalirudiwa: "Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu. Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze

mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni. "Mathayo 5:13-16. {9T 28.3}

Nikaona Mihilimili mikubwa ya nuru ikiangaza kutoka mijini na vijijini, na kutoka mahali pa juu na mahali pa chini pa dunia. Neno la Mungu likatiiwa, na matokeo yake yalikuwa ni kumbukizi Kwake Yeye katika kila mji na kijiji. Ukweli Wake ulitangazwa ulimwenguni kote. {9T 28.4}

Kisha ramani hii iliondolewa na nyingine kuwekwa mahali pake. Juu yake nuru ilikuwa ikimulika kutoka sehemu chache pekee. Sehemu nyingine za dunia zilikuwa gizani, kukiwa na mng'ao wa nuru ya hapa na pale. Kiongozi wetu akasema: "Giza hili ni matokeo ya watu kufuata njia yao wenyewe. Wamependelea mielekeo ya uovu ya kurithi na kukuzwa/kupaliliwa. Wamehoji na wamemkosoa na kumtuhumu mkuu wa maisha yao. Mioyo yao haiko sawa mbele za Mungu. Wameificha nuru yao chini ya pishi." {9T 29.1}

Ikiwa kila askari wa Kristo angefanya kazi yake, kama kila mlinzi wa kuta za Sayuni angepiga tarumbeta ya mlio fulani, ulimwengu ungeweza kuwa kabla ya hii umeusikia ujumbe wa onyo. Lakini kazi ipo nyuma ya miaka. Wakati watu wamelala, Shetani amepiga hatua juu yetu. {9T 29.2}

Tukiweka tumaini letu kwa Mungu, tunapaswa kusonga mbele kwa uthabiti, tukifanya kazi Yake bila ubinafsi, kwa kumtegemea kwa unyenyekevu, tukijikabidhi sisi wenyewe na kwa wakati wa sasa na ujao kwa mipango na majaliwa Yake ya hekima, tukiushikilia mwanzo wa ujasiri wetu hadi mwisho, tukikumbuka kwamba sio kwa sababu ya kustahili kwetu, ndiyo tunapokea baraka za mbinguni, lakini kwa sababu ya kustahili Kwake Kristo, na kukubali kwetu, kwa njia ya imani Kwake, kwa neema ya Mungu iliyo tele. {9T 29.3}

## SURA YA 3
## KAZI YA UMISHONARI NYUMBANI

Mungu anatarajia huduma binafsi kutoka kwa kila mtu aliyempa ujuzi wa Kweli kwa wakati huu. Si wote wanaoweza kwenda kama wamishonari katika nchi za kigeni, bali wote wanaweza kuwa wamishenari wa nyumbani katika familia zao na kwa majirani zao. Kuna njia nyingi ambazo washiriki wa kanisa wanaweza kutoa ujumbe kwa wale wanaowazunguka. Mojawapo ya njia inayofanikiwa zaidi ni kwa kuishi maisha ya kusaidia, yasiyo na ubinafsi, maisha ya Kikristo. Wale ambao wanapigana vita vya maisha katika hali zisizo za kawaida, wanaweza kuburudishwa na kuimarishwa kwa umakini mdogo ambao hauna gharama yoyote. Maneno ya ukarimu yanayosemwa kwa njia ya kawaida, usikivu mdogo tu unaooneshwa, vitafagilia mbali mawingu ya majaribu na mashaka yanayoijaza

nafsi. Udhihirisho wa Kweli wa moyo wa huruma kama ya Kristo, ukitolewa kwa usahili, una uwezo wa kufungua mlango wa mioyo inayohitaji mguso nyeti, sahili na wa upole wa roho ya Kristo. {9T 30.1}

Kristo hukubali, Ah!!,kwa furaha sana! kila wakala wa kibinadamu ambaye hujisalimisha Kwake. Humleta mwanadamu katika muunganiko na Uungu, ili aweze kuwasilisha kwa ulimwengu siri ya upendo wa Mungu kufanyika mwili. Uzungumzeni, uombeeni, uimbeni, ujazeni ulimwengu kwa ujumbe wa Kweli Yake, na endeleeni kusonga mbele hadi katika miisho ya nchi. {9T 30.2}

Akili za mbinguni zinangoja kushirikiana na vyombo vya kibinadamu, ili ziweze kufunua kwa ulimwengu kile ambacho wanadamu wanaweza kuwa na kile, kupitia ushawishi wao, wanaweza kufanikisha kwa ajili ya kuokoa roho zilizo tayari kuangamia. Mtu aliyeongoka kweli kweli atasheheni upendo wa Mungu naye atakuwa na shauku kuwapa wengine furaha ambayo yeye mwenyewe anayo. Bwana anatamani kanisa Lake kuuonyesha ulimwengu uzuri wa utakatifu, ili liweze kuonesha nguvu ya dini ya Kikristo. Mbingu inapaswa kuakisiwa katika tabia ya Mkristo. Wimbo wa shukrani na sifa unapaswa kusikiwa na wale walio gizani. Kwa habari njema ya Injili, kwa ahadi na uhakikisho wake, tunapaswa kuonyesha shukrani zetu kwa kutafuta kuwatendea wengine mema. Ufanyaji wa kazi hii italeta miale ya haki ya mbinguni kwa roho zilizochoka, zilizofadhaika, na roho zinazoteseka. Ni kama chemchemi iliyofunguliwa kwa msafiri aliyechoka, mwenye kiu. Katika kila kazi ya rehema, kila kazi ya upendo, malaika wa Mungu huwepo. {9T 30.3}

## Kielelezo Chetu

Kazi ya Kristo ni kuwa kielelezo chetu. Mara zote aliienda huku na kule akitenda mema. Katika hekalu na masinagogi, katika mitaa ya miji, sokoni, na maeneo ya kazi, kando ya bahari na katikati mwa miji na vilima, aliihubiri injili na kuponya wagonjwa. Maisha Yake yalikuwa ya utumishi usio na ubinafsi, na inapaswa kuwa kitabu chetu cha kujifunza. Huruma Yake, upendo wake mwororo, wenye sikitiko hukemea ubinafsi wetu na ugumu wetu wa mioyo. {9T 31.1}

Kokote Kristo alikoenda, alizitawanya baraka katika njia Yake. Ni wangapi wanaodai kumwamini Yeye ambao wamejifunza masomo Yake ya fadhili, ya huruma nyororo, ya upendo usio na ubinafsi? Sikia sauti Yake ikisema na walio dhaifu, waliochoka, na wasiojiweza:" Njooni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapa pumziko." Mathayo 11:28. Hakukuwa na kuchoka katika uvumilivu Wake, wala kukandamizwa kwa upendo Wake. {9T 31.2}

Kristo anatuita tufanye kazi kwa uvumilivu na subira kwa ajili ya maelfu wanaoangamia katika dhambi zao; wale waliotawanyika katika nchi zote, kama

mabaki ya ajali kwenye ufuo wa jangwa. Wale wanaoshiriki katika utukufu wa Kristo lazima washiriki pia huduma Yake, ya kuwasaidia walio dhaifu, wanyonge, na waliokata tamaa. {9T 31.3}

Inawapasa wale wanaoichukua kazi hii wayafanye maisha ya Kristo kuwa funzo lao la kudumu. Na waingie kwa nguvu na kwa bidii, wakitumia kila uwezo wao katika utumishi wa Bwana. Matokeo ya thamani yatafuata juhudi za dhati, zisizo za ubinafsi. Kutoka kwa Mwalimu Mkuu watendakazi watapata elimu ya juu zaidi kuliko zote. Lakini wale ambao hawaitoi nuru waliyonayo siku moja watatambua kwamba wamedumisha hasara ya kutisha. {9T 32.1}

Wanadamu hawana haki ya kufikiria kuwa kuna kikomo katika juhudi wanazopaswa kufanya katika kazi ya kuokoa roho. Je! Kristo aliwahi kuchoka katika kazi Yake? Je, aliwahi kurudi nyuma kutoka kuwa dhabihu na katika magumu? Washiriki wa kanisa wanapaswa kuweka mbele juhudi endelevu, za kudumu ambazo Yeye aliziweka. Washiriki wanapaswa kuwa tayari sikuzote kuchangamka katika kuanza kazi na kutenda wanapoisika amri ya Bwana, na kutii. Popote tunapoona kazi inayongoja kufanywa tunapaswa kuichukua na kuifanya, tukimtazama Yesu daima. Kama washiriki wa kanisa letu wangetii agizo hili, mamia ya roho zingevutwa kwenda kwa Yesu. Kama kila mshiriki wa kanisa angekuwa mmishonari aliye hai, injili ingetangazwa kwa kasi katika nchi zote, kwa watu wote, mataifa, na jamaa. {9T 32.2}

## Matokeo ya Jitihada za Moyo Wote

Acha uwezo wa kutakasa uje katika kazi ya kutangaza Kweli kwa wakati huu. Ikiwa nguvu za adui zitapata ushindi sasa, itakuwa ni kwa sababu makanisa hupuuza kazi yao waliyopewa na Mungu. Kwa miaka mingi kazi imewekwa mbele yetu, lakini wengi wamelala. Kama Waadventista Wasabato, sasa wataamka kufanya kazi waliyopewa, Ukweli utawasilishwa waziwazi kwenye miji yetu iliyopuuzwa kwa usahili, na katika nguvu za Roho. {9T 32.3}

Wakati kazi itakapofanywa kwa moyo wote, ufanisi wa neema ya Kristo utaonekana. Walinzi wa kuta za Sayuni wanapaswa kuwa macho sana, nao wanapaswa kuwaamsha wengine. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa dhati na bidii, kuwa waaminifu sana katika kazi yao kwa ajili Yake ili ubinafsi wote uondolewe katika maisha yao. Na ndipo watenda kazi wa Bwana watakuwa na mapatano, na nia moja, na mkono wa Bwana, nguvu ambayo ilionekana katika maisha ya Kristo, itafunuliwa. Ujasiri utarejeshwa, na kutakuwa na umoja kanisani katika ngazi zetu zote. {9T 32.4}

## Aina tofauti za Huduma

Bwana anawaita watu Wake wafanye kazi mbalimbali. Wale walio katika njia kuu na vichochoro vya maisha wanapaswa kuusikia ujumbe wa injili. Washiriki wa

kanisa wanapaswa kufanya kazi ya uinjilisti katika nyumba za majirani zao ambao bado hawajapokea uthibitisho kamili wa Kweli kwa wakati huu. {9T 33.1}

Mungu anaziita familia za Kikristo kwenda katika jamii zilizo katika giza na makosa, na kufanya kazi kwa hekima na kwa uvumilivu kwa ajili ya Bwana. Ili kuitikia wito huu inahitaji kujitoa nafsi. Wakati wengi wanasubiri kila kikwazo kuondolewa, roho zinakufa bila tumaini na bila Mungu duniani. Wengi, wengi sana, kwa ajili ya kutafuta manufaa ya kidunia, kwa ajili ya kutafuta kupata ujuzi wa kisayansi, watanajitosa katika maeneo yenye magonjwa na kuvumilia shida na ufukara. Wako wapi walio tayari kufanya hivi kwa ajili ya kuwaambia wengine juu ya Mwokozi? Wako wapi wanaume na wanawake ambao watakwenda kwenye maeneo yanayohitaji injili, ili wawaelekeze wanadamu walio gizani kwa Mkombozi? {9T 33.2}

## Kusambaza Machapisho Yetu

Wengi wa Watu wa Mungu wanapaswa kupeleka machapisho yetu kwenye maeneo ambayo ujumbe wa malaika wa tatu haujatangazwa kabisa. Vitabu vyetu vinapaswa kuchapishwa katika lugha nyingi mbalimbali. Wakiwa na vitabu hivi, watu wanyenyekevu, waaminifu wanapaswa kwenda kama wainjilisti wanaotembea, wakiipeleka Kweli kwa wale ambao kamwe wasingeipata nuru vinginevyo. Wale wanaochukua aina hii ya kazi wanapaswa kwenda wakiwa tayari kwa kazi ya umishenari wa tiba. Wale walio wagonjwa na wanaoteseka wanapaswa kusaidiwa. Wengi ambao kazi hii ya rehema imefanyika kwao watasikia na kuyakubali Maneno ya uzima. {9T 33.3}

Kazi ya mwinjilisti wa vitabu, ambaye moyo wake umejazwa na Roho Mtakatifu, imejaa uwezekano wa ajabu kwa wema. Uwasilishaji wa Ukweli, kwa upendo na urahisi, kutoka nyumba hadi nyumba, inapatana na maagizo ambayo Kristo aliwapa wanafunzi Wake alipowatuma kwenda katika safari yao ya kwanza ya umishenari. Kwa nyimbo za sifa, kwa sala za unyenyekevu, za kutoka moyoni, wengi watafikiwa. Mtendakazi wa mbingu atakuwepo ili kuisadikisha mioyo. “Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote,” ni ahadi Yake. Pamoja na uhakikisho wa uwepo Wake wa kudumu wa msaidizi kama huyo tunaweza kufanya kazi kwa imani na matumaini na ujasiri. {9T 34.1}

Kutoka mji hadi mji, kutoka nchi hata nchi, wanapaswa kubeba machapisho yenye ahadi ya ujio wa Mwokozi hivi karibuni. Machapisho haya yanapaswa kutafsiriwa katika kila lugha, maana injili inapaswa kuhubiriwa kwa wote ulimwenguni. Kwa kila mtendakazi Kristo anaahidi ufanisi wa mbingu ambao utafanya kazi yake iwe na mafanikio. {9T 34.2}

Wale ambao wameijua Kweli kwa muda mrefu wanahitaji kumtafuta Bwana kwa bidii zaidi, ili mioyo yao ijazwe na uamuzi wa kufanya kazi kwa ajili ya majirani zao.

Ndugu na dada zangu, watembeleeni wale wanaoishi karibu nanyi, na kwa huruma na wema tafuta kufikia mioyo yao. Hakikisha unafanya kazi kwa namna ambayo itaondoa chuki badala ya kuitengeneza. Na kumbuka kwamba wale wanaojua Ukweli kwa wakati huu na bado wanafungia juhudi zao kwenye makanisa yao wenyewe, wakikataa kufanya kazi kwa ajili ya majirani zao ambao hawajaongoka, wataitwa kutoa hesabu ya majukumu ambayo hawakuyatekeleza. {9T 34.3}

Waazime majirani zako baadhi ya vitabu vyetu vidogo. Ikiwa nia yao imeamshwa, chukua baadhi ya vitabu vikubwa zaidi. Waonyeshe kitabu cha Vielelezo na Mifano ya Kristo (*Lulu za Uzima* au *Christ Object Lessons*). Waambie historia yake, na waulize ikiwa wanataka kujipatia nakala. Ikiwa tayari wanacho, waulize ikiwa wako tayari kusoma vitabu vingine vya aina hiyo. Ikiwezekana, pata nafasi ya kuwafundisha ile Kweli. Kando ya maji tele unapaswa kupanda mbegu za Kweli, japo haujui ni ipi itafanikiwa, hii au ile. {9T 35.1}

## Kazi ya Nyumba kwa Nyumba

Katika majimbo mengi kuna makazi ya watu wenye stadi na bidii, wakulima wenye uwezo mzuri, ambao hawajaupata Ukweli wa leo. Maeneo kama haya yanapaswa kufanyiwa kazi. Hebu Washiriki wetu walei wachukue aina hii ya huduma. Kwa kukopesha au kuuza vitabu, kwa kusambaza vijizuu, na kwa kuifungua Biblia na kusomba pamoja (*Darasa la Biblia au Bible Study*), washiriki wetu wanaweza kufanya kazi kwa kiwango kikubwa sana kwa majirani zao wenyewe. Wakiwa wamejazwa na upendo kwa roho wanaweza kuutangaza ujumbe kwa nguvu kubwa kiasi cha kuwaongoa wengi. {9T 35.2}

Watendakazi wawili wa Biblia walikuwa wameketi katika familia. Wakiwa na Biblia iliyofunguliwa mbele yao, walimwasilisha Bwana, Yesu Kristo kama Mwokozi anayesamehe dhambi. Maombi ya dhati na ari yalitolewa kwa Mungu, na mioyo ikalainishwa na kutiishwa kwa ushawishi wa Roho wa Mungu. Maombi yao yalitamkwa kwa upya na nguvu. Kadri Neno la Mungu lilivyofafanuliwa, niliona kwamba, nuru laini na ang'avu iliyaangazia Maandiko, na nikasema, kwa upole: “Nenda barabarani na na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, ili nyumba Yangu ipate kujaa. "Luka 14:23. {9T 35.3}

Nuru ya thamani iliwasilishwa kutoka kwa jirani hadi kwa jirani. Madhabahu za familia ambazo zilikuwa zimebomolewa zilisimamishwa tena, na wengi wakaongolewa. {9T 36.1}

Ndugu na dada zangu, jitoeni nafsi zenu kwa Bwana kwa ajili ya utumishi. Usiruhusu fursa kupita bila kuitumia. Tembelea wagonjwa na wenye shida, na uonyeshe kupendezwa na fadhili kwao. Ikiwezekana, fanya kitu kuwafanya wajisikie vizuri na kufarijika zaidi. Kwa njia hii unaweza kuifikia mioyo yao na kulisema Neno kwa ajili ya Kristo. {9T 36.2}

Ni Umilele pekee ndio utakaofunua jinsi aina hii ya kazi inavyofanya makubwa na kwenda mbali. Aina nyingine ya manufaa itakuwa wazi mbele ya wale ambao wako tayari kufanya kazi iliyo karibu nao. Sio wasomi, na wazungumzaji wenye ufasaha ndiyo wanaohitajika sasa, bali wanaume na wanawake wanyenyekevu kama Kristo, ambao wamejifunza kutoka kwa Yesu wa Nazareti kuwa wapole na wanyenyekevu, na ambao, hutumainia nguvu Zake, na watakwenda kwenye njia kuu na viungani ili kutoa mwaliko: "Njooni, kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari." Mstari wa 17. {9T 36.3}

Wale walio na hekima katika kazi ya kilimo, katika kuulima udongo, wale ambao wanaweza kujenga majengo mepesi, na majengo ya wazi, wanaweza kusaidia. Wanaweza kufanya kazi nzuri na wakati huo huo kuonyesha katika mienendo yao kiwango cha juu ambacho ni upendeleo kwa watu hawa kufikia. Waache wakulima, wawekezaji wa fedha na watu waliosomea uchumi, wafadhili, wajenzi, na wale wenye ujuzi katika ufundi/tasnia/stadi mwingine mbalimbali, kwenda kwenye mashamba yaliyopuuzwa, kuiboresha ardhi, kuanzisha viwanda, kujitengenezea makazi sahili, na kuwapa majirani zao maarifa ya Kweli kwa wakati huu. {9T 36.4}

### Kazi kwa Wanawake

Kuna uwanda mpana wa huduma kwa wanawake kama ilivyo kwa wanaume pia. Mpishi mzuri mwenye ufanisa, mshonaji, muuguzi --msaada wa wote unahitajika. Hebu washiriki wa kaya za watu maskini,a wafundishwe kupika, kutengeneza na kurekebisha nguo zao wenyewe, jinsi ya kuhudumia wagonjwa, na jinsi ya kutunza vema nyumba. Hata watoto wanapaswa kufundishwa kufanya kazi ndogo ndogo za upendo na rehema kwa wanadamu wasiojiweza, na watu waliopata maafa na kuwa na hali ngumu kuliko wao wenyewe. {9T 36.5}

### Nyumbani kituo cha Utume

Hebu wazazi wasisahau kazi kubwa ya utume iliyo mbele yao nyumbani. Kwa kila mama limekabidhiwa jukumu takatifu kutoka kwa Mungu kwa ajili ya watoto.
“Mchukue mwana huyu, na binti huyu,” Mungu asema, “na umfundishe kwa ajili Yangu. Mpatie tabia iliyotengenezwa kwa mfano wa ikulu (jumba la Kifalme), ili ipate kung’aa katika nyua za Bwana milele.” Nuru na utukufu unaong’aa kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu hukaa juu ya mama mwaminifu anapojaribu kuwaelimisha watoto Wake ili kupinga mivuto ya uovu. {9T 37.1}

### Mahali pa Kila Mtu

Kuna kazi ya bidii kwa kila jozi ya mikono kuifanya. Hebu kila pigo lielezee kuhusu kuinuliwa kwa ubinadamu. Wapo wengi sana wanaohitaji kusaidiwa. Moyo wa yule anayeishi, si kwa kujifurahisha mwenyewe, ila kuwa mbaraka kwa wale walio

na baraka chache sana, utasisimka, na kuchangamka kwa kuridhika moyo. Hebu kila mvivu aamke na uso wake ukabili uhalisia wa maisha. Chukua Neno la Mungu na uzichunguze kurasa zake. Ikiwa ninyi mu watendaji wa Neno, maisha yatakuwa hakika ni Kweli iliyo hai, na mtajua kuwa thawabu/ujira ni mwingi. {9T 37.2}

Bwana anayo nafasi kwa kila mtu katika mpango Wake mkuu. Talanta ambazo hazihitajiki huwa hazitolewi. Ikiwa kwamba mtu ana talanta ni ndogo. Mungu ana nafasi ya hiyo talanta, na kwamba talanta hiyo moja, iwapo itatumiwa kwa uaminifu, itafanya kazi ile ile Mungu aliyokusudia ifanye. Talanta za mtu masikini mwenye nyumba ndogo na mnyenyekevu zinahitajika katika kazi ya nyumba kwa nyumba na zinaweza kutimiza zaidi katika kazi hii kuliko vipaji mahiri na vya kushangaza. {9T 37.3}

Milango elfu ya manufaa iko wazi mbele yetu. Tunalalamikia rasilimali chache zinazopatikana kwa sasa, huku mahitaji mbalimbali ya dharura yanatusukuma kuwa na mali, mbinu na watu. Tukiwa na bidii, hata sasa tunaweza kuzidisha rasilimali mara mia. Ubinafsi na kujiinua nafsi vimeziba njia. {9T 38.1}

Washiriki wa kanisa, hebu na muiangaze nuru yenu. Hebu sauti zenu zisikike katika maombi ya unyenyekevu, katika ushuhuda dhidi ya kutokuwa na kiasi, upumbavu, na anasa za dunia hii, na katika kuitangaza Kweli ya leo. Sauti yako, mvuto wako, wakati wako vyote hivi ni karama kutoka kwa Mungu na zinapaswa kutumika kuleta roho kwa Kristo. {9T 38.2}

Watembelee majirani zako na uoneshe una shauku na wokovu wa roho zao. Amsha kila nguvu ya kiroho iwe katika utendaji. Waambie wale unaowatembelea kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia. Bwana Yesu Kristo atafungua milango ya mioyo yao na atafanya ndani ya nia zao mvuto wa kudumu. {9T 38.3}

Jitahidi kuwaamsha wanaume na wanawake kutoka katika kupoa kwao kiroho. Waambie jinsi ulivyompokea Yesu na jinsi ulivyobarikiwa tangu upate uzoefu katika huduma Yake. Waambie ni baraka gani huja kwako kadri unavyoketi miguuni pa Yesu na kujifunza masomo ya thamani kutoka katika Neno Lake. Waambie juu ya furaha na shangwe iliyopo katika maisha ya Kikristo. Maneno yako ya uchangamfu, yenye bidii yatawasadikisha kwamba umeipata lulu ya thamani kubwa. Hebu maneno yako ya uchangamfu na yenye kutia moyo yaoneshe kwamba hakika umeipata njia iliyo ya juu. Hii ni kazi ya Kweli ya umishionari, na kadri inavyofanywa, wengi wataamka kama watokao katika ndoto.{9T 38.4}

Hata wanapokuwa katika kazi zao za kila siku, watu wa Mungu wanaweza kuwaongoza wengine kwa Kristo. Na wakati wakifanya hivi watakuwa na uhakikisho wa thamani kwamba Mwokozi Yuko kando yao. Hawahitaji kufikiri kwamba wameachwa wategemee juhudi zao dhaifu. Kristo atawapa Maneno ya kusema yatakayoburudisha, na kuwatia moyo, na kuwatia nguvu watu maskini, na

roho zinazohangaika zilizo gizani. Imani yao itaimarishwa kadri wanavyotambua kuwa ahadi ya Mkombozi inatimizwa. Sio tu kwamba wao watakuwa baraka kwa wengine, lakini kazi wanayofanya kwa ajili ya Kristo huleta baraka kwao wenyewe. {9T 39.1}

Kuna wengi ambao wanaweza na wanapaswa kufanya kazi ambayo nimeizungumzia. Ndugu yangu, dada yangu, Unafanya nini kwa ajili ya Kristo? Je, unatafuta kuwa mbaraka kwa wengine? Je, midomo yako inatamka maneno ya wema, huruma na upendo? Je, unaweka juhudi za dhati ili kuwavuta wengine kwa Mwokozi? {9T 39.2}

### Matokeo ya Kushindwa Kufanya Kazi

Kwa kulinganisha, ni kazi ndogo ya umishenari imefanywa, na matokeo ni nini? Kweli ambazo Kristo alizitoa haijafundishwa. Wengi wa watu Mungu hawakui katika neema. Wengi wako katika hali isiyopendeza, na akili ya kulalamika. Wale ambao hawawasaidii wengine kuona umuhimu wa Ukweli wa leo wanapaswa kujisikia wao wenyewe kutoridhika. Shetani hujinufaisha kwa hali hii katika mazoea yao na huwaongoza katika kukosoa na kutafuta makosa. Kama wangelikuwa na shughuli nyingi katika kutafuta kujua na kutenda mapenzi ya Mungu wangelihisi mzigo huo kwa roho zinazoangamia, msukosuko huo wa akili usingeweza kuwazuiwa kulitimiza agizo: “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Marko 16:15. {9T 39.3}

### Wito wa Juhudi Bila Kuchoka

Bwana huwaita watu Wake waamke katika usingizi. Mwisho wa vyote umekaribia. Wakati wale wanaoijua Kweli watakapokuwa watenda kazi pamoja na Mungu, matunda ya haki yataonekana. Kwa udhihirisho wa upendo wa Mungu katika juhudi za kimishenari, wengi wataamshwa kuona hali ya dhambi katika mtindo wa wa maisha. Wataona kuwa huko nyuma ubinafsi wao uliwanyima sifa ya kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Uonyeshaji wa upendo wa Mungu kama unavyoonekana katika huduma isiyo na ubinafsi kwa wengine itakuwa njia ya kuwaongoza watu wengi kuliamini Neno la Mungu kama linavyosomwa. {9T 40.1}

Mungu anatamani kuwaburudisha watu Wake kwa kipawa cha Roho Mtakatifu, akiwabatiza upya katika upendo Wake. Hakuna haja ya upungufu wa Roho ndani ya kanisa. Baada ya kupaa kwa Kristo, Roho Mtakatifu alikuja juu ya waliokuwa wakimngoja, wakiomba, wanafunzi waaminio kwa utimilifu na nguvu zilizoufikia kila moyo. Katika siku zijazo dunia itaangazwa kwa utukufu wa Mungu. Ushawishi Mtakatifu utakwenda ulimwenguni kutoka kwa wale ambao wametakaswa kwa ile Kweli. Dunia inapaswa kuzungukwa na angahewa ya neema. Roho Mtakatifu anapaswa kufanya kazi katika mioyo ya wanadamu, akichukua mambo ya Mungu na kuwaonesha wanadamu. {9T 40.2}

## Familia za Kimishenari

Mengi zaidi yangeweza kufanywa kwa ajili ya Kristo ikiwa wote walio na nuru ya Kweli wangeitenda ile Kweli. Kuna familia nzima ambazo wanaweza kuwa wamishionari, wakijihulisha na kazi ya binafsi, wakifanya kazi kwa bidii kwa ajili ya Bwana kwa mikono yenye shughuli nyingi na akili imara, wakibuni mbinu mpya kwa ajili ya mafanikio ya kazi Yake. Wapo wenye bidii, wanyofu na wenye busara, wanaume na wanawake wenye moyo mkunjufu ambao wangeweza kufanya mengi kwa ajili ya Kristo kama wangejitoa wao wenyewe kwa Mungu, wakimkaribia na kumtafuta kwa moyo wote. {9T 40.3}

Ndugu na dada zangu, shirikini kikamilifu kwa utendaji hai katika kazi ya kuokoa roho. Kazi hii itatoa uhai na nguvu kwa uwezo wa akili na roho. Nuru kutoka kwa Kristo itaangaza akilini. Mwokozi atafanya makazi mioyoni mwenu, na katika nuru Yake mtaona nuru. {9T 41.1}

Jiwekeni wakfu kikamilifu kabisa kwa kazi ya Mungu. Yeye Ndiye nguvu yako, na atakuwa mkono wako wa kulia, akikusaidia kuendeleza makusudi Yake ya rehema. Kwa kazi binafsi fikia wale walio karibu nawe. Fahamiana nao. Kuhubiri hakutafanya kazi inayohitajika kufanywa. Malaika wa Mungu hukuandama kwenye makazi ya wale unaowatembelea. Kazi hii haiwezi kufanywa na mwakilishi. Pesa iliyokopeshwa au hata kutolewa haitaweza kuitimiza. Mahubiri hayataifanya. Kwa kuwatembelea watu, kuzungumza nao, kuomba nao, kuwahurumia, utaileta mioyo kwa Kristo. Hii ndiyo kazi ya juu zaidi ya umishenari unayoweza kufanya, Ili kuifanya, utahitaji ujasiri, imani idumuyo, uvumilivu usiokoma, na upendo wa kina kwa roho za watu. {9T 41.2}

Tafuta kuwafikia watu ambao unaishi nao jirani. Unapowaambia Ukweli, tumia Maneno ya Huruma kama ya Kristo. Kumbuka kwamba Bwana Yesu Ndiye Mtendakazi mkuu. Yeye humwagilia mbegu iliyopandwa. Huweka katika akili yako maneno yatakayoifikia mioyo. Tarajia kuwa Mungu atamtegemeza yule aliyejiweka wakfu, mtendakazi asiye na ubinafsi. Utii, imani kama ya mtoto, kumtumaini Mungu--hivi vitaleta amani na furaha. Fanya kazi bila kuja nafsi yako, kwa upendo, kwa uvumilivu, kwa wote ambao unakutana nao. Usioneshe kutokuwa na subira. Usiseme hata neno moja lisilofaa. Hebu Upendo wa Kristo uwe ndani ya mioyo yenu, sheria ya wema midomoni mwenu. {9T 41.3}

Ni fumbo kwamba hakuna mamia kazini pale ambapo sasa kuna mmoja tu. Ulimwengu wa mbinguni unashangazwa na kutojali, ugoigoi, ubaridi, kutozingatia kwa wale wanaodai kuwa wana na binti za Mungu. Katika Kweli kuna nguvu iliyo hai. Nendeni kwa imani, na muitangaze Kweli kana kwamba mliuamini. Hebu wale unaowafanyia kazi waone kwamba kwako wewe, hakika ni Ukweli ulio hai. {9T 42.1}

## Maendeleo Kupitia Huduma

Wale wanaotoa maisha yao katika huduma kama ya Kristo wanajua maana ya furaha ya Kweli. Nia zao na maombi yao yanafika mbali zaidi ya nafsi zao. Wao wenyewe wanakua kadri wanavyojaribu kusaidia wengine. Huifahamu mipango mikubwa zaidi, miradi inayochochea zaidi, na inawezaje basi kuwa na kitu kingine isipokuwa wao kukua wakati wanajiweka wenyewe katika njia ya mbingu ya nuru na baraka? Watu kama hao hupokea hekima kutoka mbinguni. Hujitambulisha zaidi na zaidi na Kristo katika mipango Yake yote. Hakuna fursa ya udumavu na kifo cha kiroho. Tamaa za ubinafsi na kujitafutia maslahi binafsi na kujipenda hukaripiwa kwa kuwasiliana mara kwa mara na nia ivutayo, matamanio yaliyoinuliwa, ambayo ni ya shughuli za juu na takatifu. {9T 42.2}

## SURA YA 4
## HAJA YA JUHUDI ZA DHATI

Kwa uwezo wa Roho, watumishi waliokabidhiwa majukumu na wanaomwakilisha Kristo wanapaswa kumshuhudia Kiongozi wao. Shauku kubwa ya Mwokozi kwa ajili ya wokovu wa wenye dhambi inapaswa kuonekana katika juhudi zao zote. Mwaliko wenye neema, unaotolewa kwanza na Kristo, unapaswa kubebwa na sauti za kibinadamu na kutangazwa ulimwenguni kote: "Na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure." Ufunuo 22:17. Kanisa linapaswa kusema: "Njoo." Kila nguvu ndani ya kanisa inapaswa kuhusishwa kikamilifu upande wa Kristo. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kujumuishwa katika jitahada kubwa ya kuuita Ulimwengu kuuzingatia unabii wa Neno la Mungu unaotimia kwa haraka. Ukafiri na umizimu unazidi kushika kasi duniani. Je, wale ambao kwao nuru kuu

imekabidhiwa wawe baridi na kukosa imani kwa sasa? {9T 43.1}

Tuko kwenye ukingo wa wakati wa taabu, na mashaka ambayo hayakutarajiwa kuonwa yako mbele yetu. Nguvu kutoka chini inawaongoza watu kwenye vita dhidi ya Mbingu. Wanadamu wameungana na mawakala wa kishetani ili kuibatilisha sheria ya Mungu. Wakazi wa dunia wanaharakisha kuwa kama wenyeji wa ulimwengu katika siku za Nuhu, waliofutiliwa mbali na Gharika, na kama wenyeji wa Sodoma, walioteketezwa kwa moto kutoka mbinguni. Nguvu za Shetani zinafanya kazi kuziweka akili mbali na uhalisia wa umilele. Adui amepanga mambo ili yaendane na makusudi Yake Mwenyewe. Biashara za kidunia, michezo, mitindo ya siku hizi --mambo haya yanachukua mawazo ya wanaume na wanawake. Burudani/maburudisho na usomaji usio na faida huharibu uwezo wa kuamua. Katika njia pana iendayo katika upotevu wa milele kuna misafara mirefu. Ulimwengu uliojaa vurugu, karamu, na ulevi, unaliongoa kanisa. Sheria ya Mungu, kiwango cha haki cha mbingu, inatangazwa kuwa haina maana. {9T 43.2}

Wakati huu—wakati wa uovu mwingi wa kutishwa—- maisha mapya, yanayotoka katika Chanzo cha uhai wote, yanapaswa kumiliki wale walio na upendo wa Mungu mioyoni mwao, na wanapaswa kwenda kuutangaza kwa nguvu ujumbe wa Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka. Wanapaswa kuweka juhudi za dhati bila kuchoka kuokoa roho. Mfano wao unapaswa kuwa na ushawishi mkubwa kwa wema kwa wale walio karibu nao. Wanapaswa kuhesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya ubora wa ujuzi wa Kristo Yesu Bwana wetu. {9T 44.1}

Unyofu na bidii ya kina inapaswa kutumiliki. Nguvu zetu zilizolala zinapaswa kuzinduka na kuwa juhudi zisizochoka. Watendakazi waliowekwa wakfu waende mashambani wakiisafisha njia kuu ya Mfalme, na kupata ushindi katika maeneo mapya. Ndugu yangu, na dada yangu, si kitu kwako kujua kwamba kila siku roho hushuka kaburini bila kuonywa na bila kuokolewa, bila kujua hitaji lao la uzima wa milele na upatanisho uliofanywa kwa ajili yao na Mwokozi? Je! si lolote kwako kwamba hivi karibuni ulimwengu utakutana na Yehova kuhusu sheria Yake iliyovunjwa? Malaika wa mbinguni wanashangaa kwamba wale ambao kwa miaka mingi wamekuwa na nuru, hawajabeba mwenge wa Ukweli kwenda katika maeneo yenye giza duniani. {9T 44.2}

Thamani isiyo na kikomo ya dhabihu iliyohitajika kwa ajili ya ukombozi wetu inadhihirisha Ukweli kwamba dhambi ni uovu mkubwa unaotisha. Mungu angeweza kulifuta doa hili chafu wakati wa uumbaji kwa kumfagia mwenye dhambi juu ya uso wa dunia. Bali Yeye “kwa jinsi hii aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16. Sasa basi kwa nini hatuna unyofu na bidii zaidi? Kwa nini idadi kubwa ya waamin imekaa bila kazi? Kwa nini wale wanaodai kumpenda

Mungu, hawatafuti kuwaangazia jirani zao na kushirikiana nao, kwamba wasiendelee kupuuza wokovu mkuu kama huu? {9T 44.3}

### Ukosefu wa Huruma

Miongoni mwa watu wanaojiita Wakristo wa leo kuna ukosefu wa kutisha wa huruma ambayo inapaswa kuhisiwa kwa roho ambazo hazijaokolewa. Isipokuwa mioyo yetu inapiga kwa umoja na moyo wa Kristo, tunawezaje basi kuelewa utakatifu na umuhimu wa kazi ambayo tunaitiwa kwa Maneno haya: “Kesheni kwa ajili ya roho ...kama wanaopaswa kutoa hesabu?” Tunazungumza juu ya utume wa Kikristo. Milio ya sauti zetu inasikika, lakini je, tunahisi huruma ya moyo wa Kristo ikiumia kwa ajili ya nafsi? {9T 45.1}

Mwokozi alikuwa mtendakazi asiyechoka. Hakuipima kazi Yake kwa masaa. Muda Wake, Moyo Wake, nguvu Zake, vilitolewa kufanya kazi kwa faida ya ubinadamu. Mchana wote ulitolewa kwa kazi, na saa za usiku alizitoa kwa ajili ya maombi, ili apate kuwa tayari kukutana na adui mwenye hila katika udanganyifu wake wote; na aweze kuimarishwa kufanya kazi Yake ya kuuinua na kuurejesha ubinadamu. {9T 45.2}

Mtu anayempenda Mungu hapimi kazi yake kwa mfumo wa masaa nane. Anafanya kazi saa zote na hapumziki. Kadri apatavyo fursa anafanya mema. Mahali pote, katika nyakati zote na kila sehemu, hutafuta fursa ya kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Huyabeba manukato kokote aendako. Angahewa zuri huizunguka nafsi yake. Uzuri wa maisha yake yaliyopangwa vizuri na mazungumzo ya kimbingu huwatia moyo wengine katika imani, matumaini na ujasiri. {9T 45.3}

Wanahitajika wamishenari wenye moyo. Jitihada za ulegevu na za kushtukiza hazitafanya kazi vizuri sana. Ni lazima tuwe na umakini. Lazima tuwe watu dhati na wenye bidii kabisa. {9T 45.4}

Kwa vita vikali, katikati ya upinzani, hatari, upotevu, na mateso ya mwanadamu, kazi ya kuokoa roho inapaswa kuendelezwa mbele. Katika vita fulani, wakati mmoja vikosi vya jeshi la kushambulia vilirudishwa nyuma na vikosi vya adui, aliyekuwa na bendera mbele alisimama huku wanajeshi wakirudi nyuma. Kiongozi akampigia kelele arudishe nyuma bendera, lakini jibu la mshika bendera lilikuwa: "Walete watu kwenye bendera! "Hii ndio kazi inayomhusu kila mbeba-bendera mwaminifu kuwaleta watu kwenye bendera. Bwana huita wenye moyo wote. Sote tunajua kwamba dhambi ya wengi wanaojiita Wakristo ni kukosa ujasiri na nguvu ya kujileta wenyewe na wale waliounganishwa nao kufikia kiwango. {9T 45.5}

Kutoka nchi zote kilio cha Makedonia kinasikika: "Njoo huku,... na utusaidie." Mungu amefungua mashamba mbele yetu, na kama mawakala wa kibinadamu wangeshirikiana na mawakala wa kimbingu, nafsi nyingi, nyingi sana zingeletwa

kwenye Kweli. Lakini watu wa Bwana wamekuwa wakilala juu ya kazi waliyopewa, na katika sehemu nyingi kwa kulinganisha hubaki bila kuguswa. Mungu ametuma ujumbe baada ya ujumbe ili kuamsha watu wetu kufanya jambo fulani, na kulifanya sasa. Lakini kwa kilio na wito, "Nimtume nani?" kumekuwa na wachache wa kujibu, "Mimi hapa, nitume mimi." Isaya 6:8. {9T 46.1}

Wakati lawama za kutiwa ganzi, ugoigoi pamoja na ulegevu na uvivu vitakapokuwa vimetupiliwa mbali kutoka kanisani, Roho wa Bwana atatolewa kwa wingi. Nguvu za mbinguni zitafunuliwa. Kanisa litaona utendaji wa majaliwa ya Bwana wa majeshi. Nuru ya Ukweli itang'aa katika miale kwa uwazi, miale yenye nguvu, ni kama ilivyokuwa nyakati za mitume, nafsi nyingi zitageuka kuachana na upotovu na kuugeukia Ukweli. Ulimwengu utaangazwa kwa utukufu wa Bwana. {9T 46.2}

Malaika wa mbinguni kwa muda mrefu wamekuwa wakingojea mawakala wa kibinadamu - washiriki wa kanisa - kushirikiana nao katika kazi kubwa inayopaswa kufanywa. Malaika wanakungoja wewe. Shamba ni kubwa sana, na mpango ni wa kina sana, kiasi kwamba kila moyo uliotakaswa utaingizwa haraka kwenye utumishi kama chombo cha nguvu cha Bwana. {9T46.3}

Wakati huo huo kutakuwa na nguvu inayofanya kazi kutokea chini. Wakati mawakala wa Mungu wa rehema wanafanya kazi kupitia kwa wanadamu waliowekwa wakfu, Shetani anaweka wakala wake kufanya kazi, akiwaweka chini ya wajibu wake wale wote wanaojisalimisha katika udhibiti wake. Kutakuwa na mabwana wengi na miungu mingi. Kilio kitasikika, “Tazama, hapa kuna kristo,” na, “Tazama, kule kuna Kristo.” Utendaji wa kina wa Shetani utajidhihirisha kila mahali kwa kusudi la kuugeuza umakini wa wanaume na wanawake kutoka kwa wajibu wao wa sasa. Kutakuwa na ishara na maajabu. Lakini jicho la imani litatambua katika maonyesho haya yote viashiria vya wakati ujao ulio mkuu na wa kutisha, na ushindi unaowangoja watu wa Mungu. {9T 47.1}

Fanya kazi, Ah!, fanya kazi, ukiuangalia mbele umilele! Kumbuka kwamba kila uwezo lazima utakaswe. Kazi kubwa inapaswa kufanyika. Hebu maombi yatoke kwenye midomo isiyo na unafiki: “Mungu na atufadhili, aturehemu na kutubariki; na kutuangazia uso Wake…… Ili njia Yake ijulikane duniani, wakovu Wake katikati ya mataifa yote." Zaburi 67:1, 2. {9T 47.2}

Wale wanaotambua, hata kwa kiwango kidogo, nini maana ya ukombozi kwao na kwa watu wenzao, watatembea kwa imani na watafahamu kwa kiasi fulani mahitaji makubwa ya ubinadamu. Mioyo yao itasukumwa na huruma wanapoona ufukara ulioenea katika ulimwengu wetu--ufukara wa umati wa watu wanaoteseka kwa ajili ya chakula na mavazi, na ufukara wa kimaadili wa maelfu ambao wako chini ya kivuli cha adhabu ya kutisha, ambao ukilinganisha wana majanga ya kimwili hufifia na kupelea, kama si kitu. {9T 47.3}

Hebu washiriki wa kanisa wazingatie hoja kwamba kwa kuwa majina yao yameandikwa kwenye vitabu vya kanisa haitawaokoa. Ni lazima wajionyeshe kuwa wamekubaliwa na Mungu, watenda kazi wasiotahayari. Siku kwa siku wanapaswa kujenga tabia zao kulingana na maagizo ya Kristo. Wanapaswa kukaa ndani Yake, daima wakitumia imani Kwake. Hivyo watakua hadi kimo kamili cha wanaume na wanawake ndani Kristo—Wakristo walio safi, wachangamfu, wenye shukrani, wakiongozwa na Mungu katika nuru iliyo wazi na iliyo wazi zaidi. Kama huu sio uzoefu wao, watakuwa miongoni mwa wale ambao sauti zao siku moja zitapazwa kwa uchungu wakiomboleza: "Mavuno yamepita, wakati wa hari umekwisha, na nafsi yangu haikuokolewa! Kwa nini sikuikimbilia Ngome imara ya kimbilio? Kwa nini nimecheza na wokovu wa nafsi yangu, na kumdharau Roho wa neema?" {9T 48.1}

"Siku ya Bwana iliyo kuu i karibu; i karibu, nayo inafanya haraka sana." Sefania 1:14. Hebu tuvae viatu vya injili, tayari kupiga gwaride kwa tangazo la muda mfupi. Kila saa, kila dakika, ni ya thamani. Hatuna muda wa kutumia katika kujiridhisha nafsi. Kote kutuzunguka kuna nafsi zinazoangamia katika dhambi. Kila siku kuna kitu cha kufanya kwa ajili ya Bwana na Mwalimu wetu. Kila siku tunapaswa kuzielekeza roho kwa Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. {9T 48.2}

“Ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu Yuaja. Mathayo 24:44. Nenda kupumzika kwako usiku huku kila dhambi ikiwa imeungamwa. Ndivyo tulivyofanya mwaka wa 1844 tulipotarajia kukutana na Bwana wetu. Na sasa tukio hili kuu liko karibu zaidi kuliko tulipoamini mara ya kwanza. Iweni tayari kila wakati, jioni, asubuhi, na adhuhuri, ndipo kilio kitakaposikiwa, Tazama, Bwana arusi Yuaja; tokeni mwende kumlaki,” unaweza, hata kama umeamshwa kutoka usingizini, ukatoka kwenda kumlaki na taa zako zikiwa zimetolewa utambi mweusi ulioungua, na zikiwa zinawaka. {9T 48.3}

## SURA YA 5
## "MMEPOKEA BURE, TOENI BURE"

Kujikana nafsi ni Neno kuu la mafundisho ya Kristo. Mara nyingi huwasilishwa na kuamriwa katika lugha inayoonekana kuwa ya kimamlaka, kwa sababu Mungu anaona kwamba hakuna njia nyingine ya kumwokoa mwanadamu isipokuwa kutupilia mbali kutoka katika maisha yake ubinafsi ambao, kama ungeliachwa, ungeliharibu nafsi yote. {9T 49.1}

Kristo alifanyika maskini ili tuwe washiriki wa utukufu wa milele uzidio kuwa

mwingi sana.” 2 Wakorintho 4:17. Tunapaswa kujizoeza kujikana nafsi kule kule ambako kulimfanya Yeye ajitoe kwa kifo cha msalaba, ili kuwawezesha wanadamu waupate uzima wa milele. Katika namna zetu zote za matumizi tunapaswa kujitahidi kulitimiza kusudi Lake Yeye aliye Alfa na Omega wa juhudi zote za Mkristo.{9T 49.2}

Tunapaswa kuweka katika hazina ya Bwana vyote ambavyo tunaweza kutumia. Hii humaanisha, mhitaji, sehemu ambazo hazijafanyiwa kazi zinaita. Kutoka katika maeneo mengi kunasikika kilio, “Njooni huku, …… na mtusaidie. Washiriki wetu wa kanisa wanapaswa kuona shauku kubwa katika utume wa nyumbani na nchi za kigeni. Mibaraka mikubwa itakuja kwao kadri wanavyo fanya jitihada za kujitoa kafara ili kupanda kiwango cha Kweli katika eneo jipya. Fedha iliyowekezwa kwa ajili ya kazi hii italeta faida kubwa. Waongofu wapya, wakifurahia nuru waliyoipokea kutoka katika Neno. kwa upande wao watatoa mali zao kwa ajili ya kuipeleka nuru ya Ukweli kwa wengine. {9T 49.3}

**Ukarimu wa Mungu.**

Mungu huendelea hutupatia daima, bure, na kwa wingi. Kila mibaraka ya kiduniani inatoka mkononi Mwake. Itakuwaje ikiwa Bwana ataacha kutoa baraka Zake kwetu? Ni kilio cha jinsi gani cha unyonge, cha uharibifu cha mateso, na uhitaji kingepanda kutoka duniani! Tunahitaji kila siku mtiririko usikokoma wa wema wa Yehova. {9T 49.4}

Ulimwengu huu ulianzishwa, unategemezwa na unadumishwa kwa upendo wenye huruma za Muumba. Mungu Ndiye mtoaji wa vyote tulivyo navyo (mema tu). Yeye Hutuita tumrudishie sehemu tu ya vingi alivyotupatia. Fikiri juu ya utunzaji anaoipa dunia, akitoa mvua na jua kuiangaza dunia kwa majira yake, kuifanya mimea kustawi na kunawiri. Yeye Anawapa neema Zake wenye haki na wasio haki. Je! Haiwapasi wapokeaji wa baraka Zake kuonesha shukrani zao kwa kutoa mali zao kusaidia wanadamu wanaoteseka? {9T 50.1}

Kuna nafsi nyingi za kuletwa kwenye ujuzi wa ile Kweli ya kuokoa. Mwana mpotevu yuko mbali na nyumba ya Baba yake, akiteseka kwa njaa. Anapaswa kuwa kiini cha huruma yetu. Je, unauliza: "Ni kwa kiasi gani Mungu anawajali wale wanaoangamia katika dhambi zao?" Ninawaelekeza Kalvari. Mungu "alimtoa Mwanawe Wake wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” Yohana 3:16. Fikiri juu ya upendo usio na kifani wa Mwokozi. Tulipokuwa tungali bado wenye dhambi, Kristo alikufa ili kutuokoa na kifo cha milele. Kama kuonesha mrejesho kwa ajili ya upendo mkuu ambao Kristo amekupenda wewe, unapaswa kumletea sadaka yako ya shukrani. Unapaswa

kutoa sadaka ya shukrani wewe mwenyewe. Muda wako, talanta zako, mali zako vyote vinapaswa kutiririka ulimwenguni katika wimbi la upendo kwa ajili ya kuokoa waliopotea. Yesu amefanya iwezekane kwako kuukubali upendo Wake na kwa ushirikiano wa furaha pamoja Naye kufanya kazi chini ya ushawishi wake wenye harufu nzuri. Yeye Anahitaji utumie mali yako katika huduma isiyo na ubinafsi, ili mpango Wake wa wokovu wa roho uendelezwe mbele kwa nguvu. Yeye Anakutarajia wewe utoe nguvu zako zisizogawanyika kwa kazi Yake. {9T 50.2}

Je, unaweza kuzifanya mali yako kuwa salama? Weka kwenye mkono ambao una alama za misumari ya kusulubiwa. Iweke katika milki yako, na itakuwa kwako upotevu wako wa milele. Itoe kwa Mungu, na kuanzia wakati huo ina maandishi (muhuri) Yake. Imetiwa muhuri na kutobadilika Kwake. Je, ungependa kufurahia mali yako?  Itumie kuwa baraka kwa wanaoteseka. {9T 50.3}

## Hitaji la Msaada la ulimwengu

Ukubwa wa kazi yetu unahitaji ukarimu wetu wa hiari kwa upande wa watu wa Mungu. Huko Afrika, huko China, huko India, kuna maelfu, ndiyo, mamilioni, ambao hawajausikia ujumbe wa ile Kweli kwa ajili ya Ukweli kwa wakati huu. Watu hawa ni lazima waonywe. Visiwa vya bahari vinangojea maarifa ya Mungu. Katika visiwa hivi shule zinapaswa zianzishwe ili kuwatayarisha wanafunzi kwenda shule za masomo ya juu, huko wataelimishwa na kufunzwa, na kurudishwa nyumbani kwao kisiwani ili kuwapa wengine nuru waliyopokea. {9T 51.1}

Katika nchi yetu wenyewe, kuna mengi ya kufanya. Kuna miji mingi ya kuingiwa na kuonywa. Wainjilisti wanapaswa kuwa wakitafuta njia yao ya kupenya katika maeneo yote ambapo mawazo ya watu yanafadhaishwa juu ya suala la sheria ya Jumapili na Kufundisha dini katika shule za umma (nchi nyingi zina hiki kipindi, swali ni jinsi fursa hii inavyotumiwa!). Sababu inayozuia maendeleo ya kazi, ni upuuziaji wa Waadventista Wasabato katika kushugulikia fursa hizi za majaliwa ya Mungu. {9T 51.2}

Bwana ametufanya sisi kuwa mawakili Wake. Yeye Ameweka mali Zake mikononi mwetu kuzisambaza kwa uaminifu. Yeye Hutuhitaji tumpe Yeye yaliyo Yake. Yeye Ameiweka zaka kama sehemu Yake takatifu ili itumike katika kupeleka injili katika sehemu zote za dunia. Kaka na dada zangu, ungameni na kuacha ubinafsi wenu, na mleteeni Bwana matoleo, zawadi na sadaka zenu. Mleteeni pia zaka mlizomnyima. Njooni mkikiri kutokujali kwenu. Mthibitishe Bwana, kama alivyokualika kufanya. "Kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya

wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi." Malaki 3:11. {9T 51.3}

## Ubinafsi Wetu Kizuizi kwa Kazi ya Mungu

Maelekezo yametolewa kwangu kwamba kuna zaka inayozuiwa ambayo inapaswa kuletwa kwa uaminifu katika hazina ya Bwana ili kuwasaidia watumishi na wamishenari wanaowafungulia watu Maandiko na kufanya kazi nyumba kwa nyumba. Kazi ya kuieneza injili ulimwenguni imekuwa kwa kiasi kikubwa sana ikizuiwa na uchoyo/ubinafsi wa mtu binafsi. Baadhi, hata miongoni mwa wanaodai kuwa Wakristo, hawawezi kuona kwamba kazi ya injili inapaswa kuungwa mkono kwa mali ambazo Kristo amewapa. Fedha zinahitajika ili kazi inayofanywa ulimwenguni kote iweze kusonga mbele. Maelfu kwa maelfu wanaangamia katika dhambi, na ukosefu wa mali unazuia utangazaji wa Kweli ambayo inapaswa kupelekwa kwa kila taifa, kabila, lugha na jamaa. Kuna watu walio tayari kwenda kama wajumbe wa Bwana, lakini kwa sababu ya ukosefu wa mali katika hazina hawawezi kupelekwa mahali ambapo watu wanaomba mtu aje awafundishe Kweli. {9T 52.1}

Kuna wengi katika ulimwengu wetu ambao wanatamani kulisikia Neno la uzima. Lakini wanawezaje kulisikia bila mhubiri? Na wale waliotumwa kuwafundisha wanawezaje kuishi bila msaada/kutegemezwa? Mungu angetaka maisha ya watenda kazi Wake yaangaliwe kwa uangalifu. Wao ni mali Yake, na Yeye huvunjiwa heshima wanapolazimishwa kufanya kazi kwa njia inayodhuru afya zao. Yeye Anavunjiwa heshima, pia, wakati fulani kwa sababu ya kukosa mali kisha watendakazi hawawezi kupelekwa kwenye maeneo yasiyo na watendakazi. {9T 52.2}

Badala ya kulalamikia maofisa wa Konferensi Kuu (General Conference) kwa sababu hawawezi kujibu miito miingi ya  watendakazi na mali, hebu washiriki wa kanisa letu watoe ushuhuda ulio hai wa nguvu za Kweli kwa kujikana nafsi na kutoa kwa ukarimu na moyo mkunjufu kwa ajili ya kuendeleza mbele kazi. Hebu dada zetu waokoe fedha kwa kukataa kuweka mapambo ya gharama kubwa juu ya mavazi yao. Hebu kila gharama zisizo za lazima zipunguzwe. Hebu kila familia walete zaka na sadaka zao kwa Bwana. {9T 53.1}

## Mawakili Wasambazaji Sadaka wa Mungu

Wale wote ambao wameongoka kweli kweli watajiona kama wao ni mawakili tu, kama wasambazaji wa sadaka na mali wa Mungu na watatoa, kwa ajili ya maendeleo ya kazi, mali ambazo Bwana ameweka mikononi mwao. Kama Maneno ya Kristo yangelitiiwa, kungelingekuwa na mali ya kutosha katika hazina

Yake kwa mahitaji ya kazi Yake. Yeye Amewakabidhi wanaume na wanawake wingi wa mali za kuendeleza mpango Wake wa rehema na ukarimu. Yeye Anawataka mawakili Wake wa mali kuwekeza pesa zao katika kazi ya kuwalisha wenye njaa, kuwavisha walio uchi, na kuihubiri injili kwa maskini. Ukamilifu wa tabia hauwezi kupatikana bila kujikana nafsi. {9T 53.2}

Hakukuwahi kuwa na wakati muhimu zaidi katika historia ya kazi yetu kuliko wakati wa sasa. Ujumbe wa sura ya tatu ya Malaki unatujia, ukiinua juu, mbele yetu hitaji la uaminifu katika mahusiano yetu kwa Bwana na kwa kazi Yake. Ndugu zangu, pesa mnazotumia kununua na kuuza na kujitapatia faida itakuwa ni laana kwako ikiwa unamzuilia Bwana iliyo Yake. Mali ulizokabidhiwa kwa ajili ya maendeleo ya kazi ya Bwana zinapaswa kutumika katika kupeleka injili sehemu zote za ulimwengu. {9T 53.3}

Sisi ni mashahidi wa Kristo, na hatupaswi kuruhusu masilahi na mipango ya ulimwengu ya kuchukua muda na umakingi wetu. Kuna maslahi yenye thamani ya juu ambayo yako hatarini. "Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki Yake.” Mathayo 6:33. Kristo alijitoa kwa hiari, kwa moyo mkunjufu na kwa furaha katika kutekeleza mapenzi ya Mungu. Akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba. Kwa kuzingatia yote aliyoyafanya, je, tunapaswa kuhisi kuwa ni vigumu kujikana nafsi? Je, tutarudi nyuma kwa kutokuwa washirika wa mateso ya Kristo? Kifo Chake kinapaswa kuchochea kila seli/chembe ya uhai wetu, na kutufanya kuwa tayari kuweka wakfu kwa kazi Yake vyote tulivyo navyo na tulivyo. Kadri tunavyofikiria yote aliyotufanyia, mioyo yetu inapaswa kujazwa na shukrani na upendo, na tunapaswa kuachana na ubinafsi wote. Ni wajibu gani moyo unaweza kukataa kutenda chini ya ushawishi wa upendo wa Kristo unaobidisha? {9T 53.4}

Je! hatutafanya yote tuwezayo kwa kujinyima ili kuendeleza kazi ya Mungu ya rehema? Tunawezaje kuutazama kujidhili na unyenyekevu wa Mungu, mateso aliyovumilia Mwana wa Mungu, bila kujazwa na shauku ya kuruhusiwa kujinyima/kujidhabihu kitu kwa ajili Yake? Je, sio heshima kubwa kuruhusiwa kushirikiana Naye? Yeye Aliyaacha makao Yake ya mbinguni ili kututafuta. Je! sisi hatutakuwa wachungaji wasaidizi, chini yake, na hapa kutafuta wanadamu waliopotea na kupotoka? Je, hatudhihirishi katika maisha yetu rehema na huruma Yake takatifu? {9T 54.1}

Bwana anatamani watu Wake wawe wazingativu, wenye kujali, na wenye kucheua mambo. Anatamani wajifunze kuwa wachumi kwa kila kitu. Kama watendakazi katika maeneo ya utume wangeweza kuwa na mali ambazo zinatumika na waumi katika kununua katika vyombo vya gharama kubwa kama samani na katika mapambo binafsi, ushindi wa msalaba wa Kristo ungepanuliwa kwa kwenda

mbali sana. {9T 54.2}

Sio wote wanaoweza kutoa matoleo makubwa, sio wote wanaoweza kufanya kazi kubwa, ya matendo makuu; bali wote wanaweza kujizoeza kujinyima-kujikana nafsi, wote wanaweza kudhihirisha kutokuwa na ubinafsi kwa Mwokozi. Baadhi wanaweza kuleta sadaka nyingi katika hazina ya Bwana; wengine wanaweza kuleta sarafu/senti tu; lakini kila sadaka inayoletwa kwa unyofu inakubaliwa na Bwana. {9T 54.3}

Tunaomba pesa zinazotumika kwa vitu visivyo vya lazima. Ndugu,na dada zangu, msipoteze zenu pesa katika kununua vitu visivyo vya lazima. Unaweza kufikiri hesabu hizi hivi vitu vidogo, au pesa ndogo sio nyingi, lakini vidogo vingi hufanya kitu kamili kikubwa. Kata kabisa kila matumizi ya anasa. Usijihusishe na chochote kile kwa ajili ya kujionesha tu. Pesa yako humaanisha wokovu wa roho. Hebu kuwepo na utoaji wa ukarimu kwa utaratibu katika pande zote. Huenda wengine wasiweze kutoa kiasi kikubwa, lakini wote wanaweza kuweka kando kila juma kitu kwa ajili ya Bwana. Hebu watoto wafanye sehemu yao. Hebu wazazi wawafundishe watoto wao kuhifadhi senti zao ili watoe Mungu. Huduma ya injili inapaswa kuungwa mkono kwa kujikana nafsi na kujinyima. Kwa njia ya jitihada za kujikana nafsi za watu wa Mungu wengine wataletwa katika imani, na hao watasaidia kuongeza matoleo yaliyotolewa kwa ajili ya kuendeleza kazi ya Bwana. {9T 55.1}

Ushahidi usio na shaka unaelekeza kwenye mwisho unaokaribia. Njia lazima iandaliwe na kuwa tayari kwa ujio wa Mfalme wa Amani. Hebu Washiriki wa kanisa letu wasinung’unike kwa sababu wanaitwa mara nyingi kutoa. Ni nini kinachofanya wito wa kutoa mara kwa mara kuwa wa lazima? Je, sio ongezeko la haraka la kazi ya umishenari? Je, kwa kukataa kutoa, turudishe nyuma ukuaji wa kazi hizi? Je, tunasahau kuwa sisi ni watendakazi pamoja na Mungu? Kutoka katika kila kanisa, maombi yanapaswa kupanda juu kwa Mungu kwa ongezeko la ibada, kujitoa wakfu na ukarimu. Ndugu, na dada zangu, msiombe kupunguzwa kazi katika kazi ya uinjilisti. Maadamu kuna roho za kuokoa, maslahi na shauku yetu katika kazi ya kuokoa roho ni kujua kuwa hakuna kupunguza kasi. Kanisa haliwezi kurahisisha kazi yake pasipo kumkana Bwana wake. Si wote wanaoweza kwenda kama wamishenari katika nchi za kigeni, lakini wote wanaweza kutoa mali zao kwa ajili ya kuendeleza utume wa nchi za kigeni. {9T 55.2}

Kuna maeneo mapya ya kuingiwa, na lazima tupate usaidizi wenu. Je, tulipuuze agizo la utume tulilopewa, na hivyo kupoteza utimilifu wa ahadi inayoambatana na agizo la utume? Je, watu wa Mungu watakuwa wazembe na wasiojali, na kukataa

kutoa mali zao kwa ajili ya kuiendeleza kazi? Je, wanaweza kufanya hivi bila kuukata uhusiano wao Naye Bwana? Wanaweza kufikiria hivyo ni kubana matumizi, lakini ni kujibana na kushugulikia uchumi kwa jinsi ya kutisha kunakowaweka mahali ambapo wanatengwa na Mungu. {9T 56.1}

Ndugu na dada zangu, mmechelewa sana kuutoa muda na nguvu zenu kujitumikia wenyewe. Hebu siku ya mwisho isikukute huna hazina ya mbinguni. Tafuta kuusukuma ushindi wa msalaba, tafuta kuziangaza roho, jitaabisheni kwa ajili ya wokovu wa wenzenu, na kazi yenu itastahimili kujaribiwa kwa moto. {9T 56.2}

Kila mtendakazi wa Kweli na mwenye kujitoa kwa ajili ya Mungu, yuko tayari kutumia na kutumiwa kwa ajili ya wengine. Kristo anasema: “Aipendaye nafsi yake ataiangamiza; naye aichukiaye nafsi yake katika ulimwengu huu ataisalimisha hata uzima wa milele.” Yoh.12:25. Kwa jitihada dhati na za bidii na za umakini ili kusaidia pale panapohitajika msaada, Mkristo wa Kweli anaonesha upendo wake kwa Mungu na kwa viumbe wenzake. Anaweza kupoteza maisha yake katika huduma; lakini Kristo atakapokuja kukusanya vito Vyake Kwake, atayapata tena. {9T 56.3}

Ndugu na dada zangu, msitumie kiasi kikubwa cha muda na pesa kujishughulikia mwenyewe, kwa ajili ya mwonekano. Wale wanaofanya hivyo wanalazimika kuacha mambo mengi yakiwa hayajafanywa/hayajagawanywa, na endapo yangefanywa, yangefariji na kuondolea wanadamu wengine usumbufu, kwa kutuma miali ya joto kwenye roho zao zilizochoka. Sote tunahitaji kujifunza jinsi ya kuboresha kwa uaminifu fursa ambazo mara nyingi huja kwetu kuleta nuru na matumaini katika maisha ya wengine. Tunawezaje kuimarisha fursa hizi ikiwa mawazo yetu yanajikita kwenye ubinafsi au umimi? Mwanadamu mwenye ubinafsi anapoteza fursa nyingi sana za kufanya yale ambayo yangeleta baraka kwake mwenyewe na kwa wengine. Ni wajibu wa mtumishi wa Kristo, katika kila hali, ajiulize, **Ninaweza kufanya nini ili kuwasaidia wengine?** Baada ya kufanya bora kwa sehemu yake na zamu yake, basi na aache matokeo kwa Mungu. {9T 56.4}

Mungu ametoa kwa kila mtu raha (luxury!) ambayo inaweza kufurahiwa na tajiri na maskini sawa– raha inayopatikana katika kukuza na kupalilia usafi wa mawazo na kutokuwa na ubinafsi wa vitendo, raha inayotokana na kusema maneno ya huruma na kufanya matendo mema. Kutoka kwa wale wanaofanya huduma hiyo, nuru ya Kristo hung'aa na kuangaza maisha yaliyotiwa giza kwa huzuni nyingi. {9T 57.1}

Jaribu linaweza kukujia kuwekeza pesa zako kwenye ardhi. Labda watoto wako

watakushauri kufanya hivi. Lakini Je, huwezi kuonesha njia bora zaidi? Je, fedha zako hazijakabidhiwa kwako ili zitumike kwa hekima, na kuweka kwa watoao riba, ili Bwana atakapokuja, akute talanta zimeongezeka maradufu? Huoni kwamba Yeye anataka utumie mali yako katika kusaidia kujenga nyumba za mikutano (makanisa) na kuanzisha Sanitariamu? {9T 57.2}

Tunahitaji sasa kuzipa kipaumbele na thamani ya hali ya juu roho kuliko pesa. Kama unaijua kazi ya juu zaidi katika ulimwengu huu kuliko kazi ya kuokoa roho, kazi ambayo italeta matokeo bora zaidi kwa uwekezaji wa mali, Je, hauwezi kutuambia na sisi, ili tuipime thamani yake? {9T 57.3}

Ninaogopa kwamba watu wetu wengi hawatambui umuhimu wa kazi ya Mungu. Mmoja ambaye nilimwandikia kwa ajili ya pesa alijibu hivi: "Nilipokea barua yako ukiniomba nikuazime pesa. Lakini kulikuwa na kipande ya ardhi ambayo watoto walidhani ni bora kwangu kukinunua, nami nimewekeza mali yangu ya ziada katika ardhi hii.” Ingekuwa bora zaidi kwa ndugu huyu kuwekeza pesa zake katika kuanzisha vituo vya Sanitarimu, ambamo ushuhuda ungetolewa kwa Ukweli wa wakati huu, au katika shule, ambazo zitawapa vijana wetu ushawishi bora zaidi, na ambao wanaweza kufunzwa kuwa wamishonari kwa ajili ya Mungu. {9T 57.4}
Ndugu na dada zangu, wekezeni mali zenu katika kuanzisha utume wa Kikristo, ambapo kwayo nuru ya kweli itang’aa, na kuvuta roho za watu kwa Mungu. Nafsi moja, iliyoongoka kweli, na kuwa mmishenari kwa ajili ya Mungu, itazivuta roho nyingine kwa Mwokozi. {9T 58.1}

Mungu Mwenyewe aliianzisha mipango ya kuiendeleza kazi Yake, na Yeye amewapa watu Wake mali za ziada, ili atakapoita kwa ajili ya msaada waweze kuitika kwa kusema: “Bwana mali Yako imepata mali nyingine-Shilingi yako, imeleta Shilingi nyingine!" {9T 58.2}

Iwapo wale ambao fedha za Mungu zimekabidhiwa kwao watakuwa waaminifu katika kuleta mali walizokopeshwa katika hazina ya Bwana, kazi Yake itaendelea kwa kasi sana. Roho nyingi zitavutwa kwa sababu ya Kweli, na siku ya kuja kwa Kristo itaharakishwa.Wanaume na wanawake wanapaswa kuletwa chini ya mvuto wa watenda kazi wenye moyo wote, wa Kweli, wenye bidii, wanaofanya kazi kwa ajili ya nafsi kama watu wanaopaswa kutoa hesabu. Wote wanaobatizwa katika kipimo cha roho ya kiutume watabidishwa kuwa wamishenari wa Mungu. Ikiwa watakuwa wakweli, wenye imani thabiti, ikiwa hawatamuuza Bwana wao kwa ajili ya faida, bali wakadumu kuukiri ukuu na uongozi wa mbingu, Mungu atatayarisha njia mbele yao na atawabariki sana. Yeye Atawasaidia kuuwakilisha wema Wake, upendo, na rehema. Na utukufu wa Bwana atakuwa thawabu yao. Kutakuwa na furaha katika nyua za mbinguni, na shangwe, safi, shangwe ya mbinguni, itaijaza

mioyo ya watendakazi. Ili kuokoa roho zinazoangamia watakuwa tayari kutumia na kutumiwa, na mioyo yao itajawa na upendo na shukrani. Uelewa na dhamiri ya uwepo wa Mungu utatakasa na kuinua uzoefu wao, ukiwatajirisha na kuwatia nguvu. Neema ya mbinguni itadhihirishwa katika kazi yao, katika ushindi unaopatikana katika kuzivuta roho kwa Kristo. {9T 58.3}

Hivyo kazi ya Mungu katika ulimwengu wetu inapaswa kuendelezwa mbele. Mawakili waaminifu wanapaswa kuweka fedha za Bwana katika hazina Yake, ili watendakazi wapelekwe sehemu zote za ulimwengu. Kanisa hapa chini ni la kumtumikia Mungu kwa kujinyima na kujinyima/kujitoa nafsi. Hivyo kazi inapaswa kuendelezwa mbele na ushindi mtukufu zaidi kushinda. {9T 59.1}

Upendo kwa roho zilizopotea ulimleta Kristo katika msalaba wa Kalvari. Upendo kwa roho utatuongoza sisi kwenye kujinyima na kujikana nafsi, kwa ajili ya kuokoa kile kilichopotea. Na pale wafuasi wa Kristo wanapoendelea kumrudishia Bwana kilicho Chake, wao hujikusanyia hazina ambayo watakuwa nayo watakaposikia Maneno haya: “Vema, mtumwa mwema na mwaminifu:. . . ingia katika furaha ya BWANA wako,” “ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele Yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, Naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu." Mathayo 25:21; Waebrania 12:2. Furaha ya kuona roho zilizookolewa milele itakuwa thawabu ya wote wanaofuata hatua za Mkombozi.{9T 59.2}
“Yeye asiyemwachilia Mwana Wake Mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja Naye?”Warumi 8:32. {9T 59.3}

Ilikuwa ni dhabihu ya gharama ambayo Bwana wa mbinguni aliitoa. Ukarimu wa mbingu ulichochea Kwake kina kisichoelezeka; haikuwezekana kwa Mungu kutoa zaidi. “Kwa maana jinsi hii aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye Yeye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” Yohana 3:16. Kwa nini shukrani zetu ni ndogo sana? Ni kama kiwimbi kidogo tu juu ya uso wa maji, ikilinganishwa na wimbi kubwa la upendo linabubujika kwetu kutoka kwa Baba.-{9T 59.4}

Ishara zinazotabiri ujio wa pili wa Kristo zinatimia haraka. Je,watu wataachwa katika ujinga wa tukio kubwa lililo mbele yao na kukutana na siku hiyo mbaya bila kujiandaa? Mbingu imefanya sadaka kamili kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu. Je, wale wanaodai kumpenda Mungu na kushika Amri Zake wawe wasiojali roho za watu? Hapana, hapana! hawawezi kuwa wazembe hivyo. {9T 60.1}

Kwa bidii isiyochoka wale ambao wameipokea nuru ya Ukweli wa leo wanapaswa kwenda kuitoa nuru hii kwa wale wanaeketi gizani. Kwa juhudi zilizowekwa wakfu, kwa kujinyima na kujikana nafsi, wanapaswa kufanya kazi kwa nguvu za Mungu

wa Israeli. Ujumbe huu unapaswa kupelekwa katika nchi za kigeni; ni wa kutoa katika miji na majiji ya nchi yetu. Wanadamu waliochoka na wenye kulemewa na mizigo wanatamani sana ujumbe wa Kweli utakaowapa pumziko na amani katika Kristo. Nani ataupeleka ujumbe kwa wale ambao hawajawahi kuusikia? Ni nani atatafuta furaha na utukufu wa Mungu kwa kuwavuta wenye dhambi miguuni Pake Yeye aliyetoa maisha Yake sadaka kwa kila nafsi? Ni nani atamwinua Mwokozi mbele ya watu kama “Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu?” Yohana 1:29. {9T 60.2}

## SEHEMU YA 2—MACHAPISHO KATIKA HUDUMA

*[Sehemu Ya Jambo Hili Ilichapishwa Kwanza Mwaka 1908.]*

"Bwana analitoa Neno: walitangazao ni jeshi kubwa.” Zaburi 68:11.

### SURA YA 6
### MACHAPISHO YETU

Kazi kubwa na ya ajabu ya ujumbe wa mwisho wa injili inapaswa sasa kuendelezwa kuliko ilivyowahi kutokea kabla. Ulimwengu unapaswa kupokea nuru

ya Ukweli kupitia huduma ya kueneza injili ya Neno katika vitabu vyetu na majarida. Machapisho yetu yanapaswa kuonyesha kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia. Ninalazimika kuziambia nyumba zetu za chapishaji: “Inueni kiwango, inueni juu zaidi. Utangazeni ujumbe wa malaika Yule wa tatu; ili upate kusikiwa na ulimwengu wote. Hebu na ionekane kuwa 'hawa ndio wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu.' Ufunuo 14:12. Acheni machapisho yetu yatoe ujumbe kama ushuhuda kwa ulimwengu wote." {9T 61.1}

Watendakazi wetu sasa wanapaswa kutiwa moyo kuweka kipaumbele chao cha kwanza kwenye vitabu vinavyohusu ushahidi wa imani yetu—vitabu Vinavyofundisha mafundisho ya Biblia, Mafunzo Makuu ya imani na ambayo yatatayarisha watu kusimama katika nyakati za majaribu zilizo mbele yetu. Baada ya kuwaleta watu kwenye nuru ya Ukweli kwa kazi ya sala katika mafundisho ya Biblia, na kupitia matumizi yenye hekima ya machapisho yetu, tunapaswa kuwafundisha kuwa watendakazi katika Neno na mafundisho ya imani. Tunapaswa kuwahimiza kusambaza vitabu vinavyohusisha Masomo ya Biblia--vitabu ambavyo mafundisho Yake yatawatayarisha watu kusimama, wakiwa wamefungwa viuno kwa Kweli na taa zao zikiwa zinawaka. {9T 61.2}

Tumekuwa tukilala, kama ilivyokuwa, ukizingatia kazi inayopaswa kutimizwa kwa kusambaza machapisho yaliyotayarishwa vyema. Hebu sasa, kwa matumizi ya busara ya majarida na vitabu, lihubiri Neno kwa nguvu iliyodhamiriwa, ili ulimwengu upate kuuelewa ujumbe ambao Kristo alimpa Yohana kwenye Kisiwa cha Patmo. Hebu kila akili ya binadamu ambaye analikiri Jina la Kristo ashuhudie: "Mwisho wa mambo yote umekaribia; jiandae kukutana na Mungu wako." {9T 61.3}

Machapisho yetu yanapaswa kwenda kila mahali. Hebu yatolewe kwa lugha nyingi. Ujumbe wa Malaika wa tatu unapaswa kutolewa kupitia njia hii na kupitia kwa Mwalimu aliye hai. Ninyi mnaouamini Ukweli wa leo, amkeni. Ni jukumu lenu sasa kuleta mali zote zinazowezekana kusaidia wale wanaoulewa Ukweli ili kuutangaza. Sehemu ya pesa zinazopatikana kutokana na mauzo ya machapisho yetu inapasa kutumiwa kuongeza miundombinu kwa ajili ya kuzalisha machapisho mengi zaidi yatakayofungua macho ya vipofu na kuvunja/kukatua ardhi ngumu ndani ya mioyo. {9T 62.1}

Kuna hatari ya kuingia katika biashara na kujisokota-sokota na kutumbukia katika biashara ya kidunia kiasi kwamba Kweli ya Neno la Mungu katika usafi na nguvu zake haitaletwa katika maisha. Kupenda biashara na faida kunazidi kuenea. Ndugu zangu,hebu roho zenu ziongoke kweli kweli. Kama kuna wakati tulihitaji kuuelewa wajibu wetu, ni sasa, Ukweli unapoanguka njiani, basi haki haiwezi kuingia. Shetani ameshuka na nguvu nyingi kufanya kazi kwa udanganyifu wote wa udhalimu kwa hao wanaopotea; na kila kitu kinachoweza kupepetwa kitapepetwa, na vile visivyoweza kupepetwa vitabaki. Bwana anakuja upesi sana, na tunaelekea kuingia kwenye matukio ya majanga. Mawakala wa kishetani,

ingawa hawaonekani, wanafanya kazi ya kuharibu maisha ya mwanadamu. Lakini ikiwa maisha yetu yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu, tutaona neema Yake na wokovu. Kristo anakuja kusimamisha ufalme Wake duniani. Hebu ndimi zetu litakaswe na zitumike kumtukuza. Hebu tufanye kazi sasa kuliko tulivyowahi kufanya kazi hapo awali. Tunahimizwa "kuwa tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa.” 2 Timotheo 4:2.Tunapaswa kuwa tayari kwa ajili ya kuuwasilisha Kweli. Tunapaswa kuendeleza kila fursa ya kuvuta roho kwa Kristo. {9T 62.2}

Kama watu tunapaswa kuongoka, maisha yetu yakitakaswa ili kuitangaza Kweli kama ilivyo katika Yesu. Katika kazi ya kusambaza machapisho yetu, tunaweza kusema juu ya upendo wa Mwokozi kutoka kwa moyo mchangamfu na unaodunda. Mungu pekee Ndiye Mwenye uwezo wa kusamehe dhambi; ikiwa hatusemi ujumbe huu kwa wasioongoka, uzembe wetu katika hili utaweza kuthibitisha uharibifu wao. Kweli za Biblia zenye baraka na zinazookoa nafsi zimechapishwa katika kurasa zetu. Kuna wengi ambao wanaweza kusaidia katika kazi ya kuuza majarida yetu. Bwana anatuita sisi sote kutafuta kuokoa roho zinazopotea. Shetani yuko kazini kuwadanganya hata walio wateule, na sasa ni wakati wetu wa kufanya kazi kwa bidii, na tukikesha-kuwa macho. Vitabu na vijizuu vyetu, na machapisho yote yanapaswa kuletwa mbele za watu ili wavione; injili ya Ukweli wa leo inapaswa ipelekwe kwenye miji yetu bila kuchelewa. Je, hatutaamka kwa ajili majukumu yetu? {9T 63.1}

Ikiwa tunayafanya maisha na mafundisho ya Kristo kuwa somo letu, kila tukio linalopita litatoa fungu kwa ajili mazungumzo ya kuvutia. Ilikuwa hivyo Mwokozi alihubiri injili katika njia kuu na vichochoroni; na alipokuwa akinena, lile kundi dogo lililomsikiliza likaendelea kujaa na kuwa kundi kubwa. Wainjilisti wa siku hizi wanapaswa kuwa watenda kazi pamoja na Kristo. Hawa, hakika kama vile wanafunzi wa kwanza, wana uhakikisho: "Nimepewa Mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu: na kuwafundisha kuyashika yote yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Mathayo 28:18-20. {9T 63.2}

Kazi inayopaswa kufanywa na watu wa Mungu imetamkwa katika Maneno ya uvuvio: “Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wako, atakayeitengeneza njia yako. Sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito Yake.” Marko 1:2,3. “Tazama mtumishi nimtegemezaye; mteule Wangu, ambaye nafsi Yangu imependezwa Naye; Nimetia Roho Yangu juu Yake. Atawatolea hukumu mataifa. . . . Hatazimia wala hatakata tamaa hata atakapoweka hukumu duniani; na visiwa vitaingojea sheria Yake." Isaya 42:1-4. {9T 64.1}

Mungu anawaalika watu wote kwenye uchunguzi kamili wa madai ya sheria Yake. Neno Lake ni takatifu na halina kikomo. Sababu ya Ukweli ni kutoka kama taa iwakayo. Ujifunzaji na usomaji wa kina wa Neno la Mungu utafunua Ukweli. Dhambi na makosa hayatadumishwa, lakini sheria ya Mungu itathibitishwa. "Mungu Bwana anena, Yeye aliyeziumba mbingu, na kuzitandaza; Yeye aliyeitandaza nchi, na mazao Yake; Yeye awapaye pumzi watu walio juu Yake, Yeye awapaye roho wao waendao ndani Yake. Mimi, BWANA, nimekuita katika haki, Nami nitakushika mkono, na kukulinda, na kutunza. Na kukutoa uwe agano la watu, na nuru ya Mataifa; kuyafunua macho ya vipofu, kuwatoa gerezani waliofungwa, kuwatoa wale walioketi gizani watoke katika nyumba za kufungwa." 42: 5-7.  Wakristo wanapaswa kuitafuta nuru yao kutoka katika Neno la Mungu na kisha kwa imani kwenda mbele kuwapa nuru hiyo wale walioketi gizani. {9T 64.2}
Sanitarium, California, Mei 24, 1908. {9T 64.3}

## SURA YA 7
## SAMBAZA MAJARIDA

Katika Usiku wa Machi 2, 1907, nilifunuliwa mambo mengi kuhusu thamani ya machapisho yetu juu ya Ukweli wa leo na juhudi ndogo ambazo hufanywa na ndugu na dada zetu katika makanisa kwa kupanua usambazaji wake. {9T 65.1}

Nimeonyeshwa tena na tena kwamba nyumba zetu za uchapaji sasa zinapaswa kujikita daima katika uchapaji wa nuru na Kweli. Huu ni wakati wa giza la kiroho katika makanisa ya ulimwengu. Ujinga wa mambo ya kiroho na maarifa ya Mungu, umemficha Mungu na Kweli kutoonekana. Nguvu za uovu zinajikusanya kwa nguvu. Shetani huwasifu watendakazi wenzake kwa udanganyifu, wale ambao watafanya kazi ambayo itauteka ulimwengu. Wakati kufanya kazi nusu-nusu kumekuja juu ya kanisa, Shetani na majeshi yake wanafanya kazi kwa bidii sana. Makanisa yanayodai kuwa ya Kikristo hayauongoi ulimwengu kwa Kristo; kwani wao wenyewe wamepotoshwa na ubinafsi na kiburi, na wanahitaji kuhisi nguvu za Mungu inayoongoa katikati yao kabla ya kuwaongoza wengine kwenye kiwango safi au cha juu zaidi. {9T 65.2}

•

## Uzoefu Unaotia Moyo

Alasiri ya Machi 2, nilitumia kushauriana pamoja na Ndugu na Dada S. N. Haskell, tukijadili juu ya kazi ya huko Oakland na mipango yao ya kwenda Mashariki kutumia muda huko Lancaster Kusini. Baada ya mizunguko yetu nilikuwa nimechoka na kupumzika mapema. Nilikuwa na ugonjwa wa baridi yabisi katika upande wangu wa kushoto na sikuweza kupumzika kwa sababu ya maumivu. Niligeuka kutoka upande hadi upande, nikijaribu kupata afueni kutoka katika mateso. Kulikuwa na maumivu moyoni mwangu ambayo hayakunipa uzuri wowote. Hatimaye nililala. {9T 65.3}

Karibu saa tatu na nusu usiku, nilijaribu kujigeuza, na nilipofanya hivyo, nikagundua kuwa mwili wangu ulikuwa hauna maumivu kabisa. Nilipogeuka kutoka upande hadi upande, na kusogeza mikono yangu, niliona ikisogea kwa uhuru wa ajabu na wepesi ambao siwezi kuuelezea. Chumba kilijazwa na mwanga, mzuri zaidi, laini, nuru ya bluu/samawati, na nilionekana kuwa katika mikono ya viumbe vya mbinguni. {9T 65.4}

Nuru hii ya kipekee niliiona hapo awali katika nyakati za baraka maalum, lakini wakati huu ilikuwa tofauti zaidi, ya kuvutia zaidi, na niliihisi amani, amani iliyojaa na tele, iliyosheheni hakuna maneno yanayoweza kuielezea. Nilijiinua katika mkao wa kuketi, nikaona kwamba nimezungukwa na wingu angavu, jeupe kama theluji, na kingo zake ambazo zilikuwa na rangi ya waridi (pinki). Muziki laini na mtamu zaidi ulikuwa ukilijaza anga, na nikatambua muziki huo kuwa ni uimbaji wa malaika. Ndipo Sauti ikanena nami, ikisema: “Usiogope, Mimi ni Mwokozi wako. Malaika watakatifu wako kwa ajili yako." {9T 66.1}

"Basi hii ni mbingu," nilisema, "na sasa ninaweza kuwa katika kupumzika. Sitakuwa na ujumbe zaidi wa kubeba, wala sitazungumzwa kwa upotoshwaji tena na kuuvumilia. Kila kitu kitakuwa rahisi sasa, na nitafurahia amani na pumziko. Ah, ni amani isiyoelezeka huijaza nafsi yangu! Kweli hapa ni mbinguni? Je, mimi ni mmoja wa watoto wadogo wa Mungu? Na je, nitakuwa nina amani hii siku zote?" {9T 66.2}

Sauti ikajibu: "Kazi yako bado haijakamilika." {9T 66.3}

Nililala tena, na nilipoamka niliusikia muziki, na nilitaka kuuimba. Kisha mtu akapita mlangoni pangu, na nilijiuliza ikiwa mtu huyo aliuona mwanga. Baada ya muda nuru ilipotea, lakini amani ilibakia. {9T 66.4}

Baada ya muda nililala tena. Wakati huu nilionekana kuwa katika mkutano wa baraza ambapo kazi yetu ya vitabu ilikuwa inajadiliwa. Kulikuwa na idadi ya ndugu zetu waliokuwepo, viongozi katika kazi yetu, na Mzee Haskell na mkewe walikuwa

pale wakishauriana pamoja na ndugu kuhusu usambazaji wa vitabu, vipeperushi, na vijizuu vyetu. {9T 66.5}

Mzee Haskell alikuwa akiwasilisha sababu zenye nguvu kwa nini vitabu ambavyo vina maarifa ambayo yamewasilishwa kwa Dada White--vitabu vyenye ujumbe maalumu wa kwenda ulimwenguni wakati huu wa sasa--vinapaswa kusambazwa kwa bure. "Kwa nini," aliuliza, "watu wetu hawathamini na kusambaza kwa upana zaidi vitabu vinavyobeba na sifa za kimbingu? Kwa nini hakuna umaalumu uliofanywa juu ya vitabu vyenye maonyo kuhusu kazi ya Shetani? Kwa nini hatutoi juhudi kubwa katika kusambaza vitabu vinavyoonyesha mipango ya Shetani ya kupingana na kazi ya Mungu, ambavyo vinafichua mipango na kuweka wazi udanganyifu wake? Maovu ya kimaadili ya udanganyifu wake yanapaswa kuondolewa kwa kuyafungua macho ya watu ili watambue hali na hatari za nyakati zetu; ili wafanye bidii ya kumshikilia Kristo na haki Yake kwa imani na uadilifu." {9T 67.1}

Mjumbe kutoka mbinguni alisimama katikati yetu, na alizungumza maneno ya onyo na maagizo. Alitufanya tuelewe wazi kwamba injili ya ufalme ni ujumbe ambao kwa huo ulimwengu unaangamia kwa kuukosa, na kwamba ujumbe huu, kama ulivyo katika machapisho yetu ambayo tayari yamechapishwa na yale ambayo yako tayari kutolewa baadae, haya yanapaswa kusambazwa kati ya watu walio karibu na walio mbali. {9T 67.2}

### Hatari katika utafiti wa Kudhania-dhania

Nuru ya Ukweli ambayo Mungu huipanga itakuja kwa watu wa ulimwengu kwa wakati huu si ile ambayo watu wa elimu ya ulimwengu wanatafuta kutoa, kwani watu hawa katika utafiti wao mara nyingi hufikia hitimisho potofu na katika utafiti wao wengi wa waandishi huhamasishwa na nadharia zenye asili ya kishetani. Shetani, akiwa amevalia vazi la malaika wa nuru, huwasilisha masomo katika akili ya mwanadamu ambayo yanaonekana kuvutia sana na ambayo yamejaa mafumbo na siri za kisayansi. Kwa kuyachunguza masomo haya, watu wanaongozwa kukubali mahitimisho potofu na kuungana pamoja na roho zidanganyazo katika kazi ya kuibua nadharia mpya zinazoongoza kutoka kwenye Kweli. {9T67.3}

Kuna hatari kwamba hisia za uwongo zilizoonyeshwa katika vitabu ambavyo wamekuwa wakisoma vinaweza wakati mwingine kuunganishwa wachungaji/wahudumu wetu, walimu, na wahariri kwa hoja zao, hotuba, na machapisho, chini ya imani kwamba viko sawa katika kanuni na mafundisho ya Roho wa Kweli. Kitabu cha Hekalu linaloishi (*Living Temple*) ni kielelezo cha kazi hii, ambayo mwandishi (Kellog) wake alitangaza katika uungaji mkono wake kwamba ni mafundisho yalikuwa sawa na yale yaliyopatikana katika maandishi ya Bibi White. Tena na tena tutaitwa kukutana na ushawishi wa wanadamu

wanaosoma sayansi zenye asili ya kishetani, ambazo kupitia hizo Shetani anatumiwa kufanya kazi ili kusema katika nadharia au maneno yao kutokuwepo kwa nafsi ya Mungu na Kristo, au kutokuwa na Umuhimu wa Mungu. {9T 68.1}

Baba na Mwana kila mmoja ana nafsi. Kristo alitangaza: "Mimi na Baba Yangu tu umoja." Hata hivyo alikuwa Mwana wa Mungu aliyekuja ulimwenguni katika umbo la mwanadamu. Akiweka kando vazi Lake la kifalme na taji ya kifalme, aliuvisha Uungu Wake kwa ubinadamu, ili ubinadamu kupitia dhabihu Yake isiyo na kikomo uwe washirika wa tabia ya Mbingu na kuepuka uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. {9T 68.2}

Kristo alijaribiwa katika kila jambo kama vile mwanadamu ajaribiwavyo, lakini hakuna wakati wowote alileta kwa mjaribu mashtaka ya kashfa. Kwa kila jaribu aliwasilisha Neno la Bwana. “Imeandikwa” ilikuwa silaha Yake isiyoshindwa kamwe. Sisi, kama wawakilishi wa Kristo, tunapaswa kukutana na kila msukumo wa adui kwa Neno la Mungu aliye hai. Kamwe tusijiruhusu kuufuata mkondo wa nyoka kwa kutumia hoja zake za kisayansi. Shetani hawezi kamwe kupata faida kwa mtoto wa Mungu ambaye analitegemea Neno la Mungu kama ulinzi Wake. {9T 68.3}

Mshauri wetu alikazia sana akilini mwetu kwamba ni lazima watu wa Mungu wanaozitii amri kutakaswa kwa njia ya Ukweli na Ukweli huo lazima upewe nafasi ya kwanza. Hatupaswi kusahau kwamba Shetani bado anaishi kutumia nguvu zake za udanganyifu kupitia sayansi ya uwongo. {9T 69.1}

Kristo alikuwa Mkuu wa mbinguni, Mkuu wa uzima; lakini alijinyenyekeza kama mwanadamu na akawa mtiifu kwa kila sheria ya Mungu. Alipita juu ya ardhi ambayo kila mtu anayelibeba Jina Lake, ni lazima aikanyage na kutoka katika Jaribu Lake akiwa msafi na asiyechafuliwa na dhambi. Yeye Alikuwa kielelezo chetu katika mambo yote. {9T 69.2}

Ujio wa kwanza wa Kristo na maisha Yake ya huduma haujifunzwi jinsi inavyopaswa. Maisha Yake yalikuwa yale ya kujinyima, ambapo Kweli katika sifa Zake zote bora ilioneshwa. Aliishi kuubariki ubinadamu kwa kila Neno zuri na tendo. {9T 69.3}

## Heshima ya Kazi ya Vitabu

Kazi ya utengenezaji wa vitabu ni kazi kubwa na nzuri; lakini mara zote haijasimama katika nafasi ya juu na takatifu ambayo Mungu aliikusudia ichukue, kwa sababu ubinafsi umeunganishwa katika kazi kwa baadhi ambao wamejihusisha nayo. Kazi ya vitabu inapaswa kuwa njia ya haraka ya kutoa nuru takatifu ya Ukweli wa leo kwa ulimwengu. Machapisho yanayotoka katika nyumba

zetu za uchapaji leo yanapaswa kuwa ya aina hii, kuwa ya kuimarisha kila pini/kiunganishi na nguzo ya imani iliyosimamishwa kwa Neno la Mungu na kwa mafunuo ya Roho Wake. {9T 69.4}

Ukweli ambao Mungu ameutoa kwa watu Wake katika siku hizi za mwisho unapaswa kuwaweka waumini imara wakati hali ya kuingia kanisani kwa wale wanaowasilisha nadharia za uongo inapokuja. Ukweli ambao umesimama imara dhidi ya mashambulizi ya adui kwa zaidi ya nusu karne lazima bado uwe tumaini , ujasiri na faraja ya watu wa Mungu. {9T 69.5}

Ushahidi wetu kwa watu wasioukiri Ukweli kwamba tuna Ukweli wa Neno la Mungu utatolewa katika maisha ya kujinyima-kujikan nafsi. Hatupaswi kufanya mzaha kwa imani yetu, lakini daima tuweke mbele yetu mfano Wake Yeye ambaye, ingawa alikuwa Mkuu wa mbinguni, aliinama kwa maisha ya kujinyima, na kujikana nafsi na kujitoa dhabihu ili kuthibitisha haki ya Neno la Baba Yake. Hebu kila mmoja wetu aamue kufanya vyema awezavyo, ili nuru ya matendo yetu mema iweze kuangaza kwa ulimwengu. {9T 70.1}

## Umoja Unaoendelea

Maelewano kamili yanapaswa kuwepo katika mipango iliyowekwa kwa ajili ya uchapishaji wa vitabu vyetu na majarida, kwamba nuru iliyomo inaweza kubebwa kwa haraka kila kwenye makanisa ya majina (yenye mafundisho yasiyo ya kweli) na kwa ulimwengu wote. Mengi zaidi yalipaswa kukamiliswa katika uuzwaji wa vitabu vyetu kuliko tunayoona yametimizwa sasa. {9T 70.2}

Wachungaji wetu wanapaswa kuwasihi washiriki wa kanisa kuuacha Ukweli ushinde. "Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, na utukufu wa Bwana umekuzukia. Maana, tazama, giza litaifunika dunia, na giza kuu litazifunika kabila za watu; Bali BWANA atakuzukia Wewe, na utukufu Wake utaonekana juu yako. Na mataifa wataijilia nuru yako, na wafalme kuujia mwanga wa kuzuka kwako." Isaya 60:1-3. Umoja na upendo vitatimiza mambo ya ajabu kwa waumini. Je, makanisa yetu hayataamka na kuutoa ujumbe wa onyo la mwisho kwa ulimwengu? {9T 70.3}

## Vitabu vyetu vya Msaada

Vielelezo vya maisha ya Kristo (*Christ's Object Lesson*) ni kitabu kinachojieleza chenyewe, na kimetimiza kazi nzuri. Kama kilivyokuwa kikiuzwa, na kusudi la mauzo yake limeelezwa, fedha imepokelewa ambayo imeondoa deni la shule zetu. Lakini zaidi ya hili, wengi kwa kukisoma kitabu wamebarikiwa na masomo yake ya Ukweli, na wengine wengi watabarikiwa kwa kukisoma. {9T 70.4}

Kitabu Huduma ya Uponyaji (Ministry of Healing) kinaweza kufanya kazi ileile kwenye huduma zetu za sanitariamu na taasisi za afya ambayo Vielelezo vya maisha ya Kristo (Christ's Object Lesson) kimefanya kwa shule zetu. Kitabu hiki kimejumuisha hekima za Tabibu Mkuu. Kwangu imekuwa ni upendeleo wa thamani kuchangia kazi yangu ya vitabu hivi kwa ajili ya kazi ya Mungu. Katika siku zijazo kunapaswa kuwa na juhudi zilizopangwa vizuri na za kudumu ili kuongeza mauzo yake. {9T 71.1}

## Kuondoa Madeni

Mungu hukusudia kwamba tutajifunza masomo kutokana na kushindwa kwa wakati uliopita. Haipendezi Kwake kuwepo na madeni kwenye taasisi Zake. Tumefikia wakati ambao lazima tujipe tabia kazini ya kukataa kujenga majengo makubwa na ya gharama kubwa. Hatupaswi kuiga makosa ya zamani na kuwa zaidi na zaidi kushiriki katika madeni. Ni afadhali tujitahidi kuondoa deni ambalo bado linabaki kwenye taasisi zetu. Makanisa yetu yanaweza kusaidia katika jambo hili kama yatawiwa. Washiriki ambao`Bwana amewapa mali wanaweza kuwekeza fedha zao katika kusudi hili bila riba au kwa kiwango cha chini cha riba, na kwa matoleo yao ya hiari wanaweza kusaidia kazi. Bwana hukuomba kurudisha Kwake kwa moyo mkunjufu sehemu ya mali aliyokukopesha wewe, na hivyo kuwa mawakili na wasambazaji Wake. {9T 71.2}

## Mtazamo Mwingine wa Kazi ya Kitabu

Baada ya hapo tulikuwa katika mikutano ya makambi na katika mikutano mikubwa katika makanisa yetu, ambapo wachungaji/wahudumu waliwasilisha kwa uwazi hatari za nyakati tunazoishi na umuhimu mkubwa wa kufanya haraka katika usambazaji wa machapisho yetu. Kwa kuitikia hoja hizi ndugu na dada walijitokeza na kununua vitabu vingi. Wengine walichukua vichache, na wengine walinunua vingi. Wengi wa wanunuzi walilipia vitabu walivyochukua. Wachache walipanga kulipa baadaye.{9T 71.3}

Kwa sababu vitabu vilikuwa vikiuzwa kwa bei ya chini, vingine vikipunguzwa hasa kwa ajili ya tukio hilo, vingi vilinunuliwa, na vingine na watu wasio wa imani yetu. Walisema: “Lazima itakuwa vitabu hivi vina ujumbe kwa ajili yetu. Watu hawa wako tayari kujitolea ili tuwe navyo, nasi tutajinunulia kwa ajili yetu na marafiki zetu." {9T 72.1}

Lakini kutoridhika kulionyeshwa na baadhi ya watu wetu wenyewe. Mmoja alisema: "Lazima zuio liwekwe kwa hii kazi, la sivyo biashara yetu itaharibika.” Ndugu mmoja alipokuwa akibeba vitabu vingi, mwinjilisti wa vitabu akaweka mkono wake juu ya mkono wake na kusema: "Ndugu yangu, unafanya nini na hivi vitabu vingi?" Kisha nilisikia sauti ya Mshauri wetu ikisema: “Msiwakataze hawa watu. Hii ndiyo kazi inayopaswa kufanywa. Mwisho uko karibu. Tayari muda

mwingi umekwishapotea, ambao vitabu hivi vilipaswa kuwa katika mzunguko ili vitawanyike kote. Viuzeni mbali na karibu. Vitawanyeni kama majani ya wakati wa kupukutisha majani yote (Fall Season). Kazi hii ni ya kuendelea bila makatazo ya mtu yeyote. Nafsi zinaangamia nje ya Kristo. Hebu watu waonywe juu ya kutokea Kwake upesi katika mawingu ya mbinguni." {9T 72.2}
Baadhi ya watendakazi waliendelea kuonekana na huzuni nyingi. Mmoja alikuwa akilia na kusema: “Hawa wanafanya kazi ya uchapishaji isivyo haki kwa kununua vitabu hivi kwa bei ya chini sana; Isitoshe, kazi hii hutunyima baadhi ya mapato ambayo kwayo kazi yetu ingedumishwa." Sauti ikajibu: "Ninyi hampati hasara. Watendakazi hawa wanaochukua vitabu kwa bei iliyopunguzwa hawakuweza kupata mauzo yaliyo tayari kwa ajili yao isipokuwa kwa kile kiitwacho “kujitoa dhabihu”. Wengi sasa wananunua vitabu kwa ajili ya marafiki zao na wao wenyewe ambao vinginevyo wasingefikiria kununua." {9T 72.3}

## Tahadhari

Kisha agizo likatolewa kwa Mzee Haskell kwamba katika mahangaiko yake ya kuwapa watu Ukweli wa thamani uliomo katika vitabu vyake, katika shauku yake kwamba wote wahisi kwamba vitabu hivyo vina thamani zaidi kuliko vinavyogharimu, na kwamba wote watiwe moyo kuvisambaza kwa upana, alikuwa akiuza vitabu vyake kwa unafuu sana, na hivyo kuufanya mzigo wake mwenyewe kuwa mzito zaidi. {9T 73.1}

Mshauri wetu alisema: “Vitabu viuzwe kwa namna ambayo mwandishi hataachwa mikono mitupu na kwamba nyumba ya uchapishaji itakuwa na ukingo ufaao wa faida, ili iwe na fedha ya kuendeleza kazi yake mbele ." {9T 73.2}

## Mfano wetu wa kujifunza

“Ufalme wa mbinguni umefanana na mtu mwenye nyumba,”Kristo alitangaza,“aliyetoka asubuhi na mapema ili kuajiri wakulima awapeleke katika shamba lake la mizabibu. Naye alipokwisha kupatana na wakulima kuwapa kutwa dinari, aliwapeleka katika shamba Lake la mizabibu. Akatoka mnamo saa tatu asubuhi, akaona wengine wamesimama sokoni bila kazi, akawaambia; Enendeni nanyi katika shamba la mizabibu na iliyo haki nitawapa. Wakaenda. {9T 73.3}

"Akatoka tena mnamo saa sita mchana na saa tisa mchana, akafanya vile vile. Hata kama saa kumi na moja jioni akatoka akakuta wengine wamesimama, akawaambia, Mbona mmesimama hapa mchana kutwa bila kazi? Wakamwambia, kwa sababu hakuna mtu aliyetuajiri. Akawaambia, Nendeni nanyi katika shamba la mizabibu; chochote kilicho haki, hicho mtapata. Kulipokuchwa, Yule bwana wa

shamba la mizabibu akamwambia msimamizi wake, Waite wakulima, na uwalipe ujira wao, ukianzia wa mwisho hata wa kwanza. Na walipokuja wale wa saa kumi na moja jioni, wakapokea kila mtu dinari. {9T 73.4}

“Lakini wale wa kwanza walipokuja, walidhani kwamba watapokea zaidi; na hao pia`wakapokea kila mtu dinari. Basi wakiisha kuipokea, wakamnung'unikia mwenye nyumba, wakisema, Hao wa mwisho wametenda kazi saa moja tu, nawe umewasawazisha na sisi tuliostahimili taabu na hari za mchana kutwa. Naye akamjibu mmoja wao, akamwambia, Rafiki, sikudhulumu, Je, hukupatana nami kwa dinari? Chukua iliyo yako, uende zako; napenda kumpa huyu wa mwisho sawa na wewe. Si halali kwangu kutumia vilivyo vyangu kama nipendavyo? Au, jicho lako limekuwa ovu kwa Mimi kuwa mwema? Vivyo hivyo wa mwisho watakuwa wa kwanza, na wa kwanza watakuwa wa mwisho; kwa maana walioitwa ni wengi, lakini wateule wachache." Mathayo 20:1-16. {9T 74.1}

Watabarikiwa kwa malipo ya neema wale ambao wamemfanyia Mungu kazi katika usahili wa imani.na upendo. Thamani ya utumishi kwa Mungu inapimwa kwa roho iliyojitoa, kuliko kupimwa kwa urefu wa muda uliotumika katika kazi.{9T 74.2}

## Nuru kwa Wote

Nuru kwa Wote Ni shauku yangu sana, kwamba nuru iliyomo katika vitabu vyangu itakwenda kwa kila nafsi iwezekanavyo, kwani Mungu ameutuma ujumbe kwa wote. Vitabu hivi vina masomo ya thamani katika uzoefu wa Kikristo. Nisingethubutu kukataza vitabu hivi viuzwe kwa matukio maalum kwa bei ya chini, nisije nikazuia usomaji wa vitabu, na hivyo kuiondoa nuru kutoka kwa nafsi fulani ambayo inngeweza kuongoka kuja kwenye Kweli. Sina makatazo ya kuweka kwenye kazi ya kusambaza vitabu vyetu. Hebu nuru iwekwe juu ya kinara, ili iwaangazie wote waliomo ndani ya nyumba. {9T 74.3}

## Somo katika Biashara

“Yesu akaingia ndani ya hekalu la Mungu, akawafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni; akazipindua meza za wabadili fedha, na viti vyao waliokuwa wakiuza njiwa, akawaambia, Imeandikwa, Nyumba Yangu itaitwa nyumba ya sala; bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi. {9T 75.1}

“Na vipofu na viwete wakamwendea mle hekaluni, akawaponya. Lakini wakuu wa makuhani na waandishi walipoyaona maajabu aliyoyafanya, na watoto waliopaza sauti zao hekaluni, wakisema, Hosana, Mwana wa Daudi! Walikasirika, wakamwambia, wasikia hawa wasemavyo? Yesu akawaambia, Naam; hamkupata kusoma, Kwa vinywa vya watoto wachanga na wanyonyao umekamilisha sifa?”

Mathayo 21:12-16. {9T 75.2}

Sanitarium, California,
Mei 4, 1908.

Jambo moja ambalo halipaswi kusahaulika kamwe na watendakazi wetu ni kwamba Bwana Yesu Kristo Ndiye kiongozi/mkurugenzi wetu mkuu. Yeye Ameueleza mpango ambao kwa huo shule zinaweza kuondolewa kwenye madeni yao, na hatathibitisha mambo ya wale wanauweka mpango huu kando kwa kukosa kuuamini katika mafanikio yake. Wakati watu Wake watapokuja kwa umoja kusaidia kazi Yake duniani, hakuna jambo jema ambalo Mungu ameliahidi litazuiliwa kwao. {9T 75.3}

## SURA YA 8
## MTAZAMO MPANA

Katika kuiendeleza mbele kazi ya Bwana nyumbani na nje ya nchi, wale walio katika madaraka wanapaswa kupanga kwa hekima, ili kufanya matumizi bora ya rasimali-watu na mali. Mzigo wa kuendeleza kazi katika maeneo mengi ya kigeni lazima kwa kiasi kikubwa kubebwa na konferensi zetu katika nchini. Konferensi hizi zinapaswa kuwa na mali za kusaidia katika kufungua maeneo mapya, ambapo Kweli zithibitishazo za ujumbe wa malaika wa tatu hazijawahi kupenya. Ndani ya miaka michache iliyopita, milango imefunguliwa kama kwa muujiza; na wanaume na wanawake wanahitajika kuingia katika milango hii na kuanza kazi ya dhati na bidii kwa ajili ya wokovu wa roho za watu. {9T 76.1}

Taasisi zetu za elimu zinaweza kufanya mengi kufikia mahitaji ya watendakazi waliofunzwa kwa ajili ya haya maeneo ya kiutume. Mipango ya busara inapaswa kuwekwa ili kuimarisha kazi inayofanywa katika vituo vyetu vya mafunzo. Masomo yanapaswa kutolewa kwa mbinu bora za kuwastahilisha vijana wa kiume na wa kike waliojitoa wakfu kuubeba wajibu na kuleta roho kwa Kristo. Wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuwafikia watu na jinsi ya kuuwasilisha ujumbe wa malaika wa tatu kwa njia ya kuvutia. Na katika usimamizi wa masuala ya fedha, wafundishwe masomo yatakayowasaidia pale watakapopelekwa katika maeneo

yaliyotengwa ambako ni lazima watakabiliwa na ufukara mwingi na watajizoeza kuwa wachumi zaidi. {9T 76.2}

Bwana ameanzisha mpango ambapo wengi wa wanafunzi katika shule zetu wanaweza kujifunza masomo ya vitendo yanayohitajika kufanikiwa katika maisha ya baadaye. Yeye Amewapa upendeleo wa kushugulikia vitabu vya thamani ambavyo vimetolewa kwa ajili ya kuendeleza kazi yetu ya elimu na kazi ya sanitariamu.
Katika kitendo cha kushughulika na vitabu hivi, vijana watakutana na uzoefu mwingi ambao utawafundisha jinsi ya kukabiliana na matatizo ambayo yanawangoja katika maeneo ya mbali na nje. Wakati wa maisha yao ya shule, kadri wavipitiavyo vitabu hivi, wengi wanaweza kujifunza jinsi ya kuzungumza na watu kwa adabu na jinsi ya kutumia busara katika kuzungumza nao juu ya mambo mbalimbali ya Ukweli wa leo. Na kadri wanavyokutana na kiwango cha mafanikio kifedha, wengine watajifunza masomo ya utafutaji na utumiaji pesa kwa uangalifu, kubana matumizi na uchumi, ambayo yatakuwa na faida kubwa kwao wanapotumwa kama wamishenari. {9T 76.3}

Wanafunzi wanaofanya kazi ya kuuza Vitabu vya Vielelezo vya Kristo (Christ's Object Lessons) na cha Huduma ya Uponyaji (Ministry of Healing) watahitaji kujifunza kitabu wanachotarajia kuuza. Huku wakizizoeza akili zao na mada ya kitabu mkononi mwao na kujitahidi kuishi mafundisho yake watakua katika maarifa na nguvu za kiroho. Ujumbe katika vitabu hivi una nuru ambayo Mungu amenifunulia ili niupatie ulimwengu. Walimu katika shule zetu wanapaswa kuwahimiza wanafunzi kufanya usomaji wa makini wa kila sura. Wanapaswa kufundisha Kweli hizi kwa wanafunzi wao na kutafuta kuwatia moyo vijana kwa kupenda mawazo ya thamani ambayo Bwana ametukabidhi ili kuwasilisha kwa ulimwengu. {9T 77.1}

Hivyo maandalizi ya kushughulikia vitabu hivi, na uzoefu wa kila siku uliopatikana wakati wa kuvileta mbele za watu, vitathibitisha usomi wa thamani sana kwa wale wanaoshiriki katika juhudi ya aina hii. Chini ya baraka za Mungu vijana watapata stahiki kwa ajili ya huduma katika shamba la mizabibu la Bwana.{9T 77.2}

Kuna kazi maalum ya kufanywa na vijanawanaobeba majukumu katika makanisa mahalia katika konferensi zote kwa ajili ya vijana wetu. Wakati maofisa wa kanisa wanapoona vijana wenye shauku kupata stahiki wenyewe kwa manufaa katika utumishi wa Bwana, lakini ambao wazazi wao hawawezi kuwapeleka shule, wana wajibu wa kufanya katika kujifunza jinsi ya kutoa msaada na kutia moyo. Wanapaswa kufanya shauri na wazazi na vijana, na kuungana katika kupanga kwa busara. Huenda baadhi ya vijana wakafaa zaidi kushiriki katika kazi ya umishenari wa nyumbani. Kuna eneo pana la manufaa katika usambazaji wa vitabu vyetu na katika kuleta ujumbe wa malaika wa tatu kwenye umakini wa marafiki na majirani. Vijana wengine wahimizwe kuingia katika kazi ya kutembea na kuuza vitabu vyetu

vikubwa. Wengine wanaweza kuwa na sifa zinazoweza kuwafanya wasaidizi muhimu katika taasisi zetu. Na katika hali nyingi, ikiwa vijana wenye kuonyesha matumaini huko mbeleni na waliojitoa wangehamasishwa kwa busara na kuelekezwa ipasavyo, wangeweza kuongozwa kujilipia elimu yao wenyewe kwa kuanza kuuza vitabu vya Vielelezo na mifano ya Kristo (Christ's Object Lessons) au cha Huduma ya Uponyaji (Ministry of Healing). {9T 77.3}

Katika kuuza vitabu hivi vijana wangekuwa wakitenda kazi kama wamishionari, kwa kuwa wangekuwa wanaleta nuru ya thamani mbele ya macho ya watu wa ulimwengu. Wakati huo huo wangekuwa wanapata pesa za kuwawezesha wahudhurie shule, ambapo wangeweza kuendeleza maandalizi yao kwa ajili ya manufaa mapana zaidi katika kazi ya Bwana. Huko shuleni wangepata faraja na msukumo kutoka kwa walimu na wanafunzi kuendelea na kazi yao ya kuuza vitabu; na wakati utakapofika wa wao kuondoka shuleni, wangekuwa wamepata mafunzo ya vitendo ya kuwafaa kwa kazi ngumu, ya bidii, na ya kujitoa kafara inayopaswa kufanywa katika maeneo mengi ya kigeni, ambapo ujumbe wa malaika wa tatu unapaswa kupelekwa chini ya ugumu wa maisha mazingira tatanishi. {9T 78.1}

Mpango huu ni bora kiasi gani kuliko wanafunzi kupita shuleni bila kupata elimu ya vitendo katika eneo la kazi, na, mwishoni mwa kozi yao, kuondoka chini ya mzigo wa madeni, na utambuzi kidogo wa ugumu ambao watalazimika kukutana nao katika eneo jipya na ambalo halijajaribiwa! Itakuwa vigumu kiasi gani kwao kushughulikia matatizo ya kifedha yanayohusiana na kazi ya uanzilishi katika maneneo ya kigeni! (Pioneer Work) Na ni mzigo mkubwa kiasi gani, mtu ataubeba mpaka hapo madeni aliyochukua mwanafunzi yamelipwa! {9T 78.2}

Kwa upande mwingine, ni kiasi gani kinaweza kupatikana, ikiwa mpango wa kujitegemea utafuatwa! Mwanafunzi mara nyingi angewezeshwa kuondoka kwenye taasisi ya elimu bila kuwa mpango wa kulipa madeni binafsi; Hali ya kifedha ya mashule ingekuwa katika hali ya ustawi zaidi; na mafunzo yaliyojifunzwa na mwanafunzi wakati akipitia uzoefu huu katika Konferensi ya nyumbani yatakuwa yasiyoelezeka kwa thamani yake katika maeneo ya kigeni. {9T 79.1}

Hebu mipango ya busara iwekwe kuwasaidia wanafunzi wanaostahili kujilipia elimu yao wenyewe kwa kushughulikia vitabu hivi, wanapotamani kufanya hivyo. Wale wanaopata mali za kutosha kwa njia hii kulipia kozi katika moja ya shule zetu za mafunzo watapata uzoefu wenye thamani zaidi ambao utawasaidia kuwa waanzilishi wa kazi ya umishenari katika maeneo mengine (Pioneer). {9T 79.2}

Kazi kubwa inapaswa kufanywa katika ulimwengu wetu kwa muda mfupi, na lazima tujifunze kuelewa na kuthamini, zaidi ya tulivyokuwa katika miaka iliyopita, majaliwa ya Mungu katika kuweka mikononi mwetu Magombo ya thamani,

Vielelezo vya Kristo (*Christ's Object Lessons*) na cha Huduma ya Uponyaji (*Ministry of Healing*), kama njia ya kuwasaidia wanafunzi wanaostahili, kumudu gharama zao wakiwa katika mafunzo, pamoja na njia ya kukomesha madeni kwenye taasisi zetu za elimu na taasisi za kitabibu. {9T 79.3}

Baraka kuu zimehifadhiwa kwa ajili yetu tunaposhughulikia kwa hekima vitabu hivi vya thamani tulivyopewa kwa ajili ya kuendeleza kazi ya Ukweli wa leo. Na tunapofanya kazi kulingana na mpango wa Bwana, tutagundua kwamba vijana wengi waliojitoa wakfu watafaa kuingia katika maeneo yasiyofikika yaliyo nje ya nchi kama wamishenari wa vitendo; na, wakati huo huo, konferensi katika maeneo ya nyumbani zitakuwa na fedha za kuchangia kwa wingi kwa msaada wa kazi ambayo itafanywa katika eneo jipya. Sanitarium, California, Aprili 17, 1908.-{9T 79.4}

Mungu anatamani kwamba uuzaji wa Vielelezo vya Kristo (*Christ's Object Lessons*) utatambuliwa na watu wetu wote kama njia Yake Bwana ya kuzipa uhaueni shule zetu kutokana na madeni. Ni kwa sababu mpango huu umepuuzwa, ndiy maana sasa tunahisi kubanwa sana kwa ukosefu wetu wa mali za kuendeleza kazi. Laiti shule zingejiweka katika kuendana na majaliwa haya ya Bwana yaliyofanywa kwa ajili yao, kutakuwa na pesa nyingi zaidi katika hazina za shule, na pesa nyingi zaidi katika mikono ya watumishi wa Mungu, ambazo kwazo zinaweza kusaidia mahitaji ya idara nyingine zenye uhitaji wa kazi hiyo; na, bora zaidi, walimu na wanafunzi wangepokea masomo ambayo walipaswa kujifunza katika huduma ya Bwana.-{9T 80.1}

Katika miji iliyo karibu na vituo vyetu vya sanitariamu na shule za mafunzo, eneo la utume limefunguliwa kwetu ambalo bado halijafanyiwa kazi na ni kana kwamba tumegusa kidogo tu kwa ncha za vidole vyetu. Katika baadhi ya maeneo haya, mwanzo mzuri umefanywa. Lakini lilikuwa ni kusudi la Mungu kwamba kwa uuzaji wa Vielelezo vya Kristo (Ch**rist's Object Lessons**) na cha Huduma ya Uponyaji (**Ministry of Healing**), fedha nyingi zingeweza kupatikana kwa ajili ya kazi ya sanitariamu na shule zetu, na ili watu wetu waachwe huru zaidi kutoa michango yao kwa ajili ya ufunguzi wa kazi katika maeneo mapya ya umishenari. Kama watu wetu sasa watashiriki katika uuzaji wa vitabu hivi kama wanavyopaswa, tutakuwa na fedha nyingi zaidi kuliko tulizo nazo sasa kuipeleka kazi kwa njia ambayo Bwana alipanga kwamba inapaswa kupelekwa. {9T 80.2}

## SURA YA 9
## MIKUTANO YA MAKAMBI NA MACHAPISHO YETU

Kuhusianisha na mikutano yetu ya makambi katika miaka iliyopita, watumishi wa Mungu wameboresha fursa nyingi za thamani za kuwafundisha watu wetu kwa mbinu za vitendo za kuwasilisha Kweli zinazookoa za ujumbe wa malaika wa tatu kwa marafiki zao na wale wanaokutana nao. Wengi wamefundishwa jinsi ya kufanya kazi kama wamishenari wanaojitegemeza katika jumuiya zao za nyumbani. Wengi wamerudi nyumbani kutoka kwenye hii mikusanyiko ya kila mwaka na kufanya kazi kwa bidii na akili zaidi kuliko hapo awali. {9T 81.1 Swahili}

Ingempendeza Mungu ikiwa zaidi ya mafundisho haya ya vitendo yangetolewa kwa washiriki wa kanisa ambao huhudhuria mikutano ya makambi yetu, kuliko mara zote ilivyotolewa katika miaka iliyopita. Wafanyakazi wetu kwa ujumla na kaka na akina dada zetu katika kila konferensi wanapaswa kukumbuka kwamba mojawapo ya malengo ya mikusanyiko yetu ya kila mwaka ni kwamba wote wapate ujuzi wa mbinu za vitendo za kazi ya binafsi ya umishionari. Awamu hii ya mikutano yetu ya makambi imeainishwa katika Shuhuda kwa Kanisa, gombo la 6, kama ifuatavyo: {9T 81.2 Swahili}

“Mungu amekabidhi mikononi mwetu kazi takatifu sana kupita zote, na tunahitaji kukutana pamoja ili kupokea maagizo, ili tuweze kustahili kuifanya kazi hii. Tunahitajika kuelewa kila mmoja wetu atafanya sehemu gani katika kuijenga kazi ya Mungu duniani, katika kuutetea utakatifu wa sheria ya Mungu, na katika kumwinua Mwokozi kama 'Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.' Yohana 1:29. Tunahitaji kukutana pamoja na kupokea mguso wa mbingu, ili tuweze kuelewa kazi yetu ya nyumbani. Wazazi wanapaswa kuelewa jinsi wanavyoweza kuwatuma wana na mabinti zao kutoka Patakatifu pa nyumbani wakiwa waliozoezwa na kuelimishwa ili kwamba wafae kuangaza kama nuru katika ulimwengu. Tunahitaji kuelewa kuhusiana na mgawanyo wa kazi na jinsi kila sehemu ya kazi inavyopaswa kuendelezwa mbele. Kila mmoja anapaswa kuelewa sehemu anayopaswa kutenda, ili kuwe na upatanifu wa mpango na utendaji kazi katika kazi yote kwa pamoja."--Ukurasa 32, 33. {9T 81.3 Swahili}

"Ukiendeshwa ipasavyo, mkutano wa makambi ni shule ambayo wachungaji, wazee, na mashemasi wanaweza kujifunza kufanya kazi kamilifu zaidi kwa ajili ya Bwana. Inapaswa kuwa shule ambapo washiriki wa kanisa, wazee na vijana, wanapewa nafasi ya kujifunza njia ya Bwana kikamilifu zaidi, mahali ambapo

waumini wanaweza kupata elimu ambayo itawasaidia kuwasaidia wengine… {9T 82. 1 Swahili}
“Msaada bora zaidi ambao viongozi wanaweza kuwapatia washiriki wa makanisa yetu si kuhubiri, bali kupanga mipango-kazi kwa ajili yao. Mpe kila mmoja kitu cha kufanya kwa ajili ya wengine. Wasaidie wote kuona hilo kama wapokeaji wa neema ya Kristo wako chini ya wajibu wa kumfanyia kazi. Na hebu wote wafundishwe jinsi ya kufanya kazi. Hasa lazima wale walio wapya katika imani waelimishwe kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Iwapo watapangwa kufanya kazi, watu waliokata tamaa hivi karibuni watasahau kukata tamaa kwao; wanyonge watakuwa na nguvu, wajinga watakuwa wenye akili, na wote watakuwa tayari kuiwasilisha Kweli kama ilivyo ndani ya Yesu. Watapata msaidizi asiyeweza kushindwa katika Yeye aliyeahidi kuwaokoa wote wanaomjia.” Ukurasa 49, 50. {9T 82.2 Swahili}

Katika baadhi ya konferensi zetu viongozi wamesita kuzitambulisha mbinu hizi za maelekezo ya kiutendaji. Wengine kwa asili wana mwelekeo wa kuhubiri badala ya kufundisha. Lakini kwenye hafla kama za mikutano yetu ya makambi ya kila mwaka hatupaswi kamwe kupoteza fursa ya kuwafundisha waumini jinsi ya kufanya kazi ya umishenari kwa vitendo mahali watakapoweza kuishi. Katika hali nyingi itakuwa vizuri kuwatenga watu fulani kubeba mzigo wa kazi za aina mbalimbali za elimu katika hii mikutano. Hebu wengine wawasaidie watu kujifunza jinsi ya kusoma Biblia (darasa la Biblia, Bible Study) na kuendesha mikutano ya nyumba kwa nyumba. Hebu wengine waubebe mzigo wa kuwafundisha watu jinsi ya kutekeleza kanuni za afya na kiasi, na jinsi ya kutoa tiba rahisi kwa wagonjwa. Bado wengine wanaweza kufanya kazi kwa masilahi yetu ya kazi ya machapisho na kazi ya vitabu. Na waacheni watendakazi waliochaguliwa wachukue huduma maalumu katika kufundisha wengi jinsi ya kushughulika na vitabu vya Vielelezo vya maisha ya Kristo (*Christ’s Object Lesson*) Huduma ya Uponyaji (*Ministry of Healing*). {9T 82.3 Swahili}

Wengi hawajajifunza jinsi ya kuuza vitabu vilivyoelekezwa kwa ajili ya ukuzaji wa kazi ya taasisi yetu. Lakini hawa hawapaswi kujitetea au kutoa udhuru. Wanapaswa kujifunza kwa bidii jinsi wanavyoweza kufanya sehemu yao kwa uaminifu kuhusiana na usambazaji wa vitabu hivi vya thamani. Shule zetu na sanitariamu lazima ziendeshwe kwa ufanisi wa hali ya juu, na wajibu mzito uko juu yetu sote kusaidia kuweka hizi taasisi kwenye jukuwaa bora na lenye ufanisi kwa kutoa vitabu vya misaada kusambazwa kwa upana. Mungu atatukuzwa na kila mtu achukuaye kwa uthabitii kazi ya kuweka vitabu hivi mikononi mwa umati wa watu ambao wanahitaji Ukweli wa wokovu wa injili. {9T 83.1 Swahili}

Fursa tuliyo nayo ya kufanya mema kwa kujitahidi kuutekeleza mpango wa Bwana

kwa ajili ya unafuu shule na sanitariamu zetu, zimewasilishwa kwangu tena na tena kuhusiana na konferensi ya Kusini mwa California. Hali ya hapo inafaa kwa jinsi ya ajabu kwa ajili ya juhudi za muda mrefu za kusukuma uuzaji wa vitabu vya Vielelezo vya maisha ya Kristo (*Christ's Object Lesson*) Huduma ya Uponyaji (Ministry of Healing). Ndugu na dada zetu wa California Kusini hawapaswi kamwe kuchoka na mpango huu wa kukusanya pesa ili kushughulikia madeni ambayo yamelimbikizwa. Wanafunzi wa shule ya Fernando, na wauguzi wa Sanitariamu tatu ambazo zimeanzishwa, hawawezi kumudu kupoteza uzoefu wa thamani katika wa kazi ya umishenari inayowajia wale wanaoshughulikia vitabu vya msaada. Na konferensi haiwezi kumudu kupoteza matokeo mazuri, ya kiroho na ya kifedha, ambayo yangeambatana na bidii ya aina hii. {9T 83.2 Swahili}

Lakini miaka imepita, na wanafunzi ambao wangepaswa kuwa wanapata uzoefu mzuri kwa kazi halisi ya umishenari hawajahimizwa kujitoa kwa moyo wote katika kuingia kwenyea uuzaji wa Vielelezo vya maisha ya Kristo (Christ's Object Lesson). Washiriki wa kanisa katika sehemu nyingi wamekutana kila siku na wageni, watu wasiowajua -- watalii, wanaume na wanawake wenye uwezo na ushawishi,--na bado fursa kama hizi za kusambaza zimepotea bila kushughulikiwa au kuboreshwa. Watu wengi wanyoofu ambao wangeweza kuwa wamefikiwa kwa juhudi, na uadilifu na kwa moyo wote, hawajapewa nuru ya ujumbe wa malaika wa tatu. {9T 84.1 Swahili}

Kama mpango wa Bwana ungefuatwa, Jina Lake lingekuwa limetukuzwa, na ushindi mwingi wa kiroho ungelikuwa umepatikana. Wale wenye mali wangekuwa na uwezo zaidi na kunia/kuhiari kuja kwenye msaada wa Bwana, wakati Yeye alipokuwa akiongoza nje kwa namna isiyo ya kawaida katika kuanzishwa kwa vituo imara vya umishenari wa tiba karibu na njia panda, katika njia kuu za usafiri/kusafiria. Wanafunzi wangepokea mafunzo ambayo yangeongeza sana ufanisi wao kama wamishenari wa vitendo nyumbani na nje ya nchi . Makanisa yangeamshwa kwa baraka za kiroho. Wengi wangeletwa kwenye Ukweli, na hawa wangeleta katika kazi ushawishi wao na mali zao. {9T 84.2 Swahili}

Katika maeneo kama vile Kusini mwa California, ambapo wanakuja maelfu ya watalii, wengi wao katika kutafuta afya na nguvu, hawa huja na kuondoka kila mara, juhudi maalum na endelevu zinapaswa kuwekwa kuitawanya miale angavu ya nuru na Ukweli. Vitabu vya Huduma ya Uponyaji(Ministry of Healing)na Vielelezo vya maisha ya Kristo (Christ's Object Lesson) vina upekee katika matumizi ya vituo vya utalii, na kila namna iwezekanayo ifanyike ili kuweka nakala za kazi hizi katika mikono ya wale ambao wako kwenye mapumziko na wana mwelekeo wa kusoma. Hasa wale wanaotafuta urejeshwaji wa afya wanahitaji kitabu cha Huduma ya Uponyaji (Ministry of Healing). Kila fursa nzuri ya kulifikia

kundi hili inapaswa kuendelezwa na kuboreshwa. {9T 84.3Swahili}

Moyo wangu umefurahi nilipojifunza kuhusu uamsho wa kazi ya usaidizi huko Kusini mwa California wakati wa miezi michache iliyopita. Huko Loma Linda baadhi ya wauguzi wamepewa mafunzo maalum ya kazi ya kuuza kitabu cha Huduma ya Uponyaji (Ministry of Healing); na kwa vile walivyozitembelea nyumba katika miji na vijiji jirani, baraka za mbinguni zimekaa kwa wingi juu yao, na mvuto mzuri umewekwa kwa niaba ya watu wetu na kazi zao. {9T 85.1 Swahili}

Katika shule ya Fernando walimu wameongoza hivi karibuni katika kuamsha shauku ya uuzaji wa Vielelezo vya maisha ya Kristo (Christ's Object Lesson). Makundi ya wanafunzi, baada ya kusoma kitabu kwa maombi, wameutembelea mji wa Los Angeles kwa kushirikiana na walimu wao na wamepata uzoefu mzuri na thabiti ambao wanauthamini zaidi ya fedha na dhahabu. Aina hii ya kazi, kwa hakika, ni mojawapo ya njia ambazo Mungu ameweka kwa ajili ya kuwapa vijana wetu mafunzo ya umishenari; na wale wanaopuuza kutumia fursa hizo na kuziboresha hupoteza katika maisha yao sura/sehemu ya uzoefu wa thamani ya juu sana. Kwa kuingia kwa moyo wote katika kazi hii, wanafunzi wanaweza kujifunza jinsi ya kuwafikia watu kwa mbinu bora na busara wanaume na wanawake katika nyanja zote za maisha, namna ya kukabiliana nao kwa uungwana na adabu, na jinsi ya kuwaongoza wazingatie ifaavyo Kweli zilizomo katika vitabu hivyo vinavyouzwa. {9T 85.2 Swahili}

Mzigo wetu mkuu sio utafutaji wa pesa, bali wokovu wa roho; na kwa upande wetu huku, tunapaswa kufanya yote tuwezayo kuwafundisha wanafunzi jinsi ya kuziongoza roho katika kuujua ujumbe wa malaika wa tatu. Tunapofanikiwa katika kazi ya kuokoa roho, ile idadi ya watu iliyoongezwa kwenye imani itatumia uwezo wao katika kuwapa wengine Ukweli. Tunapofanya kazi kwa bidii na uaminifu kwa ajili ya wokovu wa wenzetu, Mungu atafanikisha kila juhudi zetu. {9T 85.3 Swahili}

Kwa wenyeviti wa makonferensi, na kwa wengine katika nyadhifa za uongozi, ningesema: Hebu na tufanye kila tuwezalo katika kugusa mioyo ya walimu waliounganishwa na taasisi zetu za elimu, thamani kubwa ya baraka zilizosheheni kwa wale wanaotafuta kwa uadilifu kuitumia vyema zaidi zawadi ya kitabu cha Vielelezo vya maisha ya Kristo (Christ's Object Lesson). Hebu na tuwatie moyo walimu kuungana na wengi wa wanafunzi wao katika kujifunza kwa maombi kitabu hiki, kujitayarisha kwenda pamoja nao katika kazi shambani. Hebu tuwasaidie wakufunzi kuelewa wajibu wao katika suala hili. Hebu tufanye yote tuwezayo kuamsha kazi ya Kitabu cha Vielelezo vya maisha ya Kristo (Christ's Object Lesson) na kuzindua mipango ya kampeni hai ya Kitabu cha Huduma ya

Uponyaji (Ministry of Healing) {9T 86.1 Swahili}

Kadri walimu na wanafunzi wanavyoshiriki kwa moyo wote katika aina hii ya kazi, watapata uzoefu ambao utawafaa wafanye huduma muhimu kuhusiana na mikutano yetu ya makambi. Kupitia maelekezo ambayo wao wanaweza kuyatoa kwa waumini waliohudhuria, na kwa njia ya uuzaji wa vitabu vingi mahali ambapo ile mikutano inafanyikia, wale ambao wamekuwa shuleni wataweza kufanya sehemu yao katika kufikia umati unaohitaji kupokea ujumbe wa malaika wa tatu. Hebu walimu na wanafunzi wavumilie kwa uungwana kuushiriki mzigo wa kuwaonyesha watu wetu jinsi ya kuwasilisha ujumbe kwa marafiki na majirani zao. {9T 86.2 Swahili}

Tunapofuata mipango inayotokana na Bwana "sisi ni watendakazi pamoja na Mungu." Haijalishi nafasi yetu ilivyo,-- iwe wenyeviti/marais wa konferensi, watumishi, walimu, wanafunzi, au washiriki wa kawaida,--tunawajibishwa na Bwana kwa kufanyia kazi kikamilifu fursa za kuwaangazia wale wanaohitaji Ukweli wa sasa. Na moja ya wakala mkuu ambaye Yeye amemtakasa kwa matumizi yetu ni kurasa zilizochapishwa. Katika shule zetu na sanitariamu, katika makanisa yetu ya nyumbani/mahalia, na hasa katika mikutano yetu ya kila mwaka ya makambi, lazima tujifunze kutumia kwa busara wakala huyu wa thamani-machapisho. Kwa bidii ya uvumilivu, watendakazi waliochaguliwa lazima wawaelekeze watu wetu jinsi ya kuwaendea watu wasioamini katika kwa ukarimu, njia ya ushindi na jinsi ya kuweka mikononi mwao Machapisho ambayo Ukweli wa sasa umo, na ukiwa umetolewa kwa uwazi na nguvu. {9T 86.3 Swahili}

Ndugu zangu, tusichoke katika kutenda mema. Wakati wa huduma Yake hapa duniani, Kristo alisafiri kwa miguu kutoka sehemu moja hadi nyingine. Akiwa amechoka, kama Alivyokuwa mara nyingi, asili Yake ya kibinadamu ilitindikiwa kabisa, hata hivyo alikuwa tayari kuwaponya wote waliokuja Kwake, na kuwafundisha njia ya uzima milele. Ingawa mara nyingi alikuwa ana uchovu wa kimwili, Yeye Hakuacha kazi Yake. Kulikuwa na ulimwengu wa kuokolewa. Yeye alifanya kila kujitoa wakfu kuwezekanako, kila dhabihu, ili tunuru na Kweli ziangaze wanadamu. {9T 87.1 Swahili}

Bwana Mungu wa Israeli anatutaka sisi tujiunganishe katika umoja mtakatifu na Yeye Mwenyewe na kuiishi imani iliyo hai na itendayo kazi kwa upendo na kutakasa roho. Yeye Anatamani kwamba tuwe jeshi la watendao kazi waliojaliwa, na wanaojirekebisha ili kuendana na mazingira na fursa, kwa ajili ya utumishi Wake, na kwa watu kama hao, Yeye anaahidi uwezo wa kupata ushindi mtukufu kwa ajili Yake. Sanitarium, California, Julai 10, 1908.-{9T 87.2 Swahili}

Watu wanaosimama kama viongozi katika sehemu yoyote ya kazi nzito ya ujumbe wa mwisho wa injili, lazima wakuze na kupalilia na kutoa maoni na mawazo mapana.  Ni fursa ya wote wanaobeba majukumu katika kazi ya injili kuwa wanafunzi wanaofaa, na kujifunza daima, katika shule ya Kristo. Anayejiita mfuasi wa Kristo lazima asiongozwe na maagizo ya mapenzi yake mwenyewe; akili yake lazima izoezwe kuwaza mawazo ya Kristo na kuangazwa kuyafahamu mapenzi na njia ya Mungu. Muumini kama huyo atakuwa mfuasi wa mbinu za kazi ya Kristo . {9T 87.3 Swahili}

Ndugu zetu wasisahau kwamba hekima ya Mungu imeziandalia mema shule zetu kwa namna fulani ambayo italeta baraka kwa wote wanaoshiriki katika kazi hii. Kitabu cha Vielelezo vya maisha ya Kristo (Christ's Object Lesson) kimetolewa katika  kazi ya elimu, ili wanafunzi na marafiki wengine wa shule waweze kushughulika  na vitabu hivi, na kwa mauzo yake kuongeza fedha zinazohitajika kwa uhakika katika kuondoa madeni ya shule. Lakini mpango huu haujawasilishwa kwenye shule zetu  kama imavyopaswa kuwa; walimu na wanafunzi hawajaelimishwa kubeba kitabu hiki na kukisukuma kwa ujasiri katika uuzaji wake kwa manufaa ya kusogeza mbele kazi ya elimu. {9T 88.1 Swahili}

Muda mrefu uliopita walimu na wanafunzi katika shule zetu walipaswa kujifunza kutumia fursa hii ya kupata fedha kutokana na uuzaji wa kitabu cha Vielelezo vya maisha ya Kristo (Christ's Object Lesson). Katika kuuza vitabu hivi wanafunzi watatumika katika kazi ya Mungu, na, kwa kufanya hivi, wataeneza nuru ya thamani, na kujifunza masomo muhimu sana katika uzoefu wa Kikristo. Shule zetu zote sasa zinapaswa kuja kwenye mstari huu, na kwa dhati kujitahidi kutekeleza mpango uliowasilishwa kwetu kwa ajili ya watendakazi wa elimu, kwa ajili ya kusaidia shule, na kwa ajili ya kuleta roho kwa Kristo. {9T 88.2 Swahili}

## SEHEMU YA 3—KAZI KATIKA MIJI MIKUBWA

[*Katika Makala Tano Katika Sehemu Hii Kumekusanywa Pamoja Na Kuwekwa Katika Utaratibu Rahisi Baadhi Ya Mafundisho Mengi Elekezi, Yenye Shuhuda Za Kutia Moyo, Na Za Kusisimua Kuhusu Kazi Katika Miji. Taarifa Zilizo Jumuishwa*

*Katika Mkusanyiko Huu Zimepatikana Katika Shuhuda Maalum, Katika Makala Zilizochapishwa Katika Majarida Yetu, Katika Taarifa Za Mahubiri Katika Mkutano Wa Halmashauri Kuu (General Conference) Wa 1909, Na Katika Barua Kwa Watendakazi Katika Miji Mikubwa*] {9T 89.1 Swahili}

"Nikasikia sauti ya Bwana akisema, Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi Hapa nitume mimi.” Isaya 6:8.

## SURA YA 10
## HALI KATIKA MIJI

Inakuja upesi na kwa uhakika, hatia karibu ya ulimwengu wote juu ya wakazi wa miji kwa sababu ya ongezeko la kasi la uovu uliodhamiriwa. Tunaishi katikati ya "janga la uhalifu" ambapo watu wenye kufikiri kwa kina, wanaomcha Mungu kila mahali inabidi waduwae kwa kushtuka, na midomo kuachwa wazi. Ufisadi uliokithiri ni zaidi ya uwezo wa kalamu ya binadamu kuuelezea. Kila siku magomvi ya kisiasa hufunuliwa upya, rushwa, wizi, na ulaghai; kila siku huleta kumbukumbu yake ya kuhuzunisha moyo, kuhusiana na uharibifu, na uasi wa sheria, ya kutojali mateso kwa binadamu; uharibifu wa kikatili na mbaya wa maisha ya mwanadamu, na mambo mengine mabaya ya kishetani. Kila siku hushuhudia kuongezeka kwa wenda-wazimu, mauaji, na watu kujiua. {9T 89.2 Swahili}

Miji ya siku hizi inaharakisha kuwa kama Sodoma na Gomora. Siku-kuu ni nyingi; kimbunga cha msisimko na raha huvutia maelfu kutoka kwenye majukumu ya maisha ya kuwa na kiasi. Michezo ya kusisimua-- michezo ya kuigiza, mbio za farasi, kamari, unywaji pombe, dansi, vicheko na makelele mengi, na karamu-- huchochea kila shauku kuwa katika utendaji. {9T 89.3 Swahili}

Vijana wanagafiliwa na mkondo wa umaarufu uliopo. Wale wanaojifunza kupenda matumbuizo/anasa kwa ajili tu ya hayo, wanafungua mlango wa mafuriko ya majaribu. Wanajiweka wenyewe kwenye raha za kijamii na starehe zisizo na kufikiria wengine, ikiwemo na vicheko, starehe, na maburudisho. Wanaongozwa kutoka kwa aina moja ya uchafu wa ulevi, ngono chafu na zinaa hadi mwingine, hadi wanapoteza hamu na uwezo wa kuishi maisha yenye manufaa. Matarajio yao

ya kiroho yamepoa; maisha yao ya kiroho yametiwa giza. Uwezo wote bora wa nafsi, ambao unamhusisha mwanadamu na ulimwengu wa kiroho, umeharibiwa. {9T 90.1}

Kupitia utendakazi wa amana na matokeo ya vyama vya wafanyikazi na migomo, hali ya maisha katika miji inazidi kuwa ngumu zaidi na zaidi. {9T 90.2}

Shauku kubwa ya kupata pesa, kiu ya kujionyesha, anasa na ubadhirifu--yote ni nguvu ambazo, pamoja na umati mkubwa wa wanadamu, zinageuza akili kutoka kwenye kusudi la Kweli la maisha. Hufungua mlango kwa maelfu ya maovu. Wengi, wakimezwa na kupendezwa kwao na hazina za ulimwengu, wanakuwa wasio na hisia na wasioelewa madai ya Mungu na mahitaji ya wanadamu wenzao. Wanachukulia utajiri wao kama njia ya kujitukuza nafsi. Wanaongeza nyumba kwa nyumba na ardhi kwa ardhi; wanajaza nyumba zao na anasa, wakati wote karibu yao ni wanadamu walio katika taabu na uhalifu, katika magonjwa na kifo. {9T 90.3}

Kwa kila aina ya ukandamizaji na unyang'anyi, watu wanajilimbikizia mali nyingi, huku vilio vya wanadamu wenye njaa huja mbele za Mungu. Kuna watu wengi wanahangaika na umaskini, na hawa hulazimishwa kufanya kazi kwa bidii kwa ujira mdogo, bila kupata mahitaji kidogo ya maisha. Kutaabika, kuhehenyeka na kunyimwa mahitaji muhimu, bila matumaini ya vitu bora, hufanya mzigo wao kuwa mzito. Wakati maumivu na magonjwa yanapoongezwa, mzigo hufikia hali ya kutovumilika. Wakiwa wametunzwa na kukandamizwa, hawajui waelekee wapi ili kupata nafuu. {9T 90.4}

Maandiko yanaeleza hali ya ulimwengu kabla tu ya kuja kwa Kristo mara ya pili.
Mtume Yakobo anaonyesha uchoyo na uonevu utakaotawala. Anasema: “Haya basi, enyi matajiri. . . Mmmejiwekea akiba kwa siku za mwisho. Angalieni, ujira wa wakulima waliovuna mashamba yenu, ninyi mliouzuia kwa hila, unapiga kelele; na vilio vyao waliovuna vimeingia masikioni mwa Bwana wa Majeshi. Mmefanya anasa katika dunia, na kujifurahisha kwa tamaa; mmejilisha mioyo yenu kama siku ya machinjo. Mmemhukumu mwenye haki na kumwua; wala hashindani nanyi." Yakobo 5:1-6. {9T 91.1}

Hii ni picha ya mambo yaliyopo leo. "Hukumu imegeuka ikaenda nyuma, na haki imesimama mbali sana; maana Kweli imeanguka katika njia kuu, na unyofu hauwezi kuingia. Naam, kweli imepunguka kabisa; na yeye auachaye uovu hujifanya kuwa mateka." Isaya 59:14, 15. {9T 91.2}

Hata kanisa, ambalo lilinapaswa kuwa nguzo na msingi wa Ukweli, linajikuta likihamasisha ubinafsi wa kupenda raha. Pesa zinapokusanywa kwa makusudi ya kidini, makanisa mengi hutumia kwa njia gani? Kwa minada, chakula cha jioni,

maonyesho ya kifahari, hata kwa bahati nasibu na mambo kama hayo. Mara nyingi mahali palipotengwa kwa ajili ya Mungu kuabudiwa pananajisiwa kwa karamu na kunywa pombe, kununua, kuuza, na kujipatia raha kwa kelele, karamu, dansi nk. Heshima kwa nyumba ya Mungu na uchaji kwa ajili ya ibada Yake hupungua katika akili za vijana. Vizuizi vya kujizuia, kukana nafsi hudhoofishwa. Ubinafsi, uchu wa chakula au ulafi, upendo wa kujionyesha, huvutia, na huimarishwa kadri vinavyoendekezwa na wanadamu. {9T 91.3}

Tangu enzi na enzi Bwana amejulisha namna ya utendaji Wake. Wakati zahama au taharuki imekuja, Yeye amejifunua Mwenyewe na ameingilia kati ili kuzuia utendakazi wa mipango ya Shetani. Kwa mataifa, kwa familia, na kwa watu binafsi mara nyingi ameruhusu mambo kuwa kwenye shida, ili kuingilia Kwake kuweze kuonekana. Kisha akadhihirisha kuwa Yupo Mungu katika Israeli ambaye atadumisha sheria Yake na kuwatetea watu Wake. {9T 91.4}

Katika ulimwengu wa kabla ya gharika (antediluvian) mawakala wa kibinadamu walileta kila namna ya ubunifu na mambo ya werevu ili kuibatilisha sheria ya Yehova. Walitupilia mbali mamlaka Yake kwa sababu yaliingilia mambo/dhambi yao. Kama katika siku za kabla ya Gharika, ndivyo sasa wakati u juu yetu ambapo Bwana lazima afunue Nguvu Zake, kwamba  Yeye Ndiye Mweza wa yote. Katika wakati huu wa uovu ulioenea tunaweza kujua kwamba dhiki kuu ya mwisho iko karibu. Wakati uasi dhidi ya sheria ya Mungu u karibu ulimwenguni pote, wakati watu Wake wanakandamizwa na kuteswa na wanadamu wenzao, Bwana ataingilia kati. {9T 92.1}

Shetani hajalala; amekodoa macho yake wazi ili kulibatilisha Neno la hakika la unabii. Kwa ujuzi na nguvu za udanganyifu anafanya kazi kinyume na mapenzi ya Mungu yaliyodhihirishwa, yaliyowekwa wazi katika Neno Lake. Kwa  miaka mingi Shetani amekuwa akipata udhibiti wa akili za wanadamu kupitia mbinu za hila ambazo amezibuni kuchukua nafasi ya ile Kweli. Wakati huu wa upotevu, watenda haki, kwa kumcha Mungu, watalitukuza Jina Lake wakirudia Maneno ya Daudi: "Wakati umewadia BWANA, atende kazi; kwa kuwa wameitangua sheria Yako."Zaburi 119:126. {9T 92.2}

### Hukumu za Mungu juu ya Miji yetu

Nikiwa Loma Linda, California, Aprili 16, 1906, onesho la ajabu lilipita mbele yangu. Wakati wa maono ya usiku, nilisimama mahali pa juu, ambapo niliweza kuona nyumba zikitikiswa kama mwanzi katika upepo. Majengo, makubwa na madogo, yalikuwa yakianguka chini. Sehemu za anasa (resorts), kumbi za michezo, hoteli, na nyumba za matajiri zilitikiswa na kusambaratishwa. Maisha mengi yalifutiliwa yasiwepo, na anga likajazwa kelele/mayowe/kugumia kwawatu waliojeruhiwa na waliojawa na hofu. {9T 92.3}

Malaika wa Mungu wa kuangamiza walikuwa kazini. Mguso mmoja, na majengo, yaliyojengwa kwa uangalifu sana watu waliyaona kuwa salama dhidi ya kila hatari, upesi yakawa lundo la takataka. Hakukuwa na uhakikisho wa usalama mahali popote. Sikujisikia kuwa katika hatari yoyote, lakini utisho wa matukio hayo uliopita mbele yangu, sikuweza kupata maneno ya kuuelezea. Ilionekana kuwa uvumilivu wa Mungu ulikuwa umechoka na kukoma na kwamba siku ya Hukumu ilikuwa imewadia. {9T 93.1}

Kisha Malaika aliyesimama kando yangu akanielekeza kwamba lakini ni wachache wenye utambuzi juu ya huo uovu uliopo katika dunia yetu leo, na hasa uovu katika miji mikubwa. Alitamka kwamba Bwana ameweka wakati ambapo atawaadhibu wakosaji kwa ghadhabu kwa ajili ya kutojali daima Sheria Yake. {9T 93.2}

Kama lilivyokuwa la kutisha onesho lililopita mbele yangu, ambalo kwa lenyewe liligusa hisia za ndani zaidi akilini mwangu lilikuwa ni agizo lililotolewa kuhusiana nayo. Malaika aliyesimama kando yangu alitangaza kwamba utawala mkuu wa Mungu na utakatifu wa sheria Yake lazima ufunuliwe kwa wale waliodumu kukataa kutoa utii kwa Mfalme wa wafalme. Wale wanaochagua kubaki kutokuwa waaminifu lazima watembelewe na rehema za hukumu, ili, kama yumkini, waweze kuamshwa kutambua dhambi ya mwenendo wao. {9T 93.3}

Siku nzima iliyofuata nilitafakari matukio yaliyopita mbele yangu na maagizo yaliyokuwa yametolewa. Wakati wa mchana tulisafiri hadi Glendale, karibu na Los Angeles; na usiku uliofuata nilielekezwa tena kuhusu utakatifu na mashiko/kifungo cha madai ya Amri Kumi na Ukuu wa Mungu juu ya watawala wote wa kidunia. {9T 93.4}

Nilionekana kuwa kwenye mkusanyiko, nikiweka mbele ya watu matakwa ya sheria ya Mungu. Nilisoma Maandiko kuhusu kuanzishwa kwa Sabato katika Edeni mwishoni mwa juma la uumbaji, na kuhusu kutolewa kwa sheria pale Sinai; na kisha ikatangazwa kuwa Sabato inapaswa kuadhimishwa “kama agano la milele" Ni ishara kati ya Mungu na watu wake milele, ili waweze kujua kwamba hutakaswa na Bwana, Muumba wao. {9T 94.1}

Kisha nikakazia zaidi juu ya utawala mkuu zaidi wa Mungu juu ya watawala wote wa kidunia. Sheria Yake inapaswa kuwa kipimo cha tabia. Watu wamekatazwa kupotosha hisia zao kwa kutokuwa na kiasi au kwa kusalimisha akili zao katika mivutano ya kishetani, kwa kuwa hii inafanya kutowezekana kuishika sheria ya Mungu. Wakati Mtawala wa mbingu huvumilia upotovu, Yeye Hadanganyiki na wala hatanyamaza daima. Ukuu Wake, Mamlaka Yake kama Mtawala wa ulimwengu (Sayari zote), lazima hatimaye vitambuliwe na madai ya haki ya sheria Yake yathibitishwe. {9T 94.2}

Maagizo mengi zaidi kuhusu uvumilivu wa Mungu na ulazima wa kuamsha wakosaji kutambua nafasi yao ya hatari ya upotevu machoni Pake ilirudiwa kwa watu, kama nilivyoyapokea kutoka kwa mwelekezaji wangu. {9T 94.3}

Mnamo Aprili 18, siku mbili baada ya onesho la majengo yaliyoanguka kupita mbele yangu, nilikwenda kuweka miadi katika Kanisa la Carr Street, Los Angeles. Tulipokaribia kanisani tulisikia wana-habari na wakalia: "San Francisco imeharibiwa na tetemeko la ardhi!" Kwa moyo mzito nilisoma Gazeti la kwanza la Gazeti kuchapwa kwa haraka, kuhusu zile habari za maafa haya ya kutisha. {9T 94.4}

Wiki mbili baadaye, katika safari yetu ya kurudi nyumbani, tulipitia San Francisco na tukakodisha gari la farasi, tulitumia saa moja na nusu kutazama uharibifu huo uliofanyika katika mji ule mkubwa. Majengo ambayo yalifikiriwa kuwa thabiti dhidi ya majanga yalikuwa yameharibika na kuwa magofu hapo chini ya ardhi. Katika baadhi ya matukio majengo yalizama kwa sehemu ardhini. Jiji liliwasilisha hali ya kutisha zaidi. Picha ya uzembe na werevu usio na ufanisi wa binadamu ilionekana katika kuweka miundombinu 'isiyoweza kushika moto na inayostahimili tetemeko la ardhi'. {9T 94.5}

Kupitia kwa nabii wake Sefania Bwana anabainisha hukumu atakazoleta juu ya watenda maovu: {9T 95.1}

Nitavikomesha kabisa vitu vyote, visionekane juu ya uso wa nchi, asema Bwana; nitamkomesha mwanadamu na mnyama; nitakomesha ndege wa angani, na samaki wa baharini, na hayo makwazo pamoja na wabaya; Nami nitamkatilia mbali mwanadamu asionekane juu ya uso wa nchi, asema BWANA." {9T 95.2}
"Na itakuwa katika siku ile ya dhabihu ya Bwana, nitawaadhibu wakuu, na wana wa mfalme, na watu wote waliovaa mavazi ya kigeni. Na` katika siku ile nitawaadhibu hao wote warukao juu ya kizingiti, waijazao nyumba ya bwana wao udhalimu na udanganyifu. . . . {9T 95.3}

"Kisha itakuwa wakati ule, nitauchunguza Yerusalemu kwa taa, nami nitawaadhibu watu waliokaa juu ya sira zao, wasemao mioyoni mwao, Bwana hatatenda mema, wala hatatenda mabaya. Na huko utajiri wao utakuwa mateka, na nyumba zao zitakuwa ukiwa; naam, watajenga nyumba, lakini hawatakaa ndani yake; nao watapanda mizabibu, lakini hawatakunywa divai yake. {9T 95.4}

"Hiyo Siku ya BWANA iliyo kuu i karibu, i karibu, nayo inafanya haraka sana, Naam sauti ya siku ya BWANA: shujaa hulia kwa uchungu huko. Siku ile ni siku ya ghadhabu, siku ya fadhaa na dhiki, siku ya uharibifu na ukiwa, siku ya giza na utusitusi, siku ya mawingu na giza kuu; siku ya tarumbeta na kamsa juu ya miji yenye maboma, na juu ya baruji zilizo ndefu sana. Nami nitawaletea wanadamu dhiki, hata watakwenda kama vipofu, kwa sababu wamemtenda BWANA dhambi; na damu yao itamwagwa kama mavumbi, na nyama yao kama mavi. Fedha yao

wala dhahabu yao haitaweza kuwaokoa katika siku ile ya ghadhabu ya BWANA; bali nchi yote pia itateketezwa kwa moto wa wivu Wake; maana atawakomesha watu wote wakaao katika nchi hii." Sefania 1:2, 3, 8-18. (9T 95.5}

Mungu hawezi kuvumilia zaidi. Tayari hukumu Zake zimeanza kushuka baadhi ya sehemu, na hivi punde ishara yake ya kutofurahisha itasikika katika sehemu zingine. {9T 96.1}

Kutakuwa na mfululizo wa matukio yanayodhihirisha kwamba Mungu Ndiye mtawala wa hali iliyopo. Ukweli utatangazwa kwa lugha iliyo wazi, isiyo na shaka. Kama watu lazima tuandae njia ya Bwana chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Injili inapaswa kutolewa katika usafi wake. Mto wa maji ya uzima unapaswa kuwa na kina na kupanuka katika mkondo wake. Katika mashamba yote, karibu na mbali, watu wataitwa kutoka kwenye ukulima wa plau ya ng'ombe na kutoka katika tasnia na ujasiliamali wa kawaida kabisa ambao unatawala akili kwa kiasi kikubwa, na watafunzwa kwa kuunganishwa na watu wenye uzoefu. Kadri wanavyojifunza kufanya kazi kwa ufanisi watatangaza Kweli kwa nguvu. Kupitia kazi nyingi za ajabu za majaliwa ya Mungu, milima ya magumu, itaondolewa na kutupwa baharini. Ujumbe wenye maana sana kwa wakaaji wa duniani utasikiwa na kueleweka. Watu watajua Kweli ni nini. Mbele na mbele zaidi kazi itasonga mpaka dunia yote itakapoonywa, na ndipo ule mwisho utakapokuja. {9T 96.2}

## SURA YA 11
## KAZI YA SASA HIVI

Zaidi na zaidi, kadiri siku zinavyosonga, inakuwa dhahiri kwamba hukumu za Mungu ziko ulimwenguni. Katika moto na mafuriko na matetemeko ya ardhi, Yeye anawaonya wakazi wa dunia hii juu ya ukaribu wa kuja Kwake. Muda unakaribia wakati dhiki kuu katika historia ya dunia itakuwa imekuja, wakati kila mwendo katika serikali ya Mungu utatazamwa kwa shauku kubwa na wasiwasi usioelezeka. Kwa mfululizo wa haraka hukumu za Mungu zitafuatana--moto na mafuriko na tetemeko la ardhi, pamoja na vita na umwagaji damu. {9T 97.1}

Ah! Laiti watu wangelijua majira ya kujiliwa kwao! Kuna wengi ambao bado hawajaisikia Kweli ipimayo ya wakati huu. Kuna wengi ambao Roho wa Mungu anashindana nao. Wakati wa hukumu za Mungu za uharibifu ni wakati wa rehema kwa wale ambao hawakuwa na nafasi ya kujifunza Kweli ni nini. Bwana atawatazama kwa upole. Moyo Wake wa rehema umeguswa; Mkono Wake bado umenyooshwa ili kuokoa, wakati mlango ukiwa umefungwa kwa wale ambao

hawakutaka kuingia. {9T 97.2}

Rehema ya Mungu inaonyeshwa katika uvumilivu Wake wa muda mrefu. Yeye Anazuia hukumu Zake, akingojea ujumbe wa onyo utangazwe kwa wote. Loo!, laiti kama watu wetu wangehisi jinsi wanavyopaswa kuwajibika kutulia katika wajibu wao wa kutoa ujumbe wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu, ni kazi ya ajabu iliyoje ingelikuwa imefanyika! {9T 97.3}

Tazama miji, na hitaji lao la injili! Hitaji la watenda kazi dhati na wenye bidii kati ya umati wa watu walio mijini imeletwa mbele yangu kwa zaidi ya miaka ishirini. Ni nani anayebeba mzigo wa miji mikubwa? Ni wachache tu, ndio ambao wamehisi mzigo, lakini kwa kulinganisha na hitaji kubwa na fursa nyingi, kuna umakini mdogo tu ambao umetolewa kwa kazi hii. {9T 97.4}

## Katika Miji ya Mashariki

Maagizo yametolewa kwangu kwamba ujumbe unapaswa upelekwe tena kwa nguvu katika miji ya majimbo ya Mashariki ya nchi. Katika miji mingi mikubwa ya Mashariki ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili ulitangazwa wakati wa harakati za 1844. Kwetu, sisi watumishi wa Mungu tumekabidhiwa ujumbe wa malaika wa tatu, ujumbe wa kufunga, ambao ni kuwatayarisha watu kwa ajili ya kuja kwa Mfalme. Tunapaswa kufanya kila jitahidi kuwapa ujuzi wa Ukweli watu wote watakaosikia, na kuna wengi watakaousikia. Kote katika miji mikubwa Mungu ana watu waaminifu ambao wanapendezwa na ‘Ukweli ni nini ?’. {9T 98.1}

Muda ni mfupi; Bwana anatamani kwamba kila kitu kilichounganishwa na kusudi Lake kiwe katika utaratibu. Yeye Anataka kwamba ujumbe mzito wa onyo na wa mwaliko vitangazwe kwa mapana kadri wajumbe Wake wanavyoweza kuubeba. Hakuna chochote kitakachozuia ueneaji wa ujumbe kinapaswa kuruhusiwa kuwa katika mipango yetu. "Rudia ujumbe, rudia ujumbe," ni Maneno ambayo niliambiwa mara kwa mara tena na tena. “Waambie watu Wangu warudie ujumbe katika mahali ulipohubiriwa mara ya kwanza, na ambapo kanisa baada ya kanisa lilichukua nafasi yao kwa ajili ya Ukweli, nguvu ya Mungu huushuhudia ujumbe katika ya namna ya ajabu." {9T 98.2}

Kwa miaka mingi waanzilishi wa kazi yetu walijitahidi dhidi ya umaskini na magumu mengi ili kuuweka Ukweli wa sasa juu ya ardhi bora na jukwaa muafaka. Pamoja na vifaa duni na uhaba, walifanya kazi bila kuchoka, na Bwana alibariki juhudi zao za unyenyekevu. Ujumbe ulikwenda kwa nguvu Mashariki na kupanuka

kuelekea magharibi mpaka vituo vya mvuto vikaanzishwa sehemu nyingi. Watenda kazi wa siku hizi huenda wasistahimili magumu yote ya siku hizo za awali. Hali ilivyobadilika, hata hivyo, haipaswi kusababisha kulegeza juhudi zozote. Sasa, Bwana anapotuamuru kuutangaza ujumbe kwa mara nyingine tena kwa nguvu katika Mashariki, anapotuagiza kuingia miji ya Mashariki na ya Kusini na ya Magharibi na ya Kaskazini, Je, hatutaitika kama mtu mmoja na kutekeleza agizo Lake? Je, hatuwezi kuwa na mpango wa kutuma wajumbe wetu katika maeneo haya yote na kuwasapoti kwa msaada na kuwaunga mkono kwa ukarimu na moyo mkunjufu? Je, watumishi wa Mungu hawawezi kwenda kwenye vituo hivi vilivyojaa watu na kuiinua sauti katika kuyaonya makusanyiko? Konferensi zetu ni za nini, basi ikiwa si kwa ajili ya kuendeleza sana kazi hii? {9T 98.3}

Mwanzo umefanywa katika kuutangaza ujumbe wa malaika wa tatu katika jiji la Washington na katika miji mingine ya Kusini na Mashariki; lakini ili kupatana na nia ya Bwana, itatubidi kupanga mikakati kwa ajili ya kuendeleza kazi kubwa na kwa utaratibu. Inatupasa tuingie katika kazi hii kwa uvumilivu ambao hautaturuhusu kulegeza juhudi zetu mpaka tuuone wokovu wa Mungu. {9T 99.1}

Huko Portland, Maine; huko Boston na miji inayozunguka; huko New York na miji yenye watu wengi iliyo karibu; huko Filadelfia na Baltimore na Washington, Bwana anatamani tuutangaze ujumbe wa malaika wa tatu kwa nguvu. Hatuwezi kushinikiza nguvu hii sisi wenyewe, lakini tunaweza kuchagua watu wenye uwezo na kuwahimiza kwenda katika njia hizi za fursa na huko kuutangaza ujumbe kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Ni lazima tupange kuweka katika miji hii watu wenye uwezo ambao wanaweza kuwasilisha ujumbe wa malaika watatu kwa namna ya kuusukuma hivi kwamba utagusa moyo. Watu wanaoweza kufanya kazi hii hatuwezi kumudu kukusanyika mahali pamoja kufanya kazi ambayo wengine wanaweza kufanya.{9T 99.2}

Kadri watendakazi hawa wanapouzungumza Ukweli na kuuishi Ukweli, na kuomba kwa ajili ya maendeleo ya Ukweli, Mungu ataivuta na kuigusa mioyo. Wanapofanya kazi kwa nguvu zote ambazo Mungu huwapa, na kwa unyenyekevu wa moyo kuweka tumaini lao kamili Kwake, kazi zao hazitakosa kuwa na matunda. Juhudi zao za dhati za kuleta roho kwenye ujuzi wa Ukweli kwa wakati huu zitaungwa mkono na malaika watakatifu, na roho nyingi zitaokolewa. {9T 100.1}

## Ukarimu katika Juhudi za Kimishenari

Majimbo ya Kusini yanapaswa kuwa na nuru ya Ukweli wa sasa. Usiseme: "Ofisi zetu za uchapishaji na makanisa yetu yanahitaji msaada zaidi. Tunahitaji mali zote ambazo tunaweza kupata ili kuendeleza kazi iliyo mkononi." Mmoja baada ya mwingine wamefunga mlango kwa aina fulani ya jitihada za umishenari kwa

kuogopa kwamba kazi hii ingetumia mali ambazo walizitamani kwa ajili ya mambo mengine. Ndugu zangu, mnahitaji zaidi Roho wa Kristo. Hebu kiwango chenu kiinuliwe juu zaidi; kisha wale ambao wameongoka hivi karibuni kwa Ukweli wataweza kuelewa kwamba wana kazi ya kufanya. Kwa njia hii mali ya kuiendeleza kazi itakuwa daima ikiongezeka. {9T 100.2}

Je, tunaweza kuwatarajia watu wa mijini kutujia na kusema: “Ikiwa mtatujia na kutuhubiria tutawasaidia kufanya hivi na vile"? Wanajua nini kuhusu ujumbe wetu? Hebu na tufanye sehemu yetu katika kuwaonya watu hawa ambao wako tayari kuangamia bila kuonywa na bila kuokolewa. Bwana anatamani tuiruhusu nuru yetu kuangaza mbele ya watu ili Roho Wake Mtakatifu aweze kuwasilisha Ukweli kwa unyofu kwenye moyo unaomtafuta. {9T 100.3}

Kadri tunavyofanya kazi hii tutagundua kwamba mali zitatiririka katika hazina zetu, na tutakuwa na fedha za kuendeleza kazi pana zaidi na ya mbali zaidi. Nafsi zilizo na mali zitaletwa katika Ukweli na watatoa mali zao kuiendeleza kazi ya Mungu. Nimeagizwa kuwa kuna mali nyingi mijini ambazo hazifanyiwi kazi. Mungu ana watu wanaowiwa huko. Nenda kwao; wafundishe kama Kristo alivyofundisha; wape Ukweli. Wataukubali. Na kwa hakika kadri vile watu waaminifu watakavyoongoka, mali zao zitawekwa wakfu kwa utumishi wa Bwana na tutaona ongezeko la rasilimali. {9T 100.4}

Laiti tungeliweza kuona mahitaji ya miji hii kama jinsi Mungu anavyoyaona! Kwa wakati kama huu, kila mkono ungekuwa ukitumika mahali fulani. Bwana anakuja; mwisho umekaribia, naam, unafanya haraka sana! Bado kitambo kidogo tutakuwa hatuwezi kufanya kazi kwa uhuru tunaofurahia sasa. Matukio ya kutisha yako mbele yetu, na kile tunachofanya tunapaswa kukifanya kwa haraka sana. {9T 101.1}

## Nia ya Huduma

Hivi karibuni katika majira ya usiku niliamshwa kutoka usingizini na kupewa kutazama mateso ya Kristo kwa ajili ya watu. Kafara Yake, kejeli na dhihaka Alizopokea mikononi mwa watu waovu, uchungu Wake ndani ya Bustani ya Gethsemane, kusalitiwa Kwake na kusulubishwa -- yote yalionyeshwa kwa uwazi mbele yangu. {9T101.2}

Nilimwona Kristo katikati ya kundi kubwa la watu. Alikuwa akitafuta kuzivutia akili zao kwa mafundisho Yake. Lakini alidharauliwa na kukataliwa nao. Wanadamu walikuwa wakimrundikia matusi, manyanyaso na aibu. Dhiki yangu ilikuwa kubwa sana nilipotazama maono yale. Nilimsihi Mungu: “Ni nini kifanyike kwa hili kutaniko? Hakuna atakayeacha maoni yake ya kujitukuza nafsi na kumtafuta Bwana kama watoto wadogo? Je! hakuna watakaovunja mioyo yao mbele za Mungu kwa toba na kuungama?” {9T 101.3}

Uchungu wa Kristo katika bustani ya Gethsemane uliwasilishwa kwangu, wakati kikombe cha ajabu kilipotetemeka katika mkono wa Mkombozi. Baba, ikiwezekana,” aliomba, “kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo Mimi, bali kama utakavyo Wewe.” Mathayo 26:39. Kadri alivyomsihi Baba, matone makubwa ya damu yakaanguka kutoka usoni Mwake hadi ardhini. Mawakala wa giza walijikusanya karibu na Mwokozi ili kuikatisha tamaa nafsi Yake. {9T 102.1}

Akiinuka kutoka ardhini, Kristo alikwenda mahali alipokuwa amewaacha wanafunzi Wake, akiwabidisha wakeshe na kuomba pamoja Naye wasije wakashindwa na majaribu. Angeona kama wangeelewa uchungu Wake; Alihitaji huruma yao ya kibinadamu. Lakini aliwakuta wamelala. Akawaendea hivi mara tatu, na kila wakati walikuwa wamelala. {9T 102.2}

Mara tatu Mwokozi aliomba: "Baba, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke." Ilikuwa hapa, ndiyo hatima ya ulimwengu uliopotea iliyumba katika mizani. Kama Yeye angekataa kukinywea kikombe hiki, matokeo yangekuwa upotevu wa milele kwa wanadamu. Lakini malaika kutoka mbinguni alimtia nguvu Mwana wa Mungu kukibali kikombe hiki na kunywa ole wa kikombe chenye uchungu. {9T 102.3}

Ni wachache kiasi gani wanaotambua kwamba haya yote yalibebwa kwa ajili yao binafsi! Ni wachache kiasi gani wanaosema: "Ilikuwa kwa ajili yangu mimi, ili niunde tabia kwa ajili ya uzima wa milele ujao." {9T 102.4}

Mambo haya yalipowasilishwa kwangu kwa uwazi sana, nilifikiri, sitaweza kamwe kuwasilisha mada hii mbele ya watu kama ilivyo;” nami nimekupa onyesho dogo na hafifu tu ya yale niliyooneshwa. Nilipofikiria kikombe kile kikitetemeka mikononi mwa Kristo; kama nilivyotambua kwamba Yeye angeweza kukataa kunywa, na kuuacha ulimwengu uangamie katika dhambi yake, nimeahidi kwamba kila nguvu ya maisha yangu inapaswa kujitolea kwa kazi ya kuleta roho Kwake. {9T 102.5}

Kristo alikuja duniani kuteseka na kufa, kwamba, kwa kwa njia ya imani katika Yeye na kuchukua tabia Yake, sisi tunaweza kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Lilikuwa ni kusudi la Mwokozi kwamba baada ya Yeye kupaa mbinguni awe wakili na mwombezi wa mwanadamu, wafuasi Wake wanapaswa kuendeleza kazi aliyokuwa ameianzisha. Je, wakala wa kibinadamu hataonyesha shauku maalum katika kutoa nuru ya ujumbe wa injili kwa wale wanaokaa gizani? Kuna wengine ambao wako tayari kwenda hadi miisho ya dunia ili kuibeba nuru ya Ukweli kwa wanadamu, lakini Mungu anadai kwamba kila nafsi inayoijua Kweli ifanye bidii katika kuwatafuta wengine waipende Kweli. Ikiwa hatuko tayari kujitoa dhabihu maalum ili kuokoa roho zilizo tayari kuangamia, tunawezaje kuhesabiwa kuwa tunastahili kuingia katika mji wa Mungu? {9T103.1}

Kuna kazi kibinafsi ya kufanywa kwa kila mmoja wetu. Najua kuna wengi

wanaojiweka vyema wenyewe katika uhusiano sahihi na Kristo, ambao wazo lao moja ni kuleta ujumbe wa Ukweli wa sasa mbele za watu wa dunia. Wanaendelea kuwa tayari kutoa huduma zao. Lakini moyo wangu unauma ninapotazama wengi ambao wameridhika na uzoefu hafifu, uzoefu unaowagharimu kidogo tu. Maisha yao husema kwamba kwao Kristo amekufa bure. {9T 103.2}

Ikiwa hujisikii kwamba ni heshima kuwa mshiriki wa mateso ya Kristo; ikiwa huhisi mzigo wa nafsi kwa wale walio tayari kuangamia; kama hauko tayari kujitoa ili upate kuweka akiba mali kwa ajili ya kazi inayopaswa kufanywa, hakutakuwa na nafasi kwako katika ufalme wa Mungu. Tunahitaji kuwa washirika pamoja na Kristo wa mateso Yake na kujikana nafsi katika kila hatua. Tunahitaji kuwa na Roho wa Mungu akae juu yetu, akituongoza kujitoa daima. {9T 103.3}

## Jitayarishe

“Tazama, Naja upesi,”Kristo hutangaza; "Na ujira Wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kadiri kama kazi yake ilivyo.” Ufunuo 22:12. Bwana katika kuja Kwake atachunguza/ataipembua kila talanta; atahitaji faida kwa mtaji aliotukabidhi. Kwa kudhililishwa na uchungu Wake, kwa maisha Yake ya taabu na kifo cha aibu, Kristo amelipa kwa ajili ya huduma ya wote ambao wamelichukua Jina Lake na kukiri kuwa watumishi Wake. Wote wako chini ya wajibu wa mzito wa kuboresha kila uwezo wa kazi ya kuleta roho Kwake. “Ninyi si mali yenu wenyewe,” Anasema; "maana mlinunuliwa kwa thamani;" sasa basi mtukuzeni Mungu kwa maisha ya huduma ambayo yatawaleta wanaume na wanawake kutoka katika dhambi hadi kwenye haki. 1 Wakorintho 6:19, 20. Tumenunuliwa kwa bei ya uzima wa Kristo Mwenyewe, tumenunuliwa ili tumrudishie Mungu walio Wake na yalio Yake, katika utumishi wa uaminifu. {9T 104.1}

Hatuna muda sasa wa kutoa nguvu na talanta zetu kwa miradi ya kidunia. Je, sisi tuzame katika kuutumikia ulimwengu, kujitumikia wenyewe, na kupoteza kisha uzima wa milele na furaha ya milele mbinguni? Lo, hatuwezi kumudu kufanya hivi! Hebu kila talanta itumike katika kazi ya Mungu. Wale ambao huupokea Ukweli, kwa juhudi zao, huongeza idadi ya wanaume na wanawake ambao watakuwa watendakazi pamoja na Mungu. Roho zinapaswa kuangazwa na kufundishwa kumtumikia Mungu kwa akili mahiri; watu wanapaswa kuwa wakizidi kuongezeka katika ujuzi wa haki. {9T 104.2}

Mbingu zote zinapendezwa na kuendeleza mbele kazi ambayo Kristo alikuja kufanya ulimwenguni. Mawakala wa kimbingu wanafungua njia kwa nuru ya Ukweli kuangaza mahali penye giza duniani. Malaika wanasubiri kuwasiliana na wale ambao wataichukua kazi ambayo tumekabidhiwa kwa miaka mingi. Je, sisi

tusionyeshe shauku na nia ya kuweka katika utendaji njia na mali za kuifungua kazi katika miji? Fursa nyingi zimepotea kwa kupuuzia kufanya kazi hii mara moja, kwa kushindwa kusonga mbele kwa imani. Bwana asema: “Kama mngekuwa na imani katika jumbe nilizotuma, kusingekuwa na ukosefu mkubwa wa wafanyakazi na mali za kuwawezesha kwa kuwategemeza." {9T 104.3}

Kuja kwa Kristo kumekaribia na kunafanya haraka sana. Muda wa kufanya kazi ni mfupi, na wanaume na wanawake wanaangamia. Malaika akasema: “Je! Watu wenye nuru kubwa hawapaswi kushirikiana na Yeye aliyemtuma Mwanawe ulimwenguni ili kutoa nuru na wokovu kwa watu?” Je! Watu walioupokea ujuzi wa Ukweli mstari juu ya mstari, amri juu ya amri, hapa kidogo na pale kidogo, wataonyesha kumthamini kidogo tu, Yeye aliyekuja duniani ili uweza Wake wa Mbingu uwe urithi wa kila roho iaminiyo? Ilikuwa ni kwa ajili hiyo kwamba Uungu wa Kristo ulipaswa kuwa na matokeo ya wokovu kwa wanadamu, na maombezi ya Kuhani wetu Mkuu yapae mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Mpango huo ulipangwa mbinguni. Je, wale ambao wamenunuliwa kwa gharama hiyo watashindwa kuuthamini wokovu mkuu? {9T 105.1)

Bwana hawezi kuwakubali watu ambao, wakiukiri utauwa, wakidai kuuamini ujio wa haraka wa Kristo, waiache miji bila kuonywa juu ya hukumu ambazo zitakuja juu ya nchi hivi karibuni. Wale wanaofanya hivi watahukumiwa kwa kupuuza kwao. Kristo alitoa maisha Yake ya thamani ili kuokoa roho zinazoangamia katika dhambi zao. Je, sisi tutakataa kufanya kazi tuliyopewa, tukikataa kushirikiana na Mungu na mawakala wa kimbingu? Kuna maelfu wanaofanya hivi, ambao wanashindwa kuwa wamoja na Kristo, wakishindwa kuruhusu dhabihu kuu ya Kristo kung’aa katika maisha, katika neema iokoayo inayoufunua Ukweli katika matendo ya haki. Lakini hii ndiyo kazi waliyopewa wanadamu kwa dhabihu ya Mwana wa Mungu. Tukijua hili, je, tunaweza kubaki wazembe? Nawasihi ndugu zetu waamke. Uwezo wa kiroho utadhoofika na kufa ikiwa hautafanyiwa kazi katika kuleta roho kwa Kristo. Ni kisingizio gani kinaweza kutolewa kwa kupuuza kazi kubwa, na kuu ambayo Kristo alitoa maisha Yake kuitimiza? {9T 105.2}

Hatuwezi kumudu katika siku chache tulizonazo hapa duniani kutumia muda wetu katika kufanya mambo madogo madogo na kutokufanya kitu au kufanya sifuri. Tunahitaji kunyenyekea nafsi zetu mbele za Mungu, ili kila moyo upate kunywa katika Kweli, na kuiruhusu kufanya maishani matengenezo yatakayoushawishi ulimwengu kwamba hakika huu ndio Ukweli wa Mungu. Hebu maisha yafichwe pamoja na Kristo katika Mungu. Ni pale tu tunapomtafuta Bwana kama watoto wadogo, tunapoacha kutafuta dosari za kaka na dada zetu, na kwa wale wanaotafuta kubeba kwa uaminifu majukumu ya kazi, na kutafuta kuifanya mioyo yetu kuwa sawa na Mungu, Yeye anaweza kututumia kwa utukufu wa Jina Lake. {9T 106.1}

.

Sisi sote tunahitaji kuwa na nafasi ya kujidhabihu mbele za Mungu ili kazi yetu ikubaliwe Naye. Tukumbuke kuwa kukiri tu si kitu isipokuwa tuna Ukweli ndani ya moyo. Tunahitaji nguvu za Mungu za kubadilisha kutushika, ili tupate kuelewa mahitaji ya ulimwengu unaoangamia. Mzigo wa ujumbe wangu kwenu ni huu: Jitayarisheni, jitayarisheni kukutana na Bwana. Washeni taa na utoeni utambi wa zamani wenye masinzi katika taa zenu, na muiache nuru ya Ukweli ing'ae kwenye njia na viunga. Kuna ulimwengu wa kuonywa juu ya ukaribu na mwisho wa mambo yote. {9T 106.2}

Ndugu na dada zangu, mtafuteni Bwana maadam anapatikana. Kuna wakati unakuja ambapo wale ambao walipoteza muda wao na fursa watatamani wangemtafuta Bwana. Mungu amekupa wewe uwezo wa kufikiri na kuchambua mambo. Yeye Anataka uendelee kuwa katika kufikiri na katika kazi. Yeye Anataka uende katika makanisa yetu kufanya kazi kwa bidii kwa ajili Yake. Yeye Anataka uanzishe mikusanyiko kwa wale walio nje ya makanisa, ili watu wapate kujifunza Kweli za ujumbe huu wa mwisho wa onyo. Kuna mahali ambapo utapokelewa kwa furaha, ambapo roho zitakushukuru kwa kuja kuwasaidia. Bwana akusaidie uishikilie kazi hii kwa namna ambayo hujawahi kuishikilia. {9T 106.3}

Hebu tuanze kufanya kazi kwa wale ambao hawajaipata nuru. “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani,” Mwokozi anatangaza, “na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote.” Mathayo 28:18, 20. Tunachohitaji ni imani iliyo hai, imani ya kutangaza juu ya kaburi lililoazimwa kwa Yusufu, na lililofunguka, kwamba tunaye Mwokozi aliye hai, Yeye ambaye atatutangulia mbele yetu na atakayefanya kazi pamoja nasi. Mungu atafanya kazi ikiwa tutampatia nafsi zetu. Kuna haja ya kuwa na maombi mengi miongoni mwetu zaidi kuliko kutokuamini. Tunahitaji kuinua kiwango juu na juu zaidi mbele za watu. Tunapaswa kukumbuka kuwa Kristo Yuko upande wetu wa mkono wa kuume daima, tunapoendelea kuwatangazia wafungwa uhuru na kuzipatia mkate wa uzima roho zenye njaa. Tukiweka akilini mwetu jinsi kazi yetu ilivyo ya dharura, na umuhimu wa kazi yetu, wokovu wa Mungu utafunuliwa kwa namna ya ajabu, itakayonasa mawazo ya watu. {9T 107.1}

Mungu atusaidie tuzivae silaha na kutenda kana kwamba tuna bidii, kana kwamba ni roho za watu na wanawake zilikuwa na thamani ya kuokolewa. Hebu tutafute uongofu mpya. Tunahitaji uwepo wa Roho Mtakatifu wa Mungu pamoja nasi, ili mioyo yetu ipate kulainika na tusije tukaileta roho mbaya na yenye ukali katika kazi. Ninaomba kwamba Roho Mtakatifu aweze kuitawala mioyo yetu kikamilifu. Hebu na tuenende kama watoto wa Mungu ambao wanamtazamia kwa ajili ya ushauri, walio tayari kufanya mipango Yake popote inapowasilishwa. Mungu atatukuzwa na watu kama hao, na wale wanaoshuhudia bidii yetu watasema:

Amina na amina. {9T 107.2}

Amka, amka; jivike nguvu zako, Ee Sayuni; jivike mavazi yako mazuri, Ee Yerusalemu, Mji Mtakatifu…….Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima miguu yake aletaye habari njema, yeye aitangazaye amani; aletaye habari njema ya mambo mema, yeye autangazaye wokovu; auambiaye Sayuni, Mungu wako anamiliki! Sauti ya Walinzi wako, wanapaza sauti zao; wanaimba pamoja, maana wataona jicho kwa jicho, jinsi BWANA arejeavyo Sayuni. {9T 108.1}

Pigeni kelele za furaha, imbeni pamoja, enyi mahali pa Yerusalemu palipokuwa ukiwa,kwa kuwa Bwana amewafariji watu Wake, Ameukomboa Yerusalemu. Bwana ameweka wazi mkono Wake mtakatifu machoni pa mataifa yote; na ncha zote za dunia zitauona wokovu wa Mungu wetu.” Isaya 52:1-10. {9T 108.2}

## SURA YA 12
## MBINU ZA KAZI

Kuhusiana na kutangazwa kwa ujumbe katika miji mikubwa, kuna aina nyingi za kazi ifanywe na watenda kazi wenye karama mbalimbali. Wengine wanapaswa kufanya kazi kwa njia hii, na wengine kwa njia ile. Bwana anatamani kwamba miji ifanyiwe kazi kwa juhudi za pamoja za watendakazi wenye uwezo tofauti-tofauti. Wote wanapaswa kumwangalia Yesu kwa uongozi na mwelekezo, wasimtegemee mwanadamu kwa hekima, wasije wakapotoshwa. Kama watenda kazi pamoja na Mungu wanapaswa kutafuta kuwa katika umoja wao kwa wao. Kunapaswa kuwe na mabaraza ya mara kwa mara na ushirikiano wa dhati, wa moyo wote. Hata hivyo wote wanapaswa kumtegemea Yesu ili kupata hekima, si kutegemea wanadamu peke yake kwa maelekezo. {9T 109.1}

Bwana amewapa baadhi ya watumishi uwezo wa kukusanya na kufanya mikutano mikubwa. Hii inahitaji matumizi ya busara na ujuzi. Katika miji ya leo, ambapo kuna mengi ya kuvutia na kufurahisha, watu wanaweza wasipendezwe na juhudi za kawaida. Watendakazi walioteuliwa na Mungu wataona ni muhimu kufanya hivyo, ili kuweka juhudi zisizo za kawaida katika kuvutia umakini wa umati. Na wanapofanikiwa katika kuleta pamoja idadi kubwa ya watu wanapaswa kuutoa ujumbe wa tabia nje kwa namna ya kawaida ambayo watu wataamshwa na kuonywa. Ni lazima watumie njia zote zinazowezekana kubuniwa kwa ajili ya kusababisha Ukweli uonekane wazi na kwa udhahiri. Ujumbe unaopima, kwa

wakati huu unapaswa kutolewa kwa uwazi na kwa kudharimia kiasi cha kuwashtua wasikilizaji na kuwaongoza kutamani kujifunza na kuyachunguza Maandiko. {9T 109.2}

Wale wafanyao kazi ya Bwana katika miji lazima waweke juhudi za utulivu, thabiti, za kujitolea kwa ajili ya elimu za watu. Ingawa wanapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kuvutia wasikilizaji na kuushikilia usikivu huu, bado wakati huo huo lazima wajilinde kwa uangalifu dhidi ya kitu chochote kinachopatana na mihemko/misukumo. Katika zama hizi za ubadhirifu na kujionesha kwa mambo ya nje, wakati watu wanafikiri ni muhimu kufanya maonyesho ili kupata kufanikiwa/mafanikio, wajumbe walioteuliwa, wa Mungu wanapaswa kuonesha udanganyifu wa njia za matumizi ya mali bila ulazima. Kadri wanavyofanya kazi kwa usahili, unyenyekevu, uungwana na utu wa neema, wakiepuka kila kitu chenye asili ya maburudusho yenye maonyesho, kazi yao itakuwa na matokeo yenye mguso wa moyo wa kudumu kwa mema. {9T 109.3}

Kuna ulazima, ni kweli, wa kutumia pesa kwa busara katika kutangaza mikutano na katika kuendeleza kazi kwa uthabiti. Hata hivyo nguvu za kila mfanyakazi zitaonekana kusema uongo, si katika hawa mawakala wa nje, bali kwa kumtegemea Mungu kwa uaminifu, katika maombi ya dhati na bidii Kwake kwa ajili ya msaada, katika utii kwa Neno Lake. Maombi mengi zaidi, mengi sana, kufanana na Kristo, kupatana zaidi na mapenzi ya Mungu, kunapaswa kuletwa katika kazi ya Bwana. Maonyesho ya nje na matumizi mabaya ya mali (ubaradhifu) hayatafanikisha kazi inayopaswa kufanywa. {9T 110.1}

Kazi ya Mungu inapaswa kuendelezwa kwa nguvu. Tunahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tunahitaji kukuelewa kwamba Mungu ataongeza kwenye safu za watu Wake watu wenye uwezo na ushawishi ambao wanapaswa kufanya sehemu yao katika kuuonya ulimwengu. Wote ulimwenguni si waasi na wenye dhambi. Mungu ana maelfu wengi ambao hawajapiga goti kwa Baali. Kuna wanaume na wanawake wanaomcha Mungu katika makanisa yaliyoanguka. Ikiwa isingelikuwa hivyo, hatungelipewa ujumbe wa kubeba: "Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu.... tokeni kati yake, enyi watu Wangu." Ufunuo 18:2-4. Wengi wenye moyo wa uadilifu wanahema kwa ajili ya kukosa pumzi ya uzima kutoka mbinguni. Watatambua injili inapoletwa kwao katika uzuri na usahili unaoonyeshwa kwa njia ya Neno la Mungu. {9T 110.2}

## Hitaji la Kazi ya Nyumba kwa Nyumba

Kwa umuhimu sawa na mahubiri ya hadhara ni kazi ya nyumba kwa nyumba katika makazi ya watu. Katika miji mikubwa kuna makundi fulani ambayo hayawezi kufikiwa na mikutano ya hadhara. Hawa lazima watafutwe kote kama mchungaji anavyowatafuta kondoo wake waliopotea. Bidii, na juhudi binafsi lazima ziwekwe kwa niaba yao. Wakati kazi ya binafsi inapopuuzwa, fursa nyingi za thamani zinapotea, ambazo kama zingeboreshwa, zingeendeleza kazi bila kwa uhakika na bila kukosea. {9T 111.1}

Kama matokeo ya uwasilishaji wa Ukweli katika mikutano mikubwa, roho ya utafiti inaamshwa, na ni muhimu hasa kwamba shauku hizi zifuatiliwe kwa kazi ya binafsi. Wale wanaotamani kuichunguza Kweli wanahitaji kufundishwa kujifunza Neno la Mungu kwa bidii. Mtu lazima awasaidie kujenga juu ya msingi wa uhakika. Katika wakati huu muhimu katika uzoefu wao wa kidini, ni muhimu jinsi gani kwamba watendakazi wa Biblia walioelekezwa kwa hekima huja kuwasaidia na kuwafungulia katika uelewa wao hazina za nyumba ya Neno la Mungu. {9T 111.2}

### Utume wa miji ni Shule ya Mafunzo

Kazi nzuri linganifu inaweza kufanywa vizuri zaidi pale shule ya mafunzo kwa watendakazi wa Biblia inapokuwa ikiendelea. Wakati mikutano ya hadhara inafanywa, inapaswa kuunganishwa na shule hii ya mafunzo au utume wa miji kwa watendakazi wenye uzoefu, wenye ufahamu wa kina wa kiroho ambao wanaweza kuwapa watendakazi wa Biblia maelekezo ya kila siku na ambao wanaweza pia kuungana kwa moyo wote katika juhudi za hadhara zinazoendela kufanywa. Na kadri wanaume na wanawake wanavyougeukia Ukweli, wale wanaosimama kama viongozi wa utume wa miji wanapaswa kuwaonyesha waongofu hawa wapya, kwa maombi mengi, jinsi ya kupata uzoefu wa nguvu ya Ukweli katika maisha yao. Juhudi hizi za umoja kwa upande wa watendakazi wote itakuwa kama msumari uliopigiliwa mahali pa uhakika {9T 111.3}

### Kufundisha Kanuni za Matengenezo ya Afya

Kama watu tumepewa kazi ya kujulisha kanuni za matengezo ya afya. Kuna baadhi ambao wanafikiri kwamba suala la lishe halina umuhimu wa kutosha kuingizwa katika kazi yao ya uinjilisti. Lakini hawa hufanya kosa kubwa. Neno la Mungu linasema: Basi mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.” 1Wakorintho 10:31. Mada ya kuwa na kiasi, katika mambo yote, lina nafasi muhimu katika kazi ya wokovu. {9T 112.1}

Sambamba na utume mijini kunapaswa kuwa na vyumba vinavyofaa ambapo wale wanaovutiwa na shauku zao zimeamshwa wanaweza kukusanywa kwa mafundisho. Kazi hii ya lazima si ya kufanyika katika njia dhaifu au kubana matumizi ambako kutaleta hisia zisizofaa hisia kwenye akili za watu. Yote

yanayofanyika inapaswa yatoe ushahidi mzuri kwa Muumbaji wa Ukweli na inapaswa kuwakilisha ipasavyo utakatifu na umuhimu wa Kweli za ujumbe wa malaika watatu. {9T 112.2}

Shule za upishi zinapaswa kuanzishwa (mafunzo ya mapishi). Watu wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuandaa chakula kizuri. Wanapaswa kuoneshwa hitaji la kuacha vyakula visivyofaa. Lakini hatupaswi kamwe kutetea milo mibovu yenye lishe pungufu, au chakula kisichotosha, kila siku. Inawezekana kuwa na lishe bora, yenye virutubisho bila kutumia chai, kahawa, na chakula cha nyama/samaki. Kazi ya kufundisha watu jinsi ya kuandaa lishe ambayo ni nzuri na ya kupendeza ni ya umuhimu mkubwa. {9T 112.3}

Kazi ya matengenezo ya afya ni njia ya Bwana kupunguza mateso katika ulimwengu wetu na kulitakasa kanisa Lake. Wafundishe watu kwamba wanaweza kutenda kama mkono wa kusaidia wa Mungu kwa kushirikiana na Mwalimu mkuu katika kurejesha afya ya kimwili na kiroho. Hii kazi ina muhuri wa mbinguni na itafungua milango kwa ajili ya kuingia kwa Kweli zingine za thamani. Kuna nafasi kwa wote kufanya kazi ambao wataishikilia kazi hii kwa akili mahiri. {9T 112.4}

Weka mbele kazi ya matengenezo ya afya, ndio ujumbe nimeelekezwa kuubeba. Onesha kwa uwazi sana thamani yake kiasi kwamba hitaji la ueneaji wake kila mahali litahisiwa. Kujiepusha kabisa na vyakula na vinywaji vyote vyenye madhara ni matunda ya dini ya Kweli. Yule ambaye ameongoka kabisa atatupilia mbaya kila tabia mbaya inayodhuru na uchu wa chakula. Kwa kujiepusha kabisa na vitu hivyo vibaya, atashinda tamaa yake ya kuridhisha anasa zinazoharibu afya (pombe, sigara, chai ya nyeusi, kahawa, ugoro nk). {9T 113.1}

Nimeagizwa kuwaambia wakufunzi wa matengenezo ya afya: Songeni mbele. Ulimwengu unahitaji kila nukta ya ushawishi mnaoweza kuwa nao ili kurudisha nyuma wimbi la ole wa maadili. Hebu wale wanaoufundisha ujumbe wa malaika wa tatu wasimame kweli kwa rangi zao. “Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma Zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Na msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.” Warumi 12:1. Mungu na awaimarishe na kuwavisa silaha wale wafanyao kazi katika Neno na mafundisho, wenye ujumbe wa Kweli ulio wazi zaidi. Ikiwa watenda kazi Wake watatoa huu ujumbe kwa usahili, uhakika, na mamlaka yote, Bwana atafanya kazi nao. {9T 113.2}

### Tabaka La Matajiri Kamwe Lisipitwe au Kuachwa Kando

Watumishi wa Kristo wanapaswa kufanya kazi kwa uaminifu kwa ajili ya matajiri

katika miji yetu, pamoja na maskini na na kwa watu wa chini. Kuna watu wengi walio matajiri ambao wanaweza kuathiriwa na mvuto na hisia za ujumbe wa injili na ambao, wakati Biblia, na Biblia pekee, imewasilishwa kwao kama mfafanuzi wa Imani ya Kikristo na matendo, watasukumwa na Roho wa Mungu kufungua milango kwa ajili ya maendeleo ya injili. Wataifunua imani iliyo hai katika Neno la Mungu na watatumia mali walizokabidhiwa kuitayarisha njia ya Bwana, kuinyosha jangwani njia kuu kwa Mungu wetu. {9T 113.3}

Kwa miaka mingi swali la kutatanisha limekuwa mbele yetu: Tunawezaje kupata fedha zinazotosheleza ili kusaidia utume ambao Bwana ameuweka mbele yetu kuufunua? Tunalisoma wazi agizo la injili; na la utume, pote katika maeneo ya nyumbani na ya nje ya nchi, huwasilisha mahitaji yao. Viashiria, na mafunuo chanya ya mibaraka, huungana nasi katika kutuhimiza kufanya haraka kazi ambayo inatakiwa kufanywa. Bwana anahitaji kwamba watu wenye pesa wataongoka na kutenda kama mkono Wake wa msaada katika kuwafikia wengine. Yeye Anatamani kwamba wale wanaoweza kusaidia katika kazi ya matengenezo na urejeshaji waione nuru iliyo ya thamani ya Ukweli na kugeuzwa tabia na kuongozwa kutumia mali zao walizokabidhiwa katika utumishi Wake. Bwana huwataka wawekeze mali alizowaazima, katika kutenda mema, katika kufungua njia kwa ajili ya injili kuhubiriwa kwa watu wa tabaka zote za karibu na za mbali. {9T 114.1}

Je! mbingu haitathaminiwa na wenye hekima wa kiulimwengu? Oh, ndiyo; huko watapata raha na amani na kutulia kutoka katika mambo madogo madogo, tamaa zote, na kujitumikia mwenyewe. Wahimize hawa watu kutafuta amani, furaha na shangwe ambayo Kristo anatamani kuwapa. Wahimize kuweka mkazo wao katika kutafuta karama ya thamani zaidi ambayo inaweza kutolewa kwa mwanadamu anayeweza kufa - vazi la haki ya Kristo. Kristo huwapa uzima unaopimwa kama uzima wa Mungu (milele), na utukufu wa milele uzidio kupita kiasi. Kama wakimkubali Kristo watakuwa na heshima kuu, heshima ambayo ulimwengu hauwezi kutoa wala kuiondoa. Watatambua kuwa katika ushikaji/utunzaji wa amri za Mungu kuna thawabu kubwa. {9T 114.2}

Mkombozi Mwenye huruma anawaagiza watumishi Wake wawape matajiri na maskini wito wa kula mezani pake. Nendeni nje kwenye barabara kuu na njia njia, na kwa bidii yenu ya kudumu, isiyozimia, washurutisheni kuja ndani. Hebu watumishi wa injili wawazingatie watu hawa wenye pesa za kidunia na kuwaleta kwenye karamu ya Ukweli ambayo Kristo amewaandalia. Yeye aliyetoa uhai Wake wa thamani kwa ajili yao anasema: Waleteni ndani na kuwaketisha kwenye meza Yangu, Nami nitawahudumia." {9T 115.1}

Watumishi wa Kristo, jiungenisheni na tabaka hili. Usiwapite kama watu wasio na tumaini. Fanya kazi kwa ushawishi wote unaowezekana, na kama matunda ya juhudi zako za uaminifu utaona katika ufalme wa mbinguni wanaume na

wanawake watakaotawazwa kuwa washindi ili kuuimba wimbo wa ushindi. "Nao watakwenda pamoja Nami hali wamevaa mavazi meupe," asema Yeye aliye Mwanzo na Mwisho, "kwa kuwa wamestahili." Ufunuo 3:4. {115.2}

Pamoja nao, juhudi ndogo sana imefanywa kwa watu wenye vyeo ulimwenguni. Wengi wao wana sifa za juu zaidi; wana mali na ushawishi. Hizi ni karama za thamani, zilizokabidhiwa kwao na Mungu ili ziongezwe na kutumiwa kwa manufaa ya wengine. {9T 115.3}

Tafuta kuwaokoa watu wenye mali. Uwasihi kumrudishia Bwana hazina alizowakopesha kwa uaminifu, ili kwamba huko New York na miji mingine mikuu kunaweza kuwa na vituo ya mvuto vilivyoanzishwa ili katika huo Ukweli wa Biblia katika usahili wake utaenea kwa watu. Wasihi watu kuweka hazina zao katika kiti cha enzi cha Mungu kwa kumrudishia Bwana mali zao, ili kuwawezesha watenda kazi Wake kutenda mema na kuuendeleza utukufu Wake. {9T 115.4}

## Mipango ya Kuongeza Nguvu Kazi zetu

Nguvu ya jeshi hupimwa kwa kiasi kikubwa na ufanisi wa watu katika safu. Kamanda mwenye busara anawaagiza maafisa wake kumfundisha kila askari kwa ajili ya utumishi imara. Anatafuta kukuza ufanisi wa hali ya juu kwa upande wa wote. Kama angewategemea maafisa wake pekee, hangeweza kutarajia kufanya kampeni yenye mafanikio. Anahesabu utumishi mwaminifu na usiochoka kutoka kwa kila mtu katika jeshi Lake. Wajibu unawategemea zaidi watu walio katika safu. {9T 116.1}

Na ndivyo lilivyo katika jeshi la Mfalme Immanuel. Kamanda wetu, ambaye hajawahi kushindwa vita, anatarajia huduma ya hiari na uaminifu kutoka kwa kila mtu ambaye amejiandikisha chini ya bendera Yake. Katika pambano la kufunga sasa Akipigana kati ya majeshi ya wema na majeshi ya uovu, Yeye Anawatazamia wote, watu wa kawaida yaani walei, pamoja na watendakazi wa kanisa walioajiriwa kukuchua nafasi. Wote ambao wamejiandikisha kama askari Wake, wanapaswa kutoa huduma ya uaminifu kama askari wenye kasi, wakiwa na uelewa wa kina wa wajibu ulio juu yao binafsi. {9T 116.2}

Wale walio na jukumu la uangalizi wa kiroho kwa kanisa wanapaswa kubuni mbinu na njia ambazo kwazo nafasi zinaweza kutolewa kwa kila mshiriki wa kanisa kutenda sehemu fulani katika kazi ya Mungu. Mara nyingi sana, siku za huko nyuma, hili limekuwa halifanyiki. Mipango haijawekwa wazi na kutekelezwa kikamilifu ambapo karama za wote zinaweza kuingizwa katika utendaji wa huduma. Ni wachache tu wanaotambua ni upotevu gani umeletwa kwa kufanya hivi. {9T 116.3}

Viongozi katika kazi ya Mungu, kama majenerali/majemedari wenye hekima, wanapaswa kuweka mipango ya hatua za mapema katika haya yote. Katika

mipango yao wanapaswa kujifunza na kuchunguza kazi inayoweza kufanywa na waumini/walei kwa marafiki na majirani zao. Kazi ya Mungu katika dunia hii haiwezi kuisha kamwe hadi wanaume na wanawake wanaounda ushirika wa kanisa letu wamejikusanya kwa kazi na kuunganisha juhudi zao na zile za wachungaji na maofisa wa kanisa. {9T 116.4}

Wokovu wa wenye dhambi unahitaji bidii ya kazi binafsi. Tunapaswa kupeleka kwao neno la uzima, sio kuwasubiri waje kwetu. Laiti ningeweza kusema maneno kwa wanaume na wanawake ambayo yangewaamsha kufanya kazi kwa bidii! Nyakati tulizopewa sasa ni chache. Tunasimama juu mipaka ya ulimwengu wa milele. Hatuna muda wa kupoteza. Kila wakati ni wa dhahabu na wa thamani sana kutumiwa tu kwa kuitumikia -nafsi. Ni akina nani watamtafuta Mungu kwa dhati n abidii na kupata nguvu kutoka Kwake na neema ya kuwa watendakazi Wake waaminifu katika maeneo ya umishenari? {9T 117.1}

### Ukuzaji wa Vipaji Makanisani

Katika kila kanisa kuna talanta, ambazo, kwa aina ya kazi ifaayo, zinaweza kukuzwa na kuwa na msaada mkubwa katika kazi hii. Kinachohitajika sasa kwa ajili ya ujenzi wa makanisa yetu ni kazi nzuri ya watenda kazi wenye busara ili kutambua na kukuza talanta katika kanisa, talanta ambazo zinaweza kuelimishwa kwa ajili ya kutumiwa na Bwana. Kuwe na mpango uliopangwa vizuri wa kuwaajiri watendakazi kwenda katika makanisa yetu yote, makubwa kwa madogo, kuwaelekeza washiriki jinsi ya kufanya kazi kwa ajili ya kulijenga kanisa na pia kwa ajili ya wasioamini. Ni mafunzo, na elimu, ambavyo vinahitajika. Wale wanaofanya kazi katika kutembelea makanisa wanapaswa kuwapatia ndugu na akina dada mafundisho katika njia za vitendo za kufanya kazi ya umishionari. {9T 117.2}

l Rally workers who possess true missionary zeal, and let them go forth to diffuse light and knowledge far and near. Let them take the living principles of health reform into the communities that to a l

Mahubiri yote ulimwenguni hayatawafanya watu wahisi uhitaji wa roho zinazoangamia kando yao. Hakuna kitakachoamsha bidii ya kujitoa nafsi kwa wanaume na wanawake kama kuwapeleka katika maeneo mapya ya kazi kwenye watu walio gizani. Tayarisha watendakazi kwenda kwenye njia kuu na vichochoroni. Tunahitaji wapanda-vitalu vya miti wenye busara, ambao watapandikiza miti katika maeneo mbalimbali na kuisaidia ili iweze kukua (transplant nursery) Ni wajibu chanya kwa watu wa Mungu kwenda katika

maeneo ya nje na mbali. Hebu majeshi yawekwe kazini kusafisha eneo jipya, kuanzisha vituo vipya vya mvuto popote ambapo vinapoweza kufunguliwa. Wahamasishe Watendakazi walio na ari ya kweli ya kimishenari kuja pamoja kuunga mkono kazi hii, hebu hawa na waachwe waende kueneza nuru na maarifa mbali na karibu. Acha wachukue kanuni hai za matengenezo ya afya katika jamii ambazo kwa kiwango kikubwa hawazijui kanuni hizi. {9T 117.3}

Watu walio katika hali duni za maisha wanapaswa kutiwa moyo kuifanya kazi ya Mungu. Kadri wanavyofanya kazi ndivyo watakavyopata uzoefu wa thamani. Kuna upungufu wa watendakazi, na hatuna yeyote wa kumwacha akae bila kazi. Badala ya kuwakatisha tamaa wale wanaojaribu kumtumikia Bwana, tunapaswa kuwatia moyo watenda kazi wengi zaidi kuingia shambani mwa Bwana. {9T 118.1}

### Huduma ya Shangwe

Wote wanaowasiliana na Mungu watapata kazi nyingi za kumfanyia. Wale wanaotenda katika Roho wa Bwana, wakitafuta kuzifikia roho kwa ile Kweli, hawataona kazi ya kuleta roho kwa Kristo ni ya kusumbua, duni, inayoboa na isiyovutia. Wanachajiwa kana kwamba kwa umeme na kazi ya kuwa kama wakulima wa Mungu, nao watakuwa wenye nguvu zaidi na zaidi wanapojitoa katika utumishi wa Mungu. Ni kazi ya shangwe kuwafunulia wengine Maandiko. {9T 118.2}

Vijana wa kiume na wa kike wanapaswa kuelimishwa ili kuwa watendakazi katika maeneo yao na katika maeneo mengine. Hebu wote waweke mioyo na akili zao kuwa na akili mahiri kuhusiana na kazi ya wakati huu, wakijistahilisha wenyewe kufanya yale ambayo kwayo wameweza kufanywa bora na kuchukuliana nayo kwa ufanisi. {9T 118.3}

Vijana wengi ambao wamekuwa na aina sahihi ya elimu nyumbani wanapaswa kufunzwa kwa ajili ya huduma na kutiwa moyo kuinua kiwango cha Ukweli katika maeneo mapya kwa kazi iliyopangwa vizuri na ya uaminifu. Kwa kushirikisha pamoja na watumishi wetu na watendakazi wenye uzoefu katika kazi za mijini, watapata aina bora ya mafunzo. Wakitenda kazi chini ya mwongozo wa Mungu na kuungwa mkono na maombi ya watendakazi wenzao wenye uzoefu zaidi, wanaweza kufanya kazi nzuri na yenye baraka. Wanapounganisha utumishi wao na ule wa watendakazi wenye umri mkubwa, kwa kutumia nguvu zao za ujana kwa ubora kabisa, watakuwa na ushirika wa malaika wa mbinguni; na kama watendakazi pamoja na Mungu, ni fursa yao kuimba na kuomba na kuamini, na kufanya kazi kwa ujasiri na uhuru. Ujasiri na imani ambao uwepo wa mawakala wa mbinguni utaleta kwao na kwa watendakazi wenzao, utawaongoza kwenye sala na sifa na usahili wa imani ya Kweli. {9T 119.1}

Haipaswi kuwa na kuchelewa katika juhudi hii iliyopangwa vizuri ya kuwaelimisha

washiriki wa kanisa. Watu wanapaswa kuchaguliwa kufanya kazi katika miji mikubwa, watu waliojitoa wakfu kikamilifu na ambao wanaelewa utakatifu na umuhimu wa kazi hii. Msiwatume wale ambao hawana sifa katika mambo haya. Watu wanahitajika ambao watausukuma ushindi wa msalaba, ambao watavumilia katika kukatishwa tamaa na hali ngumu na umasikini, wale watakaokuwa na bidii na kuazimia, na imani ambayo ni ya lazima katika eneo la umishenari. Na kwa wale ambao binafsi, hawajishughulishi katika kazi ningesema: Msiwazuie wale wengine ambao wako tayari kufanya kazi, lakini muwatie moyo na kuwaunga mkono. {9T 119.2}

Kazi hii yote ya mafunzo inapaswa kuambatana na kumtafuta Bwana kwa bidii kwa ajili ya Roho Wake Mtakatifu. Hebu hili lihimizwe nyumbani kwa wale walio tayari kujitoa kwa ajili ya utumishi wa Bwana. Mwenendo wetu unatazamwa na ulimwengu. Kila kitendo linachunguzwa na kutolewa maoni. Lazima kuwe na utendaji wa bidii wa neema za Kikristo, ili wale wanaoukiri Ukweli waweze kuwafundisha wengine kama ilivyo ndani Yesu, ili wao wenyewe wawe vielelezo, kisha adui zetu wasiweze kwa uaminifu kusema lolote baya juu yao. Mungu anatutaka tuwe na utauwa zaidi, utakatifu wa maisha na usafi wa mwenendo, kulingana na kanuni ziinuazo, kanuni za utakaso tunazozikiri. Maisha ya watenda kazi wa ajili ya Kristo yanapaswa kuwa yale ambayo, wale wasioamini, wakiona mwenendo wao wa kumcha Mungu, na kuyatazama mazungumzo yao, wapate kuvutwa kama kwa sumaku na imani hiyo iletayo matokeo kama haya. {9T 119.3}

### Juhudi Za Binafsi Kuhusiana Na Mikutano Ya Makambi

Kazi katika mikutano yetu ya kambi inapaswa kuendeshwa, si kulingana na usanifu wa mwanadamu, bali kufuatisha namna ya utendaji kazi wa Kristo. Washiriki wa kanisa wanapaswa kuvutwa kufanya kazi ya Bwana. Malaika wa Mungu watawaelekeza katika ufunguzi wa maeneo yaliyo karibu na ya mbali, ili kazi ya kuuonya ulimwengu iwe imekamilika kwa haraka. Mungu anawaita waaminio kupata uzoefu katika kazi ya umishenari kwa kugawanyika katika eneo jipya na kufanya kazi kwa akili kwa watu katika njia za vichochoroni. Kwa wale ambao watafanya hivi, nafasi za kazi zitakuja. {9T 120.1}

Katika kufuatilia mambo baada ya mkutano wa kambi, wasaidizi wanahitajika katika stadi mbalimbali, na tasnia hizi zinapaswa kuwa kama shule za mafunzo kwa watendakazi. Hebu vijana wafanye kazi kwa kushirikiana na watenda kazi wenye uzoefu ambao watakaomba pamoja nao na kuwafundisha kwa subira. Wanawake waliowekwa wakfu wanapaswa kushiriki katika kazi ya Biblia-Mafunzo ya Biblia, nyumba kwa nyumba. Baadhi ya wafanyakazi wanapaswa kuwa wainjilisti wa vitabu, wakiuza machapisho yetu na kutoa kwa busara kwa wale ambao hawawezi kununua. {9T 120.2}

Wale ambao wameongoka kweli kweli lazima wawe na akili mahiri zaidi na zaidi katika ufahamu wao wa Maandiko, ili waweze kunena Maneno ya nuru na wokovu kwa wale walio gizani, nawanaoangamia katika dhambi zao. Kama watendakazi pamoja na Mungu tunapaswa kutarajia baraka maalum na matokeo ya uhakika tunapojitahidi kuokoa roho kutoka kwenye mitego ya Shetani ili wapate kuwa wana wa nuru. {9T 121.1}

### Vituo vya Watalii na Vituo vya Biashara

Wale ambao kwa kuitikia wito wa saa walioingia katika huduma ya Mtendakazi Mkuu, wajifunze vema mbinu zake za kazi. Wakati wa huduma Yake duniani Mwokozi alitumia fursa zilizopatikana kando ya njia kuu za usafiri. Yesu alikaa Kapernaumu katika vipindi vya safari Zake kwenda huku na kule, na ukaja kujulikana kama "mji Wake Mwenyewe". Mji huu ulikuwa mzuri na ukichukuliwa kuwa kitovu cha kazi ya Mwokozi. Ikiwa kwenye barabara kuu kutoka Dameski kwenda Yerusalemu na Misri, na hadi Bahari ya Mediterania, ilikuwa njia kuu ya usafiri. Watu kutoka nchi nyingi walipita katikati ya Mji au walisubiri kwa muda mfupi, na hata kupumzika katika safari zao za kwenda huku na huko. Hapa Yesu aliweza kukutana na watu wote, wa nyadhifa zote, matajiri kwa wakuu, pia maskini na wa hali ya chini; na mafundisho Yake yangebebwa kwenda nchi nyingine na katika familia nyingi. Hivyo Uchunguzaji wa unabii ungesisimua watu; na usikivu ungeelekezwa kwa Mwokozi, na utume Wake ungepelekwa mbele ya ulimwengu. {9 T121.2}

Katika zama hizi za safari nyingi, fursa za kukutana na wanaume na wanawake wa tabaka zote na wa mataifa mengi ni kubwa zaidi kuliko katika siku za Israeli. Njia za usafiri zimeongezeka mara elfu. Mungu kwa ajabu ameandaa njia. Wakala wa nyumba ya uchapishaji, pamoja na vifaa vyake vingi, iko katika amri yetu. Biblia, na machapisho katika lugha nyingi, vinavyoeleza Kweli ya wakati huu, viko mikononi mwetu na vinaweza kupelekwa upesi katika kila sehemu ya dunia. {9T 121.3}

Wakristo wanaoishi katika vituo vikuu vya biashara na vya usafiri wana fursa maalum. Waumini katika miji hii wanaweza kufanya kazi kwa ajili ya Mungu katika ujirani wa nyumba zao. {9T 122.1}

Katika vituo vya afya maarufu duniani kote na vituo vya watalii wanaosafiri, vilivyojaa maelfu ya watu wanaotafuta afya na starehe, hebu pawepo na watumishi na wainjilsti wa vitabu walio na uwezo wa kuukamata umakini wa umati wa watu. Hebu watendakazi hawa wawe macho kwa fursa na nafasi zao za kuwasilisha ujumbe wa wakati huu, na kufanya mikutano kadiri wanavyopata fursa. Hebu wawe wepesi wa kukamata fursa ya kuzungumza na watu. Wakisukumwa na nguvu za Roho Mtakatifu, hebu wakutane na watu wakiwa na ujumbe uliotolewa na Yohana Mbatizaji: "Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni

umekaribia."Mathayo 3:2. Neno la Mungu linapaswa kuwasilishwa kwa uwazi na nguvu, ili wale walio na masikio ya kusikia waweze kuusikia Ukweli. Hivyo injili ya Ukweli wa sasa itawekwa katika njia ya wale ambao hawaijui, na itakubaliwa, sio na wachache tu, bali hatimaye itapelekwa nao kwa wengi, hadi majumbani mwao katika sehemu zote za nchi za dunia. {9T 122.2}

## Kwa Bidii Isiyokoma

Tunapaswa kulitoa onyo la mwisho la Mungu kwa wanadamu, na bidii yetu inapaswa kuwaje katika kujifunza Biblia na katika kuieneza nuru! Hebu kila nafsi iliyopokea nuru ya mbingu itafute kuiangaza. Hebu watenda kazi waende nyumba kwa nyumba, wakiifungua Biblia kwa watu, wakiyasambaza machapisho, wakiwaambia wengine juu ya nuru ambayo imebariki roho zao wenyewe. Hebu na vitabu visambazwe kwa busara, kwenye treni, barabarani, kwenye meli kubwa zinazozunguka baharini, na kupitia barua (hata mtandaoni). {9T 122.3}

Kazi kubwa inapaswa kufanywa, na wale wanaoujua Ukweli wanapaswa kuwa na maombezi makuu ili kusaidia. Upendo wa Kristo lazima ujaze mioyo yao wenyewe. Roho wa Kristo lazima amwagwe juu yao, na lazima wawe wanajitayarisha kusimama katika hukumu. Kadri wanavyojiweka wakfu kwa Mungu, nguvu isadikishayo itazifikia jitihada zao za kuwasilisha Ukweli kwa wengine. Hatupaswi kulala tena katika utawala wa Shetani wenye sumaku zake, bali tutumie rasilimali zetu zote, tukitumia kila kitu ambcho tumejaliwa kupewa. Onyo la mwisho linapaswa kutolewa juu ya "juu ya watu na taifa, na lugha, na wafalme wengi," na ahadi inatolewa, "Tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata mwisho wa dahari." Ufunuo 10:11; Mathayo 28:20. {9T 123.1}

Nimeagizwa kuwaelekeza watumishi wetu kwenye miji ambayo haijafanyiwa kazi na kuwasihi kwa kila inayowezekana kufungua njia kwa ajili ya kuuwasilisha Ukweli. Katika baadhi ya miji ambapo ujumbe wa ujio wa pili wa Bwana ulikuwa umeshatolewa kabla, tunasukumwa kuichukua kazi kana kwamba ni eneo mpya. Je, ni mpaka lini haya maeneo tasa, miji hii isiyofanyiwa kazi itaendelea kuachwa? Bila kuchelewa upandaji wa mbegu unapaswa kuanza katika sehemu nyingi, nyingi sana. {9T 123.2}

Bwana anataka kwamba ndani ya watumishi Wake zipatikane roho ambazo ni nyepesi za kuhisi thamani ya roho za watu, nyepesi za kutambua wajibu unaopaswa kufanywa, nyepesi za kuitikia wajibu ambao Bwana ameweka juu yao. Ni lazima kuwe na kujitolea ambako hakutajali maslahi ya kidunia, yenye thamani ya kutosha kuchukua nafasi ya kazi inayopaswa kufanywa katika kuzileta nafsi kwenye ujuzi wa Ukweli. {9T 123.3}

Watumishi, hubirini Kweli zitakazopelekea kazi ya binafsi kwa wale walio nje ya Kristo. Himiza juhudi binafsi kwa kila namna iwezekanayo. Kumbuka kwamba kazi ya mtumishi haihusishi kuhubiri pekee. Anapaswa kutembelea familia majumbani mwao, kuomba nao, na kuwafunulia Maandiko. Anayefanya kazi ya uaminifu nje ya mimbari atafanikiwa mara kumi zaidi ya yule afanyaye kazi zake kwenye kibweta. Hebu watumishi wetu wabebe mzigo wao wa majukumu kwa hofu na wakitetemeka, wakimtazamia Bwana kwa hekima na kuomba daima neema Yake. Hebu wamfanye Yesu kuwa mfano wao, wasome kwa bidii maisha Yake na kuleta katika mazoezi ya kila siku kanuni ambazo zilimchochea Yeye katika utumishi Wake akiwa duniani. {9T 124.1}

"Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha." Hii ni tiba kwa uponyaji wa magonjwa yote ya kiakili na kimwili na kiroho. Ni karama ya Kristo kwa wale wanaomtafuta kwa uaminifu na Ukweli.
Yeye Ndiye Tabibu Mkuu. Kisha unakuja mwaliko mwingine: “Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira Yangu ni rahisi, na mzigo Wangu ni mwepesi." Mathayo 11:28-30. Kuivaa nira ya Kristo na kujifunza Kwake somo la upole na unyenyekevu, tunapata pumziko katika imani, na ujasiri na uaminifu. Tunaona kwamba nira ya Kristo ni rahisi na mzigo Wake ni mwepesi. {9T 124.2}

## SURA YA 13
## WITO KWA WALEI

Juhudi maalum inapowekwa na watenda kazi wenye uzoefu katika jumuiya ambayo watu wetu wenyewe huishi, kuna wajibu mzito sana unaowahusu waumini katika eneo hilo wa kufanya yote wawezayo kufungua njia ya Bwana kufanya kazi. Wanapaswa kuchunguza mioyo yao kwa maombi, na kusafisha njia kuu ya Mfalme kwa kuweka kando kila dhambi ambayo ingewazuia kushirikiana na Mungu na pamoja na ndugu zao. {9T 125.1}

Hili mara nyingi halijaeleweka kikamilifu. Shetani mara nyingi ameleta roho iliyoifanya isiwezekane kwa washiriki wa kanisa kutambua fursa za huduma. Waumini si kwa nadra wamemruhusu adui kuwatumia kwa wakati ule ambao walipaswa kujiweka wakfu kikamilifu kwa Mungu na kwa kuiendeleza kazi Yake. Bila kujua wametangatanga mbali na njia ya haki. Wakiwa na roho ya ukosoaji na kutafuta makosa, utauwa wa kifarisayo na kiburi, wamemhuzunisha Roho wa Mungu na wamerudisha nyuma sana kazi ya wajumbe wa Mungu. {9T 125.2}

Uovu huu umebainika na kusondwa mara nyingi na katika sehemu nyingi. Wakati mwingine wale ambao wamejiingiza katika roho ya chuki, ya kuhukumu wametubu na kuongoka. Ndipo Mungu ameweza kuwatumia kwa heshima na utukufu wa Jina Lake. {9T 125.3}

Tunaishi katika kipindi maalum cha historia ya dunia hii. Kazi kubwa lazima ifanyike kwa muda mfupi sana, na kila Mkristo anapaswa kuchukua sehemu katika kuiendeleza kazi hii. Mungu anawaita watu ambao watajiweka wakfu kwa kazi ya kuokoa roho. Tunapoanza kuelewa ni nini dhabihu Kristo aliifanya ili kuokoa ulimwengu unaoangamia, kutaonekana ushindani mkuu wa kuokoa roho. Laiti makanisa yetu yote yangepata kuona na kutambua dhabihu isiyo na kifani ya Kristo! {9T 125.4

### Harakati za Matengenezo

Katika maono ya usiku, maono yalipita mbele yangu ya harakati kubwa za

matengenezo kati ya watu wa Mungu. Wengi walikuwa wakimsifu Mungu. Wagonjwa waliponywa, na miujiza mingine ikafanyika. Roho ya maombezi ilionekana, kama ilivyodhihirishwa kabla ya Siku kuu ya Pentekoste. Mamia kwa maelfu walionekana wakizitembelea familia na kulifunua mbele yao Neno la Mungu. Mioyo ilisukwa-sukwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, na roho ya uongofu wa kweli ikadhihirishwa. Katika kila upande wa milango kuliwekwa wazi kwa ajili ya kuitangaza Kweli. Dunia ilionekana kuangazwa na msukumo wa mbinguni. Baraka kuu zilipokelewa na watu wa Kweli na wanyenyekevu wa Mungu. Nilisikia sauti za shukrani na sifa, na ilionekana kuwa kuna matengenezo kama vile tulivyoyashuhudia mwaka wa 1844. {9T. 126.1}

Hata hivyo wengine walikataa kuongoka. Hawakuwa tayari kutembea katika njia ya Mungu, na wakati, ili kazi ya Mungu isonge mbele, miito ilitolewa kwa ajili ya matoleo ya hiari, wengine wakang'ang'ania kwa ubinafsi mali zao za duniani. Hawa wenye choyo walijitenga na kundi la waaminio. {9T 126.2}

### Kufanya Kazi Huku Rehema Ingalipo

Hukumu za Mungu ziko duniani, na, chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu, lazima tuutoe ujumbe wa onyo ambao ametukabidhi. Lazima tuutoe ujumbe huu haraka, mstari juu kwa mstari, amri juu kwa amri. Hivi karibuni watu watalazimika kufanya maamuzi mkuu, na ni wajibu wetu kuona kwamba wanafanya hivyo kwa kupewa nafasi ya kuuelewa Ukweli, ili waweze kuchukua msimamo wao kwa akili katika upande wa sahihi. Bwana anawaita watu Wake kufanya kazi—kufanya kazi kwa bidii na kwa hekima—wakati rehema ingalipo. {9T 126.3}

### Umuhimu wa Kazi ya binafsi

Miongoni mwa washiriki wa makanisa yetu kunapaswa kuwa na kazi zaidi ya nyumba kwa nyumba katika kuisoma Biblia na kusambaza vitabu. Tabia ya Kikristo inaweza kuundwa kwa ulinganifu na kikamilifu pale tu wakala wa kibinadamu anapoona kama ni fursa kufanya kazi bila kujali katika kuutangaza Kweli na kulitegemeza kusudi la Mwenyezi Mungu kwa mali. Ni lazima tupande kando ya maji yote, tukiweka roho zetu ndani ya upendo wa Mungu, tukifanya kazi maadamu ni mchana, na kutumia mali ambazo Bwana ametupa kufanya wajibu wowote unaojitokeza mbele yetu. Chochote ambacho mikono yetu itapata kufanya, tunapaswa kukifanya kwa uaminifu; dhabihu yoyote tuliyoitwa kutoa, tunapaswa kuitoa kwa furaha. Tunapopanda kando ya maji ya aina zote tutatambua kwamba "Yeye apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu." 2 Wakorintho 9:6. {9T 127.1}

Mfano wa Kristo lazima ufuatwe na wale wanaodai kuwa wana Wake. Punguzeni mahitaji ya kimwili ya binadamu wenzenu, na shukrani zao zitavunja vizuizi na kuwawezesha kuifikia mioyo yao. Zingatieni sana jambo hili kwa bidii. Kama

makanisa mmepata fursa ya kufanya kazi kama watenda kazi pamoja na Mungu. Ikiwa mngelitii Neno la Mungu, ikiwa mngeliingia kwenye kazi hii, mngelibarikiwa na kutiwa moyo, na mngeliupata uzoefu wa kutosha. Mngejikuta ninyi wenyewe, kama mawakala wa kibinadamu wa Mungu, mkihubiri kwa bidii mpango wa kuokoa, wa urejeshwaji, wa wokovu. Mpango huu usingeonekana kusimama, bali wenye kuendelea, ukisonga mbele kutoka neema hadi neema na kutoka nguvu hadi nguvu. {9T 127.2}

Bwana amewasilisha mbele yangu kazi inayopaswa kufanywa katika miji yetu. Waumini katika miji hii wanapaswa kufanya kazi kwa ajili ya Mungu katika ujirani wa nyumba zao. Wafanye kazi kwa utulivu na unyenyekevu, wakibeba pamoja nao popote waendako angahewa la mbinguni. Ikiwa watajiweka mbali na ubinafsi, wakielekeza daima kwa Kristo, nguvu ya ushawishi wao itasikika. {9T 128.1}

Si kusudi la Bwana kwamba watumishi waachwe wafanye sehemu kubwa zaidi ya kazi ya kupanda mbegu za Ukweli. Watu ambao hawajaitwa katika utumishi wanapaswa kufanya kazi kwa ajili ya Bwana wao kulingana na uwezo wao kadhaa. Mfanyakazi anapojitoa bila kusita kwa ajili ya utumishi wa Bwana, anapata uzoefu unaomwezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na zaidi kwa ajili ya Bwana. Mvuto uliomvuta kwa Kristo hamsaidia kuwavuta wengine kwa Kristo. Kazi ya kunena hadharani inaweza kamwe isiwe juu yake, lakini yeye ni mtumishi wa Mungu, na kazi yake inashuhudia kwamba amezaliwa na Mungu. {9T 128.2}

Wanawake kama kwa wanaume wanaweza kushiriki katika kazi ya kuuficha Ukweli ambapo unaweza kufanikiwa na kudhihirishwa. Wanaweza kuchukua nafasi yao katika kazi katika zahama hii, na Bwana atafanya kazi kupitia wao. Ikiwa wao watajazwa na hisia za wajibu wao, na kufanya kazi chini ya ushawishi wa Roho wa Mungu, watamiliki uwezo unaohitajika kwa wakati huu. Mwokozi ataaksi kwa wanawake hawa waliojitolea, nuru ya uso Wake, na hii itawapa uwezo ambao utapita ule wa wanaume. Wanaweza kufanya katika familia kazi ambayo wanaume hawawezi kuifanya, kazi inayofikia maisha ya ndani. Wanaweza kuwa karibu na mioyo ya wale ambao wanaume hawawezi kuwafikia. Kazi yao inahitajika. Wanawake wenye busara na wanyenyekevu wanaweza kufanya kazi nzuri katika kueleza Ukweli kwa watu katika nyumba zao. Neno la Mungu linaloelezwa hivi litafanya kazi yake ya chachu, na kwa ushawishi wake familia nzima itaongoka. {9T 128.3}

Ndugu na dada zangu, jifunzeni mipango yenu; shika kila fursa ya kuzungumza na majirani zako na unaochangamana nao au kuwasomea jambo fulani kutoka katika vitabu vilivyo na Ukweli wa sasa. Onesha kwamba unajali kama umuhimu wa kwanza wokovu wa roho ambazo Kristo ametoa dhabihu kubwa sana kwao. {9T 129.1}

Katika kufanya kazi kwa ajili ya roho zinazoangamia, unakuwa na ushirika wa

malaika. Maelfu kwa maelfu, na malaika elfu kumi mara elfu kumi wanangoja kushirikiana na washiriki wa makanisa yetu katika kuwasilisha nuru ambayo Mungu ameitoa kwa ukarimu, ili watu wawe tayari kwa ajili ya kuja Kwake Kristo. "Sasa ndio wakati uliokubalika; tazama, siku ya wokovu ndiyo sasa." Hebu kila familia imtafute Bwana katika maombi ya bidii kwa ajili ya msaada wa kufanya kazi ya Mungu. {9T 129.2}

Usivipite vitu vidogo, na ukiitazamia kazi kubwa. Unaweza kufanya kazi ndogo kwa mafanikio, lakini ukashindwa kabisa katika kujaribu kazi kubwa na ukakatishwa tamaa. Shikilia popote unapoona kuna kazi ya kufanya. Uwe tajiri au maskini, mkubwa au mdogo, Mungu anakuita ufanye kazi ya huduma imara kwa ajili Yake. Itakuwa kwa kufanya kwa nguvu zako kile ambacho mikono yako itaweza kufanya ndivyo utaendeleza karama na uwezo wa kufanya kazi. Na ni kwa kupuuza fursa zako za kila siku ndipo unakuwa usiye na matunda na uliyedumaa. Ndiyo maana kuna miti mingi isiyo na matunda katika bustani ya Bwana. {9T 129.3}

Katika mzunguko wa nyumbani, kando ya moto kwa jirani yako, kando ya kitanda cha wagonjwa, kwa njia ya utulivu unaweza kuyasoma Maandiko na kulisema Neno kwa ajili ya Yesu na Ukweli. Kwa hiyo mbegu ya thamani inaweza kupandwa ambayo itachipuka na kuzaa baada ya siku nyingi. {9T 129.4}

Kuna kazi ya umishonari inayopaswa kufanywa katika sehemu nyingi zisizotarajiwa. Roho ya umishionari inapaswa kuzishikilia nafsi zetu, kututia moyo kufikia matabaka ambayo hatukuwa tumepanga kuyafanyia kazi na kwa njia na maeneo ambayo hatukuwa na wazo la kufanya kazi. Bwana ana mpango Wake wa kupanda mbegu ya injili. Katika kupanda kulingana na mapenzi Yake, tutazizidisha mbegu ili Neno Lake liwafikie maelfu ambao hawakuwahi kuusikia Ukweli. {9T 130.1}

Fursa zinafunguka kila upande. Sogea kwenye kila zinazotolewa. Macho yanahitajika kupakwa mafuta kwa dawa ya macho ya mbinguni ili kuona na kuhisi fursa zake. Mungu anaita sasa wamishionari walio macho sana. Kuna njia ambazo zitawasilishwa mbele yetu. Tunapaswa kuona na kuelewa hizi fursa za zitolewazo. {9T 130.2}

Wajumbe wa Mungu wameagizwa kuchukua kazi ileile ambayo Kristo aliifanya alipokuwa hapa duniani. Wanapaswa kujitoa wenyewe kwa kila aina ya huduma aliyoifanya. Kwa bidii na uaminifu wanapaswa kuwaambia watu juu ya utajiri usiochunguzika na hazina ya mbinguni isiyoweza kuharibika. Wanapaswa kujazwa na Roho Mtakatifu. Wanapaswa kurudia matoleo ya Mbingu ya amani na msamaha. Wanapaswa kuelekeza kwenye malango ya mji wa Mungu, wakisema: "Heri wazishikao amri Zake, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake.” Ufunuo 22:14. {9T 130.3}

### Kuonesha Roho ya Kujinyima

Kila mshiriki wa kanisa anapaswa kuonesha roho ya kujitoa. Katika kila nyumba kunapaswa kufundishwa masomo ya kujinyima. Akina baba na mama, wafundisheni watoto wenu kuwa wachumi. Wahimize kuhifadhi senti zao kwa ajili ya kazi ya umishionari. Kristo Ndiye kielelezo chetu. Kwa ajili yetu alifanyika maskini, ili sisi kwa umaskini wake tupate kuwa matajiri. Alifundisha kwamba wote wanapaswa kuja pamoja katika upendo na umoja, kufanya kazi kama alivyofanya kazi, kujitoa kama alivyojitoa, kupenda kama watoto wa Mungu. {9T 130.4}

Ndugu zangu, lazima muwe tayari kuongoka ninyi wenyewe ili kujizoeza kujikana kwa Kristo. Vaeni kwa kawaida lakini kwa unadhifu. Tumieni kidogo iwezekanavyo kwa ajili yenu mwenyewe. Wekeni kwenye nyumba zenu kisanduku cha kujinyima ambalo mnaweza kuweka pesa zilizookolewa kwa vitendo vidogo vya kujinyima. Siku kwa siku pateni ufahamu ulio wazi zaidi wa neno la Mungu, na tumieni kila fursa ya kuusambaza maarifa mliyoyapata. Msichoke katika kutenda mema, kwa maana Mungu huwapa ninyi daima baraka kuu ya karama Yake kwa ulimwengu. Shirikiana na Bwana Yesu, Naye atakufundisha mafundisho ya upendo Wake usio na kifani. Muda ni mfupi; kwa wakati wake ambao hautakuwapo tena, utapokea thawabu yako. {9T 131.1}

Kwa wale wanaompenda Mungu kwa dhati na wana mali, nimeagizwa kusema: Sasa ndio wakati wako wa kuwekeza mali zako katika kuitegemeza kazi ya Bwana. Sasa ni wakati wa kuiinua mikono ya watumishi katika juhudi zao za kujikana nafsi zao ili kuokoa roho zinazopotea. Mtakapokutana katika nyua za mbinguni roho mlizoziokoa, je hamtapata thawabu tukufu? {9T 131.2}

Mtu awaye yote asiwanyime senti zao, na wale walio na vingi watafurahi kwamba wanaweza kuweka akiba mbinguni hazina isikokoma. Pesa ambayo tunakataa kuiweka katika kazi ya Bwana, itapotea. Kwa hiyo hakuna faida itajiweka katika hazina ya mbinguni. {9T 131.3}

Katika maneno yafuatayo mtume Paulo anaeleza wale wanaomzuilia Mungu vilivyo Vyake: “Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu na tanzi, na tamaa nyingi zisizo na maana, zenye kudhuru, ziwatosazo wanadamu katika upotevu na uharibifu. Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani wamefarakana na imani, na kujichoma kwa maumivu mengi.” 1Timotheo 6:9, 10. {9T 132.1}

Ina maana kubwa kupanda kando ya maji yote. Inamaanisha utoaji wa kila mara wa zawadi na sadaka. Mungu atafanya kuandaa vifaa ili wakili mwaminifu wa mali aliyokabidhiwa awe na utoshelevu katika mambo yote, na kuwezeshwa kuzidi sana katika kila tendo jema. “Kama ilivyoandikwa, Ametapanya; amewapa maskini,

haki Yake yakaa milele. Na Yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye atayangeza mazao ya haki yenu." 2 Wakorintho 9:9,10. Mbegu iliyopandwa kwa mkono mkarimu, mkono huru huhudumiwa na Bwana. Anayemhudumia mpanda mbegu humpa mfanyakazi wake kile kinachomwezesha kushirikiana na Mtoaji wa mbegu. {9T 132.2}

Sasa Bwana anawaita Waadventista Wa Sabato katika kila eneo kujiweka wakfu Kwake na kufanya yote wawezayo, kulingana na hali zao, kusaidia katika kazi Yake. Kwa ukarimu wao katika kutoa zawadi na sadaka, anawataka waonyeshe kuthamini kwao baraka Zake na shukrani zao kwa rehema Zake. {9T 132.3}

Ndugu na dada zangu wapendwa, pesa zote tulizo nazo ni za Bwana. Sasa nawasihi kwa Jina la Bwana kuungana katika kufanikisha kumaliza kazi ambazo zimechukuliwa katika shauri la Mungu. Hebu kazi ya kuweka kumbukumbu kwa ajili ya Mungu mahali pengi isifanywe kuwa mgumu na nzito kwa sababu mali zinazohitajika zimezuiliwa. Tusiruhusu wale wanaopambana kuijenga kazi muhimu, kubwa na ndogo, kukata tama kwa sababu tunachelewa kuungana nao katika kufanya kazi hii katika namna ya kuifanya huduma kwa ufanisi. Hebu watu wetu wainuke na kuona wanachoweza kufanya. Hebu waoneshe kwamba kuna umoja na nguvu kati ya Waadventista Wa Sabato. {9T 132.4}

### Masharti ya Huduma Inayokubalika

Kama watu lazima tuje katika ukaribu mtakatifu wa Mungu. Tunahitaji nuru ya mbinguni kuangaza ndani ya mioyo yetu na ndani ya vyumba vya akili zetu; tunahitaji hekima ambayo Mungu pekee anaweza kuitoa, ikiwa tutaupeleka ujumbe katika miji hii kwa mafanikio. Hebu makanisa yetu kila mahali yaingie kwenye kazi. Msimruhusu yeyote aliyejiapiza wenyewe kwa ubatizo kuishi kwa ajili ya huduma na utukufu wa Mungu kutupa kando kiapo chake. Kuna ulimwengu wa kuokolewa; wazo hili na lituhimize kujitoa dhabihu kubwa zaidi na kufanya kazi kwa bidii zaidi walio nje ya njia. {9T 133.1}.

Unapofuata kanuni za Neno la Mungu, mvuto wako utakuwa wa thamani kwa kanisa lolote, na shirika lolote. Unapaswa kuja kwa ajili ya usaidizi wa Bwana, kwa msaada wa Bwana dhidi ya watu wenye nguvu. Maneno yote ya kipuuzi, mizaha na upuuzi wote, ni vishawishi vya adui ili kukuondolea nguvu za kiroho. Jifungeni wenyewe dhidi ya uovu huu, kwa Jina la Mungu wa Israeli. Ikiwa mtajinyenyekeza wenyewe mbele za Mungu, Yeye atawapa ujumbe kwa wale walio katika njia kuu na nia njia, na kwa ajili ya walio katika nchi za kigeni wanaohitaji msaada wenu. Ziandaeni taa zenu, na ziendelee kuwaka, ili popote pale mtakapoweza kwenda mdhihirishe kwa maneno na matendo miale ya thamani ya nuru. {9T 133.2}

Ikiwa tutajitoa kwa ajili ya utumishi kwa Bwana, atatuelekeza ni nini cha kufanya.

Ikiwa tutakuwa na uhusiano wa karibu na Mungu, atafanya kazi pamoja nasi. Tusijishughulishe sana na ubinafsi na masilahi binafsi kiasi kwamba tukawasahau wale wanaopanda ngazi ya uzoefu wa Kikristo na wanaohitaji msaada wetu. Ni lazima tuwe tayari kutumia uwezo wetu tuliopewa na Mungu katika kazi ya Bwana,tukiwa tayari kunena Maneno ambayo yatasaidia na kubariki. {9T 134.1}

Ndugu na dada zangu, je, tunatilia maanani mahitaji ya miji mikubwa ya Mashariki? Je hatujui kwamba wanapaswa kuonywa juu ya ukaribu wa kuja kwa Kristo? Kazi tunayopaswa kufanya ni kazi kubwa ajabu. Kuna ulimwengu wa kuokolewa; kuna roho za kuvunwa katika miji ya Mashariki ya Marekani, katika majimbo ambapo ujumbe wa kuja kwa Bwana wetu ulihubiriwa kwa mara ya kwanza. Ni akina nani watajitoa wao wenyewe kufanya aina hii ya kazi ya umishionari? Kuna mamia ya watu wetu ambao wanapaswa kuwa nje shambani ambao wanafanya kidogo au hawafanyi chochote kwa ajili ya kuuendeleza ujumbe. Wale ambao wamekuwa na kila manufaa ya kuijua Kweli, ambao wamepokea mafundisho juu ya kanuni, amri juu ya amri; huku kidogo na kule kidogo, wana jukumu kubwa lililo juu yao katika roho hizi ambazo kamwe hazijausikia ujumbe wa mwisho wa injili. {9T 134.2}

Ikiwa katika wakati huu ufaao washiriki wa makanisa watakuja kwa unyenyekevu mbele za Mungu, wakijiweka nje ya mioyo zao yale yote yaliyo mabaya na kufuata mashauri kwa kila hatua, atajidhihirisha kwao na atawapa ujasiri katika Yeye. Na kadri washiriki wa kanisa wanavyofanya sehemu yao kwa uaminifu, Bwana atawaongoza na kuwaelekeza watumishi Wake waliochaguliwa, na kuwaimarisha kwa ajili ya kazi yao muhimu. Katika maombi mengi tuungane sote katika kuishikilia mikono yao na katika kuchukua miale angavu kutoka patakatifu pa mbinguni. {9T 134.3}

Mwisho umekaribia, ukitujia kwa siri, bila kuonekana, kama ujio usio na kelele wa mwizi usiku. Bwana atujalie tusilale tena kama wengine, bali tukeshe na kuwa na kiasi. Kweli hivi karibuni itashinda kwa utukufu, na wote wanaochagua sasa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu watashinda Pamoja nayo. Muda ni mfupi; usiku waja upesi ambapo hapana mtu awezaye kufanya kazi. Hebu wale wanaoshangilia katika nuru ya Ukweli wa sasa wafanye haraka kuwasambazia wengine Ukweli. Bwana anauliza: "Nimtume nani?" Wale wanaotaka kujinyima kwa ajili ya Ukweli sasa wanapaswa kujibu: “Mimi hapa; nitume mimi.” Isaya 6:8. - {9T 135.1}

Hebu wale wanaobeba majukumu wakumbuke kwamba ni Roho Mtakatifu anayepaswa kufanya marekebisho. Ni Bwana atawalaye. Hatupaswi kujaribu kufinyanga kulingana na mawazo yetu wenyewe, wale tunaowafanyia kazi, bali kumwacha Kristo afanye ufinyanzi Mwenyewe. Yeye hafuati matakwa ya kibinadamu. Anatenda kazi kulingana na nia na Roho Yake mwenyewe. Ni jukumu la mwanadamu kuufunulia ulimwengu kile ambacho Kristo ameweka moyoni

mwake; kwa neema Yake mwanadamu anakuwa mshirika wa tabia ya Uungu, akiisha kuepuka uharibifu uliomo duniani kupitia tamaa. Nguvu za juu za yule anayempokea Kristo huimarishwa na kukuzwa, na yeye hupokea kufaa kwa ajili ya huduma ya Mungu. {9T 135.2}

Watu wengi wenye elimu duniani wamepata elimu ya juu sana kiasi kwamba hawawezi kuwagusa watu wa kawaida. Maarifa yao ni magumu. Inainua juu, lakini haina pumziko popote. Mfanyabiashara Mwenye akili Zaidi anatamani Ukweli rahisi kama vile Kristo aliowapa watu wakati Yeye alipokuwa katika dunia hii--Kweli anayotangaza kuwa ni roho na uzima. Maneno yake ni kama majani ya mti wa uzima. Kile ulimwengu unachohitaji leo ni nuru ya mfano wa Kristo unaoakisiwa kutoka katika maisha ya wanaume na wanawake walio kama Kristo. Akili yenye nguvu zaidi kwa ajili ya Ukweli ni akili ambayo Kristo anaitawala, kuikuza na kuitakasa kwa utakaso wa Roho Mtakatifu. - {9T 135.3}

Kristo ametoa agizo Lake: "Enendeni ulimwenguni mwote." Marko 16:15. Wote lazima wausikie ujumbe wa onyo. Thawabu yenye thamani kubwa zaidi imetunzwa kwa wale wanaozikimbia mbio za Kikristo. Wale wakimbiao kwa saburi watapokea taji ya uzima isiyodumaa. - {9T 136.1}

Kuzeni utulivu, na zikabidhini nafsi zenu katika ulinzi kwa Mungu kama Muumba mwaminifu. Atalinda kile kilichowekwa kwenye amana Yake. Hafurahii sisi kujaza madhabahu Yake kwa machozi na manung’niko yetu. Unayo tayari ya kutosha kumsifu Mungu, kama huoni nafsi nyingine ikiongoka. Lakini kazi nzuri itaendelea ikiwa utasonga mbele tu na usijaribu kurekebisha kila kitu kwa mawazo yako mwenyewe. Amani ya Mungu na itawale mioyoni mwenu na kuwa na shukrani. Mpe Bwana nafasi apate kufanya kazi. Usiizuie njia Yake. Anaweza na atafanya kazi ikiwa tutamruhusu. - {9T 136.2}

Wakati mipango ya kina inapaswa kuwekwa, uangalifu mkubwa lazima uchukuliwe kwamba kazi katika kila tawi kuunganishwa kwa upatanifu na ile katika kila tawi lingine, hivyo kufanya yote kuwa kamili. {9T 136.3}

## SURA YA 14
## MANENO YA USHAURI KWA WATUMISHI.

Sanitarium, California,
Novemba 3, 1901.

Kwa Mtendakazi mzoefu wa muda Mrefu katika jiji la New York—

Nilivyozingatia hali ya New York, mzigo mkubwa umekuja nafsini mwangu. Katika majira ya usiku mambo yamewasilishwa kwangu katika mwanga huu: New York itafanyiwa kazi; fursa zitakupatikana katika sehemu za jiji ambamo hakuna makanisa, ambamo Kweli itapata nafasi ya kusimama. Kuna kazi kubwa sana ya kufanywa katika kuitangaza Kweli ya wakati huu kwa wale waliokufa katika makosa na dhambi. Jumbe nyingi za kushangaza zitabebwa na watu walioteuliwa na Mungu, jumbe za tabia za kuwaonya watu, kuwaamsha. Na wakati wengine watachukizwa na onyo na kuongozwa kuipinga nuru na ushahidi, tunapaswa kuona kutokana na hili kwamba tunatoa ujumbe upimao kwa wakati huu. {9T 137.1}

Ujumbe utatolewa kwa namna isiyo ya kawaida. Hukumu za Mungu ziko katika nchi. Wakati utume wa miji unapaswa kuanzishwa mahali ambapo wainjilisti wa vitabu, wafanyakazi wa Biblia, na wamishonari wa kitabibu wanaweza kufundishwa kuyafikia matabaka fulani, lazima pia, katika miji yetu, tuwe na wainjilisti waliowekwa wakfu ambao kupitia kwao ujumbe unapaswa kutolewa kwa uthabiti ili kuwashtua wasikilizaji.- {9T 137.2}

"Walete vipofu walio na macho, na viziwi walio na masikio. N wakakusanyike Mataifa yote, kabila zote na wakutane; ni nani miongoni mwenu awezaye kuhubiri neno hili, na kutuonyesha mambo ya zamani? Na walete mashahidi wao, wapate kuhesabiwa kuwa na haki; au na wasikie, wakaseme, ni Kweli. Ninyi ni mashahidi Wangu, asema Bwana, na mtumishi aliyemchagua; mapate kujua, na kuniamini ,

na kufahamu Mimi Ndiye; kabla Yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu Mimi hatakuwepo mwingine. Mimi, naam, Mimi, Mimi ni Bwana; zaidi yangu Mimi hapana mwokozi. Nimetangaza habari, nimeokoa, nimeonyesha, naa hapakuwa na mungu wa kigeni kati yenu; kwa sababu hiyo ninyi ni mashahidi wangu, asema Bwana, Nami ni Mungu. Naam, tangu siku ya leo Mimi Ndiye; wala hapana awezaye kuokoa katika mkono wangu; Mimi nitatenda kazi, naye ni nani awezaye kuizuia?" Isaya 43:8-13. {9T 137.3}

“Nitawaleta vipofu kwa njia wasiyoijua, katika mapito wasiyoyajua nitawaongoza; Nitafanya giza kuwa nuru mbele yao, na mahali palipopotoka kuwa pamenyooka. Haya nitayatenda, wala sitawaacha. Watarudishwa nyuma, wataabishwa sana, hao wanaotumainia sanamu za mawe, na kuziambia sanamu za madini, Ninyi ndinyi miungu yetu. Sikilizeni, enyi viziwi; tazameni, enyi vipofu, mpate kuona. Ni nani aliye kipofu, ila mtumishi wangu? au aliye kiziwi, kama mjumbe wangu nimtumaye? Ni nani aliye kipofu, kama yeye aliye na amani? Naam, kipofu kama mtumishi wa Bwana? Unaona mambo mengi, lakini huyatii moyoni; masikio yake ya wazi, lakini hasikii. Bwana akapendezwa, kwa ajili ya haki Yake; Kuitukuza sheria, na kuiadhimisha." Isaya 42:16-21. {9T 138.1}

Kazi iliyoainishwa katika maandiko haya ni kazi iliyo mbele yetu. Maneno "Mtumishi Wangu," "Israeli," " Mtumishi wa Bwana,” maana yake ni mtu ye yote ambaye Bwana anaweza kumchagua na kumweka kufanya kazi Fulani. Anawafanya kuwa watumishi wa mapenzi Yake, ingawa wengine waliochaguliwa wanaweza kuwa hawayajui mapenzi yake kama alivyokuwa Nebukadneza. {9T 138.2}

Mungu atafanya kazi na wale watu wake ambao watajinyenyekeza katika utendaji wa Roho Mtakatifu. Ameahidi utukufu Wake kwa ajili ya mafanikio ya Masihi na ufalme Wake. “Mungu Bwana ananena, Yeye aliyeziumba mbingu, na kuzitandaza; Yeye ayeitandaza nchi na mazao yake; Yeye awapaye pumzi watu walio juu yake, Yeye awapaye roho wao waendao ndani yake; Mimi, Bwana nimekuita katika haki, Nami nitakushika mkono, na kukulinda, na kukutoa uwe agano la watu, na nuru ya Mataifa; kuyafunua macho ya vipofu, kuwatoa gerezani waliofungwa, kuwatao wale walioketi gizani katika nyumba ya kufungwa." {9T 138.3}

"Ni nani miongoni mwenu atakayetega sikio lake kuyasikia hayo? Atakayesikiliza na kusikia kwa wakati ujao?" Mstari wa 5-7, 23. {9T 139.1} Watu wa Mungu ambao wamekuwa na nuru na maarifa hawajatekeleza makusudi ya Mungu yaliyo juu na matakatifu. Hawajasonga mbele kutoka ushindi hadi ushindi, na kuongeza eneo jipya, kuinua juu kiwango katika miji na viunga vyake. Upofu mkubwa wa kiroho umeonyeshwa na wale walio na nuru kuu waliyoangazia na Bwana, bali

hawajasonga mbele katika nuru hata nuru kuu zaidi na Zaidi. Washiriki wa kanisa hawajahimizwa kutumia ujasiri na neva na misuli ya kiroho katika kuindeleza kazi. Wanapaswa waeleweshe ya kwamba watumishi hawawezi kufanyia kazi wokovu kwa kuelea juu yao. Ni njia hii wanafanywa wanyonge wakati wanapaswa kuwa na watu wenye nguvu. {9T 139.2}

Katika kila kanisa vijana wa kiume na wa kike wanapaswa kuchaguliwa kubeba majukumu. Hebu wafanye kila jitihada ili wastahili kuwasaidia wale wasioijua kweli. Mungu anawaita watendakazi wenye bidii ya moyo wote. Wanyenyekevu na waliotubu watajifunza kwa uzoefu binafsi kwamba kando Yake hakuna mwokozi.-{9T 139.3}

Kweli ya Biblia lazima ihubiriwe na kutekelezwa. Kila mwale wa nuru inayotolewa inapaswa kung'aa kwa uwazi. Mwangaza wa pekee. Ukweli unapaswa kutolewa kama taa iwakayo. Kuna mamia ya watumishi wa Mungu ambao lazima waitikie mwito huu na kuchukua kazi kama watenda kazi wenye bidii, ya kuokoa roho, wakija kwenye usaidizi ya Bwana, kwa msaada wa Bwana juu ya hodari. Mungu huwaita watu walio hai, watu waliojazwa nao msukumo wa kuhuisha wa Roho Wake, watu wanaomwona Mungu kama Mtawala Mkuu na kupokea kutoka Kwake uhakika wa utimizwaji wa ahadi Zake, watu ambao si vuguvugu, bali ni moto katika Upendo Wake. {9T 140.1}

Kama kazi yote ambayo imekuwa ikitumika kwenye makanisa katika kipindi cha miaka ishirini iliyopita iwe tena ikitumiwa kwao, itashindwa, kama ilivyoshindikana huko nyuma, ya kuwafanya washiriki kujikana wenyewe. wafuasi wa msalaba wa Kristo. Wengi wamevembewa na chakula cha kiroho, huku maelfu ulimwenguni wanaangamia kwa ajili ya mkate wa uzima. Washiriki wa kanisa lazima wafanye kazi; lazima wajielimishe wenyewe, wakijitahidi kufikia kiwango cha juu kilichowekwa mbele yao. Hiki Bwana atawasaidia kukifikia kama watashirikiana Naye. Wakiziweka nafsi zao katika kuipenda ile Kweli hawatawarudisha nyuma watumishi katika kuiwasilisha Kweli katika maeneo mapya. {9T 140.2}

Miji mikubwa ilipaswa kufanyiwa kazi mara tu makanisa yalipoipokea nuru, lakini wengi hawajaubeba mzigo wowote kwa ajili ya roho hizi, na Shetani, akiwaona ni rahisi kwa majaribu yake, ameuharibu uzoefu wao. Mungu anataka watu Wake watubu, waongoke, na kuurudia upendo wao wa kwanza, ambao wamaupoteza kwa kushindwa kufuata nyayo za Mkombozi aliyejitoa mwenyewe.{9T 140.3}

## Kwa Ujasiri Na Unyenyekevu

Wakati umefika wa kufanya jitihada thabiti mahali ambapo Kweli bado

haijatangazwa. Je, kazi ya Bwana itafanywaje? Katika kila mahali panapoingilika, msingi thabiti unapaswa kuwekwa kwa kazi ya kudumu. Mbinu za Bwana zinapaswa kufuatwa. Hampaswi kutishwa na mambo ya kuonekana kwa nje, hata kama yanatatiza kiasi gani. Ni jukumu lenu kuiendeleza mbele kazi kama Bwana alivyosema inavyopaswa kupelekwa. Lihubirini Neno, na Bwana kwa Roho wake Mtakatifu atatuma usadikisho akilini mwa watu wanaosikiliza. Neno hili ni: “Nao wale wakatoka, wakahubiri kila kote kote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo." Mk 16:20. {9T 141.1}

Watendakazi wengi wanapaswa kutenda sehemu yao, kufanya kazi ya nyumba kwa nyumba na kuisoma Biblia katika familia. Wanapaswa kuonesha kukua kwao katika neema kwa kujitoa katika mapenzi ya Kristo. Hivyo watapata uzoefu mwingi. Kama kwa imani wanapokea, kuamini, na kulitii Neno la Kristo, ufanisi wa Roho Mtakatifu utafanywa kuonekana katika kazi zao za maisha. Kutaonekana ukubwa wa juhudi za dhati. Kutakuwa na imani ambayo hufanya kazi kwa upendo na kuitakasa roho. Matunda ya Roho yataonekana katika maisha. {9T 141.2}

Kristo ni Nuru ya ulimwengu. Wale wanaomfuata hawatembei gizani, bali wanayo nuru ya uzima. Yohana anatangaza hivi kumhusu Kristo: “Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina Lake." Yohana 1: 12. Mtazame Kristo. Kumtazama Yeye huleta moyo na moyo.akili na tabia katika kupatana na mapenzi ya Mungu. {9T 141.3}

Kuna haja ya maelekezo yote ambayo utume wetu unaweza kutoa. Endeleeni katika kazi yenu katika nguvu za Roho Yule Yule aliyeongoza katika uanzishwaji wake. Kwa kuyafungua Maandiko, kwa kuomba, kwa kuidhihirisha imani, waelimisheni watu katika njia ya Bwana; na kutakuwa na kanisa lililojengwa juu ya Mwamba, Kristo Yesu. {9T 141.4}

Kazi lazima iendelezwe mbele katika usahili wa ukweli. Mungu anasema: “Ninalo Neno ya faraja kwa ajili yenu." Bwana katika miji yetu mikubwa ana watu wengi wa thamani ambao hawajampigia goti Baali, na Anao wale ambao wamemwabudu Baali kwa kutokujua. Juu ya hawa nuru ya Ukweli inapaswa kungaza, ili wapate kumwona Kristo kama njia, Kweli na uzima. {9T 142.1}

Songa mbele katika kazi yako kwa unyenyekevu. Kamwe usiinuke juu ya usahili wa injili ya Kristo. Sio katika sanaa ya kujionesha, bali katika kumwinua Kristo, Mkombozi Mwenye kusamehe dhambi, utapata mafanikio katika kuzivuta roho. Unapomfanyia Mungu kazi kwa unyenyekevu na moyo wa kujishusha, atajidhihirisha kwako. {9T 142.2}

Kwa kutumia chati, ishara, na vielelezo vya aina mbalimbali mtumishi anaweza kuufanya ukweli kuwa wazi na thabiti. Huu ni msaada, na inapatana na neno la Mungu; lakini ikiwa mtendakazi anafanya kazi yake kuwa ghali kiasi kwamba wengine hawawezi kupata kutoka hazina mali ya kutosha ili kuwategemeza kazini, hafanyi kazi kulingana na mpango wa Mungu. Kazi katika miji mikubwa inapaswa kufanywa kwa utaratibu wa Kristo, si kwa utaratibu wa maonyesho ya drama za burudani. Sio utendaji wa kuigiza wa maonesho unaomtukuza Mungu, bali uwasilishaji wa ukweli katika upendo wa Kristo. {9T 142.3}

Usiuhahafishie Ukweli mvuto na hadhi yake kwa utangulizi uliopitiliza ambao ni wa utaratibu wa kidunia kuliko utaratibu wa mbinguni. Hebu wasikilizaji wako waelewe kwamba unafanya mikutano, sio kuwavutia hisia na muziki na mambo mengine, bali kuuhubiri Ukweli katika thamani yake yote, ili uweze kuwafikia kama onyo, likiwaamsha kutoka katika usingizi wao wa kufa wa kujifurahisha nafsi. Ni Ukweli mtupu ambao kama upanga mkali, wenye makali kuwili hukata pande zote mbili. Ni huu ndio utawaamsha wale waliokufa katika makosa na dhambi. {9T 142.4}

Yeye aliyetoa maisha Yake ili kuwaokoa wanaume na wanawake kutokana na ibada ya sanamu na anasa aliacha kielelezo cha kufuatiwa na wote wanaobeba kazi ya kuiwasilisha injili kwa wengine. Watumishi wa Mungu katika zama hizi wamepewa Kweli nyingi za thamani za kutangaza, na matendo, mbinu zao na mipango yao lazima viendane na umuhimu wa ujumbe wao. Ikiwa unaliwasilisha Neno kwa njia ya Kristo, wasikilizaji wako watavutiwa sana na Kweli unazofundisha. Usadikisho utawajia kwamba hili ni Meno la Mungu aliye hai. {9T 143.1

## Utaratibu Katika Ibada

Katika juhudi zao za kuwafikia watu, wajumbe wa Bwana hawapaswi kufuata njia za ulimwengu. Katika mikutano inayofanyika, wasitegemee waimbaji wa kiulimwengu na maonyesho ya kuigiza kuamsha hisia. Je, wanawezaje wale ambao hawapendezwi na Neno la Mungu, ambao hawajawahi kulisoma Neno Lake kwa shauku ya dhati ya kuuelewa Ukweli Wake, watatarajiwe kuimba kwa roho na akili? Mioyo yao inawezaje kupatana na utakatifu wa maneno ya wimbo? Kwaya ya mbinguni inawezaje kuungana katika muziki na ile iliyo katika maoenesho tu? {9T 143.2}

Uovu wa ibada za kawaida za maonyesho hauwezi kuonyeshwa kwa nguvu sana, lakini hakuna maneno yanayoweza kueleza ipasavyo baraka nyingi za ibada ya kweli. Wanadamu wanapoimba kwa roho na akili, wanamuziki wa mbinguni

huchukua mzigo na kujiunga katika wimbo wao wa shukrani. Yeye ambaye ametukirimia karama zote zinazotuwezesha kufanya kazi pamoja na Mungu; anatarajia watumishi Wake kukuza sauti zao ili waweze kusema na kuimba kwa njia ambayo wote wanaweza kuelewa. Sio uimbaji wa sauti kubwa unaohitajika, bali kupanda na kushuka kwa sauti kwa wazi, matamshi sahihi, na utamkaji wa wazi. Hebu sote tuchukue muda kukuza sauti ili sifa za Mungu ziweze kuimbwa kwa sauti safi na laini, si kwa harara na ukali kunakoudhi sikio. Uwezo wa kuimba ni karama ya Mungu; hebu itumike kwa utukufu Wake. {9T 143.3}

Katika mikutano inayofanyika hebu idadi ichaguliwe kushiriki katika huduma ya nyimbo. Na uimbaji usindikizwe na ala za muziki zinazopigwa kwa ustadi. Hatupaswi kupinga matumizi ya vyombo vya muziki katika kazi yetu. Sehemu hii ya ibada inapaswa kuendeshwa kwa uangalifu, kwa kuwa ni sifa kwa Mungu katika nyimbo. {9T 144.1}

Uimbaji si mara zote ufanywe na wachache. Mara nyingi kadri iwezekanavyo, acha kutaniko zima lijiunge. {9T 144.2}

**Umoja Katika Tofauti**

Katika juhudi zetu kwa ajili ya umati wa watu wanaoishi katika miji, lazima tujaribu kufanya huduma iliyo kamili. Kazi katika kituo kikubwa cha watu ni kubwa kuliko kwa mtu mmoja kuweza kushughulikia kwa mafanikio. Mungu ana njia tofauti za kufanya kazi, na anao watenda kazi mbalimbali ambao Yeye huwakabidhi karama mbalimbali. {9T 144.3}

Mtendakazi mmoja anaweza kuwa tayari ni mzungumzaji; mwingine mwandishi; mwingine anaweza kuwa na karama ya uaminifu, maombi ya dhati, yenye bidii; mwingine karama ya uimbaji; mwingine anaweza kuwa na uwezo maalum wa kuelezeaa Neno la Mungu kwa ufasaha. Na kila karama inapaswa kuwa nguvu ya Mungu kwa sababu Yeye hufanya kazi pamoja na mtenda kazi. Mungu humpa mmoja Neno la hekima, mwingine maarifa, na mwingine imani; lakini zote zinapaswa kufanya kazi chini ya  Mkuu huyo huyo. Tofauti za karama huongoza kwenye utendaji kazi mbalimbali, bali "Mungu ni Yeye Yule azitendaye kazi zote katika wote." 1 Wakorintho 12:6. {9T 144.4}

Bwana anatamani watumishi Wake waliochaguliwa wajifunze jinsi ya kuungana pamoja katika juhudi patanifu. Inaweza ikaonekana kwa wengine kwamba utofauti kati ya karama zao na karama za mtendakazi mwenzao ni kubwa mno kuwaruhusu kuungana kwa juhudi upatanifu; lakini wakumbukapo kwamba kuna akili mbalimbali za kufikiwa, na kwamba wengine wataikataa Kweli kama inavyowasilishwa na mtenda kazi mmoja, ili tu kuifungua mioyo yao kwa Kweli ya

Mungu kama inavyowasilishwa kwa namna tofauti na mtendakazi mwingine, watajitahidi kwa matumaini kufanya kazi pamoja kwa umoja. Vipaji vyao, hata viweje tofauti, vinaweza kuwa chini ya udhibiti sawa wa Roho. Katika kila Neno na tendo, wema na upendo vitadhihirishwa; na kadri kila mtendakazi anavyoitimiza kazi alipoteuliwa, kwa uaminifu, ombi la Kristo kwa ajili ya umoja wa wafuasi Wake litajibiwa, na ulimwengu utajua ya kuwa hawa ni wanafunzi Wake. {9T 145.1}

Katika huruma ya upendo na ujasiri watendakazi wa Mungu wanapaswa kuungana wao kwa wao. Anayesema au kutenda chochote kinachoelekea kuwatenganisha washiriki wa kanisa la Kristo anapingana na kusudi la Bwana. Mabishano na mafarakano katika kanisa, kuwa na moyo wa mashaka na kushuku, kutoamini, humwaibisha Kristo. Mungu anatamani watumishi Wake wakuze shauku ya Kikristo kati yao wenyewe. Dini ya kweli inaunganisha mioyo si tu pamoja na Kristo, bali na mtu mwingine katika muungano mwororo zaidi. Tutakapojua maana ya kuunganishwa hivyo na Kristo na ndugu zetu, mvuto wenye harufu nzuri utaambatana na kazi yetu popote tutakapokwenda. {9T 145.2}

Watendakazi katika miji mikubwa lazima wachukue sehemu zao kadhaa, wakifanya kila juhudi kuleta matokeo bora. Wanapaswa kuizungumza imani na kutenda kwa namna ambayo inaweza kuwavutia watu. Hawapaswi kuihafifisha kazi kwa mawazo yao wenyewe. Hapo nyuma mengi ya haya yamefanywa na sisi kama watu, na yamekuwa kikwazo kwa mafanikio ya kazi. Hebu tukumbuke kwamba Bwana ana njia tofauti za kufanya kazi, kwamba ana watenda kazi tofauti ambao kwao amekabidhi karama tofauti. Tunapaswa kuona kusudi Lake katika kuwatuma watu fulani mahali fulani. {9T 145.3}

Bado kitambo kidogo sauti ya rehema itasikika; kitambo kidogo kutatolewa mwaliko wa neema:"Kama mtu akiona kiu, na aje Kwangu, anywe.” Yohana 7:37. Mungu anatuma ujumbe wake wa onyo kwa miji kila mahali. Hebu wajumbe anaowatuma wafanye kazi kwa upatanifu ili wote wachukue maarifa ambayo wamejifunza juu ya Yesu. {9T 146.1}

## Katika Upole Wa Kristo

Hakuna mwanadamu anayepaswa kuwafunga wanadamu wengine kwake kana kwamba ndiye anayewadhibiti. akiwaambia kufanya hili na kuwakataza kufanya lile, akiwaamuru, kuwalazimisha, akijifanya kama afisa juu ya kundi la askari. Hivi ndivyo makuhani na watawala walivyofanya katika siku za Kristo, lakini siyo njia sahihi. Baada ya Ukweli kuwa na mvuto kwenye mioyo, na wanaume na wanawake wameyakubali mafundisho Yake. wanapaswa kuchukuliwa kama mali ya Kristo, na si kama mali ya mwanadamu. Kwa kuzivuta akili zao kwako

unawaongoza kujitenga na chanzo cha hekima na utoshelevu wao. Utegemezi wao wote lazima uwe kwa Mungu; ndivyo pekee wanaweza kukua katika neema. {9T 146.2}

Hata kama yanaweza kuwa ni makubwa kiasi gani madai ya mtu ya elimu na hekima, asipokuwa chini ya mafundisho ya Roho Mtakatifu anazidi kuwa mjinga tu wa mambo ya kiroho. Anahitaji kutambua hatari yake na uzembe wake, na kuweka utegemezi kamili kwa Yule ambaye peke Yake Ndiye awezaye kuzilinda nafsi zilizowekwa chini ya amana yake, awezaye kuzijaza na Roho wake, na kuzijaza kwa upendo usio na ubinafsi wao kwa wao, hivyo kuwawezesha kutoa ushahidi kwamba Mungu amemtuma Mwana Wake ulimwenguni ili kuwaokoa wadhambi. Wale ambao wameongoka kweli kweli watasonga mbele pamoja katika umoja wa Kikristo. Hebu kusiwe na mgawanyiko katika kanisa la Mungu, kusiwepo na mamlaka isiyo ya busara inayotumiwa juu ya wale wanaoukubali ukweli. Upole wa Kristo wapaswa uonekane katika yote yanayosemwa na kutendwa. {9T 146.3}

Kristo Ndiye msingi wa kila kanisa la kweli. Tunayo ahadi Yake isiyobadilika kwamba uwepo Wake na ulinzi wake vitatolewa kwa waaminifu wake wanaotembea katika shauri Lake. Hadi mwisho wa wakati Kristo anapaswa kuwa wa kwanza. Ndiye chanzo cha uzima na nguvu, haki na utakatifu. Na Yeye Ndiye haya yote kwa wale ambao wanaivaa nira Yake na kujifunza Kwake jinsi ya kuwa wapole na wanyenyekevu. {9T 147.1}

Katika jukumu na furaha ya huduma zote ni kumwinua Kristo mbele za watu. Hii ndiyo jumla ya ya kazi zote za kweli. Hebu Kristo aonekane; nafsi ijifiche nyuma yake. Huku ndiyo dhabihu inayokubalika. Kujitoa kwa jinsi hii Mungu anakukubali. Maana Yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele, ambaye jina Lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa Mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu, tena pamoja naye yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo ya waliotubu." Isaya 57:15. {9T 147.2}

### Kukutana na Upinzani

Mara nyingi, mnapotafuta kuuwasilisha Ukweli, upinzani utaamshwa; na ikiwa mtatafuta kukabiliana na upinzani kwa hoja, mtauzidisha tu, na hivyo hamtakuwa na uwezo wa kuukabili. Angalieni kwenye uthibitisho. Malaika wa Mungu huwatazama, na wanaelewa jinsi ya kuwashawishi wale ambao mnaacha kukutana nao kwa hoja. Msing'ang'anie kwenye hoja hasi za maswali yanayojitokeza, bali pelekeni akili zenu kwenye Kweli za uthibitisho, na kuzielekeza huko kwa kusoma sana na maombi ya dhati na moyo ulio wakfu.

Wekeni taa tayari na na ikiwaka, mruhusu miali ing’aayo iangaze, ili watu wapate kuyatazama matendo yenu mema. wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni. {9T 147.3}

Kama Kristo asingeushikilia uthabiti Wake katika jangwa la majaribu, angelipoteza yote ambayo alitamani kuyapata. Njia ya Kristo ndiyo njia bora ya kukutana na wapinzani wetu. Tunaimarisha hoja zao tunapoyarudia wanayoyasema. Shilikilia uthabiti kila wakati. Huenda mtu yule yule aliyekuwa akikupinga akaondoka na maneno yako nyumbani na akaongolewa kulingana na Ukweli wa busara uliomfikia katika ufahamu wake. {9T 148.1}.

Mara nyingi nimekuwa nikiwaambia ndugu zetu: "Wapinzani wenu watatoa kauli kuhusu kazi yako ambazo ni za uongo. Msizirudie kauli zao; bali shikilieni uthabiti wenu wa Kweli iliyo hai, na malaika wa Mungu wataifungua njia mbele yenu. Tuna kazi kubwa ya kuipeleka mbele, na lazima tuibebe kwa njia ya busara. Hebu kamwe tusisimke au kuruhusu hisia mbaya kututokea. Kristo hakufanya hivi, Naye ni mfano wetu katika mambo yote. Kwa kazi tuliyopewa kufanya tunahitaji zaidi hekima ya mbinguni, iliyotakaswa, na kunyenyekezwa, na isiyo na kiasi cha ubinafsi. Tunahitaji kuegemea kwa uthabiti nguvu za kimbingu." {9T 148.2}

Wale ambao wameiacha imani watakuja kwenye mikutaniko yetu ili kugeuza mawazo yetu kutoka katika kazi ya Mungu ambayo ingelikuwa imefanyika. Hamwezi kumudu kuyageuza masikio yenu kutoka kwenye ukweli na kujielekeza kwwenye hadithi za kubuni. Usiache kujaribu kumwongoa anenaye maneno ya kashfa juu ya kazi yako; lakini ionekane kuwa wewe unaongozwa na Roho wa Yesu Kristo, na malaika wa Mungu wataweka midomoni mwako maneno ambayo yataifikia mioyo ya wapinzani. Ikiwa watu hawa watang'ang'ania kuendeleza mambo yao, wale walio na akili timamu walio katika kusanyiko wataelewa kwamba maneno yako ni ya kiwango cha juu zaidi. Kwa hiyo nena kwa namna itakavyojulikana kuwa Yesu Kristo anazungumza kupitia wewe. {9T 148.3}

### Haja Ya Kufanya Kazi Kwa Bidii Na Moyo Wote

Ikiwa watumishi wetu wangetambua ni muda gani wakazi wa dunia watafikishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, kujibu matendo yaliyofanywa katika mwili, wangefanya kazi kwa bidi kiasi gani pamoja na Mungu kuuwasilisha Ukweli! Ni jinsi gani wangefanya kazi bila kuchoka kuiendeleza kazi ya Mungu katika ulimwengu, wakitangaza kwa maneno na matendo: "Mwisho wa mambo yote umekaribia." 1 Petro 4:7. {9T 149.1}

"Jitayarishe kukutana na Mungu wako" ndio ujumbe tunapaswa kuutangaa kila

mahali. Baragumu i tayari kutoa sauti fulani. Kwa uwazi na dhahiri ikitoa sauti ya onyo: “Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu. . . . Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake." Ufunuo 18:2-4. Maneno ya andiko hili yanapaswa kutimizwa. Karibuni jaribu la mwisho litakuja. kwa wakazi wote wa dunia. Wakati huo maamuzi ya haraka yatafanywa. Wale waliosukwa sukwa na hatia chini kutokana na uwasilishaji wa Neno watajipanga wenyewe chini ya bendera iliyotiwa damu ya Mfalme Immanuel. Wataona na kutambua kuliko hapo awali kuwa wamekosa fursa nyingi kwa ajili ya kutenda mema waliyopaswa kuwa wameyafanya. Watatambua kwamba hawajafanya kazi kwa bidii kama inavyopaswa, kutafuta na kuokoa waliopotea. ili kuwanyakua, kana kwamba, kutoka kwenye moto. {9T 149.2}

Watumishi wa Mungu wanapaswa kuwa “wasio wavivu katika kazi; wawe na bidii katika roho; wakimtumikia Mungu. Kutokuwa na majukumu na uzembe sio ucha Mungu. Tunapotambua kwamba tunamfanyia Mungu kazi tutakuwa na shauku ya juu sana kuliko tuliyowahi kuwa nayo hapo awali ya utakatifu wa huduma ya kiroho. Utambuzi huu utaweka maisha na umakini na nguvu ya kudumu katika utekelezaji wa kila wajibu. {9T 150.1}.

Dini, iliyo safi, dini isiyo na waa, inahitajika sana. Hakuna ila bidi ya kazi kwa moyo wote ndiyo itasaidia kuziokoa roho za watu. Tunapaswa kufanya kazi zetu za kila siku kuwa matendo ya ibada, tukizidi kuongezeka kwa kutumika, kwa sababu tunaiona kazi yetu katika nuru wa umilele. {9T 150.2}.

Kazi yetu imewekewa alama na Baba yetu wa mbinguni. Tunapaswa kuzichukua Biblia zetu na kwenda kuuonya ulimwengu. Tunapaswa kuwa mikono ya usaidizi ya Mungu katika kuokoa roho--njia ambazo upendo Wake unapitia siku baada ya siku kutiririka kwa wanaoangamia. Utambuzi wa kazi kubwa ambayo amependelewa kuishiriki, humtukuza na kumtakasa mtenda kazi wa kweli. Amejazwa na imani itendayo kazi kwa upendo na husafisha roho. Hakuna kitu kigumu kwa yule ajitoaye katika mapenzi ya Mungu. Kumfanyia Bwana” ni jambo linalompa haiba yeyote Mungu ampaye kazi yoyote kuifanya. {9T 150.3}

Endelea na kazi zako zote kulingana na kanuni za kidini. Hebu ombi lako la dhati liwe: Ninaweza kufanya nini kumpendeza Bwana?” Tembelea mahali ambapo waumini wanahitaji kutiwa moyo na kusaidiwa. Katika kila hatua uliza: Je! hii ndiyo njia ya Bwana? Je, katika roho, katika neno, katika matendo, na katika nia ninapatana na mapenzi Yake?” Ikiwa unafanya kazi kwa ajili ya Mungu kwa jicho moja kwenye utukufu wake, kazi yako itaubeba uungu, na utakuwa unatekeleza makusudi ya Bwana. {9T 150.4}

Katika kujifunza kwaenuneno la Mungu, zameni ndani zaidi na Zaidi kwenye kina. Shikilieni imani juu ya nguvu za kimbingu na sauti ya kina ya uvuvio. Tumieni nguvu za Mungu katika huduma yenu, mkikumbuka kuwa Bwana Yu nyuma yenu. Hebu upendo Wake uangaze kupitia yote mnayofanya na kuyasema. Hebu Ukweli, wa thamani, ulio sahili wa Neno la Mungu, ung'ae kwa uangavu kamili. Nyenyekezeni nafsi mbele za Mungu. Kristo atakuwa ufanisi wenu. Amewaweka ninyi kuwa wasimamizi juu ya nyumba Yake, ili kutoa chakula kwa wakati wake. Watenda kazi wa Kristo wako karibu sana na moyo Wake wa upendo. Anatamani kuikamilisha nyumba Yake kwa ukamilifu wa watumishi Wake. - {9T 151.1}

Kristo ni Mkombozi Mwenye huruma. Katika uwezo Wake wa kutegemeza, wanaume na wanawake huwa hodari kuyashinda maovu. Mwenye dhambi anayesukwa sukwa moyoni anapoitazama dhambi, kwake inakuwa dhambi kupita kiasi. Anashangaa kwamba hakuja kwa Kristo mapema. Huona kwamba makosa yake yanapaswa kushindwa na kwamba tamaa na uchu wake vinapaswa kuyatitii mapenzi ya Mungu, kwamba awe mshirika wa tabia ya Uungu; akiisha kuushinda ufisadi uliomo duniani uletwao na tamaa. Akiwa ametubia uasi wake wa sheria ya Mungu, anajitahidi sana kuishinda dhambi. Anatafuta kuifunua nguvu ya neema ya Kristo, na yeye analetwa katika upatanifu binafsi na Mwokozi. Daima anamweka Kristo mbele yake. Akiomba, akiamini, hupokea baraka anazohitaji, husogea karibu zaidi na zaidi kwenye kiwango cha Mungu kwa ajili yake. {9T 151.2}

Fadhila mpya zinafunuliwa katika tabia yake anapojikana nafsi yake na kuuinua msalaba, akifuata pale Kristo anapoiongoza njia. Anampenda Bwana Yesu kwa moyo wake wote, na Kristo anakuwa hekima yake, haki yake, utakaso wake, na ukombozi wake. {9T 151.3}

Kristo ndiye kielelezo chetu, msukumo wetu, thawabu yetu kuu sana. "Ninyi ni shamba la Mungu, ninyi ni Jengo la Mungu." 1 Wakorintho 3:9. Mungu Ndiye Mjenzi Mkuu, lakini mwanadamu ana sehemu ya kutenda. Anapaswa ushirikiana na Mungu. "Sisi tu watendakazi pamoja na Mungu." Fungu la 9. Kamwe msisahau Maneno: "pamoja na Mungu." "Utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa hofu na kutetemeka. Kwa maana Ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu kutaka na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema." Wafilipi 2:12, 13. Nguvu ya neema ya Kristo ya kutenda miujiza inadhihirishwa katika uumbaji wa mwanadamu mwenye moyo mpya, maisha ya juu, shauku takatifu zaidi. Mungu anasema: nami nitawapa ninyi moyo mpya." Ezekieli 36:26 Je! Huu sio uumbaji mpya wa mwanadamu? Muujiza mkubwa uwezao kutendwa? Je, Nini wakala wa kibinadamu hawezi kufanya ambaye kwa imani anashikilia uwezo wa Mungu? - {9T 152.1}

Kumbuka kwamba katika kufanya kazi na Kristo kama Mwokozi wako binafsi ndipo zilipo nguvu zako na ushindi wako. Hii ndio sehemu ambayo wote wanapaswa kutenda. Kristo Ndiye njia, Ukweli na uzima. Anasema: “Bila Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.” Yohana 15:5. Na nafsi iliyotubu, iaminiyo hujibu: Nayaweza mambo yote katika Kristo. anitiaye nguvu.” Wafilipi 4:13. Kwa wale wafanyao hivi huja uhakikisho. Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu." Yohana 1:12. {9T 152.2}

## SEHEMU YA 4—KAZI YA AFYA

"Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo yote, Na kuwa na afya yako." 3 Yohana 1:2.

## SURA YA 15
## UAMINIFU KATIKA MATENGENEZO YA AFYA

[*Manuscript Iliyosomwa Mbele Ya Wajumbe Wa Mkutano Mkuu Wa Kanisa (G.C), Washington D. C., Mei 31, 1909*.]

Nimeagizwa kutoa ujumbe kwa watu wetu wote juu ya somo la matengenezo ya afya, kwani wengi wamerudi nyuma kutoka kwenye uaminifu wao wa zamani kwa kanuni za matengenezo ya afya. {9T 153.1}

Kusudi la Mungu kwa watoto Wake ni kwamba wakue na kufikia kimo kamili cha wanaume na wanawake katika Kristo. Ili kufanya hivyo, ni lazima watumie ipasavyo kila nguvu ya akili, nafsi, na mwili. Hawawezi kumudu kupoteza nguvu zozote za mwili au za kiakili. {9T 153.2}

Swala la jinsi ya kuihifadhi afya ni moja ya mambo ya msingi yenye umuhimu. Tunapojifunza hili swala katika hofu ya Mungu tutajifunza kwamba ni bora, kwa maendeleo yetu yote ya kimwili na kiroho, kuzingatia usahili katika chakula. Hebu tujifunze kwa subira swala hili. Tunahitaji maarifa na uamuzi ili kuenenda kwa busara katika jambo hili. Sheria za asili hazipaswi kupingwa, bali zifuatwe. {9T 153.3}

Wale ambao wamepokea maelekezo kuhusu ubaya wa matumizi ya vyakula vya nyama, chai na kahawa, na maandalizi ya chakula yasiyofaa, na ambao wameazimia kufanya agano na Mungu kwa kujitoa kafara, hawataendelea kuendekeza hamu yao ya kula chakula wanachojua kuwa hakina afya. Mungu hudai kwamba uchu wa chakula utakaswe, na kwamba kujinyima kuzingatiwe kwa yale yote yasiyofaa. Hii ni kazi ambayo itabidi ifanywe kabla ya watu Wake kusimama mbele Zake wakiwa wakamilifu. {9T 153.4}

### Wajibu Binafsi

Watu wa Mungu waliosalia lazima wawe watu walioongoka. Uwasilishaji wa ujumbe huu ni unapaswa ulete matokeo ya uongofu na utakaso wa roho. Tunapaswa kuhisi nguvu za Roho wa Mungu katika jambo hili. Huu ni ujumbe wa ajabu na wa uhakika; una maana ya kila kitu kwa mpokeaji, na unapaswa kutangazwa kwa sauti kuu. Ni lazima tuwe na imani ya kweli, yenye kudumu kwamba ujumbe huu utasonga mbele kwa umuhimu zaidi hadi mwisho wa wakati. {9T 154.1}

Kuna baadhi ya wanaojiita waumini ambao hukubali sehemu fulani za Shuhuda kama ujumbe wa Mwenyezi Mungu, huku wakizikataa sehemu zile zinazokemea tamaa wazipendazo. Watu kama hao hufanya kazi kinyume na ustawi wao na ustawi wa kanisa. Ni muhimu tutembee katika nuru wakati tungali tunayo nuru. Wale wanaodai kuamini katika matengenezo ya afya, na bado wanakua kinyume na kanuni zake katika maisha ya kila siku, wanatesa nafsi zao na wanaacha maoni yasiyo sahihi katika akili za waumini na wasioamini. {9T 154.2}

### Nguvu Kupitia Utii

Wajibu mzito upo juu ya wale wanaoijua Kweli, kwamba matendo yao yote yalingane na imani yao, na kwamba maisha yao yatasafishwa na kutakaswa, na kuwekwa tayari kwa kazi ambayo lazima ifanyike haraka katika siku hizi za mwisho za ujumbe. Hawana muda wala nguvu za kutumia katika kuendekeza uchu wa chakula. Maneno yanapaswa kuja kwetu sasa kwa msukumo, Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako Kwake Bwana." Matendo 3:19. Kuna wengi miongoni mwetu ambao wana upungufu wa kiroho na ambao, isipokuwa wameongoka kabisa, hakika watapotea. Je, unaweza kumudu kukimbia hatari? {9T 154.3}

Kiburi na udhaifu wa imani vinawanyima wengi baraka nyingi za Mungu. Wapo wengi ambao, isipokuwa wainyenyekeze mioyo yao mbele za Bwana, watashangaa na kukata tamaa wakati kilio kitakaposikika: "Tazama, Bwana arusi

anakuja." Mathayo 25:6. Wana nadharia ya Ukweli, lakini wao hawana mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao. Imani yetu kwa wakati huu lazima isiishie kwenye dhana ya, au imani katika nadharia ya ujumbe wa malaika wa tatu. Ni lazima tuwe na mafuta ya neema ya Kristo ambayo yataijaza taa na kuifanya nuru ya uzima iangaze, ikionyesha njia kwa wale walio gizani. {9T 155.1}

Ikiwa tutaepuka kuwa na uzoefu mbaya, lazima tuanze kwa bidii bila kukawia kushughulikia wokovu wetu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kuna wengi ambao hawatoi uthibitisho imara kwamba ni wa kweli katika viapo vyao vya ubatizo. Bidii yao inapozwa na desturi, tamaa ya kilimwengu, kiburi, na kujipenda nafsi. Mara kwa mara hisia zao huchochewa, lakini hawaanguki juu ya Mwamba, Kristo Yesu. Hawaji kwa Mungu wenye mioyo iliyovunjika katika toba na maungamo. Wale wanaopitia kazi ya uongofu wa kweli katika mioyo yao watadhihirisha matunda ya Roho katika maisha yao. Oh Laiti wale ambao wana hali duni ya kiroho wangetambua kwamba uzima wa milele unaweza kutolewa kwa wale tu ambao wanakuwa washirika wa asili ya kimbingu na kuepuka uharibifu uliomo duniani utokanao na tamaa! {9T 155.2}

Nguvu ya Kristo pekee ndiyo inaweza kufanya mabadiliko katika moyo na akili, kwamba vyote vinapaswa kufanywa kushiriki pamoja Na Kristo maisha mapya katika ufalme wa mbinguni. "Mtu asipozaliwa mara ya pili," Mwokozi alisema, "hawezi kuuona ufalme wa Mungu." Yohana 3:3. Dini itokanayo na Mungu ni dini pekee iongozayo kwa Mungu. Ili tumtumikie Yeye ipasavyo, ni lazima tuzaliwe kwa Roho Mtakatifu. Hii itatufanya kukesha. Itasafisha moyo na kufanya upya akili, na kutupa uwezo mpya wa kumjua na kumpenda Mungu. Itatupatia utii wa hiari kwa matakwa Yake yote. Hii ndiyo ibada ya kweli. {9T 156.1}

Mungu anahitaji watu Wake kuendelea daima. Tunahitaji kujifunza kuwa uchu wa chakula ni kizuizi kikubwa cha ubora wa akili na utakaso wa roho. Pamoja na kukiri kwetu kwa matengenezo ya afya, wengi wetu tunakula vibaya. Kuendekeza uchu wa kula ndio sababu kuu ya unyonge wa kiakili na kimwili, na kwa kiasi ndiyo msingi wa udumavu na vifo vya mapema. Hebu mtu ambaye anatafuta kuwa na usafi wa roho akumbuke kwamba ndani ya Kristo kuna uwezo wa kudhibiti uchu wa kula.
{9T 156.2}

## Vyakula vya Nyama

Ikiwa tungeweza kufaidika kwa kuendekeza kutamani vyakula vya nyama, nisingewasihi kuhusu jambo hili; lakini najua hatuwezi. Vyakula vya nyama vinadhuru ustawi wa kimwili, na tunapaswa kujifunza kuishi bila nyama. Wale

ambao wako katika nafasi ambayo inawezekana kupata chakula cha mboga, lakini wanachagua kufuata mielekeo yao wenyewe katika suala hili, kula na kunywa kama wanavyotaka, taratibu watakuwa hawayajali maagizo ambayo Bwana ametoa kuhusu maeneo mengine ya Ukweli wa sasa na watapoteza mtazamo wao wa kile ambacho ni Ukweli; hakika watavuna kama walivyopanda. {9T 156.3}

Nimeagizwa kuwa wanafunzi katika shule zetu wasipewe vyakula vya nyama au vilivyoandaliwa isivyofaa. Hakuna kitu ambacho kitatumika kuchochea uchu wa chakula kinapaswa kuwekwa mezani. Natoa wito kwa wazee na vijana na watu wa makamo. Kataeni uchu wa vitu ambavyo vinawadhuru. Mtumikieni Bwana kwa kujinyima. {9T 157.1}

Hebu watoto wawe na akili katika jambo hili. Sisi sote ni washirika wa familia ya Bwana, na Bwana angetaka watoto Wake, wadogo kwa wakubwa, waamue kukataa uchu wa chakula na kuokoa mali zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za mikutano na kusaidia wamishionari. {9T 157.2}

Nimeagizwa kuwaambia wazazi: Jiwekeni wenyewe, nafsi na roho zenu, upande wa Bwana kwa swala hili. Tunapaswa kukumbuka kwamba katika siku hizi za rehema tuko kwenye kujaribiwa mbele za Bwana wa ulimwengu. Je, hamtaacha uchu wa chakula unaowadhuru? Maneno ya kukiri ni rahisi; hebu matendo yako ya kujikana nafsi yashuhudie kwamba utakuwa mtiifu kwa maagizo ya Mungu aliyoyatoa kwa watu Wake wa pekee. Kisha weka kwenye hazina sehemu ya mali unayohifadhi kwa matendo yako ya kujinyima, na huko kutakuwa ni ile ya kuiendeleza kazi ya Mungu. {9T 157.3}

Kuna wengi wanaohisi kwamba hawawezi kuishi bila chakula cha nyama; lakini kama wangejiweka wao wenyewe katika upande wa Bwana, wakiwa wameazimia kwa uthabiti kutembea katika njia ya uongozi Wake, wangepokea nguvu na hekima kama ya Danieli na wenzake. Wangeona kwamba Bwana angewapa uamuzi mzuri. Wengi wangeshangaa kuona ni kiasi gani kingeweza kuokolewa kwa ajili ya kazi ya Mungu kwa matendo ya kujinyima. Kiasi kidogo kilichohifadhiwa kwa matendo ya kujikana nafsi kitafanya zaidi kwa ajili ya kuijenga kazi ya Mungu kuliko kiasi kubwa kitakavyofanya katika kuitimiza ambacho hakikutolewa kwa kujikana nafsi. {9T 157.4}

Waadventista Wasabato wanashikilikia Kweli muhimu. Zaidi ya miaka arobaini iliyopita Bwana alitupa nuru maalum juu ya matengenezo ya afya, lakini tunatembeaje katika nuru hiyo? Ni wangapi wamekataa kuishi kulingana na mashauri ya Mungu! Kama watu, tunapaswa kuendelea kulingana na nuru tuliyoipokea. Ni wajibu wetu kuelewa na kuheshimu kanuni za matemgenezo ya

afya. Juu ya jambo la kiasi tunapaswa kuwa mbele ya watu wengine wote; na bado wako miongoni mwetu washiriki wa kanisa wenye uelewa, na hata watumishi/wachungaji wa injili, ambao wana heshima ndogo kwa nuru ambayo Mungu ameitoa juu ya jambo hili. Wanakula wapendavyo na kutenda wapendavyo. {9T 158.1}

Hebu wale ambao ni waalimu na viongozi katika kazi yetu wachukue msimamo wao kwa uthabiti katika msingi wa Biblia kuhusiana na matengenezo ya afya, na kutoa ushuhuda wa wazi kwa wale wanaoamini tunaishi katika siku za mwisho za historia ya dunia. Mstari wa wazi lazima uchorwe kati ya wale wanaomtumikia Mungu na wale wanaojitumikia wenyewe. {9T 158.2}

Nimeonyeshwa kwamba kanuni tulizopewa siku za mwanzo za ujumbe ni zina umuhimu na zinapaswa kuzingatiwa kwa uangalifu leo kama ilivyokuwa kwa wakati huo. Kuna ambao hawajawahi kuifuata nuru iliyotolewa juu ya swala la chakula. Sasa ni wakati wa kuichukua nuru kutoka chini ya pishi liangaze kwa miale ya wazi na angavu. {9T 158.3}

Kanuni za maisha ya kiafya zina maana kubwa sana kwetu kwa mtu binafsi na kama jumuiya. Wakati ujumbe wa matengenezo ya afya uliponijia kwa mara ya kwanza, nilikuwa dhaifu na mnyonge, nikiwa na tabia ya kuzirai mara kwa mara. Nilikuwa nikimwomba Mungu kwa ajili ya msaada, na alifungua mbele yangu somo kuu la matengenezo ya afya. Yeye aliniagiza kwamba wale walio wanaozishika amri Zake lazima waletwe katika uhusiano mtakatifu Naye, na kwamba kwa kuwa na kiasi katika kula na kunywa wanapaswa kuhifadhi vema hali zao za kiakili na kimwili kwa ajili ya huduma. Nuru hii imekuwa mbaraka mkubwa kwangu. Nilichukua msimamo wangu kama mwanamatengenezo ya afya, nikijua kwamba Bwana angeniimarisha. Nina afya bora leo, licha ya umri wangu, kuliko nilivyokuwa katika siku zangu za ujana. {9T158.4}

Imekuwa ikisemekana na baadhi kwamba sijazifuata kanuni za matengenezo ya afya kama nilivyoyatetea kwa kalamu yangu; lakini naweza kusema kwamba nimekuwa mwanamatengenezo mwaminifu wa afya. Wale ambao wamekuwa washiriki wa familia yangu wanajua kwamba hili ni kweli. {9T 159.1}

### "Kwa Utukufu wa Mungu"

Hatuwekei mstari wowote wa wazi wa kufuatwa katika lishe; lakini tunasema kwamba katika nchi ambazo kuna matunda, nafaka, na karanga kwa wingi, chakula cha nyama si chakula sahihi kwa watu wa Mungu. Ninalo agizo kuwa chakula cha nyama kina tabia ya kufanya tabia ya mnyama katika asili zetu, kuwaondolea wanaume na wanawake upendo na huruma ambayo wanapaswa kuihisi kwa kila mtu, na kuzipa hisia za chini udhibiti juu ya nguvu za juu za kiumbe. Ikiwa ulaji wa nyama ulikuwa wenye afya, si salama sasa. Saratani,

uvimbe, na magonjwa ya mapafu kwa kiasi kikubwa husababishwa na ulaji wa nyama. {9T 159.2}

Hatupaswi kufanya matumizi ya chakula cha nyama kuwa kipimo cha ushirika, lakini tunapaswa kuzingatia mvuto walio nao wanaojiita waumini wanaotumia vyakula vya nyama juu ya wengine. Kama wajumbe wa Mungu, Je, hatuwezi kuwaaambia watu: "Basi mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu?" 1 Wakorintho 10:31. Je, hatutatoa ushuhuda thabiti dhidi ya uchu wa tamaa potovu? Je, wowote ambao ni watumishi wa injili, wanaotangaza ukweli wa thamani kuu zaidi kuwahi kutokea waliopewa wanadamu, wataweka kielelezo katika kuvirudia vyungu vya nyama za Misri? Je wale wanaotegemezwa kwa zaka kutoka katika ghala ya Mungu watajiruhusu wenyewe kwa kujifurahisha nafsi ili kutia sumu mkondo uletao uhai upitao katika mishipa yao? Je, watapuuza nuru na maonyo ambayo Mungu amewapa? Afya ya mwili inapaswa kuzingatiwa kuwa muhimu kwa ukuaji wa neema na kuiweka sawa hasira. Ikiwa tumbo halijatunzwa vizuri, uundaji wa tabia ya haki, ya maadili hautawezekana. Ubongo na mishipa vinahurumiwa na huruma ya tumbo. Ulaji na unywaji mbaya huleta matokeo mabaya ya kufikiri na kutenda. {9T 159.3}

Wote sasa wanapimwa na kuthibitishwa. Tumebatizwa katika Kristo, na kama tutatenda sehemu yetu kwa kujitenga na kila kitu ambacho kingetuburuza chini na kutufanya tusivyopaswa kuwa, tutapewa nguvu za kukua katika Kristo, aliye kiongozi wetu aliye hai, nasi tutauona wokovu wa Mungu. {9T 160.1}

Ni wakati tu tutakapokuwa na akili kuhusiana na kanuni za maisha ya kiafya ndipo tutaweza kuamshwa kikamilifu kutazama ubaya unaotokana na ulaji mbaya usiofaa. Wale ambao, baada ya kuona makosa yao, wana ujasiri kubadilisha tabia zao, watatambua kwamba mchakato wa matengenezo unahitaji mapambano na uvumilivu mwingi; lakini wakati ladha sahihi itakapotengenezwa, watatambua kwamba matumizi ya chakula ambacho hapo awali walikiona kuwa hakina madhara kilikuwa polepole lakini kwa hakika kikiweka msingi wa "dyspepsia/kuvembewa" na magonjwa mengine. {9T 160.2}

Akina baba na akina mama kesheni katika maombi. Jilindeni sana dhidi ya kutokuwa na kiasi kwa kila namna. Fundisheni watoto wenu kanuni za matengenezo ya kweli ya afya. Wafundisheni ni mambo gani ya kuepuka ili kuihifadhi afya. Tayari ghadhabu ya Mungu imeanza kufika juu ya watoto wa kuasi. Ni uhalifu kiasi gani, dhambi gani, maovu ya namna gani yanayofunuliwa kila upande! Kama watu tunapaswa kuwa waangalifu sana kuwalinda watoto wetu dhidi ya washirika waovu. {9T 160.3}

## Kufundisha Kanuni za Afya

Juhudi kubwa zaidi zinapaswa kuwekwa kuwelimisha watu katika kanuni za

matengenezo ya afya. Shule za upishi zinapaswa kuanzishwa, na mafundisho ya nyumba kwa nyumba yatolewe katika ufundi wa kupika chakula kizuri. Watu wazima na vijana wanapaswa kujifunza jinsi ya kupika kwa urahisi zaidi. Popote Ukweli unapowasilishwa, watu wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuandaa chakula kwa njia rahisi, lakini kwa namna iletayo ladha nzuri. Wanatakiwa waoneshwe kuwa lishe bora inaweza kutolewa bila kuwa na matumizi ya vyakula vya nyama. {9T 161.1}

Wafundishe watu kwamba ni bora kujua jinsi ya kujikinga vizuri kuliko jinsi ya kujiponya magonjwa. Madaktari wetu wanapaswa kuwa waelimishaji wenye hekima, na kuwaonya wote dhidi ya kujifurahisha nafsi na kuonyesha kwamba kujiepusha na mambo ambayo Mungu amekataza ndiyo njia pekee ya kuzuia uharibifu wa mwili na akili. {9T 161.2}

Busara na umakini mwingi vitumike katika kuandaa chakula chenye lishe ili kuchukua mahali pa hicho ambacho hapo awali kilikuwa lishe kwa wale wanaojifunza kuwa wanamatengenezo wa afya. Imani kwa Mungu, bidii ya kusudi, na utayari wa kusaidiana utahitajika. Mlo unaokosa virutubisho sahihi vya lishe huleta aibu juu ya swala la matengenezo ya afya. Sisi ni binadamu hivyo tunakufa na lazima tujipatie chakula kitakachoupa mwili lishe ifaayo. {9T 161.3}

### Ulaji Uliopitiliza Kiasi

Baadhi ya watu wetu, ingawa kwa dhamiri wanajizuia kula vyakula visivyofaa, wanapuuza kujipatia virutubisho muhimu kwa ajili ya riziki ya mwili. Wale wanaozingatia sana na kupitlizaa katika matengenezo ya afya wako katika hatari ya kuandaa chakula kisichokuwa na ladha, na kuwajifanya kuwa  wajinga kwamba hakiwaridhishi. Chakula kinapaswa kutayarishwa kwa njia ambayo itakuwa ya kupendeza na yenye lishe. Hakipaswi kuwa kunyimwa kile ambacho mwili unahitaji. Mimi natumia kiasi cha chumvi, na mara nyingii natumia, kwa sababu chumvi, badala ya kuwa na madhara , ni muhimu kwa ajili ya damu. Mboga mboga zinapaswa kufanywa kuwa ya kupendeza na maziwa kidogo au krimu, au kitu cha aina hiyo. {9T 161.4}

Wakati maonyo yametolewa kuhusiana na hatari ya ugonjwa utokanao na siagi, na ubaya wa matumizi ya kupitiliza ya mayai kwa watoto wadogo, lakini hatupaswi kuona kuwa ni uvunjaji wa kanuni kwa kutumia mayai yanayokana na kuku wanaotunzwa vyema na kulishwa ipasavyo. Mayai yana viini ambavyo hurekebisha na kukabiliana na sumu fulani mwilini. {9T 162.1}

Baadhi, kwa kujiepusha na maziwa, mayai, na siagi, wameshindwa kuupatia mwili lishe inayofaa, na kama madhara yake wamekuwa dhaifu na kutoweza kufanya kazi. Hivyo matengenezo ya afya hupewa sifa mbaya. Hivyo kazi ambayo tumejaribu kuijenga imara imechanganywa na mambo ya hovyo ambayo Mungu

hayahitaji, na nguvu za kanisa zimelemazwa. Lakini Mungu ataingilia kuzuia matokeo ya mawazo haya magumu sana. Injili hupaswa kuipatanisha jamii ya wenye dhambi. Ni ya kuwaleta matajiri na maskini pamoja miguuni pa Yesu. {9T 162.2}

Wakati utakuja ambapo huenda tukalazimika kuacha baadhi ya makundi ya lishe tunayoyatumia sasa, kama vile maziwa na krimu na mayai; lakini si lazima kujiletea fadhaa mapema na vikwazo vilivyokithiri. Subiri hadi hali itakapobidi na Bwana hutayarisha njia kwa ajili ya hilo. {9T 162.3}

Wale ambao watafanikiwa katika kutangaza kanuni za matengenezo ya afya lazima walifanye Neno la Mungu kuwa kiongozi na mshauri wao. Ni pale tu walimu wa kanuni za matenegenzo ya afya wanapofanya hili wanaweza kusimama juu ya ardhi ya kifahari. Hebu kamwe tusitoe ushuhuda dhidi ya matengenezo ya afya kwa kushindwa kutumia chakula kitamu, kifaacho, badala ya vyakula vyenye madhara ambavyo tumevitupilia mbali. Usihimize kwa njia iwayo yote vichocheo vya hamu ya chakula. Kula tu chakula cha kawaida, rahisi na kizuri, na umshukuru Mungu daima kwa kanuni za matengenezo ya afya. Katika mambo yote uwe mkweli na mnyofu, nawe utapata ushindi wa thamani. {9T 162.4}

## Lishe katika Nchi Tofauti

Tunapofanya kazi dhidi ya ulafi na kutokuwa na kiasi, lazima tutambue hali ambayo inatawala familia ya mtu. Mungu ameweka riziki kwa wale wanaoishi katika nchi mbalimbali duniani. Wale wanaotamani kuwa watenda kazi pamoja na Mungu lazima wafikirie kwa makini kabla ya kubainisha ni vyakula gani vinapaswa na visivyopaswa kuliwa. Tunapaswa kuunganishwa na watu wengi. Matengenezo ya afya katika hali yake  ya juu sana yafundishwe kwa wale ambao changamoto zao zinawazuia kupata madhara zaidi kuliko mema ambavyo yangefanya. Ninapowahubiri injili walio maskini, ninaagizwa kuwaambia wale chakula ambacho kina lishe zaidi. Siwezi kuwaambia: "Usile mayai, au maziwa, au krimu. Msitumie siagi katika utayarishaji wa chakula. "Injili lazima ihubiriwe kwa watu maskini, lakini wakati bado haujafika wa kuwaagiza katika zuio kali zaidi. {9T 163.1}

## Neno kwa Wanaositasita

Wachungaji na Watumishi ambao wanahisi wako na uhuru wa kujifurahisha katika uchu wa chakulaa wanapungukiwa sana na ubora. Mungu anawataka kuwa wanamatengenezo wa afya. Anawataka waishi kulingana na nuru ambayo imetolewa juu ya jambo hili. Ninajisikia huzuni wakati Ninapoona wale ambao wanapaswa kuwa na bidii kwa kanuni zetu za afya, bado hawajaongoka katika njia sahihi za maisha. Ninaomba Bwana aweze kushawishi fahamu zao kwamba wanakabiliana na upotevu mkubwa. Ikiwa mambo yangelikuwa kama

yalivyopaswa kuwa katika nyumba zinazounda makanisa yetu, tungeliweza kufanya kazi maradufu kwa ajili ya
Bwana. {9T 163.2}

## Masharti ya Kujibiwa Maombi

Ili kutakaswa na kubaki kuwa safi, Waadventista Wa Sabato lazima wawe na Roho Mtakatifu ndani ya mioyo yao na nyumba zao. Bwana amenipa nuru kwamba wakati Israeli wa leo watakapojinyenyekeza mbele Zake, na kulisafisha hekalu la nafsi na uchafu wote, atasikia maombi yao kwa niaba ya wagonjwa na atabariki matumizi ya dawa Zake kwa magonjwa. Wakati kwa imani wakala wa kibinadamu anapofanya yote awezayo ili kupambana na magonjwa, kwa kutumia njia rahisi za matibabu ambazo Mungu ametoa, jitihada zake zitabarikiwa na Mungu. {9T 164.1}

Ikiwa, baada ya nuru kubwa hivyo kutolewa, watu wa Mungu watathamini mazoea mabaya, kuifurahisha nafsi na wakikataa kufanya matengenezo, watapata matokeo ya hakika ya uasi wa sheria. Ikiwa wamedhamiria kuridhisha uchu wao mpotovu kwa gharama yoyote, Mungu hatafanya muujiza kuwaokoa kutokana na matokeo ya tamaa zao. "Watalala kwa huzuni." Isaya 50:11. {9T 164.2}

Wale wanaochagua kuwa na kiburi, wakisema, “Bwana ameniponya, wala sina haja ya kujizuiakatika kula; Ninaweza kula na kunywa nipendavyo,” watakuwa na uhitaji wa muda mrefu, katika mwili na roho, wa uweza wa Mungu wa kurejesha. Kwa kuwa Bwana, kwa neema amekuponya, hupaswi kufikiri kwamba unaweza kujihusisha na mazoea ya kiulimwengu ya kuendekeza tamaa. Fanya kama Kristo alivyoamuru baada ya kazi Yake ya uponyaji--"nenda, na usitende dhambi tena." Yohana 8:11. Hebu uchu wa chakula usiwe mungu wako. {9T 164.3}

Bwana alitoa Neno Lake kwa Israeli ya kale, kama wangeshikamana Naye kabisa na kufanya yote anayohitaji, angewaepusha na magonjwa yote kama vile alivyokuwa amewaletea walipokuwa Misri; lakini ahadi hii ilitolewa kwa sharti la utii. Kama Waisraeli wangetii maagizo waliyopewa, na kufaidika na faida zake, wangekuwa fundisho kwa dunia la afya na ustawi. Waisraeli walishindwa kulitimiza kusudi la Mungu, na hivyo kushindwa kupokea baraka ambazo zingeweza kuwa zao. Lakini kwa Yusufu na Danieli, kwa Musa na Eliya, na wengine wengi, tunayo mifano mizuri ya matokeo ya mpango wa Kweli wa kuishi. Kama uaminifu leo utaleta matokeo kama hayo. Imeandikwa kwetu sisi: “Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu; mpate kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu." 1 Petro 2:9. {9T 165.1}

## Kujisalimisha na Kupumzika

Lo, ni wangapi wanapoteza baraka nyingi sana ambazo Mungu amewawekea

katika majaliwa ya kiafya na kiroho! Kuna roho nyingi ambazo hupambana kuwa na ushindi maalum na baraka maalum ili waweze kufanya jambo Fulani kubwa. Mwisho wa hili wanahisi kwamba lazima wafanye mapambano ya uchungu kwa sala na machozi. Watu hawa watakapochunguza Maandiko kwa maombi ili kujua mapenzi ya Mungu yaliyoelezwa, na kisha wafanye mapenzi yake kutoka moyoni bila kizuizi hata kimoja au kujitukuza nafsi, watapata pumziko. Uchungu wote, machozi na mapambano yote hayatawaletea baraka wanazozitamani. Binafsi lazima iwe kujisalimisha kabisa. Ni lazima nafsi isalimishwe kikamilifu. Wanapaswa kufanya kazi inayojitokeza, ikilinganishwa na wingi wa neema ya Mungu ambayo imeahidiwa kwa wote wamwombao kwa imani. {9T 165.2}

“Mtu yeyote akitaka kunifuata,” Yesu alisema, “na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate.” Luka 9:23. Hebu tumfuate Mwokozi kwa unyenyekevu, usahili na kujinyima. Hebu tumwinue Mtu wa Kalvari kwa Neno na kwa maisha matakatifu. Mwokozi anakuja karibu sana kwa wale wanaojiweka wakfu kwa Mungu. Ikiwa kuna wakati tulihitaji kazi ya Roho wa Mungu juu ya mioyo na maisha yetu, ni sasa. Hebu tuishikilie nguvu hii ya mbingu kwa ajili ya nguvu ya kuishi maisha ya utakatifu na kujisalimisha. - {9T 165.3}

Neno la Mungu liwe kitabu chetu cha kujifunzia. Bwana Ndiye msaidizi wetu na Mungu wetu. Hebu tumtazame Yeye ili kufungua njia kwa ajili ya ufanikishaji wa mipango yetu. {9T 166.1}

## SURA YA 16
## WITO KWA WAINJILISTI WAMISHENARI WA KITABIBU

[*Manuscript/Mswada Ilisomwa Mbele Ya Wajumbe Wa Mkutano Mkuu, Washington, D. C., Juni 1, 1909*.]

Tunaishi katika siku za mwisho. Mwisho wa mambo yote umekaribia. Ishara zilizotabiriwa na Kristo zinatimia haraka. Kuna nyakati za dhoruba mbele yetu, lakini hebu tusiseme neno moja la kutoamini au kukatisha tamaa. Yeye anayeyaelewa mahitaji ya hali anapanga kwamba faida ziletwe na watendakazi katika maeneo mbalimbali ili kuwawezesha kuwa na ufanisi zaidi wa kuamsha shauku za watu. Yeye anajua mahitaji yetu na mahitaji ya walio dhaifu katika kundi Lake, na anatuma ujumbe Wake katika barabara kuu na njia njia. Anatupenda kwa upendo wa milele. Tukumbuke kuwa tunaubeba ujumbe wa uponyaji kwa ulimwengu uliojaa roho za wagonjwa ya dhambi. Bwana atuzidishie imani na atusaidie kuona kwamba anatamani sisi sote tuifahamu huduma Yake ya uponyaji pamoja na kiti cha rehema. Yeye anataka nuru ya neema yake iangaze kutoka sehemu nyingi. {9T 167.1}

### Sanitariamu Kama Mawakala Wa Umishionari

Kuna roho katika sehemu nyingi ambazo bado hazijausikia ujumbe. Tangu sasa kazi ya umishionari wa kitabibu inapaswa kuendelezwa kwa bidii ambayo haikuwahi kuendelezwa kabla. Kazi hii ni mlango ambao Ukweli hupata kuingia katika miji mikubwa, na sanitariamu zinapaswa kuanzishwa katika maeneo mengi. {9T 167.2}

Kazi ya sanitariamu ni mojawapo ya njia zenye ufanisi zaidi za kufikia tabaka zote za watu. Sanitariamu ni mkono wa kuume wa injili, unaofungua njia ambazo wanadamu wanaoteseka wanaweza kufikiwa kwa na habari njema ya uponyaji kwa njia ya Kristo. Katika taasisi hizi wagonjwa wanaweza kufundishwa kutoa haja zao kwa tabibu Mkuu, ambaye atashirikiana na juhudi zao za dhati za kurejesha afya, na kuwaletea uponyaji wa kiroho vile vile na uponyaji wa kimwili. {9T 167.3}

Kristo hayuko tena katika ulimwengu huu katika mwili, akipita katika miji na vijiji, akiwaponya watu mgonjwa; bali Ametuagiza kuiendeleza kazi ya umishonari wa kitibabu ambayo Yeye aliianzisha. Katika hili kazi tunayopaswa kufanya kwa ubora kadri tuwezavyo. Taasisi za kutunza wagonjwa zianzishwe, ambapo wanaume na wanawake wanaougua magonjwa wanaweza kuwekwa chini ya uangalizi wa matabibu na wauguzi wanaomcha Mungu; na kutibiwa bila dawa. {9T 168.1}

Nimeagizwa kwamba tusichelewe kufanya kazi inayotakiwa kufanywa katika kazi ya matengenezo ya afya. Kupitia kazi hii tunapaswa kuzifikia roho katika barabara kuu na njia njia. Nimepewa nuru maalum kwamba kupitia sanitariamu zetu nafsi nyingi zitaupokea na kuutii Ukweli wa sasa. Katika taasisi hizi wanaume na wanawake wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuitunza miili yao wenyewe na wakati huo huo jinsi ya kuwa imara katika imani. Wanapaswa kufundishwa nini maana ya kuula mwili na kuinywa damu ya Mwana wa Mungu. Kristo alisema: "Maneno hayo niwaambiayo ni roho, tena ni uzima." Yohana 6:63. {9T 168.2}

Sanitariamu zetu zinapaswa kuwa shule ambamo mafundisho yatatolewa katika kazi za umishionari wa kitabibu. Zinapaswa kuwaletea watu wanaougua kwa dhambi majani ya mti wa uzima, ambayo yatawarudishia amani, tumaini na imani katika Kristo Yesu. {9T 168.3}

Hebu kazi ya Bwana isonge mbele. Hebu umishionari wa kitabibu na kazi ya elimu zisonge mbele. Nina hakika kwamba hii ndio bahati yetu kubwa—yaani watendakazi wenye bidii, wanaojitolea, wenye akili na wenye uwezo. Katika kila mji mkubwa lazima kuwa uwasilishaji wa kazi ya kweli ya umishionari wa kitabibu. Hebu wengi sasa waulize: “Bwana, inanipasa kufanya nini?” Matendo 9:6. Ni kusudi la Bwana kwamba njia Yake ya kuponya bila dawa italetwa katika kila mji mkubwa kupitia taasisi zetu za matibabu. Mungu huwekeza utu mtakatifu kwa wale ambao husonga mbele zaidi na zaidi, katika kila mahali panapowezekana

kupata njia ya kuingia. Shetani ataifanya kazi kuwa ngumu iwezekanavyo, lakini nguvu za kimbingu zitajidhurisha kwa watenda kazi wote wenye mioyo ya kweli. Tukiongozwa na mkono wa Baba wa mbinguni, tusonge mbele, tukitumia kila fursa ya kupanua kazi ya Mungu. {9T 168.4}

Bwana anazungumza na wamisionari wote wa kitabibu, akisema: Nendeni, mkafanye kazi leo katika shamba Langu la mizabibu kuokoa roho. Mungu husikia maombi ya wote wamtafutao kwa kweli. Anao uwezo ambao sisi sote tunauhitaji. Anaujaza moyo kwa upendo, furaha, amani, na utakatifu. Tabia inaendelezwa kila mara. Hatuwezi kumudu kutumia muda kufanya kazi tofauti na makusudi Mungu. {9T 169.1}

Kuna madaktari ambao, kwa sababu ya uhusiano wa zamani na sanitaramu zetu, wanaona kuwa ni faida kukaa karibu na taasisi hizi; nao hulifumbia macho lile shamba kubwa, lililopuuzwa na ambalo halijalimwa; ambamo kazi isiyo ya ubinafsi ingekuwa baraka kwa wengi. Madaktari wamishionari wanaweza kutoa ushawishi, usafishao, na kutakasa. Madaktari ambao hawafanyi hivyo hutumia vibaya nguvu zao na kufanya kazi ambayo Bwana anaikataa. {9T 169.2}

## Mafunzo Ya Watendakazi

Ikiwa wakati wowote Bwana amesema kupitia mimi, Yeye huzungumza nisemapo kuwa watenda kazi wajishughulishao na elimu, katika kazi za huduma, na katika kazi za umishionari wa kitibabu lazima wasimame kwa umoja, wote wakifanya kazi chini ya uangalizi wa Mungu, mmoja akimsaidia mwenzake, kila mmoja akimbariki mwingine. {9T 169.3}

Wale waliounganishwa na shule zetu na sanitariamu wanapaswa kufanya kazi kwa bidii. Kazi ambayo inafanywa chini ya huduma ya Roho Mtakatifu, kwa upendo kwa Mungu na kwa wanadamu, itabeba sahihi ya Mwenyezi Mungu na itafanya itakuwa na msukumo wake kwenye akili za wanadamu. {9T 170.1}

Bwana anawaita vijana wetu kuingia katika shule zetu na kujitayarisha haraka kwa ajili ya huduma. Katika maeneo mbalimbali nje ya miji, shule zinapaswa kuanzishwa ambapo vijana wetu wanaweza kupata elimu ya kuwatayarisha kwenda kufanya kazi ya kiinjilisti na kazi ya umishionari wa tiba. {9T 170.2}

Bwana lazima apewe nafasi ya kuwaonyesha wanadamu wajibu wao na kufanya kazi katika nia zao. Hakuna mtu wa kujifunga kutumika kwa muda wa miaka kdhaa chini ya uongozi wa kundi moja la watu au katika tawi moja fulani la kazi ya Mwalimu mkuu; kwa maana Bwana mwenyewe atawaita wanadamu, kama zamani alivyowaita wavuvi wanyenyekevu, na Yeye Mwenyewe atawapa maelekezo kuhusuiana na eneo lao la kazi na mbinu wanazopaswa kufuata. Atawaita watu kutoka kwenye jembe la kukokotwa na kutoka kwenye kazi zingine kutoa sauti ya mwisho ya onyo kwa roho zinazopotea. Kuna njia nyingi za kufanya

kazi kwa Bwana, na Mwalimu Mkuu atafungua ufahamu wa watendakazi hawa, kuwawezesha kuona mambo ya ajabu katika Neno Lake. {9T170.3}

### Wauguzi Kama Wainjilisti

Kristo, Tabibu Mmisionari mkuu, Ndiye mfano wetu. Juu Yake imeandikwa kwamba "Naye alikuwa akizunguka Galilaya yote, akifundisha katika masunagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya Ufalme, na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu." Mathayo 4:23. Aliponya wagonjwa na kuihubiri Injili. Katika huduma Yake, uponyaji na kuhubiri injili viliunganishwa pamoja. Leo haipaswi kutenganishwa. {9T 170.4}

Wauguzi ambao wamefunzwa katika taasisi zetu wanapaswa kutayarishwa ili kwenda nje kama wamishonari matababu walio wainjilisti, wakiunganisha huduma ya neno na ile ya uponyaji wa kimwili. {9T 171.1}

Ni lazima tuache nuru yetu iangaze katikati ya giza la maadili. Wengi ambao sasa wako gizani, kadri wanavyoona kuakisiwa kwa Nuru ya ulimwengu, watatambua kwamba wanalo tumaini la wokovu. Nuru yako inaweza kuwa ndogo, lakini kumbuka kwamba ndiyo ambayo Mungu amekupa, na kwamba amekupa jukumu la kuingaza. Mmoja anaweza kuwasha utambi wake kutoka kwako, na nuru yake inaweza kuwa njia ya kuwaongoza wengine kutoka gizani. {9T 171.2}

Kote kutuzunguka kuna milango wazi kwa ajili ya huduma. Tunapaswa kufahamiana na majirani zetu na kutafuta kuwavuta kwa Kristo. Tunafanyapo hivi, Yeye atatukubali na kushirikiana nasi. {9T 171.3}

Mara nyingi wenyeji wa miji ambayo Kristo alifanya kazi walitamani abaki nao na kuendelea kufanya kazi kati yao. Lakini anliwaambia kwamba lazima aende kwenye miji ambayo haikuwa imesikia Ukweli ambao Ilimbidi auwasilishe. Baada ya kuwapa Ukweli wale waliokuwa mahali pamoja aliwaacha wajenge juu ya kile alichokuwa amewapa, huku akienda mahali pengine. Mbinu Zake za kazi zinapaswa kufuatwa leo na wale ambao amewaachia kazi Yake. Tunapaswa kwenda kutoka mahali hadi mahali pengine, tukiubeba ujumbe. Punde Ukweli unapokuwa umetangazwa mahali hapo, tunapaswa kwenda kuwaonya wengine. {9T 171.4}

Kunapaswa kuwa na makundi yaliyopangwa na kuelimishwa kikamilifu kufanya kazi kama wauguzi, kama wainjilisti, kama wahudumu, kama wauza vitabu, kama wanafunzi wa injili, ili kukamilisha tabia kwa kuufuata mfano wa kimbingu. Kujiandaa kupokea elimu ya juu katika shule ya juu ndiyo liwe kusudi letu. {9T 171.5}

Kutoka kwenye maagizo ambayo Bwana amenipa mara kwa mara, najua kwamba kunapaswa kuwa watendakazi wanaofanya ziara za uinjilisti wa kitibabu katika ya miji na vijiji. Wale wanaofanya kazi hii watakusanya mavuno mengi ya roho kutoka

kwenye mtabaka ya juu na ya chini. Njia ya kazi hii itaandaliwa kwa ubora zaidi na juhudi za mwinjilisti wa vitabu anayeshawishi watu na mwaminifu. {9T 172.1}

Wengi wataitwa shambani kufanya kazi nyumba kwa nyumba, wakitoa mafundisho ya Biblia na kuomba pamoja na walio na nia. {9T 172.2}

Hebu watumishi wetu, ambao wamepata uzoefu katika kuhubiri Neno, wajifunze jinsi ya kutoa kwa tiba rahisi na kisha kufanya kazi kwa akili kama wainjilisti wamishonari wa kitabibu. {9T 172.3}

Watendakazi - wamishenari wa injili ya matibabu - wanahitajika sasa. Hamwezi kuendelea kutumia miaka mingi katika maandalizi. Hivi karibuni milango iliyofunguliwa kwa ukweli itafungwa milele. Pelekeni ujumbe sasa. Msikawie, mkamruhusu adui kumiliki mashamba yaliyofunguliwa sasa mbele yenu. Hebu makundi madogo yaende kufanya kazi ambayo Kristo aliwapa wanafunzi Wake. Waache wafanye kazi kama wainjilisti, wakitawanya yetu machapisho na kuzungumza juu ya kweli kwa wale wanaokutana nao. Hebu wawaombee wagonjwa, wakiwahudumia mahitaji yao, si kwa kutumia dawa, lakini kwa tiba za asili, na kuwafundisha jinsi ya kuirejesha afya na kuepuka magonjwa. {9T 172.4}

## SURA YA 17
## CHUO CHA WAINJILISTI CHA LOMA LINDA

[*Manuscript Ilisomwa Mbele Ya Wajumbe Katika Mkutano Mkuu, Washington, D.C., Juni 1, 1909.*]

Nilipokuwa nikihudhuria Mkutano Mkuu wa 1905, huko Washington, D. C., nilipokea barua kutoka kwa J. A. Burden inayoelezea mali ambayo alikuwa ameipata kama maili nne kutoka Redlands. Nilipokuwa naisoma barua yake Nilivutiwa na kwamba hii ilikuwa moja ya sehemu ambazo nilikuwa nimeona katika maono, na mara moja nikamtumia ujumbe kuichukua mali bila kukawia. Baadaye, nilipotembelea eneo hilo, nilitambua kuwa ni mojawapo ya maeneo ambayo Nilikuwa nimeyaona karibu miaka miwili kabla katika maono. Nina shukrani kiasi gani kwa Bwana Mungu wetu kwa ajili ya mahali hapa! {9T 173.1}

Moja ya faida kuu za Loma Linda ni aina tofauti ya mandhari ya kupendeza kila upande. Mwonekano wa kina wa bonde na mlima ni mzuri. Lakini muhimu zaidi kuliko mandhari nzuri na majengo mazuri na viwanja vizuri ni ukaribu wa wa taasisi hii kuwa karibu nae eneo lililo na watu wengi na fursa hiyo inayotolewa ya kuwasiliana na watu wengi, ujuzi wa ujumbe wa malaika wa tatu. Tunapaswa kuwa na utambuzi wa kina wa kiroho, vinginevyo tutashindwa kutambua majaliwa ya Mungu yaliyofunguliwa ambayo yanatayarisha njia kwa ajili yetu kuuangaza ulimwengu. {9T 173.2}

Pamoja na kupamiliki mahali hapa linakuja jukumu zito la kufanya kazi ya taasisi ya elimu katika tabia. Loma Linda haitakiwi kuwa sanitarium tu, bali pia kituo cha elimu. Shule inapaswa ianzishwe hapa kwa ajili ya mafunzo ya wainjilisti wamishonari wa kitabibu. Mengi yanahusika katika kazi hii, na ni muhimu sana kwamba mwanzo mzuri ufanyike. Bwana ana kazi maalum ya kufanywa katika eneo hili. Aliniagiza niwaite bwana na Bibi Haskell kusaidia katika kuianza vizuri kazi hii sawa na ile waliyoifanya pale Avondale. Watendakazi wenye uzoefu wamekubali kuungana na vikosi vya Loma Linda kuendeleza shule hiyo ambayo lazima iendelezwe huko. Wanaposonga mbele kwa imani, Bwana atatangulia mbele yao, akiitayarisha njia. {9T 173.3}

Kuhusiana na shule ningesema: Ifanyeni iwe imara hasa katika elimu kwa wauguzi na waganga. Katika shule za kimishonari za kitabibu watendakazi wengi wanapaswa kuhitimu na uwezo wa madaktari kufanya kazi kama wainjilisti wamishonari wa matibabu. Mafunzo haya, Bwana ameyabainisha, yanapatana na kanuni za msingi za elimu ya juu ya kweli. Tunasikia mengi kuhusu elimu ya juu. Elimu ya juu kabisa ni kufuata nyayo za Kristo, tukiiga mfano alioutoa wakati Yeye alipokuwa duniani. Hatuwezi kupata elimu ya juu zaidi ya hii, hivyo darasa hili la mafunzo litawafanya watu kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. {9T 174.1}

Kuwa na elimu ya juu ni kuwa na uhusiano hai na Kristo. Mwokozi aliwachukua wavuvi wasio na elimu kutoka kwenye mashua zao na nyavu zao na akawaunganisha Naye Mwenyewe kadri alivyosafiri kutoka mahali hadi mahali, akiwafundisha watu na kuwahudumia mahitaji yao. Akiketi juu ya mwamba au juu ya mahali palipoinuka, aliwakusanya wanafunzi Wake kando Yake na kuwafundisha, na muda si mrefu, mamia ya watu wangekuja kuyasikisikiliza maneno Yake. Kuna wanaume na wanawake wengi ambao husema kwamba wanajua yote yafaayo kujua, wakati wanahitaji sana kukaa kwa unyenyekevu chini ya miguu ya Yesu na kujifunza Kwake Yeye ambaye alitoa maisha Yake ili apate kuukomboa ulimwengu ulioanguka. Sisi sote tunamhitaji Kristo, ambaye aliziacha nyua za kifalme, akiweka kando vazi Lake la kifalme na taji na utukufu Wake mbinguni, na kujivika ubinadamu. Mwana wa Mungu alikuja kama mtoto mchanga, ili apate kuelewa uzoefu wa wanadamu na kujua jinsi ya kushughulika nao. Anayajua mahitaji ya watoto. Katika siku za huduma Yake duniani hakuwaruhusu kuzuiliwa kuja Kwake. Wala mziwazuie, aliwaambia wanafunzi wake, kwa maana walio kama hawa ufalme wa mbinguni ni wao." {9T 174.2}

Katika kazi ya shule dumisheni usahili. Hakuna hoja yenye nguvu kama mafanikio yale yanavyoanzishwa katika usahili. Mnaweza kupata mafanikio katika elimu ya wanafunzi kama wamishonari wa matibabu bila ya kuwa na shule ya utabibu

inayoweza kuhitimisha waganga/matabibu wanaoweza kushindana na waganga wa ulimwengu. Hebu wanafunzi wapewe elimu ya vitendo. Kadiri msivyozidi kutegemea mbinu za kielimu za kidunia ndivyo wanafunzi watakavyokuwa bora. Maelekezo maalum yanapaswa kutolewa katika sanaa ya kutibu wagonjwa bila kutumia dawa zenye sumu na kupatana na nuru ambayo Mungu ameitoa. Katika matibabu ya wagonjwa, dawa zenye sumu hazihitajiki kutumiwa. Wanafunzi wanapaswa kutoka shuleni bila kuachana na kanuni za matengenezo ya afya au upendo wao kwa Mungu na uadilifu. {9T 175.1}

Elimu inayokidhi viwango vya ulimwengu ni ya kutothaminiwa na wale wanaotafuta kwa ufanisi katika kuifanya kazi ya kimisionari wa kitabibu ikipatana na kazi ya ujumbe wa malaika wa tatu. Wanapaswa kuelimishwa kutoka katika mtazamo wa dhamiri, na, kama kwa uangalifu na kwa uaminifu wakifuata njia sahihi katika matibabu yao ya wagonjwa, njia hizi zitakuja kupendwa kuliko njia ambazo wengi wamezizoea, ambazo zinadai matumizi ya dawa zenye sumu. {9T 175.2}

Hatupaswi kwa wakati huu kutafuta kushindana na shule za matibabu za kidunia. Ikiwa tutafanya hivi, nafasi zetu za kufanikiwa zitakuwa ndogo. Hatujawa tayari sasa kutekeleza kwa mafanikio kazi ya kuanzisha taasisi kubwa za mafunzo ya matibabu. Zaidi ya hayo, kwa kufuata mbinu za ulimwengu za mafunzo ya matibabu, tukitoza ada kubwa ambazo waganga/matabibu wa kidunia wanatoza katika huduma zao, kwa kufanya hivi, tungeenda mbali na mpango kazi wa Kristo wa huduma yetu kwa wagonjwa. {9T 175.3}

Kunapaswa kuwa katika sanitariamu zetu wanaume na wanawake wenye akili wanaoweza kufundisha njia za Kristo za utumishi. Chini ya maelekezo ya walimu wenye uwezo, waliowekwa wakfu, vijana wanaweza kuwa washiri wa asili ya kimbingu na kujifunza jinsi ya kuepuka uharibifu uliomo duniani utokanao na tamaa. Niimeagizwa kuwa tunapaswa tuwe na wanawake wengi zaidi ambao wanaweza kukabiliana hasa na magonjwa ya wanawake, wauguzi wanawake wengi zaidi ambao watawatibu wagonjwa kwa njia rahisi bila kutumia dawa. {9T 176.1}

Haipatani na maagizo yaliyotolewa kule Sinai kwamba madaktari wa kiume wanapaswa kufanya kazi ya wakunga. Biblia inaeleza juu ya wanawake kuhudumiwa wakati wa kujifungua na wanawake, na ndivyo inapaswa kuwa daima. Wanawake wanapaswa kuelimishwa na kufundishwa kutenda kwa ustadi kama wakunga na waganga kwa jinsia zao. Huu ni mpango wa Bwana. Hebu tuwaelimishe mabinti wawe na akili katika kazi ya kutibu magonjwa ya jinsia zao. Tunaweza kuwa na shule ambapo wanawake wanaweza kuelimishwa na

madaktari wanawake kufanya kazi bora zaidi katika kutibu magonjwa ya wanawake. Miongoni mwetu kama watu kazi ya utabibu inapaswa kusimama juu kabisa. {9T 176.2}

Huko Loma Linda tuna kituo chenye faida kwa ajili ya kuendeleza shughuli mbalimbali za umishonari. Tunaweza kuona kwamba ilikuwa katika majaliwa ya Mungu kwamba hii sanitarium iliwekwa katika umiliki wa watu wetu. Tunapaswa kuthamini Loma Linda kama mahali ambapo Bwana aliona tunapaswa kuhitaji na ambapo alitupa. Kuna kazi ya thamani sana ya kufanywa kuhusiana na maslahi ya sanitarium na shule ya Loma Linda, na hii itafanywa, wakati sisi sote tunafanya kazi kulifikia lengo hilo, tukienda kwa umoja katika utaratibu wa Mungu. {9T 176.3}

Huko Loma Linda wengi wanaweza kuelimishwa kufanya kazi kama wamisionari kwa ajili ya afya na kiasi. Walimu wanapaswa kuwa tayari kwa aina nyingi za kazi. Shule zinapaswa kuanzishwa katika maeneo ambayo bado hakuna juhudi zilizokwishafanywa. Wamishonari wanapaswa kwenda katika majimbo mengine ambako kazi ndogo imefanywa. Kazi ya kutangaza kanuni za Matengenezo ya afya lazima itimie. Mungu atusaidie kama watu kuwa na hekima. {9T 177.1}

Nina shauku kubwa kwamba uchunguzi makini uzingatiwe kuhusiana na mahitaji ya taasisi ztu za Loma Linda na hatua stahaki zichukuliwe. Katika kuendeleza kazi mahali hapa, watu wenye vipaji na hali ya kiroho iliyo imara wanahitajika. Walimu bora zaidi wanapaswa kuajiriwa katika kazi ya elimu, wanaume na wanawake watakaokwenda kwa uangalifu, wakimtegemea Bwana kabisa. Ikiwa walimu katika kazi ya matibabu watasimama mahali pao katika kumcha Mungu, tutaona kazi nzuri ikifanywa. Na Kristo kama mwalimu wetu tunaweza kufikia kiwango cha juu katika ujuzi wa sayansi ya Kweli ya uponyaji. {9T 177.2}

Jambo la muhimu zaidi ni kwamba wanafunzi wafundishwe jinsi ya kuwasilisha kwa usahihi kanuni za matengenezo ya afya. Wafundisheni kuchukua aina hii ya masomo kwa uaminifu, ikiunganishwa na aina zingine muhimu za elimu. Neema ya Yesu Kristo itawapa hekima wote wanaofuata mpango wa Bwana wa elimu ya Kweli. Hebu wanafunzi wafuate kwa ukaribu kielelezo cha Yule aliyenunua jamii ya wanadamu kwa bei ghali ya maisha Yake Mwenyewe. Hebu wamsihi Mwokozi na wamtegemee Yeye ambaye Ndiye anayeponya kila aina ya magonjwa. Bwana angetaka watenda kazi wafanye juhudi maalum kuwaelekeza wagonjwa na wanaoteseka kwa Tabibu Mkuu aliyeufanya mwili wa mwanadamu. {9T 177.3}

Ni vyema shule zetu za mafunzo kwa wafanyakazi wa Kikristo zianzishwe karibu na taasisi zetu afya, ili wanafunzi waelimishwe katika kanuni za maisha yenye afya. Taasisi zinazotuma watenda kazi wawezao kutoa hoja za imani yao, na

walio na imani itendayo kazi kwa upendo na kuitakasa nafsi, ni za thamani kubwa. Nina maagizo wazi kwamba, popote inapowezekana, shule zianzishwe karibu na vituo vyetu vya sanitariamu, ili kila taasisi iwe msaada na nguvu kwa ajili ya nyingine. Yeye aliyemuumba mwanadamu ana maslahi na wale wanaoteseka. Ameelekeza katika uanzishwaji wa sanitariamu zetu na katika ujenzi wa shule zetu karibu na sanitariamu, ili ziwe njia bora katika kuwafunza wanaume na wanawake kwa ajili ya kazi ya kuwahudumia wanadamu wanaoteseka. {9T 178.1}

Hebu wahudumu wa tiba Waadventista Wa sabato wakumbuke kwamba Bwana Mungu Mweza yote anatawala. Kristo alikuwa tabibu mkuu aliyepata kukanyaga dunia hii iliyolaaniwa na dhambi. Bwana angetaka watu Wake waje Kwake kwa ajili ya nguvu yao ya uponyaji. Atawabatiza kwa Roho Wake Mtakatifu na kuwafanya kufaa kwa huduma ambayo itakuwa baraka katika kurejesha afya ya kiroho na kimwili ya wale wanaohitaji uponyaji. {9T178.2}

## SEHEMU YA 5—ROHO YA UMOJA

[*Sehemu Za Makala, Shuhuda Maalum, Sehemu B, Namba. 4, Zimejumuishwa Katika Sehemu Hii.*]

"Wote wawe na umoja." Yohana 17:21.

## SURA YA 18
## UMOJA MIONGONI MWA WATU WA MATAIFA TOFAUTI

[*Ujumbe Uliwasilishwa Katika Baraza La Umoja Wa Ulaya, Basel, Switzerland, Septemba 24, 1885.*]

"Mtu akiona kiu, na aje Kwangu, anywe." “Walakini yeyote atakayekunywa maji yale nitakayompa Mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji yakibubujika uzima wa milele." Yohana 7:37; 4:14. {9T 179.1}

Ikiwa, kwa ahadi hizi zilizo mbele yetu, tunachagua kubaki tukiwa tumekauka na kunyauka kwa kukosa maji ya uzima, ni makosa yetu wenyewe. Ikiwa tungekuja kwa Kristo na unyenyekevu wa mtoto anayekuja kwa wazazi wake wa kiulimwengu, na kuomba mambo ambayo ameahidi, tukiamini kwamba tunayapokea, tungeliyapokea. Kama sisi sote tungekuwa na imani ambayo tungepaswa kuwa nayo tungelibarikiwa zaidi kwa wingi wa Roho wa Mungu katika mikutano yetu kuliko ambavyo tumekwisha pokea. Nina furaha kwamba siku chache za mkutano bado zimebaki. Sasa swali ni: Je, tutakuja kwenye chemchemi na kunywa? Je, walimu wa Ukweli watakuwa mfano? Mungu

atatufanyia mambo makuu ikiwa kwa imani tutamkubali katika Neno Lake. Laiti, kwamba hapa tungeweza kuuona unyenyekevu wa jumla wa moyo mbele za Mungu! {9T 179.2

Tangu mikutano hii ilipoanza, nimehisi kuhimizwa kukaa sana katika upendo na imani. Hii ni kwa sababu mnahitaji ushuhuda huu. Baadhi ya watu ambao wameingia katika nyanja hizi za umishonari wamesema: “Ninyi hamuwaelewi watu wa Ufaransa; hamuwaelewi wajerumani. Wanapaswa kufikiwa kwa njia hiyo." {9T 179.3}

Lakini nauliza: Je! Mungu hawafahamu? Je! si Yeye anaye wapa watu Wake ujumbe kwa ajili ya watu? Anajua kile wanachohitaji; na ikiwa ujumbe unatoka Kwake moja kwa moja kupitia watumishi Wake kwenda kwa watu, utatimiza uliotumwa kwayo; itawafanya wote kuwa wamoja katika Kristo. Ingawa baadhi ni Wafaransa, wengine wa Kijerumani, na wengine wakiamua kuwa Waamerika, watafanyika hivyo kuwa sawa sawa na Kristo. {9T 180.1}

Hekalu la Kiyahudi lilijengwa kwa mawe ya kuchongwa yaliyochongwa kutoka milimani; na kila jiwe lilikuwa lililofaa kwa ajili ya mahali pake katika hekalu, likichongwa, liking'arishwa, na kujaribiwa kabla ya kuletwa Yerusalemu. Na yote walipoletwa chini, jengo lilikua pamoja bila sauti ya shoka au nyundo. Jengo hilo linawakilisha hekalu la kiroho la Mungu, ambalo limefanyizwa kwa nyenzo zilizokusanywa kutoka kwa kila taifa, na lugha, na jamaa, wa matabaka yote, wa juu na wa chini, matajiri na maskini, wasomi na wasio na elimu. Hivi si vitu vilivyokufa vya kutengenezwa kwa nyundo na patasi. Ni mawe yaliyo hai, yaliyochongwa kutoka ulimwenguni kwa Ukweli; na Mjenzi Mkuu, Bwana wa hekalu, sasa anayachonga na kuyang'arisha, na kuwafanya kufaa kwa ajili ya mahali pao katika hekalu la kiroho. Wakati, hekalu hili litakapokamilika litakuwa kamilifu katika sehemu zake zote, wakilishangaa na kulipenda, wote malaika na wanadamu; kwa maana Mjenzi na Muumba Wake ni Mungu. {9T 180.2}

Mtu yeyote asifikirie kwamba hakuna haja ya kupondwa. Hakuna mtu, hakuna taifa, lililo kamilifu katika kila tabia na wazo. Mtu lazima ajifunze kutoka kwa mtu mwingine. Kwa hiyo Mungu anataka mataifa tofauti kuchangamana pamoja, kuwa katika kusudi moja, na katika nia moja. Ndipo umoja uliomo ndani ya Kristo utakuwa umeigwa. {9T 180.3}

Nilikaribia kuogopa kuja katika nchi hii kwa sababu nilisikia wengi wakisema tofauti ya mataifa ya Ulaya, yalikuwa ya kipekee na ilibidi yafikiwe kwa njia maalum. Lakini hekima ya Mungu imeahidiwa kwa wale wanaohisi uhitaji wake na wanaoiomba. Mungu anaweza kuwaleta watu pale wanapoweza kuupokea Ukweli.

Bwana na atawale akili zenu na kuzifinyanga kama udongo unavyofinyangwa mikononi ya mfinyanzi, na tofauti hizi hazitakuwepo. Ndugu, mwangalieni Yesu; nakili tabia na roho Yake, na hutakuwa na shida katika kufikia matabaka haya tofauti. Hatuna vielelezo sita vya kufuata, wala vitano; tunaye Mmoja tu, Naye ni Kristo Yesu. Ikiwa ndugu wa Italia, ndugu wa Kifaransa, na Ndugu Wajerumani wakijaribu kuwa kama Yeye, wataweka miguu yao juu ya msingi uleule wa Ukweli; na Roho Yule Yule akaaye ndani ya mmoja atakaa ndani ya yule mwingine-Kristo ndani yao, tumaini la utukufu. Ninawaonya, ndugu na dada, tusijenge ukuta wa utengano kati ya mataifa mbalimbali. Kinyume chake, tafuteni kuuvunja popote ulipo. Tunapaswa kujitahidi kuleta wote katika upatanifu uliopo katika Yesu, tukifanya kazi kwa ajili ya jambo moja, wokovu wa wenzetu. {9T 181.1}

Je, ndugu watumishi wenzangu, mnazifahamu ahadi nyingi za Mungu? Je, mtaweka ubinafsi mbali na macho yenu na kumwacha Yesu aonekane? Nafsi lazima ife kabla Mungu hajafanya kazi kupitia kwenu. Ninahisi wasiwasi ninapoona kujigawa mmoja hapa na mwingine pale. Ninakuambia, kwa jina la Yesu wa Nazareti, mapenzi yenu lazima yafe; lazima muwe kama mapenzi ya Mungu yalivyo. Anataka kukuyeyusha na kukusafisha na kila unajisi. Kuna kazi kubwa ya kufanywa kwa ajili yako kabla hujajazwa na nguvu za Mungu. Ninakusihi umkaribie Yeye, ili upate kutambua baraka Zake nyingi kabla ya huu mkutano kufungwa. {9T 181.2}

Kuna wale ambao nuru kubwa katika maonyo na makaripio imewamulika. Wakati wowote wapewapo makaripio, adui hutafuta kuunda ndani ya wale waliokemewa shauku ya huruma ya kibinadamu. Kwa hiyo ningependa kukuonya kuwa mwangalifu usije ukavutwa na huruma za wengine na kuyarudia majaribu yako ya zamani, tena ukakosea katika mambo yale yale katika kutafuta kujijenga mwenyewe. Bwana huwaleta watoto Wake wanaokosea katika mambo yale yale tena na tena; lakini wakiendelea kushindwa kuyatii maonyo ya Roho wake, kama watafanya hivyo kushindwa kurekebisha kila mahali ambapo wamekosea, hatimaye atawaacha kwenye udhaifu wao wenyewe. {9T 182.1}

Nawasihi, ndugu, njooni kwa Kristo na kunywa; kunywa bure maji ya wokovu. Usisikilize hisia zako mwenyewe. Usifikiri kwamba hisia (sentimentalism)ni dini. Jitikise kutoka kwa kila kichocheo cha kibinanadamu na mwegemee sana Kristo. Unahitaji uimarishwaji mpya kabla ya kuwa tayari kujihusisha katika kazi ya kuokoa roho. Maneno yako, matendo yako, yana mvuto kwa wengine, na lazima ukutane na ushawishi huo katika siku ya Mungu. Yesu anasema: “Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, wala hakuna mtu awezaye kuufunga.” Ufunuo 3:8. Nuru inamulika kutoka kwenye mlango huo, na ni faida kwetu kuipokea tukipenda. Hebu na tuelekeze macho yetu ndani ya mlango huo

uliofunguliwa na tujaribu kupokea yote ambayo Kristo yuko tayari kutoa. {9T 182.2}

Kila mmoja atakuwa na mapambano ya kushinda dhambi moyoni mwake. Hii wakati mwingine ni kazi chungu sana na kazi ya kukatisha tamaa; kwa sababu, tunapoona mapungufu ya tabia zetu, tunaendelea kuyatazama, wakati tunapaswa kumwangalia Yesu na kuvaa vazi la haki Yake. Kila aingiaye katika malango ya lulu ya mji wa Mungu ataingia humo kama mshindi, na ushindi wake mkuu utakuwa ni ushindi wa nafsi yake . {9T 182.3}

“Kwa hiyo nampigia Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti, ambaye kwa jina Lake ubaba wote wa mbinguni na duniani unaitwa,awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, kufanywa imara kwa nguvu,kwa kazi ya Roho Wake katika utu wa ndani; Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani; mkiwa na shina na msingi katika upendo, ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana; na urefu, na kina, na kimo; na kuujua upendo Wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi,mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu." Waefeso 3:14-19. {9T 183.1}

Kama watenda kazi pamoja kwa ajili ya Mungu, ndugu na dada, egemeeni sana kwenye mkono wa Mwenyezi. Fanyeni kazi kwa umoja, fanyeni kazi kwa upendo, nanyi mtakuwa nguvu ulimwenguni. {9T 183.2}

## SURA YA 19
## UMOJA KATIKA YESU KRISTO

Loma Linda, California, Agosti 24, 1905.

Kwa Ndugu zetu walioshikamana na kazi ya uchapaji Chuo cha College View—

Wakati nilipohudhuria baraza la kamati ya mkutano wa Konferensi kuu (General Conference) uliofanyika mwezi Septemba, 1904, fikra zangu zilizama ndani kufanyia kazi kuhusiana na umoja utakao kuwepo kwa kazi yetu. Sikuweza kuhudhuria mikutano, lakini wakati wa majira ya usiku tukio baada ya tukio yalipita mbele yangu, na nilihisi kuwa nilikuwa na ujumbe wa kupeleka kwa watu wetu katika sehemu nyingi. {9T 184.1}

Moyo wangu uliumia kila ninapoona kwamba, tuna motisha wa ajabu wa kuleta nguvu zetu na uwezo wetu kwenye kiwango cha juu cha hali ya maendeleo, tumeweza kuridhika tu kuwa mbilikimo kwa kazi ya Kristo. Mungu anatamani watendakazi Wake wote wakue katika kimo halisi cha wanaume na wanawake katika Kristo. Mahala palipo na Uhai, huwa ukuaji; ukuaji unadhihirisha Uhai. Maneno na matendo yanaakisi ushuhuda unaoishi kwa ulimwengu ambao ukristo

unatenda kwa wafuasi wa Kristo. {9T 184.2} Unapokuwa unafanya kazi yako uliyoteuliwa kwayo bila ubishi na kukosoa wengine, uhuru, vuru, na nguvu vitakuwepo na kutoa tabia na ushawishi kwa taasisi na mashirika ambayo umeshikamana nayo. {9T 184.3}

Kumbuka kwamba wewe kamwe hauko katika nafasi nzuri wakati unapotikiswa na wakati unapoubeba mzigo wa kusahihisha kila nafsi inayokukaribia. Ukikubali kujaribiwa kuwakosoa wengine, kuonesha makosa yao, na kubomoa wanachokifanya, unaweza kuwa na uhakika kwamba utashindwa kufanya sehemu yako kwa usahihi na vema. {9T 184.4}

Huu ni wakati ambapo kila mtu katika nafasi ya uwajibikaji, na kila mshiriki wa kanisa, anapaswa kuleta kila kipengele cha kazi yake katika upatanifu wa karibu na mafundisho ya Neno la Mungu. Kwa kukesha, kwa maombi ya bidii, kwa maneno na matendo kama ya Kristo, tunapaswa kuuonyesha ulimwengu kile ambacho Mungu anatamani Kanisa lake liwe. {9T 185.1}

Kutoka katika cheo Chake cha juu, Kristo, Mfalme wa utukufu, Mkuu wa mbinguni, aliiona hali ya wanadamu. Aliwasikitikia wanadamu katika udhaifu na dhambi zao, na akaja hapa duniani kudhihirisha vile Mungu alivyo kwa mwanadamu. Akiziacha nyua za kifalme, na kuuvisha Uungu Wake kwa ubinadamu, alikuja ulimwenguni Mwenyewe, katika niaba yetu kuionesha tabia kamilifu. Hakuchagua makao Yake miongoni mwa matajiri wa dunia. Alizaliwa katika umaskini, katika malezi na wazazi wa hali ya chini, na aliishi katika kijiji kilichodharauliwa cha Nazareti. Mara tu alipokuwa mtu mzima vya kutosha kubeba zana za kazi, aliushiriki mzigo wa kutunza familia. {9T 185.2}

Kristo alijinyenyekeza kusimama juu ya ubinadamu, ili kukabiliana na majaribu na kustahimili majaribu ambayo ubinadamu lazima ukutane nayo na kuyastahimili. Lazima ajue kile ambacho ubinadamu unapaswa kukutana nacho kutoka kwa adui aliyeanguka, ili apate kujua jinsi ya kuwasaidia wale wanaojaribiwa. {9T 185.3}

Na Kristo amefanywa kuwa hakimu wetu. Baba sio hakimu. Malaika sio mahakimu. YEYE aliyeuchukua ubinadamu, na katika ulimwengu huu akaishi maisha makamilifu, Ndiye wa kutuhukumu. Yeye pekee ndiye awezaye kuwa Hakimu wetu. Je, ndugu, mtalikumbuka hili? Je, watumishi, mtalikumbuka? Je, akina baba na akina mama mtalikumbuka? Kristo aliuchukua ubinadamu ili Yeye awe mhukumu/jaji wetu. Hakuna hata mmoja wenu aliyeteuliwa kuwa mhukumu wa wengine. Ni yote mnayoweza kufanya ili kujitia adabu. Ninawasihi katika jina la Kristo, shikeni amri kwamba Yeye hajawapa kamwe kujiweka wenyewe kwenye kiti cha hukumu. Siku hadi siku ujumbe huu umekuwa ukasikika masikioni mwangu: "Shukeni kutoka kwenye kiti cha hukumu. Shukeni katika unyenyekevu." {9T 185.4}

Hakujawahi kuwa na wakati ambapo ni muhimu zaidi kujikana nafsi na kuuchukua msalaba kila siku kuliko sasa. Je, ni kwa kiasi gani tuko tayari kuonesha kujikana

nafsi? {9T 186.1}

## Maisha ya Neema na Amani

Katika sura ya kwanza ya waraka wa pili wa Petro mtapata ahadi ya kwamba neema na amani zitazidishwa kwenu, kama mtaongeza “katika Imani yenu wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu, kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa; na utauwa wenu upendano wa ndugu; na katika upendano wa ndugu upendo.” 2 Petro 1:5-7. Fadhila hizi ni hazina za ajabu. Humfanya " mwanadamu kuwa wa thamani kuliko dhahabu safi; na, watu kuliko dhahabu ya Ofiri." Isaya 13:12. {9T 186.2}

“Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu, wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo." 2 Petro 1:8. {9T 186.3}

Je, hatutajitahidi kutumia kwa kadiri ya uwezo wetu muda mchache uliobaki kwetu katika maisha haya, na kuongeza neema kwa neema, uwezo kwa uwezo, tukidhihirisha kwamba tuna chemchemi ya nguvu juu mbinguni? Kristo anasema: "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani." Mathayo 28:18. Huu ni uwezo aliopewa? Kwa ajili yetu. Anatamani tutambue kwamba amerudi mbinguni akiwa Kaka Yetu Mkubwa na kwamba uwezo usio na kipimo aliopewa umewekwa kwetu. {9T 186.4}

Wale ambao watatekeleza katika maisha yao maagizo walilopewa kanisa kupitia mtume Petro watapokea nguvu kutoka juu. Tunapaswa kuishi juu ya mpango wa kuongeza, tukifanya bidii yote kuuhakikisha wito na kuchaguliwa kwetu. Tunapaswa kumwakilisha Kristo ndani ya yote tunayosema na kuyafanya. Tunapaswa kuyaishi maisha Yake. Kanuni ambazo Yeye aliongozwa nazo zinapaswa kuunda mienendo yetu kwa wale tunaohusiana nao. {9T 186.5}

Tunapowekwa salama ndani ya Kristo, tunakuwa na uwezo ambao hakuna mwanadamu anayeweza kutunyang'anya. Kwa nini hii? Kwa sababu sisi ni washirika wa tabia ya Uungu, tukiokolewa dhidi uharibifu ulioko ulimwenguni utokanao na tamaa, washirika wa asili Yake Yeye aliyekuja hapa duniani akiwa amevikwa tabia ya ubinadamu, ili Yeye asimame juu ya ubinadamu na kukuza tabia ambayo haina doa wala waa la dhambi. {9T 187.1}

Kwa nini wengi wetu ni dhaifu na hatufai? Ni kwa sababu tunaitazama nafsi, tukijifunza tabia zetu wenyewe na kushangaa jinsi tunavyoweza kutengeneza mahali kwa ajili yetu, utu wetu na upekee wetu, badala ya kujifunza kwa Kristo na tabia Yake. {9T 187.2}

Ndugu ambao wangeweza kufanya kazi pamoja kwa upatanifu ikiwa wangejifunza juu ya Kristo, na kusahau kwamba wao ni Wamarekani au wa Ulaya, Wajerumani au Wafaransa, Wasweden, Wadenmark, au Wanorwei, wanaonekana kuhisi kwamba ikiwa wanapaswa kuchanganyikana na watu wa mataifa mengine,

kitu ambacho ni cha upekee kwa nchi na taifa lao kingepotea na kitu kingine kingechukua nafasi yake. {9T 187.3}

Ndugu zangu, haya yote tuyaweke kando. Hatuna haki ya kuweka mawazo yetu juu yetu wenyewe, yetu tuyapendayo, na matamanio yetu. Hatupaswi kutafuta kudumisha utambulisho wetu wa pekee, au utu, na umimi, ambao utatutenganisha na wetendakazi wenzetu. Tunayo tabia ya kudumisha, ambayo ni tabia ya Kristo. Tukiwa na tabia ya Kristo, tunaweza kuiendeleza kazi ya Mungu pamoja. Kristo ndani yetu atakutana na Kristo ndani ya ndugu zetu, na Roho Mtakatifu atatoa muunganiko huo wa moyo na matendo ambao utadhihirisha kwa ulimwengu kwamba sisi ni watoto wa Mungu. Bwana na atusaidie ili tufe katika ubinafsi wetu na tuzaliwe upya, ili Kristo apate kuishi ndani yetu, kanuni hai, itendayo kazi, nguvu ambayo itatuweka kuwa watakatifu. - {9T 187.4}

Jitahidini sana kuwa wamoja. Uombeeni, na kuutenda. Italeta afya ya kiroho, kuyainuaa mawazo, tabia yenye heshima, nia ya mbinguni, ya kukuwezesha kushinda ubinafsi na dhana mbaya, na kuwa zaidi ya washindi katika Yeye aliyewapenda ninyi na kujitoa kwa ajili yenu. Jisulubishe nafsi; wathaminini wengine kuliko nafsi zenu. Hivyo mtaletwa katika umoja na Kristo. Mbele ya ulimwengu wa kimbingu, na mbele ya kanisa na ulimwengu, mtakuwa na ushahidi usio na shaka kwamba ninyi ni wana na binti za Mungu. Mungu atatukuzwa kwa kielelezo mnaachokiweka. {9T 188.1}

Ulimwengu unahitaji kuona muujiza unaofunga mioyo ya watu wa Mungu pamoja katika upendo wa Kikristo ukitendeka mbele yao. Unahitaji kuona watu wa Bwana wameketi pamoja katika ulimwengu wa roho ndani ya Kristo. Je, hamtatoa katika maisha yenu uthibitisho wa kile ambacho Kweli ya Mungu inaweza kufanya kwa wale wanaompenda na kumtumikia? Mungu anajua mnachoweza kuwa. Anajua neema ya Mungu inaweza kuwafanyia nini ikiwa mtakuwa washirika asili ya Uungu. {9T 188.2}

## SURA YA 20
## KAZI YA UCHAPISHAJI KATIKA CHUO CHA COLLEGE VIEW,

Loma Linda, California, Agosti 24, 1905.

Ninaidhinisha juhudi ambazo zimefanywa kuanzisha kazi yetu ya uchapishaji Ujerumani na Skandinavia katika College View. Natumaini kwamba mipango itaundwa kwa ajili ya kutia moyo na kuiimarisha kazi hii. {9T 189.1}

Mzigo mzima wa kazi haupaswi kuachwa kwa ndugu zetu wa kigeni. Wala hawapaswi ndugu zetu katika eneo lote kuuacha mzigo mzito kwenye Jimbo lililo karibu na College View. Washiriki katika Konferensi hizi wanapaswa kuongoza na kufanya kwa ubora wao, na wote wanapaswa kuja kwa kwa ajili ya usaidizi wao. Ukweli unapaswa kuhubiriwa kwa mataifa yote na kabila na lugha na jamaa. {9T 189.2}

Ndugu zetu Wajerumani, Wadenmarki na Waswideni hawana sababu nzuri ya kutoweza kuingiza maelewano katika kazi ya uchapishaji. Wale wanaouamini Ukweli wanapaswa kukumbuka kwamba wao ni Watoto wadogo wa Mungu, na

kwamba wako chini ya mafunzo Yake. Hebu na wamshukuru Mungu kwa rehema Zake nyingi na wawe wema kwa kila mmoja kwa mwenzake. Wana Mungu mmoja na Mwokozi mmoja; na Roho mmoja—Roho wa Kristo—anapaswa kuleta umoja katika tofauti zao. {9T 189.3}

Baada ya kufufuka Kwake, Kristo alipaa mbinguni, na sasa anawasilisha mahitaji yetu kwa Baba. “Nimekuchora kwenye vitanga vya mikono Yangu,” Anasema. Isaya 49:16. Iligharimu kitu kuwachora wao huko. Iligharimu uchungu usioelezeka. Ikiwa tungejinyenyekeza mbele ya Mungu, na kuwa wema na adabu na wenye moyo mwororo na wenye kuhurumiana, kungekuwa na uongofu wa mamia kwa ajili ya Ukweli ambao sasa ni mmoja tu. Lakini, ingawa tunadai kuwa tumeongoka, tunabeba pamoja nasi rundo la ubinafsi ambalo linachukuliwa kuwa la thamani sana kuachwa. Ni upendeleo kwetu kuuweka mzigo huu miguuni pa Kristo na mahali pake kuchukua tabia na mfano wa Kristo. Mwokozi anatungoja sisi kufanya hivi. {9T 189.4}

Kristo aliliweka kando vazi Lake la kifalme, taji Yake ya kifalme, na mamlaka yake kuu, akashuka chini, chini, chini hadi vilindi vya chini kabisa vya unyonge. Akiwa ameibeba asili ya mwanadamu, alikutana na majaribu yote ya ubinadamu na kwa niaba yetu kumshinda adui kwa kila nukta. {9T 190.1}

Haya yote aliyafanya ili apate kuwaletea watu uwezo wa kuwa washindi. "Nimepewa mamlaka yote," anasema. Mathayo 28:18. Na haya huwapa wote wanaomfuata. Wanaweza kuudhihirishia ulimwengu uwezo uliopo katika dini ya Kristo kwa ajili ya kuishindia nafsi. {9T 190.2}

"Jifunzeni kwangu," Kristo asema, "nanyi mtapata raha nafsini mwenu." Mathayo 11:29. Kwa nini hatujifunzi juu ya Mwokozi kila siku? Kwa nini sisi hatuishi daima katika ushirika na Yeye, ili katika ushirikika wetu tuweze kusema na kutenda kwa upole na adabu? Kwa nini hatumtukuzi Bwana kwa kudhihirisha huruma na upendo kwa mtu na mwenzake? Ikiwa tunazungumza na kutenda kulingana na kanuni za mbinguni, wasioamini watavutwa kwa Kristo kwa ushirika wao nasi. {9T 190.3}

## Uhusiano wa Kristo na Utaifa

Kristo hakutambua tofauti ya utaifa au cheo au imani. Waandishi na Mafarisayo walitamani kujinufaisha wao na taifa lao karama zote za mbinguni na kuwatenga wengine walio familia ya Mungu duniani. Lakini Kristo alikuja kubomoa kila ukuta wa utengano. Alikuja kuonyesha kwamba karama Yake ya rehema na upendo haufungiki kama vile hewa, mwanga, au manyunyu ya mvua yanayoburudisha nchi. {9T 190.4}

Maisha ya Kristo yalianzisha dini ambayo ndani yake hakuna tabaka, dini ambayo

kwayo Myahudi na Myunani, walio huru na wafungwa, wameunganishwa katika udugu wa pamoja, sawa mbele za Mungu. Hakuna suala la sera lililosukuma mienendo yake. Hakufanya tofauti kati ya majirani na wageni, marafiki na maadui. Kile ambacho kiliuvutia moyo Wake kilikuwa ni nafsi yenye kiu ya maji ya uzima. {9T 191.1}

Hakumpita mwanadamu yeyote kama asiyefaa kitu, bali alitafuta kutumia dawa ya uponyaji kwa kila nafsi. Katika kundi lolote alimokuwa, alitoa somo linalolingana na wakati na mazingira. Kila kupuuza au matusi yaliyoonyeshwa na wanadamu kwa wanadamu wenzao yalimfanya kunia zaidi mahitaji yao ya huruma Yake ya Uungu wa kibinadamu. Alitafuta kuwahuisha kwa tumaini walio wabaya zaidi na walioachwa, akiweka mbele yao uhakikisho wa kuwa wanaweza kuwa wakamilifu na wasio na hatia; kuipata tabia ambayo ingewafanya kuwa watoto wa Mungu. {9T 191.2}

## Msingi wa Uhakika

“Kwa hiyo ndugu,” asema mtume Petro, “jitahidini Zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu, maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. Maana hivi, mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia kwa wingi katika ufalme wa milele wa Bwana na wetu , Mwokozi wetu Yesu Kristo.” 2 Petro 1:10, 11. {9T. 191.3}

Miaka mingi iliyopita, wakati kundi la waaminio katika upesi wa ujio wa Kristo lilipokuwa dogo sana, Washika Sabato huko Topsham, Maine, walikutana kwa ajili ya ibada jiko kubwa katika nyumba ya Ndugu Stockbridge Howland. Asubuhi moja ya Sabato Ndugu Howland hakuwepo. Tulishangazwa na hili, kwa sababu alikuwa imara kila wakati. Mara akaingia, uso wake ukiwa umewaka, uking'aa kwa utukufu wa Mungu. "Ndugu," alisema, "nimeipata. Nimepata kwamba tunaweza kuifuata njia ambayo ina uhakikisho wa Neno la Mungu: nayo ni: 'Hamtaanguka kamwe.' Nitawaambia juu yake." {9T 191.4}

Kisha akatuambia kwamba alikuwa ameona kwamba ndugu mmoja, mvuvi maskini, amekuwa akihisi kwamba hakuwa akiheshimiwa sana kama inavyopaswa kuheshimiwa na kwamba Ndugu Howland na wengine walikuwa wakififikiri wapo juu yake. Hii haikuwa kweli, lakini ilionekana kuwa kweli kwake; na kwa wiki kadhaa hakuwa amehudhuria mikutano. Kwa hiyo Ndugu Howland akaenda nyumbani kwake na kupiga magoti mbele yake, akisema: “Ndugu yangu, nisamehe. Ni nini nimefanya?" Mtu huyo alimshika mkono na kujaribu kumwinua na kusimsimamisha. "Hapana," alisema Ndugu Howland, "una nini dhidi yangu?" "Sina chochote dhidi yako." "Lakini lazima uwe nacho," alisema Ndugu Howland, “kwa sababu mwanzo tuliweza kuzungumza sisi kwa sisi, lakini sasa husemi nami hata kidogo na ninataka kujua kuna jambo gani." {9T 192.1}

“Amka, Ndugu Howland,” alisema. "Hapana," alisema Ndugu Howland, "sitaamka."

"Basi lazima nishuke," akasema, akapiga magoti, akakiri jinsi alivyokuwa na utoto na dhana nyingi ovu alizokuwa akizionyesha. "Na sasa," alisema, "nitayaweka yote mbali." {9T 192.2}

Ndugu Howland alipokuwa akisimulia habari hii, uso wake uling'aa kwa utukufu wa Bwana. Alipomaliza tu, mvuvi na familia yake waliingia, na tulikuwa na mkutano mzuri sana. {9T 192.3}

Tuseme kwamba baadhi yetu tunapaswa kufuata namna ilioyofuatwa na Ndugu Howland. Ikiwa ndugu zetu watayadhania maovu, tungewaendea tukisema:" Nisameheni ikiwa nimefanya lolote kukudhuru" tungevunja hila za Shetani na kuwaweka ndugu zetu huru kutokana na majaribu yao. Usiruhusu kitu chochote kuingilia kati yako na ndugu zako. Ikiwa kuna kitu chochote ambacho unaweza kujitoa sadaka ili kuondoa takataka za tuhuma, fanya hivyo. Mungu anataka tupendane sisi kwa sisi kama ndugu. Yeye anataka tuwe na huruma. sikitiko na adabu. Anataka tujielimishe kuamini kwamba ndugu zetu wanatupenda sisi, na kuamini kwamba Kristo anatupenda. Upendo huzaa upendo. {9T 192.4}

Je, tunatarajia kukutana na ndugu zetu mbinguni? Ikiwa tunaweza kuishi nao hapa kwa amani na maelewano tungeweza kuishi nao huko. Lakini tunawezaje kuishi nao mbinguni ikiwa hatuwezi kuishi nao hapa bila ugomvi na mafarakano kuendelea? Wale wanaofuata mkondo huo unaowatenganisha na ndugu zao na kuleta mifarakano na magomvi, wanahitaji uongofu kamili. Mioyo yetu lazima iyeyushwe na kutiishwa na upendo wa Kristo. Ni lazima tuthamini upendo aliooonesha kwa kutufia msalabani Kalvari. Tunahitaji kumkaribia Zaidi na zaidi Mwokozi. Tunapaswa sana kuwa katika sala, na ni lazima tujifunze kuitumia imani. Lazima tuwe mioyo miororo zaidi, wenye huruma zaidi na mwenye adabu. Tutapita katika dunia hii lakini mara moja tu. Je, hatujitahidi kuwaachia wale tunaochangamana nao msukumo wa tabia ya Kristo? {9T 193.1}

Mioyo yetu migumu inahitaji kuvunjwa. Tunahitaji kuja pamoja katika umoja kamili, na tunahitaji kutambua kwamba tumenunuliwa kwa damu ya Yesu Kristo wa Nazareti. Kila mmoja aseme: “Aliutoa uzima Wake kwangu, na ananitaka, ninapopita katika ulimwengu huu, niudhihirishe upendo alioufunua katika kujitoa Kwake kwa ajili yangu.” Kristo alibeba dhambi zetu katika mwili wake msalabani, ili Mungu awe Mwenye haki na bado ni Mwenye haki mwenye kuwahesabia haki wale wanaomwamini. Kuna uzima, uzima wa milele, kwa wote ambao watajisalimisha kwa Kristo. {9T 193.2}

Nataka kumuona Mfalme katika uzuri Wake. Nataka kuutazama uzuri Wake usio na kifani. Ninataka nanyi mumtazame pia. Kristo atawaongoza waliokombolewa kando ya mto waa uzima na atawaelezea yale yote yaliyokuwa yanawatatanisha katika ulimwengu huu. Siri za neema zitafichuka mbele yao. Pale akili zao zenye kikomo zilipotambua kuchanganyikiwa tu na makusudi yaliyovunjika, wataona

upatanifu kamili na mzuri. {9T 193.3}

Tumtumikie Mungu kwa uwezo wetu wote, na kwa akili zetu zote. Akili zetu zitaongezeka kama tutatumia kile tulichonacho. Uzoefu wetu wa kidini utaimarika tunapouleta kila siku katika maisha. Kwa hivyo tutapanda mzunguko baada ya mzunguko kwa ngazi kufikia mbinguni, hadi mwishowe tutakapotoka kutokea juu kabisa kuingia katika ufalme wa Mungu. Hebu tuwe Wakristo katika ulimwengu huu. Kisha tutakuwa na uzima wa milele katika ufalme wa utukufu. - {9T 194.1}

Umoja uliopo kati ya wafuasi wa Kristo ni uthibitisho kwamba Baba amemtuma Mwanawe kuwaokoa wenye dhambi. Ni ushahidi wa uwezo Wake; kwa maana hakuna chochote zaidi ya uwezo wa muujiza wa Mungu kinachoweza kuwaleta wanadamu viumbe wenye tabia zao tofauti pamoja katika tendo lenye upatano, lengo lao moja likiwa ni kusema Ukweli katika upendo. {9T 194.2}

Maonyo na mashauri ya Mungu yako wazi na imara. Tunaposoma Maandiko na kuona nguvu Zake za wema zilipo katika umoja na nguvu ya uovu ambayo iko katika mgawanyiko, tunawezaje kushindwa kulipokea Neno la Mungu ndani ya mioyo yetu? Tuhuma na kutoaminiana ni kama chachu mbaya. Umoja unashuhudia nguvu ya Ukweli. {9T 194.3}

## SURA YA 21
## KONFERENSI ZA UJERUMANI NA SCANDINAVIA

Loma Linda, California, Septemba 1, 1905.

Ndugu mpendwa: Baadhi ya watumishi wetu wameniandikia, wakiuliza ikiwa kazi miongoni mwa Wajerumani na waskandinavia haipaswi kupelekwa mbele chini ya miundo tofauti. Jambo hili limeoneshwa kwangu mara kadhaa. Nilipokuwa College View, Bwana alinipa ushuhuda wa moja kwa moja kuubeba, na tangu wakati huo jambo hilo limewasilishwa kwangu tena. {9T 195.1}

Wakati fulani nilionekana kuwa katika kikao cha baraza ambapo mambo haya yalikuwa yakizingatiwa. Moja ya mamlaka ilisimama katikati ya wale waliokusanyika na kufungua mbele yao kanuni zinazopaswa kufuatiwa katika kazi ya Mungu. Maagizo yaliyotolewa ni kwamba ikiwa utengano huo ungetokea, itakuwa si mwelekeo wa kuendeleza maslahi ya kazi kati ya mataifa mbalimbali.

Haingesababisha maendeleo ya juu zaidi ya kiroho. Kuta zingejengwa ambazo zingelazimika kuondolewa muda si mrefu baadaye. {9T 195.2}

Kulingana na nuru niliyopewa na Mungu, asasi tofauti, badala ya kuleta umoja, itajenga mafarakano. Ikiwa ndugu zetu watamtafuta Bwana pamoja kwa unyenyekevu wa akili, wale wanaofikiri sasa kuna umuhimu wa kuunda majimbo tofauti ya Ujerumani na Skandinavia wataona kwamba Bwana anatamani wafanye kazi pamoja kama ndugu. {9T 195.3}

Kwa wale wanaotaka kuisambaratisha kazi ya Mungu, ili kutimiza kusudi lao, wengine wangefanya kujikutuza kufanya kazi isiyopaswa kufanywa. Mpangilio kama huo ungecheleweshwa sana kusudi la Mungu. Ikiwa tunataka kuiendeleza kazi kwa mafanikio zaidi, karama zinazopatikana miongoni mwa Waingereza na Wamarekani zinapaswa kuunganishwa na talanta za mataifa mengine. Na kila taifa linapaswa kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya taifa lingine. Kuna Bwana Mmoja tu, na imani moja. Juhudi zetu zinapaswa kuwa kujibu maombi ya Kristo kwa wanafunzi wake, ili wawe na umoja. {9T 195.4}

Uwatakase kwa ile Kweli; Neno lako ndiyo Kweli, Kama ulivyonituma Mimi ulimwenguni, Nami vivyo hivyo, naliwatuma hao ulimwenguni. Na kwa ajili yao najiweka wakfu Mwenyewe, ili na hao watakaswe katika Kweli. {9T 196.1}

“Wala si hao tu ninaowaombea, lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya Neno lao.Wote wawe na umoja; kama Wewe, Baba, ulivyo ndani Yangu, Nami ndani yako, hao nao wawe ndani Yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba Ndiwe uliyenituma." Yohana 17:17-21. {9T 196.2}

Inapaswa kueleweka kwamba umoja kamili kati ya watenda kazi ni muhimu kwa mafanikio kamili ya kazi ya Mungu. Ili kulinda amani, ni lazima wote watafute hekima kutoka kwa Mwalimu Mkuu. Hebu wote wawe waangalifu jinsi wanavyoanzisha mapendekezo kabambe ya matamanio ambayo yataleta mafarakano. {9T 196.3}

Tunapaswa kujielekeza mmoja kwa mwezake. Hakuna mtu, ndani yake mwenyewe, aliye kamili. Kwa usalimishaji wa akili na mapenzi kwa Roho Mtakatifu tutakuwa wanafunzi wa Mwalimu Mkuu sikuzote. {9T 196.4}

Jifunze sura ya pili ya Matendo Ya Mitume. Katika kanisa la kwanza Roho wa Mungu alitenda kazi kwa nguvu kwa wale ambao walikuwa wameunganishwa katika umoja. Siku ya Pentekoste walikuwa wote na nia moja mahali pamoja. {9T 196.5}

Tunapaswa kuudhihirishia ulimwengu kwamba watu wa kila taifa ni wamoja katika Kristo Yesu. Kisha na tuondoe kila kizuizi na kuja katika umoja katika utumishi wa Bwana. {9T 196.6}

Katika uwekaji wa vizuizi vya kitaifa unawasilisha kwa ulimwengu mpango wa uvumbuzi wa wanadamu ambao Mungu anaweza asiudhinishe kamwe. Kwa wale ambao wangefanya hivyo, mtume Paulo asema hivi: “hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana ikiwa kuna kuna husuda na fitina, Je, si watu wa tabia ya mwilini ninyi? … Basi Paulo ni nani, na Apolo ni nani, Ni wahudumu ambao kwao mliamini, na kila mtu kama Bwana alivyompa. Mimi nilipanda, Apolo akatia maji; bali mwenye kukuza ni Mungu. Hivyo apandaye si kitu, wala yeye atiaye maji, bali Mungu akuzaye. Basi yeye apandaye na yeye atiaye maji ni wamoja: lakini kila mtu atapata thawabu yake mwenyewe sawasawa na taabu yake mwenyewe. Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu: ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu." 1 Wakorintho 3:3-9. {9T 197.1}

## Mfano Wa Ukarimu Wa Kindugu

Wakati ndugu zetu katika Skandinavia walipokabiliana na changamoto ya kifedha, ushuhuda ulitolewa kwamba hatupaswi kufanya hivyo kuwaruhusu ndugu zetu kusimama kama waliofilisika mbele ya ulimwengu. Hilo lingekuwa ni kumvunjia Mungu utukufu. Na hatua ya haraka na thabiti ya ndugu zetu wa Marekani ilikuwa ni kukiri kwamba tofauti hiyo katika utaifa haikuweza kuwafungia kutoka katika wajibu wao wa kusaidiana katika kazi ya Mungu. "Nyinyi nyote ni ndugu." Mathayo 23:8. Sisi tu wamoja katika umoja wa Kweli. {9T 197.2}
Inatupasa sasa, kwa bidii, juhudi za kujitolea, kujitahidi kutembea katika upendo wa Kristo, katika umoja wa Roho kwa utakaso wa Kweli. Hakuna kazi nusu itatosha kutimiza uwakilishi uliotolewa katika maombi ya Kristo. Tunapaswa kufanya mazoezi ya kanuni za mbinguni hapa chini. Mbinguni kuna pahali pamoja pazuri pa kukutania. {9T 197.3}

Lazima niandike kwa uwazi kuhusu ujenzi wa kuta za utengano katika kazi ya Mungu. Kitendo kama hicho kimefunuliwa kwangu kama uvumbuzi wa uwongo wa mwanadamu. Si mpango wa Bwana kwa watu Wake kujitenga katika makundi tofauti kwa sababu ya tofauti za utaifa na lugha. Wangefanya hivi, mawazo yao yangekuwa finyu, na ushawishi wao ungepungua sana. Mungu anatoa wito wa kuchanganya aina mbalimbali za talanta. {9T 197.4}

Nayarudia tena maneno ya Kristo. Ningeyaweka kwa undani katika akili zenu. "Wala siwaombei hawa peke yao, bali na wale watakaoniamini kwa sababu ya Neno lao; ili wote wawe na umoja; kama Wewe, Baba, ulivyo ndani Yangu, Nami

ndani Yako, hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki. ya kwamba Wewe Ndiye uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja, kama vile Sisi tulivyo na umoja: Mimi ndani yao, nawe ndani Yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; na kwamba ulimwengu upate kujua ya kuwa Ndiwe uliyenituma, na kuwapenda wao kama ulivyonipenda Mimi." {9T 198.1}

Kristo amewatenga watu Wake kutoka ulimwenguni, lakini wale ambao watajenga utengano wa kitaifa, watafanya kazi ambayo Bwana Yesu Kristo hajawatia moyo kwayo. {9T 198.2}

Ndugu, unganeni; sogeleaneni karibu pamoja, mkiweka kando kila uvumbuzi wa mwanadamu na kuzifuata kwa karibu nyayo za Yesu, Mfano wenu mkuu. {9T 198.3}

# SEHEMU YA 6—MIONGONI MWA WATU WEUSI (WASIO WAZUNGU)

“Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno Yake.” Mathayo 9:38.

## SURA YA 22
## WITO KWA WATENDAKAZI WEUSI

Juhudi nyingi madhubuti zifanywe kuwaelimisha na kuwafunza wanaume na wanawake weusi kufanya kazi kama wamishionari katika Majimbo ya Kusini mwa Amerika. Wanafunzi weusi wa Kikristo wanapaswa kujiandaa kutoa ukweli kwa watu wa rangi yao. Wale wanaofanya kumcha Bwana kuwa mwanzo wa hekima yao na kuzingatia ushauri wa watu wenye uzoefu wanaweza kuwa mbaraka mkubwa kwa jamii ya Weusi kwa kupeleka kwa watu wao nuru ya Ukweli wa sasa. Kila mfanyakazi akifanya kazi kwa unyenyekevu na kupatana na ndugu zake atakuwa njia ya mwanga kwa wengi ambao sasa wako katika giza la ujinga na ushirikina. {9T 199.1}

Badala ya kujiuliza kama hawafai kufanya kazi kwa ajili ya watu weupe, waache

ndugu na kina dada weusi wajitoe wenyewe kwa kazi ya umishionari miongoni mwa watu weusi. Kuna wingi wa fursa kwa wanaume na wanawake weusi wenye akili kufanya kazi kwa ajili ya watu wao wenyewe. Kazi kubwa bado haijafanyika katika eneo la Kusini. Juhudi maalum zinapaswa kufanywa katika miji mikubwa. Katika kila moja ya miji hii huko kuna maelfu ya watu weusi, ambao ujumbe wa mwisho wa onyo la rehema lazima utolewe kwao. Hebu roho ya umishionari iamshwe katika mioyo ya washiriki wa makanisa yetu ya watu weusi. Hebu kazi ifanyike kwa bidii kwa wale wasioujua Ukweli. {9T 199.2}

Kwa kila kaka na dada mweusi ningesema: Angalia hali jinsi ilivyo. Jiulize: "Kwa kuzingatia fursa na faida nilizopewa, je, nina deni gani kwa Bwana wangu? Ninawezaje kumtukuza vyema na kuhamasisha nia za watu wangu? Ninawezaje kuutumia kwa ubora ujuzi niliojaaliwa na Mungu? Je, siwezi kuifungua Biblia yangu na kuwafundisha watu wangu Ukweli? Hawapo maelfu wanaoangamia kwa kukosa maarifa, ambao ninaweza kuwasaidia ikiwa nitajisalimisha kwa Mungu ili aweze kunitumia kama chombo Chake? Je! sina kazi ya kuwafanyia wenzangu walioonewa, na waliokata tamaa?" {9T 200.1}

Eneo la Kusini linateseka kwa watendakazi. Je, utawapita watu wako, bila kufanya jitihada yoyote kuwasaidia wao, au utafanya kazi kwa moyo mnyenyekevu kuwaokoa wanaoangamia? Kuna kazi unayoweza kufanya ukijinyenyekeza mbele za Mungu. Kwa kumtumaini Yeye, utapata amani na faraja, lakini ukifuata njia yako mwenyewe na mapenzi yako mwenyewe, utapata miiba na michongoma, na hutapata thawabu. {9T 200.2}

Muda ni mfupi, na unachopaswa kufanya lazima kifanyike haraka. Azimia kuukomboa wakati. Usiitafute furaha yako mwenyewe. Amka mwenyewe! Shikilia kazi kwa nia mpya ya moyo. Bwana ataifungua njia mbele yako. Fanya kila juhudi uwezavyo kufanya kazi katika njia na safu ya Kristo, kwa upole na unyenyekevu, ukimtegemea Yeye kwa ajili ya nguvu. Elewa kazi ambayo Bwana anakupa kufanya, na, ukimtumaini Mungu, atakuwezeshwa kuendelea kutoka nguvu hadi nguvu, kutoka neema hadi neema. Utawezeshwa kufanya kazi kwa bidii,kwa subira kwa watu wako maadamu mchana ungalipo kwa maana usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi. {9T 200.3}

Kuna hitaji kubwa zaidi la kila aina ya kazi ya umishonari huko Kusini. Bila kuchelewa, wafanyikazi lazima wawekwe tayari kwa ajili ya eneo hili . Watu wetu wanapaswa kutoa fedha kwa ajili ya elimu ya wanaume na wanawake katika majimbo ya Kusini ambao, kwa kuizoea hali ya hewa, wanaweza kufanya kazi huko bila kuhatarisha afya zao. {9T 200.4}

Vijana wa kiume na wa kike wenye haiba na uwezo mzuri wanapaswa kuelimishwa ili wawe walimu. Wanapaswa kuwa wa faida bora sana. Nyumba za shule na za mikutano inapaswa kujengwa katika sehemu tofauti, na walimu waaajiriwe. {9T 201.1}

Wale ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakifanya kazi kusaidia watu weusi wanafaa vyema kutoa shauri kuhusu ufunguliwaji wa shule hizo. Kwa kadri inavyowezekana shule hizi zianzishwe nje ya miji. Lakini mijini kuna watoto wengi ambao hawawezi kuhudhuria shule mbali na miji; na kwa manufaa ya hawa, shule zinapaswa zianzishwe mijini kama ilivyo na mashambani.{9T 201.2}

Watoto na vijana katika shule hizi wanapaswa kufundishwa kitu zaidi ya jinsi ya kusoma tu. Aina ya kazi ya viwandani inapaswa kuendelezwa. Wanafunzi wanapaswa kupewa vifaa kwa ajili ya kujifunza ufundi-stadi utakaowawezesha kujikimu. {9T 201.3}

Makanisa yetu ya Kaskazini, na pia Kusini, yanapaswa kufanya yale yanayoweza kusaidia kazi ya shule kwa watoto weusi. Shule ambazo tayari zimeanzishwa zinapaswa kutunzwa kwa uaminifu. Uanzishwaji wa shule mpya utahitaji fedha za ziada. Hebu ndugu na dada zetu wote wafanye sehemu yao kwa moyo wote kuweka shule hizi kwenye uwanja wa kuvutia. {9T 201.4}

Mbali na kushiriki katika aina hii ya kazi ya shule, ndugu zetu weusi wanaweza kufanya kazi nzuri kwa kuanzisha shule za utume za Jumapili na shule za Sabato miongoni mwa watu wao wenyewe--shule ambamo vijana wanaweza kufundishwa na walimu ambao mioyo yao imejaa upendo kwa nafsi. {9T 201.5}

Fursa zinaendelea kujionyesha katika majimbo ya Kusini, na wengi wenye hekima, wakristo weusi wataitwa kazini. Lakini kwa sababu kadhaa watu weupe lazima wachaguliwe kuwa viongozi. Sisi sote tu viungo vya mwili mmoja na tunakamilika ndani ya Kristo Yesu tu, ambaye atawainua watu Wake kutoka kiwango cha chini ambacho dhambi imewashusha hadhi na atawaweka pale watakapokubaliwa na nyua za mbinguni kama watenda kazi pamoja na Mungu. {9T 202.1}

Kuna kazi ya kufanywa katika sehemu nyingi ngumu, na kutoka katika maeneo haya magumu watendakazi mahiri wanapaswa kuja. Hebu kazi isimamiwe ili watendakazi weusi waelimishwe kufanya kazi kwa ajili ya watu wa rangi yao. Miongoni mwa watu weusi kuna wengi ambao wana talanta na uwezo. Hebu tuwatafute hawa wanaume na wanawake, na kuwafundisha jinsi ya kushiriki katika kazi ya kuokoa roho. Mungu atashirikiana nao na kuwapa ushindi. {9T 202.2}

"Watendakazi Pamoja na Mungu"

Sikio la Bwana li wazi kwa kilio cha wale walio katika huduma Yake. Ameahidi: “Nitakuongoza kwa jicho Langu." Zaburi 32:8. Tembea kwa unyenyekevu na Mungu, na umwombe aifanye kazi yako iwe nyepesi. Anapozungumza na wawakilishi Wake na kuwataka wawe watenda kazi pamoja Naye, watafanya aina ile ile ya kazi ambayo Yesu alitangaza kama kazi Yake aliposimama kusoma katika sinagogi Nazareti. Alikifungua kitabu cha nabii Isaya na kusoma: “Roho ya Bwana Mungu i juu Yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; Amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao.”Isaya 61:1.{9T 202.3}

Ukweli sasa umegubikwa na mawingu ya upotofu unaoshinda ulimwenguni. Anayeweza kushawishi hata walio wa hali ya chini zaidi, na kuwaleta kwa Kristo, anashirikiana na mawakala wa kimbingu katika kutafuta kuokoa wale wanaopotea. Katika kuwasilisha kwa mwenye dhambi Mwokozi wao binafsi, anayesamehe dhambi, tunafikia mkono wa huruma. na upendo kama wa Kristo kushika mkono wa mtu aliyeanguka, na kuushika mkono wa Kristo kwa imani, tunaunda muunganiko kati ya mwenye dhambi na Mwokozi. {9T 203.1}

Mwisho umekaribia, na kila nafsi sasa inapaswa kutembea kwa uangalifu, unyenyekevu, upole pamoja na Kristo Yesu. Mwokozi wetu wa thamani, ambaye kutoka Kwake miale yote ya Ukweli huangaza ulimwenguni, anataka tusiweke tumaini letu kwa wakuu, wala kwa mwanadamu ambaye hapana msaada kwake; bali kumwegemea Yeye kabisa. Anasema: "Bila Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote." Yohana 15:5. Tunahitaji kumwangalia Yesu daima ili aweze kusisitiza juu yetu sura Yake Mwenyewe nzuri. Yatupasa kumtazama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Kisha tutamfunua Kristo kwa wanadamu wenzetu. {9T 203.2}

## SURA YA 23
## KUUTANGAZA UKWELI MAHALI PALIPO NA UBAGUZI WA RANGI

Ninalemewa, ninalemewa sana, kwa ajili ya kazi miongoni mwa watu weusi. Injili inapaswa kuwasilishwa kwa watu weusi waliokandamizwa. Lakini tahadhari kubwa itabidi ionyeshwe katika juhudi zinazowekwa mbele kwa ajili ya kuwainua watu hawa. Miongoni mwa watu weupe katika sehemu nyingi kuna chuki yenye nguvu dhidi ya watu weusi. Tunaweza kutamani kupuuzia ubaguzi huu, lakini hatuwezi kufanya hivi. Ikiwa tungefanya kana kwamba ubaguzi huu haupo tusingeweza kupata nuru mbele ya watu weupe. Ni lazima kukutana na hali kama

ilivyo na kukabiliana nayo kwa hekima na akili. {9T 204.1}

Kwa miaka mingi nimebeba mzigo mzito kwa niaba ya watu weusi. Moyo wangu umeniuma kama nilivyoona hisia dhidi ya watu weusi zikizidi kuwa na nguvu na kuzidi kuwa na nguvu, na kama nilivyoona wengi Waadventista Wa Sabato ni dhahiri hawawezi kuelewa umuhimu wa kuwa na kazi ya bidii ya kufanywa haraka. Miaka inapita kuuelekea umilele na inaonekana kwa sasa ni kwa uchache sana kazi imefanywa kuwasaidia wale ambao walikuwa hivi majuzi jamii ya watumwa. {9T 204.2}

Moja ya changamoto zinazoikabili kazi ni kwamba watu wengi weupe wanaoishi ambapo watu weusi ni wengi, hawako tayari kwamba juhudi maalum zifanyike ili kuwainua. Wanapoona shule zimeanzishwa kwa ajili yao, wanapoona wanafundishwa kujitegemea, kufuata biashara/stadi, kujipatia nyumba za starehe badala ya kuendelea kuishi kwenye majumba, wanaona kwamba mipango yao ya ubinafsi itaingiliwa --kwamba hawataweza tena kuajiri watu weusi kwa pesa kidogo tu; na uadui wao unaamshwa. Wanahisi kuwa wamejeruhiwa na kunyanyaswa. Wengine hutenda kana kwamba utumwa haujawahi kukomeshwa. Roho hii inakua na nguvu kama Roho wa Mungu anavyoondolewa kutoka ulimwenguni, na katika sehemu nyingi haiwezekani sasa kufanya kazi ambayo ingeweza kufanywa kwa watu weusi katika miaka iliyopita. {9T 204.3}

Mengi yangeweza kutekelezwa na watu wa Amerika ikiwa juhudi za kutosha kwa niaba ya watu waliowekwa huru waliokuwa wametolewa na Serikali na makanisa ya Kikristo mara baada ya ukombozi wa watumwa. Pesa zilipaswa kutumika kwa uhuru kuwatunza na kuwaelimisha huko wakati walipokuwa wakihitaji sana msaada. Lakini Serikali, baada ya juhudi kidogo, iliwaacha watu weusi kupambana, bila kusaidiwa, na mzigo wao wa matatizo. Baadhi ya makanisa ya Kikristo yenye nguvu yaliianza kazi njema, lakini cha kusikitisha yameshindwa kuwafikia wengi ukilinganisha na wachache; na Kanisa la Waadventista Wa Sabato limeshindwa kutekeleza sehemu yake. Baadhi ya juhudi za kudumu zimewekwa na watu binafsi na jamii ili kuwainua watu weusi, na kazi nzuri imefanywa. Lakini ni wachache kiasi gani wameshiriki katika kazi hii ambayo inapaswa kuwa na huruma na msaada kwa wote! {9T 205.1}

Juhudi tukufu zimetolewa na baadhi ya Waadventista Wasabato kufanya kazi iliyohitajika kufanywa kwa watu weusi. Laiti wale waliojishughulisha na kazi hii wangepokea ushirikiano wote wa ndugu zao wahudumu, matokeo ya kazi yao sasa yangekuwa tofauti kabisa na ilivyo. Lakini idadi kubwa ya watumishi wetu hawakutoa ushirikiano, kama walivyopaswa kufanya, na wachache ambao wamekuwa wakijitahidi kuiendeleza kazi iliyohitajika sana katika eneo gumu. {9T

205.2}

Kadiri wakati unavyosonga mbele, na upinzani ukiimarika, hali hutuonya kwamba busara ndiyo bora Zaidi sehemu ya ushujaa. Ikiwa hatua zisizo za busara zimefanywa katika kazi iliyofanywa kwa watu weusi, sio kwa sababu maonyo hayajatolewa. Kutoka Australia, kuvuka maji ya Pasifiki, tahadhari zilitumwa kwamba kila hatua lazima iangaliwe, kwamba watendakazi hawakutakiwa kutoa hotuba za kisiasa, na kwamba mchanganyiko wa wazungu na weusi katika usawa wa kijamii ulikuwa hauna budi ya kuhimizwa. {9T 205.3}

Katika mkutano wa baraza uliofanywa mwaka 1895 huko Armadale, kitongoji cha Melbourne, Victoria, nilizungumzia juu ya haya mambo, kwa kujibu maswali ya ndugu zangu, na kuhimiza umuhimu wa tahadhari. Nilisema kwamba nyakati za hatari zilikuwa zinakuja, na kwamba hisia ambazo zingeweza kuonyeshwa kuhusiana na nini kinapaswa kufanywa kwa kufuata njia za umisionari kwa watu weusi hazikuweza kuelezwa katika siku zijazo bila kuhatarisha maisha. Nilisema wazi kwamba kazi iliyofanywa kwa watu Weusi itabidi iwe ikiendelea kwa kufuata namna tofauti ya zile zilizofuatwa katika baadhi ya sehemu za nchi katika miaka ya awali. {9T 206.1}

Hebu isemwe kidogo iwezekanavyo kuhusu mambo ya utofauti wa rangi, na hebu watu Weusi wafanye kazi hasa kwa wale wa rangi yao. {9T 206.2}

Kuhusiana na watu weupe na weusi wanaoabudu katika jengo moja, hili haliwezi kufuatwa kama desturi ya jumla yenye faida kwa kila sehemu--hasa Kusini. Jambo bora litakuwa kuwapatia watu weusi wanaoikubali Ukweli, kuwa na mahali pao pa kuabudia, ambamo wanaweza kuendeleza huduma zao peke yao. Hii ni muhimu hasa Kusini ili kwamba kazi kwa ajili ya watu weupe iweze kupelekwa bila kizuizi kikubwa. {9T 206.3}

Hebu waumini weusi wapewe nyumba za ibada zilizo nadhifu na zenye mvuto mzuri. Waoneshwe kwamba hili linafanywa sio kuwatenga kuabudu pamoja na watu weupe, kwa sababu wao ni weusi, bali kwamba maendeleo ya Ukweli yaweze kuendelezwa. Waelewe kwamba mpango huu unapaswa kufuatwa hadi Bwana atakapoonyesha kwetu njia bora mbadala. {9T 206.4}

Washiriki Weusi wenye uwezo na uzoefu wanapaswa kuhimizwa kuongoza huduma za watu wao wenyewe; na sauti zao zinapaswa kusikika katika kusanyiko la uwakilishi. {9T 207.1}

Miongoni mwa waumini weusi kuna wengi ambao wanaweza kufanya kazi kwa

faida kwa ajili ya watu wao wenyewe--wafanyakazi ambao Bwana amewapa nuru na maarifa na ambao wana uwezo usio wa kawaida. Hawa wanapaswa kufanya kazi kwa bidii na kwa kila njia yenye ufanisi. Wanapaswa kutumia vitabu vyetu na kufanya mikutano ya mahema na mikutano katika kumbi. Na wakati mwingine (inaporuhusiwa) watumishi wazungu wanapaswa kuwasaidia. Jitihada maalum zinapaswa kufanywa ili kuongeza nguvu ya watendakazi weusi. Watu weusi wanapaswa kuelimishwa kikamilifu na kufunzwa kutoa mafundisho ya Biblia na kufanya mikutano ya mahema miongoni mwa watu wao wenyewe. Kuna wengi wenye uwezo, ambao wanapaswa kufanywa tayari kwa kazi hii. {9T 207.2}

Tunapaswa kupendezwa sana na uanzishwaji wa shule kwa ajili ya watu weusi. Na sisi lazima tusipuuze umuhimu wa kuuweka Ukweli wa sasa mbele ya walimu na wanafunzi katika vyuo vikubwa vilivyoannzishwa na watu wa ulimwengu kwa ajili ya watu weusi. {9T 207.3}

Shule na hospitali za tiba asilia kwa watu Weusi zinapaswa kuanzishwa, na katika hizi vijana weusi wanapaswa kufundishwa na kupewa mafunzo kwa ajili ya utumishi na walimu bora kabisa wanaoweza kuajiriwa. {9T 207.4}

Watumishi/wachungaji Weusi wanapaswa kufanya kila jitihada iwezekanayo kuwasaidia watu wao kuulewa ukweli wa sasa.Kadri muda unavyoendelea na ubaguzi wa rangi kuongezeka,itawezekana kuwa ngumu,katika mahali pengi kwa watendakazi weupe kufanya kazi kwa ajili ya watu weusi.Mara nyingine watu weupe wasio na huruma na kazi yetu wataungana na watu weusi kuipinga, wakidai kuwa mafundisho yetu ni jitihada za kuyavunja makanisa na kuleta taabu kuhusu swala la Sabato. Watumishi/wachungaji weusi kwa weupe watatoa maneno ya uongo,wakiamsha hisia za ubaguzi zitakazoeleka kuua na kuharibu- {9T 207.5}

Nguvu za kuzimu zinafanya kazi kwa werevu wao wote ili kuzuia kutangazwa kwa ujumbe wa mwisho wa rehema miongoni mwa watu weusi. Shetani anafanya kazi ili kuifanya iwe ngumu zaidi kwa mtumishi wa injili na mwalimu kupuuza ubaguzi uliopo kati ya watu weupe na weusi. {9T 208.1}

Hebu tuufuate mpango wa hekima. Tusifanye lolote litakaloamsha upinzani bila ya lazima-- chochote kitakachozuia utangazwaji wa ujumbe wa injili. Inapoonekana kuwa ni desturi au mahali juhudi zaidi inatakiwa kufanywa, hebu waumini wa kizungu na waumini weusi wakutane katika maeneo tofauti ya ibada. Hebu tuoneshe upole wa Kristo. Alikuwa Mkuu mbinguni, Mwana pekee wa Mungu. Lakini “Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16. {9T 208.2}

Ikiwa, ili kuuokoa ulimwengu unaoangamia, Mungu alijinyenyekeza kumtoa Mwanawe katika kifo cha uchungu na cha aibu; Je, wamishionari wa Bwana hawapaswi kuwa tayari kufanya kila juhudi katika uwezo wao kuwavuta na kuwasaidia wale walio katika kina cha dhambi, na kuwamulikia nuru wale walio gizani kuhusu upi ni Ukweli? Kristo aliuvisha Uungu Wake kwa ubinadamu, ili apate kufika chini na kuinua wanadamu walioanguka. Je, wafuasi Wake, kwa ajili Yake, hawatakuwa tayari kunyenyekea  kwa mambo mengi yasio ya haki na yenye kuhuzunisha kubebwa, ili kuwasaidia wale wanaohitaji msaada? Hebu kazi ifanyike katika namna ambayo haitaamsha chuki ambayo ingefunga milango iliyofunguliwa sasa kwa ajili ya Ukweli kuingia. {9T 208.3}

Watu wenye talanta miongoni mwa waumini weusi wanapaswa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu kwa ajili ya watu wao wenyewe. Na bado wakati mwingine kutakuwa na fursa kwao kutoa ushuhuda katika mikutano ya mahema na katika mikusanyiko mikubwa, ambao utawafikia watu wengi sana. Fursa hizi zitaonekana ikiwa eneo la Kusini litafanyiwa kazi na kilio kikuu kinatolewa. Roho Mtakatifu atakapomiminwa, kutakuwa na ushindi wa ubinadamu juu ya chuki katika kutafuta wokovu wa roho za wanadamu. Mungu atafanya kuzidhibiti akili. Mioyo ya wanadamu itapenda kama Kristo alivyopenda. Na swala la ubaguzi wa rangi litazingatiwa na wengi sana kwa namna tofauti na jinsi inavyozingatiwa sasa. Kupenda kama Kristo apendavyo, huiinua akili kuwa katika usafi, na anga ya mbinguni, isiyo na ubinafsi. {9T 209.1}

Yule ambaye ameunganishwa kwa karibu na Kristo ameinuliwa juu ya ubaguzi wa rangi au utabaka. Imani yake inashikilia uhalisia wa umilele. Mwandishi wa Kweli ya Mungu anapaswa kuinuliwa. Mioyo yetu inapaswa kujazwa na imani itendayo kazi kwa upendo na kuitakasa roho. Kazi ya Msamaria mwema ni mfano ambao sisi tunapaswa kuufuata. {9T 209.2}

Hatupaswi kuchochea swala la ubaguzi wa rangi, na hivyo kuamsha chuki na kuleta migogoro. Nuru ya ujumbe wa malaika wa tatu inapaswa kutolewa kwa wale wanaoihitaji nuru. Tunapaswa kufanya kazi kwa utulivu, kimya, kwa uaminifu, tukimwamini Ndugu yetu mkubwa. Hatupaswi kuwa na haraka kufafanua njia halisi ya kufuatwa katika siku zijazo kuhusu uhusiano unaopaswa kudumishwa kati ya watu weupe na weusi. Ukweli wa sasa unapaswa kutangazwa mbele ya maelfu ya watu wa majimbo ya Kusini. Njia inapaswa kusafishwa, iwezekanavyo, kwa ajili ya kuondoa kizuizi chochote. Hebu ujumbe wa injili utolewe kwa watu. Hebu watu weupe na weusi watumike kwa utengano, kwa njia tofauti, na Bwana atafanya hayo mengine. Ukweli lazima ufike mbele ya wanaume na wanawake weupe wa majimbo ya Kusini. Kisha kutakuwa na kazi itakayofanywa katika familia zao ambayo italeta wokovu wa roho nyingi. {9T 209.3}

## "Katika Hekima Yote na Busara"

Wakati watu wanajaribu kutatua swala la ubaguzi wa rangi, muda unasonga, na roho zinashuka kaburini, bila kuwa na onyo na kuokoka. Hebu hali hii ya mambo isiendelee kwa muda mrefu. Hebu wanaume na wanawake waende kufanya kazi, na wafanye kazi kama vile Roho wa Mungu atakavyozisukuma akili zao. Tunahitaji talanta za waumini weusi, kila nukta zake, katika kazi hii. Hebu watendakazi Weusi wafanye kazi kwa ajili ya watu wao wenyewe, wakisaidiwa na wafanyakazi wa kizungu kadri mazingira yatakavyoruhusu. Mara nyingi watahitaji ushauri na maoni. Hebu waumini Weusi wawe na mahali pao pa kuabudia na waumini wa kizungu wawe na mahali pao pa kuabudia. Hebu kila kundi liwe na bidii kufanya kazi ya Kweli ya kimishionari kwa ajili ya watu wake na kwa watu weusi popote pale na wakati wowote wanapoweza. {9T 210.1}

Wakati kuwa Ukweli umewasilishwa, na watu weupe wengi kadiri watakavyosikia na kuamini kuukubali Kkweli, wakati mwingine fursa zitaonekana kwa juhudi kufanywa, kwa utulivu, namna ya kawaida, na watendakazi weupe kwa watu weusi. Fursa kama hizo hazipaswi kupuuzwa. {9T 210.2}

Lakini hatupaswi kuamsha ubaguzi ambao ungefunga njia dhidi ya tangazo la ujumbe wa malaika wa tatu kwa watu weupe. Wanauhitaji huu ujumbe; kwa maana mbele yetu kuna wakati wa taabu, ambao haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa. {9T 210.3}

Uangalifu mkubwa lazima ufanyike ili kwamba hakuna kitu cha kusema au kufanywa cha kuamsha hisia za watu Weusi dhidi ya wazungu. Tusizidishe changamoto ambayo tayari ipo. Hata kwa busara watendavyo kazi, watendakazi watakutana na upinzani, wasijenge fadhaa juu ya ubaguzi wa rangi. Hebu tuisafishe barabara kuu ya Mfalme. Tumwache Mungu apate nafasi ya kufanya kazi. Hebu watu waitunze njia Yake. Atapanga na kuisimamia vyema kuliko wanadamu wanavyoweza. Hebu tukumbuke kwamba kazi yetu kuu ya kwanza ni kulihubiri Neno la Mungu, kutoa maonyo ya Biblia. {9T 211.1}

Bwana anawaita wote waifanye kazi hiyo kwa unyenyekevu wa akili. Wahudumu sio wote waliotakaswa kwa Kweli. Bwana anawaita wote kuweka chini mapambano yao. Hebu watu wajihadhari na kufanya ambayo yangekatisha tumaini letu la mwisho la kuingia katika maeneo magumu ambamo kuna ubaguzi na uadui wa rangi. {9T 211.2}

Kama njia ya kushinda chuki na kupata ufikiaji wa akili, kazi ya umishonari ya matibabu lazima ifanyike, si katika sehemu moja au mbili tu, bali katika sehemu nyingi ambako kweli bado haijatangazwa. Tunapaswa kufanya kazi kama wamishenari wa injili wa matibabu, kuponya roho zilizo wagonjwa wa dhambi kwa kuwapa ujumbe wa wokovu. Kazi hii itaondoa ubaguzi kuliko kitu kingine kinavyoweza. {9T 211.3}

## Sabato

Swala la Sabato ni jambo ambalo litahitaji uangalifu mkubwa na wa hekima katika uwasilishaji wake. Wingi wa neema na nguvu za Mungu zitahitajika ili kuangusha sanamu ambayo imesimamishwa kwa umbo la sabato ya uongo. Inua kiwango, inua juu, juu na juu zaidi. Waelekeze watu kwenye sura ishirini ya kitabu cha Kutoka, ambako sheria ya Mungu imeandikwa. Amri nne za kwanza kati ya zile Amri Kumi zinaeleza wajibu wetu kwa Muumba. Anayemdanganya Mungu Wake hawezi kuwa mwaminifu kwa jirani yake. Anayempenda Mungu zaidi atampenda jirani yake kama nafsi yake. Kiburi hujiinua juu kwa ubatili, humfanya wakala wa kibinadamu kujifanya mungu mwenyewe. Injili ya Kristo inatakasa roho, ikiondoa kujipenda nafsi. {9T 211.4}

"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase." Kutoka 20:8. Sabato ilianzishwa katika Edeni, baada ya Mungu kuwa ameumba ulimwengu. "Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote. Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; na akastarehe siku ya saba akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa: kwa sababu katika siku hiyo, Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi Yake yote aliyoiumba na kuifanya." Mwanzo 2:1-3. {9T 212.1}

"BWANA akanena na Musa, na kumwambia, Kisha nena wewe na wana wa Israeli, kuwaambia, Hakika mtazishika Sabato Zangu kwa kuwa ni ishara kati ya Mimi na ninyi katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua ya kuwa Mimi Ndimi Bwana niwatakasaye ninyi. Basi Mtaishika Sabato; kwa kuwa ni takatifu kwenu; kila atakayeitia unajisi hakika yake atauawa; kwa kuwa kila mtu afanyaye kazi katika siku hiyo nafsi hiyo itakatiliwa mbali na watu wake. Kazi itafanywa Siku sita ;lakini katika saba ni Sabato ya kustarehe kabisa, takatifu kwa Bwana; kila mtu atakayefanya kazi yoyote katika siku ya Sabato, hakika yake atauwawa. Kwa ajili ya hayo wana wa Israeli wataishika Sabato, kuiangalia sana hiyo Sabato katika vizazi vyao vyote, ni agano la milele." Kutoka 31:12-16. Oktoba 19, 1908. {9T 212.2}

## SURA YA 24
## SWALA LA UTOFAUTI WA RANGI

Nina baadhi ya mambo ya kusema kuhusiana na watu weusi wa Majimbo ya Kusini mwa Marekani na uhusiano ambao tunapaswa kudumisha kwao. Kwa muda mrefu walikuwa chini ya laana ya utumwa ambalo ni tatizo gumu kujua jinsi wanapaswa sasa kutendewa. {9T 213.1}

Watenda kazi wa Mungu wanaporuhusu Roho Wake kufanya kazi katika akili zao, mengi yatatimizwa katika kazi ya kuokoa roho. Bwana Ndiye msaidizi wetu.

Atatuongoza katika mambo yote ikiwa tutamtegemea. Jambo moja ni hakika: Ni lazima tuwe na imani katika Mungu--imani kwamba ataweka mambo kwa namna ambayo itatuwezesha kufanya kazi kwa mafanikio. Hakuna aliyewahi kumwamini Mungu bure. Hatawakatisha tamaa wale wanaoweka tumaini lao Kwake. {9T 213.2}

Tunapaswa kuepuka kuingia katika ugomvi juu ya tatizo la ubaguzi wa rangi. Ikiwa suala hili tukilitibua tibua sana, matatizo yatatokea ambayo yatatumia muda mwingi wa thamani kuyaondoa. Hatuwezi kuweka kando njia ya uhakika ya kufuatwa katika kushughulikia swala hili. Katika maeneo tofauti na katika hali tofauti, jambo hili litahitaji kushughulikiwa kwa utofauti. Katika Kusini, ambapo ubaguzi wa rangi una nguvu, hatungeweza kufanya chochote katika kuuwasilisha Ukweli ikiwa tungeshughulikia suala la ubaguzi wa rangi kama tulivyokabiliana nalo katika baadhi ya maeneo ya Kaskazini. Watendakazi wazungu huko Kusini watalazimika kwenda kwa namna fulani ambayo itawawezesha kuwapata watu weupe. {9T 213.3}

Ni mpango wa Shetani kuwaita watu kwenye kuungalia ubaguzi wa rangi. Ikiwa madai yake yatazingatiwa, kutakuwa na tofauti ya maoni na mkanganyiko mkubwa. Hakuna mtu anayeweza kufafanua wazi nafasi sahihi ya watu weusi. Watu wanaweza kuendeleza nadharia, lakini ninakuhakikishia kwamba haitatufaa sisi kufuata nadharia za kibinadamu. Hata hivyo, kama iwezekanavyo, swala la ubaguzi wa rangi liachwe kutulia. {9T 213.4}

Miji ya Kusini inapaswa kufanyiwa kazi, na kwa kazi hii talanta bora zitapatikana, na hivyo bila kuchelewa. Hebu wafanyakazi weupe wafanye kazi kwa ajili ya watu weupe, wakiutangaza ujumbe wa Ukweli wa sasa kwa usahili wake. Watapata fursa ambazo kupitia hizo wanaweza kulifikia tabaka la juu. Kila fursa ya kulifikia tabaka hili inapaswa kutumiwa. {9T 214.1}

Hebu watendakazi weusi wafanye wawezavyo ili kujiendeleza, kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya watu wao wenyewe. Ninamshukuru Mungu kwamba miongoni mwa waumini weusi kuna watu wenye vipaji ambao wanaweza kufanya kazi kwa ufanisi kwa ajili yao watu wao wenyewe, wakiuwasilisha Ukweli kwa namna iliyo sahili. Kuna watu wengi Weusi wenye vipaji vya thamani ambao wataongolewa na Ukweli ikiwa wahudumu wetu Weusi wana hekima katika kubuni njia za kuwafunza walimu kwa ajili ya shule na watendakazi wengine kwa ajili ya eneo hili. {9T 214.2}

Watu Weusi hawapaswi kuhimiza kuwekwa kwenye usawa na watu weupe. Uhusiano wa jamii hizI mbili umekuwa jambo gumu kushughulika nalo, na

ninahofia kwamba litabaki kuwa tatizo kubwa la kutatanisha. Kwa kadiri inavyowezekana, kila kitu ambacho kingeweza kuchochea ubaguzi wa rangi kwa wazungu kinapaswa kuepukwa. Kuna hatari ya kufunga mlango ili watendakazi wetu wazungu wasiweze kufanya kazi katika baadhi ya maeneo ya Kusini. {9T 214.3}

Ninajua kwamba ikiwa tutajaribu kukidhi mawazo na mapendekezo ya baadhi ya watu weusi, tutajikuta njia yetu imefungwa kabisa. Kazi ya kutuangaza Ukweli wa sasa si ya kuzuiwa kwa jitihada za kurekebisha nafasi ya watu weusi. Tukijaribu kufanya hivi tutapata vizuizi kama vile milima vitainuliwa ili kuzuia kazi ambayo Mungu anatamani iwe imefanywa. Ikiwa tutaenda kimya kimya na kwa busara, kufanya kazi kwa njia ambayo Mungu ameiweka, watu weupe na Weusi wote watafaidika na kazi zetu. {9T 214.4}

Wakati bado haujafika kwetu kufanya kazi kana kwamba hakuna ubaguzi. Kristo alisema: "Basi iweni wenye hekima kama nyoka, na wapole kama hua." Mathayo 10: 16. Ukiona kuwa kwa kufanya mambo fulani ambayo una haki kamili ya kuyafanya, unazuia maendeleo ya kazi ya Mungu, Jizuie kufanya mambo hayo. Usifanye chochote kitakachofunga akili za wengine dhidi ya Ukweli. Kuna ulimwengu wa kuokoa, nasi hatutapata chochote kwa kujitenga na wale tunaojaribu kuwasaidia. Vitu vyote vinaweza kuwa halali, lakini si vyote vifaavyo. {9T 215.1}

Njia ya busara ni bora zaidi. Kama watenda kazi pamoja na Mungu, tunapaswa kufanya kazi kwa njia ambayo itatuwezesha kutimiza mengi kwa ajili Yake. Hebu mtu yeyote asiwe na kupitiliza. Tunahitaji hekima itokayo juu; kwa maana tunalo tatizo gumu la kutatua. Ikiwa hatua za harara zitafanywa sasa, uharibifu mkubwa utafanyika. Jambo linapaswa kuwasilishwa kwa namna ambayo watu weusi walioongoka kweli kweli watashikamana na Ukweli kwa ajili ya Kristo, wakiacha kukana kanuni hata moja ya fundisho la Biblia lenye uzima kwa sababu wanaweza kufikiri kwamba jambo fulani bora halifuatwi kuhusuiana na watu weusi. {9T 215.2}

Ni lazima tuketi kama wanafunzi miguuni pa Kristo, ili atufundishe mapenzi ya Mungu na tuweze kujua jinsi ya kufanya kazi kwa watu weupe na watu Weusi katika eneo la Kusini. Tunapaswa kufanya kama Roho wa Bwana atuamuruvyo, na kulitazama swala la ubaguzi wa rangi kuwa dogo iwezekanavyo. Lazima tutumie kila nguvu kuuwasilisha ujumbe wa injili ya wakati wa mwisho kwa matabaka yote ya Kusini. Kadri Tunavyoongozwa na tukidhibitiwa na Roho wa Mungu tutagundua kwamba swala hili litajirekebisha katika akili za watu wetu. {9T 215.3}

Kila mmoja wetu na tumtafute Bwana. Hebu wale ambao uzoefu wao wa kidini

huko nyuma umekuwa tu wa juu juu, wamkaribie Mungu. Tubuni, tubuni, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe. {9T 216.1}

Tunapojitayarisha kushikilia kazi kwa bidii tutakuwa na uwezo bora zaidi kuliko tunavyoweza sasa kushughulikia maswala yanayohusika na kazi hii. Hebu kila muumini afanye bidii yake kuandaa njia kwa ajili ya kazi ya umishonari ya injili ambayo inapaswa kufanywa. Lakini mtu yeyote asiingie katika ugomvi. Ni lengo la Shetani kuwaweka Wakristo katika mabishano kati yao wenyewe. Anajua kwamba ikiwa hawatakesha, basi siku ya Bwana itawajilia kama mwivi wakati wa usiku. Hatuna muda sasa wa kuipa nafasi roho ya adui na kuuthamini ubaguzi unaochanganya akili na kutupeleka mbali na Kristo. {9T 216.2}

Itachukua pesa na bidii, juhudi za kudumu kufanya kile kinachohitajika kufanywa miongoni mwa watu weusi. Kila mtu anahitaji sasa kusimama katika sehemu yake na mahali pake, kuungama na kuziacha dhambi zake, na akifanya kazi kwa amani na ndugu zake. Watumishi wa Mungu wanapaswa kuwa na nia moja na moyo mmoja, wakiomba kumwagwa kwa Roho na kuamini kwamba Mungu atalitimiza
Neno Lake. {9T 216.3}

## Funzo Kutoka Katika Kazi Ya Kristo

Wakati mmoja, Kristo alipokuwa katikati ya kazi Yake ya kufundisha na kuponya, moja ya kundi la watu waliokusanyika Kwake wakasema: "Bwana, sema na ndugu yangu agawanye urithi nami." Luka 12:13. {9T 216.4}

Mtu huyu alikuwa ameshuhudia kazi za ajabu za Kristo. Alikuwa ameshangazwa na wepesi wa ufahamu, utambuzi Wake mkuu, na uadilifu/haki ambao aliutazama kutokana na kesi zilizoletwa Kwake. Alisikia maombi ya Kristo yenye kusisimua na utakatifu Wake wa shutuma kwa waandishi na Mafarisayo. Kama maneno ya amri kama hii yangesemwa kwa ndugu huyu, asingethubutu kumkatalia mtu aliyedhulumiwa sehemu yake. Aliomba ushawishi wa Kristo upande wake. Akasema, Mwambie ndugu yangu anigawie urithi. {9T 216.5}

Roho Mtakatifu alikuwa akimsihi mtu huyu awe mrithi wa urithi usioharibika usio na unajisi, na usioharibika. Alikuwa ameona ushahidi wa nguvu za Kristo. Sasa ilikuwa ni fursa yake ya kuongea na Mwalimu Mkuu, kueleza tamaa iliyo ya juu zaidi moyoni mwake. Lakini kama mtu mwenye matope kwa mfano wa Bunyan (Pilgrim’s progress), macho yake yalikuwa yameelekezwa duniani. Hakuona taji juu ya kichwa chake. Kama Simon Magus alithamini karama ya Mungu kama njia ya kupata faida ya kidunia. {9T 217.1}

Utume wa Mwokozi duniani ulikuwa unakaribia mwisho. Miezi michache tu ilibaki kwa Yeye kukamilisha kile alichokuja kufanya katika kuusimamisha ufalme wa neema Yake. Hata hivyo tamaa pupa ya binadamu ilimfanya aache kazi Yake na kuuchukua mzozo wa kipande cha ardhi. Lakini Yesu hakupaswa kukengeushwa kutoka katika utume Wake. Jibu Lake lilikuwa: "Mwanadamu, ni nani aliyeniweka Mimi kuwa mwamuzi au mgawanyi juu yenu?" Luka 12:14. {9T 217.2}

Kristo alimfanya mtu huyo kwa uwazi kuelewa kwamba hii haikuwa kazi Yake. Alikuwa akijitahidi kuokoa roho. Hakupaswa kugeuzwa kando na hili ili kuchukua majukumu ya hakimu wa kiraia. {9T 217.3}

Ni mara ngapi leo kazi inalazimishwa kwa kanisa ambayo haikupaswa kamwe kuruhusiwa kuingilia kazi ya huduma ya injili! {9T 217.4}

Tena na tena Kristo alikuwa ameombwa aamue maswala ya kisheria na ya kisiasa. Lakini alikataa kuingilia mambo yapitayo. Alijua kwamba katika ulimwengu wa kisiasa kulikuwa na kesi za uovu na udhalimu mkubwa. Lakini ufunuo Wake wa pekee wa haya ulikuwa kutangazwa kwa Kweli ya Biblia. Kwa makutano makuu yaliyosongamana katika hatua Zake aliwasilisha kanuni safi, takatifu za sheria ya Mungu na kusema baraka inayopatikana katika kutii kanuni hizi. Kwa mamlaka kutoka juu aliutekeleza umuhimu wa haki na huruma. Lakini alikataa kujiingiza katika migogoro ya kibinafsi. {9T 218.1}

Kristo alisimama katika ulimwengu wetu kama Kichwa cha ufalme mkuu wa kiroho ambao ulikuja kuanzishwa katika ulimwengu wetu -ufalme wa haki. Mafundisho Yake yaliweka wazi kanuni za kuinua na kutakasa zinaotawala ufalme huu. Alionesha kwamba haki na rehema na upendo ni nguvu zinazotawala katika ufalme wa Yehova. {9T 218.2}

## Wakati wa Maandalizi

Tunaishi katika siku kuu ya mfano ya upatanisho. Ni lazima kila mmoja wetu tumtafute Mungu. Hii ni kazi ya kibinafsi. Na tumkaribie Mungu, tusiruhusu chochote kiingie katika jitihada zetu ambacho kingetufanya kupotosha Ukweli wa sasa. Kila mtu na auungame, si dhambi ya ndugu yake, bali dhambi yake mwenyewe. Hebu aunyenyekeze moyo wake mbele za Mungu na kujazwa na Roho Mtakatifu hivi kwamba maisha yake yataonyesha kwamba amezaliwa mara ya pili. Tunasoma: “Wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina Lake." Yohana 1:12. {9T 218.3}

Injili ya Kristo inapaswa kuishiwa, kutekelezwa katika maisha ya kila siku. Watumishi wa Mungu wanapaswa kusafishwa kutoka kwenye ubaridi wote, na ubinafsi wote. Unyenyekevu, upole, kujishusha vina thamani kubwa katika kazi ya Mungu. Jaribuni kuwaunganisha watendakazi kwa ujasiri na upendo. Ikiwa hamwezi kufanya haya, fanyeni haki, na hayo mengine mwachie Mungu. Fanyeni kazi kwa imani na maombi. Chagueni vijana wa Kikristo, na kuwazoeza kuwa, si wafanyakazi wenye mioyo kama chuma, bali wafanyakazi walio tayari kupatana. {9T 218.4}

Ninaomba kwamba Bwana abadilishe mioyo ya wale ambao, isipokuwa wamepata neema zaidi, wataingia katika majaribu. Ninaomba kwamba aulainishe na kuutiisha kila moyo. Tunahitaji kuishi katika ushirika wa karibu pamoja na Mungu, ili tupendane sisi kwa sisi kama Kristo alivyotupenda sisi. Ni kwa njia hii ulimwengu unapaswa kujua sisi ni wanafunzi Wake. Hebu kusiwepo na kujikweza. Ikiwa watenda kazi watanyenyekea mioyo yao mbele za Mungu, mbaraka utakuja. Wakati wote watakuwa wakipokea mawazo ang'avu, mapya, na kutakuwa na uamsho wa ajabu wa kazi ya umishonari wa matibabu wa injili. {9T 219.1}

Kazi kuu iko mbele yetu sote, kama Wakristo, tunapaswa kupanua ufalme wa Kristo kwa haraka iwezekanavyo, kulingana na Shuhuda kwa kanisa, Gombo la 9. Injili inapaswa kusonga mbele kutoka ushindi hadi ushindi, kutoka ushindi hadi ushindi. Ukuu wa ufalme chini ya mbingu zote utapewa watu kwa watakatifu Wake Aliye Juu, nao watautwaa ufalme na kuumiliki huo ufalme milele na milele. {9T 219.2}

### Vita Mbele Yetu

Watumishi wa Mungu wanapaswa kuvaa kila sehemu ya silaha za Kikristo. Hatushindani tu na maadui wa kibinadamu. Mungu anamwita kila Mkristo kuingia katika vita na kupigana chini ya uongozi Wake, kutegemea kufanikiwa kwa neema na msaada wa Mbinguni. {9T 219.3}

Tunapaswa kwenda mbele kwa nguvu za Mwenyezi. Kamwe tusikubali kushindwa na mashambulizi ya Shetani. Kwa nini sisi, kama mashujaa wa Kikristo, tusimame dhidi yake falme na mamlaka, na juu ya wakuu wa giza hili? Mungu anatuita kusonga mbele, kwa kutumia karama tulizokabidhiwa. Shetani ataweka majaribu mbele yetu. Atajaribu kutushinda kwa mbinu za ulaghai. Lakini kwa nguvu za Mungu tunapaswa kusimama imara kama mwamba katika kanuni. {9T 219.4}

Katika vita hivi hakuna kupumzika. Mawakala wa Shetani hawatulii kamwe katika kazi yao ya uharibifu. Wale ambao wako katika huduma ya Kristo lazima wakeshe

kila kituo. Lengo letu ni kuokoa roho zinazoangamia kutokana na uharibifu. Hii ni kazi ya ukuu usio na kikomo, na mwanadamu hawezi kutumaini kupata mafanikio ndani yake isipokuwa aungane na Mtendakazi wa Mbinguni. {9T 220.1}

Tangu milele Kristo amekuwa Mkombozi wa mwanadamu. Tangu anguko limekuja kwa wale wanaoungana pamoja Naye katika kazi Yake kuu, Neno hili: "Msichoke katika kutenda mema." 2 Wathesalonike 3:13.  Mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana sikuzote." 1 Wakorintho 15:58. {9T 220.2}

Mkristo anahimizwa kuonyesha ustahimilivu katika kuendeleza kazi ya injili huduma inayohusiana na kazi ya umishonari wa matibabu. Anapopata uzoefu katika dini ya Kweli, anapata ujuzi wa kiroho utengenezao tabia. {9T 220.3}

Maisha ya Mkristo wa kweli ni duru moja endelevu ya huduma. "Sisi ni watenda kazi pamoja na Mungu." Kila siku huleta kwa Yule aliye katika huduma ya utumishi wa Mungu majukumu yaliyo sawia na uwezo Wake. Umuhimu wake unaongezeka, kama chini ya uongozi wa Mamlaka kuu, anayatimiza majukumu haya. Utimilifu wa wajibu mmoja hutufanya tujiandae vyema kuuchukua wajibu mwingine. Wale ambao wana uelewa wa Kweli ya kile kinachopaswa kufanywa watajiweka wenyewe katika nuru ya moja kwa moja ya Neno la Mungu, katika umoja na watendakazi. Kila siku, wakiwa wamevaa silaha zote, watatoka kwenda vitani. Kwa maombi na kukesha na ustahimilivu watafanya kazi, wakidhamiria kwamba mwisho wa kazi yao ya maisha hautawakuta hawajajitayarisha, bila kufanya yote wawezayo kwa ajili ya wokovu wa roho zinazopotea. {9T 220.4}

Ikiwa Wakristo wangetenda kwa pamoja, wakisonga mbele kama kitu kimoja, chini ya uongozi wa Nguvu moja, kwa ajili ya kutimiza kusudi moja, wangeupindua ulimwengu. - {9T 221.1}

Kanuni zinazopaswa kutuchochea tukiwa wafanyakazi katika kazi ya Mungu ziliwekwa na mtume Paulo. Yeye anasema: "Sisi ni watenda kazi pamoja na Mungu." 1 Wakorintho 3:9. “Lolote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo kama kwa Bwana, si kwa wanadamu.” Wakolosai 3:23. Naye Petro anawasihi waumini: “Kila mmoja kwa kadri alivyoipokea Karama itumieni kwa kuhudumiana, kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu. Mtu akinena na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu, ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo.” 1 Petro 4:10, 11-{9T 221.2}

Kuna sheria kuu zinazotawala ulimwengu wa asili, na mambo ya kiroho hutawaliwa na kanuni za namna sawa. Njia za mwisho lazima zitumike, ikiwa matokeo yanayotarajiwa yanatarajiwa kufikiwa. Mungu amemwekea kila mtu kazi

yake kadiri ya uwezo wake. Ni kwa elimu na mazoezi kwamba watu wawe na sifa za kukidhi dharura yoyote inayoweza kujitokeza; na mipango ya busara inahitajika kuweka kila mmoja katika nyanja/duru yake sahihi, ili aweze kupata uzoefu ambao utamfaa kubeba jukumu. {9T 221.3}

Mungu anataka tusaidiane sisi kwa sisi kwa kudhihirisha huruma na upendo usio na ubinafsi. Kuna wale ambao wamerithi hasira na tabia tofauti. Wanaweza kuwa vigumu kukabiliana nao; lakini Je, sisi hatuna dosari? Hawapaswi kukatishwa tamaa. Makosa yao hayapaswi kufanywa kuwa bidhaa ya kila mtu kujua habari zake. Kristo huwahurumia na kuwasaidia wanaokosea katika kuamua. Aliteseka hadi kifo kwa ajili ya kila mtu, na kwa sababu hii Yeye ana shauku ya kina inayogusa kila mtu. {9T 222.1}.

Mwanadamu anaweza kuwa anajaribu kumtumikia Mungu, lakini majaribu kutoka ndani na nje yanamshambulia. Shetani na Malaika zake humhimiza/humsukuma na kumshawishi kuasi. Bila kutarajia anaanguka katika mawindo ya vishawishi vyao. Jinsi gani basi ndugu zake wanavyomtendea? Je, wanazungumza maneno makali, yenye kuumiza, wakimpeleka mbali zaidi na Mwokozi? Ni jambo gani baya kwa Kristo na Malaika kulitazama? { 9T 222.2}

Hebu tukumbuke kwamba tunajitahidi na kuanguka, tukishindwa katika maneno na matendo kumwakilisha Kristo, tukianguka na kuinuka tena, tukikata tamaa na kuwa na matumaini. Tujihadhari na kushughulika bila fadhili na wale ambao, kama sisi wenyewe wako chini ya majaribu na ambao, kama sisi pia, ni walengwa wa upendo usioshindwa wa Kristo. – {9T 222.3}.

Mungu hushughulika na wanadamu kama viumbe wanaowajibika. Atafanya kazi kwa Roho Wake kupitia nia aliyoiweka kwa mwanadamu ikiwa mwanadamu atampa tu nafasi ya kufanya kazi na atatambua utendaji Wake. Anamtengeneza kila mmoja kutumia akili na dhamiri yake mwenyewe. Hajakusudia mtu mmoja kuwa kivuli cha mwingine, kutamka tu hisia za mwingine. {9T 222.4}

## SURA YA 25
## KUWAZINGATIA WATENDAKAZI WEUSI

Dini ya Biblia haitambui tabaka wala rangi. Inapuuza cheo, mali, na heshima ya kidunia. Mungu huwatambua watu kama watu. Kwake, tabia huamua thamani yao. Nasi tunapaswa kumtambua Roho wa Kristo kwa kila ambaye ndani yake anafunuliwa. Hakuna haja ya kuwa na aibu kuzungumza na mtu mweusi

mwaminifu katika mahali na hali yoyote au kumshika mkono. Yule anayeishi katika mazingira ambayo Kristo huishi atafundishwa kumhusu Mungu na atajifunza kumpa thamani Yake kwa wanadamu. {9T 223.1}

Watumishi wetu Weusi wanapaswa kuzingatiwa. Hili halijafanywa kila wakati. Hawa watu wanapaswa kutiwa moyo kupata ujuzi kamili wa Ukweli. Wanapaswa kujifunza jinsi ya kuwa na ufasaha katika kuwafundisha wengine Kweli. Na wanaposhiriki kwa uaminifu katika kazi wanapaswa kupokea ujira wao. Kumbuka kwamba lazima wapate mkate. {9T 223.2}

Bwana anatamani watu Wake wa Kaskazini wadumishe mtazamo mzuri kwa ndugu na dada weusi. Hatupaswi kuwa na haraka/harara katika kutafuta makosa kwao. Hatuwezi kutarajia wawe katika heshima yote kama wale ambao wamefurahia manufaa makubwa zaidi. Tunapaswa kukumbuka madhira ambayo watu weusi wameyapitia. Mazingira yao yamekuwa tofauti sana na mzingira ya watu weupe. Watu wa Kaskazini wameishi katika mazingira ya salama, safi zaidi ya maadili kuliko waliyokuwa nayo watu Weusi ya Kusini. Hatuwezi kutarajia kwamba, katika mambo yote, watakuwa thabiti na safi katika mawazo yao ya maadili. Kristo angekuwa duniani leo, angeifundisha jamii ya weusi kwa namna ambayo ingetushangaza. Anatutaka tukumbuke kwamba hata wale ambao wamekuwa na manufaa makubwa katika mambo mengi mara nyingi huumizwa ikiwa makosa yao yatagunduliwa isivyofaa na ikiwa maneno ya nasaha na mawaidha yatasemwa katika namna isiyo na huruma. {9T 223.3}

Wakati mambo ya asili yasiyotarajiwa yanapotokea miongoni mwa watu weusi, kumbuka kwamba Bwana anatamani utende kwa hekima ya mchungaji mwema. Kumbuka kwamba wema utatimiza mengi zaidi ya kukemea. Hebu ndugu na dada weusi waone kwamba ndugu zao wanawataka wafikie kiwango cha juu zaidi na kwamba wako tayari kuwasaidia. Na ikiwa katika baadhi ya mambo watu weusi hushindwa, usiwe mwepesi wa kuwahukumu na kuwatenganisha na kazi. {9T 224.1}

Haki kamili na isiyo na upendeleo inapaswa kuonyeshwa kwa jamii ya Weusi. Kristo anadai upole ya upole kutoka kwa watumishi wake kwa wanaoteseka, huruma kwa wanaotelekezwa, na kuwajali kwa ukarimu wenye makosa. -{9T 224.2}

Maskini hawajazuiliwa katika fursa ya kutoa. Wao, vile vile kama matajiri, wanaweza kufanya sehemu katika kazi hii. Somo ambalo Kristo alilitoa kuhusu senti mbili za mjane linatuonyesha kwamba matoleo madogo zaidi ya hiari ya maskini, yakitolewa kwa moyo wa upendo, yanakubalika sawa na michango mikubwa ya matajiri. Katika mizani ya Patakatifu, karama za maskini, zizonatoka kwa upendo kwa Kristo, hazichukuliwi kulingana na kiasi kilichotolewa, bali kulingana na upendo unaoichochea dhabihu. {9T 224.3}

## SURA YA 26
## MAHITAJI YA ENEO LA KIUTUME

Kwa miaka mingi Bwana amekuwa akiweka mbele ya watu Wake mahitaji ya kazi miongoni mwa watu weusi katika majimbo ya Kusini mwa Marekani. Giza la kimaadili la eneo hili, kwa lenyewe ni, ombi lenye nguvu kwa ajili ya utekelezaji wa ukarimu. Huko nyuma wengine wamefanya walichoweza kusaidia tawi hili la kazi

yetu, na wema wao umezaa matunda katika kuongoa roho nyingi. {9T 225.1}

Ingawa bado kuna mengi ya kufanywa kwa ajili ya watu weusi, tuna sababu ya kushangilia juu ya mwanzo mwema uliofanywa. Katika idadi ya hivi karibuni ya The Gospel Herald [1907] inaripotiwa kwamba"miaka kumi na tano iliyopita hakukuwa na zaidi ya Waadventista Wa sabato weusi ishirini kusini mwa Mason na mstari wa mpaka wa Dixon; lakini leo wako mia saba. Miaka kumi na miwili iliyopita kulikuwa na kanisa moja tu la watu weusi la Waadventista Wa Sabato; leo yapo hamsini, bila kuhesabu yale ya Afrika na Wahindi wa Magharibi… Zaka ya watu Weusi mwaka jana nchini Marekani ilifikia dola elfu tano; miaka kumi na tano iliyopita haikuwa zaidi ya dola hamsini." {9T 225.2}

Hebu na tumshukuru Mungu, ndugu na dada wapendwa, na tujipe moyo! Mungu anauweka wazi mkono Wake kufanya kazi kuu katika eneo hili la utumei ndani ya mipaka ya nchi yetu wenyewe. Sasa anawapa watu Wake fursa zisizo za kawaida za kueneza ujumbe kwa haraka huko Kusini. Tunapaswa hasa kuonesha roho ya fadhila wakati sadaka ya mwaka kwa ajili ya kusaidia ya kazi ya watu weusi itakapochukuliwa. Mungu ameweka tuamini kwa kutufanya kuwa mawakili wa mali na wa neema Yake kubwa; na sasa anatuelekeza kwa maskini na wanaoteseka na walioonewa, kwa roho zilizofungwa minyororo ya ushirikina na makosa, na kutuhakikishia kwamba tukiwafanyia wema hawa, atalikubali tendo kana kwamba tumemtendea Yeye Mwenyewe. “Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo sana,” anatangaza, “mlinitendea Mimi.” Mathayo 25:40. {9T 225.3}

Maelfu ya watu weusi Kusini wanaweza sasa kuinuliwa, na kuwa mawakala wa kibinadamu wa kuwasaidia wenzao, ikiwa wataweza kupokea msaada ambao Mungu anatuita sisi kuwapa. Makundi ya wanaume na wanawake katika eneo hili wanahisi umaskini wao mkubwa na hitaji lao la kuinuliwa. Na waalimu waaminifu watakapowafungulia Maandiko kama vile wayasomavyo, wakiuwasilisha Ukweli katika usafi wake wa asili giza litatoweka. Miale ang’avu ya nuru itaangaza juu ya nafsi itafutayo Ukweli. Na wakiwa na wale ambao wamekuwa na manufaa, uchunguzi wa karibu na wa akili utafanyika juu ya masomo ya Ukweli uliofunuliwa katika Maandiko. Wengi watafundishwa juu ya Mungu. Watajifunza moja kwa moja kutoka kwa Mwalimu Mkuu, na watakubali kwa furaha weli ambazo zitatakasa na kuinua. Sura ya maadili ya Mungu itarejeshwa katika nafsi, na wengi wataokolewa milele. {9T 226.1}

Ndugu na dada zangu wapendwa, Kristo sasa anawaambia ninyi: “Inueni macho yenu mkatazame eneo hili la Kusini.; kwa maana linahitaji wafanyakazi, wapandaji wa mbegu na wavunaji. Linahitaji mali zako kwa ajili ya matengenezo ya watenda kazi hawa." Neema ya Kristo haina kikomo, ni karama ya bure ya Mungu. Basi kwa

nini hawa watu waliopuuzwa wasiwe na baadhi ya matumaini na ujasiri na imani kupelekwa katika maisha yao? Kuna mwanga wa jua moyoni kwa wote watakaomkubali Kristo. Septemba, 1907. {9T 226.2}

## SEHEMU YA 7—KAZI YA UHURU WA DINI

[*Katika Hiki Kipengele, Sehemu Za Machapisho Machache Tu (Hapa Hayajachapishwa) Zimetolewa. Kwa Jambo Lingine, La Moja Kwa Moja Muhimu, Kuhusika Na Kazi Ya Uhuru Wa Dini, Tazama Shuhuda Kwa Kanisa, Gombo La 5, Uk. 449-454, 467-476, 711-720; Gombo La. 6, Uk. 394-410; Pia Pambano Kuu, Sura Ya 2, Uk 16, 25, 36, 38-40.]*

"Piga mbiu ya uhuru katika nchi yote kwa watu wote wanaoikaa."
"Basi iweni na busara kama nyoka, na kuwa watu wapole kama hua."
Mambo ya Walawi 25:10; Mathayo 10:16.

## SURA YA 27
## WAKATI WA KUJARIBIWA U MBELE YETU

Majira kujaribiwa yako mbele yetu. Inatuapasa sasa kutumia uwezo na karama zetu zote katika kuiendeleza kazi ya Mungu. Nguvu Bwana alizotupatia zitumike

kujenga, si kubomoa. Wale ambao wamedanganyika kwa ujinga hawatakiwi kubaki katika hali hii. Bwana anawaambia wajumbe wake: Nendeni na kuwaeleza hayo niliyosema, kwamba watasikia au kwamba hawataki kusikia. {9T 227.1}

Wakati u mbele yetu ambapo mateso yatakuja kwa wale wanaoitangaza Kweli. Hali ya mambo haibembelezi; hata hivyo, bila kujali hayo, tusiache juhudi zetu za kuwaokoa walio tayari kuangamia, ambao Mfalme Mkuu wa mbinguni alitoa uhai Wake wa thamani uwe fidia. Njia moja inaposhindikana, jaribu nyingine. Juhudi zetu zisiwe mfu na zisizo na zisizo na uhai. Maadamu maisha yamehifadhiwa, tufanye kazi kwa ajili ya Mungu. Katika zama zote za kanisa Wajumbe walioteuliwa na Mungu wameingizwa katika malaumu na mateso kwa ajili ya Ukweli. Lakini popote ambapo watu wa Mungu wanaweza kulazimika kwenda, ingawa, kama wanafunzi wapendwa, watatelekezwa kwenye visiwa vya jangwa, Kristo atajua walipo na atawaimarisha na kuwabariki, akiwajaza amani na furaha. {9T 227.2}

Hivi karibuni kutakuwa na taabu katika ulimwengu wote. Inampasa kila mtu kutafuta kumjua Mungu. Hatuna muda wa kuchelewa. Kwa bidii na juhudi ujumbe lazima utolewe: “Haya, kila aonaye kiu, njooni majini, na yeye asiye na fedha; njooni, nunueni mle; naam, njooni, nunueni divai na maziwa, bila fedha na bila thamani." Isaya 55:1. "Bwana asema hivi, Shikeni hukumu, mkatende haki, kwa maana wokovu Wangu u karibu kuja, na haki Yangu kufunuliwa. Heri mtu afanyaye haya, na mwanadamu ayashikaye sana; azishikaye Sabato asizivunje, auzuiaye mkono wake usifanye uovu wowote." Isaya 56:1, 2. {9T 228.1}

Upendo wa Mungu kwa kanisa Lake hauna kikomo. Utunzaji Wake juu ya urithi Wake haukomi. Yeye hana mateso ya kuja juu ya kanisa lakini kile ambacho ni muhimu kwa utakaso wake, wa sasa na wa milele. Atalitakasa kanisa Lake kama vile alivyolitakasa hekalu mwanzoni na mwishoni mwa huduma Yake duniani. Yote ambayo huleta juu ya kanisa katika majaribu na mitihani huja ili watu Wake wapate uchaji wa ndani zaidi nguvu ya kuubeba ushindi wa msalaba sehemu zote za dunia. Ana kazi kwa wote kuifanya. Lazima kuwepo na upanuzi na maendeleo ya daima. Kazi lazima ienee kutoka jiji hadi jiji, kutoka nchi hadi nchi, na kutoka taifa hata taifa, ikisonga mbele na juu, ikianzishwa, ikiimarishwa; na kuwekwa sawa. - {9T 228.2}

"Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu,… amejaa neema na kweli." Lakini wale ambao Kristo alikuja kuwaokoa, hawakumpokea. "Alikuja kwake, wala walio Wake hawakumpokea.” Yohana 1:14, 11. Wakijitoa wenyewe chini ya udhibiti wa Shetani, walimkataa Masihi na kutafuta nafasi ya kumwua. {9T 228.3}

Shetani na malaika zake waliazimia kufanya kifo cha Kristo kuwa aibu kadiri wawezavyo. Walijaza mioyo ya viongozi wa Kiyahudi kwa hisia za chuki kali dhidi ya Mwokozi. Wakidhibitiwa na adui, makuhani na watawala walichochea umati wa watu kumpinga Mwana wa Mungu. Mbali na tangazo la Pilato la kutokuwa na hatia Kwake, hakuna aliyenena neno kwa kwa faida Yake. Na hata Pilato, akijua kutokuwa na hatia Kwake, alimtoa kwenye unyanyasaji wa wanadamu chini ya udhibiti wa Shetani. {9T 229.1}

Matukio kama haya yatatokea hivi karibuni. Watu watainuka na kutekeleza kwa ukali sheria ambazo ziko kinyume cha sheria ya Mungu. Ingawa wana bidii katika kutekeleza amri zao wenyewe, watageuka kutoka katika Ukweli wazi wa "Hivi ndivyo asemavyo Bwana." Wakiinua siku ya mapumziko ya uwongo, watatafuta kuwalazimisha watu kuidharau sheria ya Yehova, nakala ya tabia Yake. Ingawa hawana hatia ya kufanya makosa, watumishi wa Mungu wataachiliwa ili kuteseka, kudhalilishwa na kunyanyaswa na wale ambao, wakiongozwa na roho wa Shetani, wamejawa na husuda na ubaguzi wa kidini.- {9T 229.2}

Mamlaka za kidini, wakidai kuungana na mbingu midomo, na kudai kuwa na sifa za mwana-kondoo, wataonyesha kwa matendo yao kwamba wana moyo wa joka na kwamba wanachochewa na kudhibitiwa na Shetani. Wakati unakuja ambapo watu wa Mungu watahisi mkono wa mateso kwa sababu wanashika siku takatifu ya saba. Shetani amesababisha mabadiliko ya Sabato kwa matumaini ya kutekeleza makusudi yake dhidi ya mipango ya Mungu. Anatafuta kufanya amri za Mungu kuwa na nguvu kidogo duniani kuliko sheria za binadamu. Mtu wa kuasi, ambaye alifikiria kubadili nyakati na sheria, na ambaye amewahi siku zote kuwatesa watu wa Mungu, atasababisha sheria zitungwe zinazolazimisha ushikaji wa siku ya kwanza ya juma. Lakini watu wa Mungu wanapaswa kusimama imara kwa ajili yake. Na Bwana atafanya kazi kwa niaba yao, akionesha wazi kwamba Yeye ni Mungu wa miungu. - {9T 229.3}

Bwana amesema: “Hakika mtazishika Sabato Zangu, kwa kuwa ni ishara kati ya Mimi na ninyi katika vizazi vyenu vyote.” Kutoka 31:13. Hakuna yeyote anayepaswa kuiasi amri Yake ili kuyaepuka mateso. Lakini hebu wote wayazingatie maneno ya Kristo: “Watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine”. Mathayo 10:23. Ikiwa yanaweza kuepukwa, msijitie wenyewe chini ya mamlaka ya watu wanaoendeshwa na roho ya mpinga Kristo. Kila kitu ambacho tunaweza kufanya kinapaswa kufanyika kwamba wale ambao wako tayari kuteseka kwa ajili ya Ukweli wanaweza kuokolewa kutoka katika dhuluma na ukatili. {9T 230.1} Kristo Ndiye kielelezo chetu. Azimio la mpinga-Kristo kutekeleza uasi aliouanzisha mbinguni litaendelea kufanya kazi katika watoto wa kuasi. Wivu wao na chuki yao dhidi ya wale wanaotii amri ya nne itazidi kuwa kali.

Lakini watu wa Mungu hawatakiwi kuificha bendera. Hawapaswi kupuuza amri za Mungu na, ili kuwa na wakati rahisi, kwenda na umati wa watu kutenda maovu. {9T 230.2}

Bwana huwatia moyo wote wanaomtafuta kwa moyo wote. Huwapa Roho Wake Mtakatifu, yaani udhihirisho wa uwepo Wake na neema. Lakini wale wanaomwacha Mungu ili kuokoa maisha yao wataachwa naye. Katika kutafuta kuokoa maisha yao kwa kuachilia Ukweli, wataupoteza uzima wa milele. {9T 230.3}

Usiku wa kujaribiwa unakaribia kuisha. Shetani anatenda kwa uwezo wake mkuu kwa sababu anajua kwamba wakati wake ni mfupi. Adhabu ya Mungu iko juu ya ulimwengu kuwaita wote waijuao Kweli wajifiche katika ufa wa Mwamba na kuutazama utukufu wa Mungu. Ukweli haupaswi kunyamazishwa sasa. Kauli za wazi lazima zitolewe. Ukweli unaodumu lazima usemwe, katika vipeperushi na majarida, na hivi lazima vitawanywe kama majani ya wakati wa kupukutisha/vuli. - {9T 230.4}

Kanisa la masalio litaletwa katika majaribu na dhiki kuu. Wale wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu watahisi hasira ya joka na majeshi yake. Shetani anahesabu ulimwengu kuwa mali yake, amepata udhibiti wa makanisa yaliyoasi; lakini hapa kuna kundi dogo linaloupinga ukuu wake. Kama angeweza kuwafuta kutoka duniani, ushindi wake ungekuwa kamili. Kama alivyoyashawishi mataifa ya kipagani ili kuwaangamiza Israeli, ndivyo, katika siku za usoni atazichochea nguvu mbaya za dunia kuwaangamiza watu wa Mungu. Wote watatakiwa kutoa utii kwa amri za wanadamu kwa kukiuka sheria ya kimbingu. Wale ambao watakuwa waaminifu kwa Mungu na wajibu watatishwa, watalaaniwa, na kupigwa marufuku. Watasalitiwa "na wazazi na ndugu, na jamaa, na marafiki." Luka 21:16. [SHUHUDA KWA KANISA, GOMBO. 5, UK. 472, 473.] {9T 231.1}

"Nisikilizeni, ninyi mjuao haki, watu ambao mioyoni mwenu mna sheria Yangu; msiogope matukano ya watu, wala msifadhaike kwa sababu ya dhihaka zao. Maana nondo itawala kama vazi; na funza atawala kama sufu; bali wokovu wangu utakuwa wa milele, na haki yangu haitatanguka."— Isaya 51:7, 8, 6. {9T 231.2}

## SURA YA 28
## KUFANYA KAZI SIKU YA JUMAPILI

Sanitarium, California, Agosti 17, 1902.

Ndugu Mpendwa: Nitajaribu kujibu swali lako kuhusu kile unachopaswa kufanya wakati sheria za Jumapili zikiwa zimelazimishwa. {9T 232.1}

Nuru niliyopewa na Bwana wakati tulipokuwa tunatazamia taabu kama mnavyoonekana kuliaribia, ilikuwa kwamba wakati watu waliposukumwa na nguvu kutoka chini ili kulazimisha maadhimisho ya Jumapili, Waadventista Wasabato walipaswa kuonesha hekima yao kwa kujiepusha na kazi zao za kawaida katika siku hiyo, wakijielekeza kwa ajili ya juhudi za umishionari. {9T 232.2}.

Kuziasi sheria za Jumapili kutaimarisha tu mateso ya wakereketwa wa mambo ya kidini wanaotafuta kuyatekeleza. Msiwape nafasi ya kuwaita ninyi wavunja sheria. Ikiwa wataachwa kuwashika na watu wasiomwogopa Mungu wala mwanadamu, uimarikaji wao punde utapoteza nguvu, na wataona kuwa hakuna maana wala haifai kwao kuwa wakali kuhusiana na utunzaji wa Jumapili. Endeleeni katika kazi yenu ya umishonari, mkiwa na Biblia zenu mikononi mwenu, na adui ataona kwamba amezidi kuwa mbaya kwa kusudi lake mwenyewe. Mtu yeyote hapokei alama ya mnyama kwa sababu anaonesha kwamba anatambua hekima ya kulinda amani kwa kujiepusha kufanya kazi zile ambazo zingelimletea mzozo, na kufanya kazi wakati huohuo ya umuhimu wa juu zaidi. {9T 232.3}

Tunapoitumia Jumapili kwa kazi ya umishionari, mjeledi utaondolewa mikononi mwa watu wakereketwa ambao wangefurahi kuwadhalilisha Waadventista Wa Sabato. Wanapoona tunajitoa wenyewe siku ya Jumapili katika kuwatembelea watu na kuyafungua Maandiko kwao, watajua kwamba haina maana kwao kujaribu kuzuia kazi yetu kwa kutunga sheria za Jumapili. {9T 232.4}

Jumapili inaweza kutumika kwa kuendeleza kazi mbalimbali ambazo zitatimiza mengi kwa ajili ya Bwana. Siku hii mikutano ya ndani na nje inaweza kufanyika. Kazi ya nyumba kwa nyumba inaweza kufanywa Wale wanaoandika wanaweza kuitumia siku hii kuandika makala zao. Inapowezekana, hebu mikutano ya dini ifanyike katika siku ya Jumapili. Fanyeni mikutano hii iwe ya kuvutia sana. Imbeni nyimbo nzuri za uamsho kwa unyofu, na hubirini kwa nguvu na hakika juu ya upendo wa Mwokozi. Hubirini juu ya kiasi na juu uzoefu wa dini ya Kweli. Hivyo mtajifunza mengi juu ya jinsi ya kufanya kazi, na mzitafikia roho nyingi. {9T 233.1}

Hebu walimu katika shule zetu waitoe Jumapili kwa ajili ya juhudi za kimishenari. Niliagizwa kuwa wakifanya hivyo watweza kuyashinda makusudi ya adui. Hebu walimu wawachukue wanafunzi pamoja nao kufanya mikutano kwa wale ambao hawaujui Ukweli. Hivyo watafanikisha mengi zaidi ya njia nyingine yoyote. {9T 233.2}

Mungu ametupa maelekezo ya wazi kuhusuiana na kazi yetu. Tunapaswa kuutangaza Ukweli kuhusiana na Sabato ya Bwana, ili kuweka wazi

uvunjaji/mpasukuko ambao umefanywa katika sheria yake. Tunapaswa kufanya yote tuwezayo kuwaangazia wale walio katika ujinga; lakini hatupaswi kamwe kushirikiana na watu wa ulimwengu ili tuweze kupokea msaada wa kifedha. {9T 233.3}

Tunasoma hivi kuhusu wana wa Israeli: "Basi nikawatoa katika nchi ya Misri, nikawaleta jangwani.Nikawapa amri Zangu, na kuwaonesha hukumu Zangu, ambazo mwanadamu ataishi kwazo, kama akizitenda. Tena naliwapa sabato Zangu ziwe ishara kati yao Mimi na wao, wapate kujua ya kuwa Mimi, BWANA, Ndimi niwatakasaye. Lakini nyumba ya Israeli waliniasi jangwani; hawakuenda katika amri Zangu, wakazikataa hukumu Zangu, ambazo mwanadamu ataishi kwazo kama akizitenda; na Sabato Zangu walizitia unajisi sana ndipo nikasema, Nitamwaga ghadhabu yangu juu yao jangwani, ili kuwaangamiza. {9T 233.4}

"Lakini nalitenda kwa ajili ya jina Langu, lisitiwe unajisi mbele ya mataifa, ambao naliwatoa mbele ya macho yao. Tena naliwainulia mkono Wangu jangwani, kwamba sitawaingiza katika nchi ile niliyokuwa nimewapa, ijaayo maziwa na asali, ambayo ni fahari ya nchi zote; kwa sababu walizikataa hukumu Zangu, wala hawakuenenda katika amri Zangu, wakazitia unajisi sabato Zangu; kwa maana mioyo yao ilifuata sanamu zao. Lakini jicho Langu likawahurumia nisiwaangamize, wala sikuwakomesha kabisa jangwani. Kisha nikawaambia watoto wao jangwani, Msiende katika amri za baba zenu, wala msizishike hukumu zao, wala msijitie unajisi kwa vinyago vyao; Mimi NI BWANA, Mungu waenu; endeni katika amri Zangu, na kuzishika hukumu Zangu, na kuzitenda; zitakaseni Sabato Zangu; zitakuwa ishara kati ya Mimi na ninyi, mpate kujua ya kuwa Mimi ndimi BWANA, Mungu wenu." Ezekieli 20:10-20. {9T 234.1}

Sabato ni kipimo cha Bwana, na hakuna mtu, awe mfalme, kuhani, au mtawala, aliye na mamlaka ya kuingilia kati ya Mungu na mwanadamu. Wale wanaotafuta kuwa juu ya dhamiri za wanadamu wenzao, wanajiweka juu ya Mungu. Wale walio chini ya msukumo wa dini ya uongo, wanaoadhimisha siku ya pumziko isiyo ya kweli, watauweka kando ushahidi chanya zaidi kuhusiana na Sabato ya Kweli. Watajaribu kuwalazimisha watu kutii sheria zilizotengenezwa na wao wenyewe, sheria ambazo zinapingana moja kwa moja na sheria ya Mungu. Juu ya wale ambao wanaendelea katika jambo hili, ghadhabu ya Mungu itamwagwa. Isipokuwa wakibadilika, hawawezi kuikwepa adhabu. {9T 234.2}

Sheria ya utunzaji wa siku ya kwanza ya juma ni kutoka kwa Jumuiya ya Wakristo walioasi imani. Jumapili ni mwana wa upapa, aliyeinuliwa na ulimwengu wa Kikristo juu ya siku ya pumziko takatifu la Mungu. Hakuna sababu ya watu wa Mungu kuipa heshima. Lakini natamani waelewe kwamba hawafanyi yaliyo mapenzi ya Mungu wanapoinua upinzani wakati anapowataka waepuke. Hivyo wanaufanya ubaguzi kuwa mkali sana kiasi kwamba haiwezekani kuutangaza Ukweli. Usifanye maandamano siku ya Jumapili kinyume cha sheria. Kama hili

linafanyika mahali fulani, na mnafedheheshwa, jambo lile lile litafanyika mahali pengine. Tunaweza kuitumia Jumapili kama siku ya kuendeleza kazi ambayo itasema upande wa Kristo. Tunapaswa kufanya kwa ubora wetu, tukifanya kazi kwa upole wote na unyenyekevu. {9T 235.1}

Kristo aliwaonya wanafunzi Wake kuhusiana na kile ambacho wangekutana nacho katika kazi yao kama wainjilisti. Alijua mateso yao yangekuwaje, majaribu na magumu gani wangeitwa kubeba. Asingeweza kuwaficha ujuzi wa yale watakayokumbana nayo, isije shida ikaja bila kutarajia, ikaitikisa imani yao.
Nimewaambia kabla halijatokea," Yeye alisema, ", kusudi litakapotokea, mpate kuamini." Yohana 14:29. Imani yao ilipaswa kuimarishwa, badala ya kudhoofika; kwa kuja kwa jaribu. Watakuwa wakiambiana: "Alituambia kwamba hili litakuja, na tunayopaswa kufanya ili kulikabili." {9T 235.2}

"Angalieni," Kristo alisema, "nawatuma kama kondoo kati ya mbwa-mwitu; basi iweni na busara kama nyoka, na wapole kama hua." "Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina Langu; lakini mwenye kuvumilia hata mwisho ndiye atakayeokoka." Mathayo 10:16, 22. Walimchukia Kristo bila sababu. Je! Ni ajabu kuwachukia wale wanaoibeba alama Yake, wanaomtumikia? Wanahesabiwa kama uchafu katika nchi. {9T 235.3}

"Lakini watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine." Sio mapenzi ya
Mungu kwamba maisha yako yatolewe sadaka kizembe. "Kwa maana ni Kweli nawaambia, Hamtaimaliza miji ya Israeli hata ajapo Mwana wa Adamu." Fungu la 23. {9T 236.1}

Ni lazima watu wapewe Ukweli, Kweli ulionyooka, na chanya. Lakini Ukweli huu unapaswa kuwasilishwa katika roho ya Kristo. Tunapaswa kuwa kama kondoo kati ya mbwa-mwitu. Wale wasiotaka, kwa ajili ya Kristo, kushika maonyo aliyotoa, ambao hawatakuwa na subira na kujizuia, watapoteza nafasi za thamani za kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Bwana hajawapa watu Wake kazi ya kukosoa kwa hasira wale wanaovunja sheria Yake. Kwa vyovyote vile hatupaswi kufanya mashambulizi kwa makanisa mengine. Hebu tukumbuke kwamba, kama watu waliokabidhiwa Ukweli mtakatifu, tumekuwa wazembe na wasio waaminifu. Kazi imekuwa ya kwenye vituo vichache hadi watu wamekuwa wagumu wa injili. Ni vigumu kuwavuta wale ambao wameusikia Ukweli mara nyingi, na bado wakaukataa… {9T 236.2}

Haya yote yapo kinyume chetu sasa. Laiti tungeweka juhudi za dhati kuwafikia wale ambao, kama wangeongolewa wangetoa ushuhuda halisi wa kile ambacho Ukweli wa sasa ungefanya kwa wanadamu, kazi yetu ingekuwa imeendelea kiasi gani sasa. Sio vema kwamba maeneo machache yawe kuwa na manufaa makubwa wakati maeneo mengine yamepuuzwa. - {9T 236.3}

Katika shule yetu ya Avondale, karibu na Cooranbong, Australia, swali la kufanya kazi Jumapili lilikuja kwa ajili ya kuamualiwa. Ilionekana kana kwamba mistari

ingechorwa hivi karibuni sana kutuhusu ili kwamba tusifanye kazi siku ya Jumapili. Shule yetu ilikuwa katikati ya msitu, mbali na kijiji chochote au kituo cha gari moshi. Hakuna mtu aliyekuwa akiishi karibu nasi kiasi cha kusumbua kwa njia yoyote ile tunayoweza kufanya. Hata hivyo, bado tulikuwa tukittupiwa jicho. Maafisa waliagizwa kuja na kutukagua majengo yetu, na walikuja. Wangeweza kuona mambo mengi kama wangetaka kutushtaki, lakini hawakubahatika kuona waliokuwa kazini. Walikuwa na imani kubwa kwetu kama watu, na heshima kubwa sana kwetu kwa sababu ya kazi tuliyoifanya katika jumuiya hiyo, kwamba waliamini wanaweza kutuamini popote pale. {9T 236.4}

Wengi walitambua ukweli kwamba jumuiya nzima ilikuwa imebadilishwa tangu tuende huko. Mwanamke ambaye hakuwa Msabato akaniambia: "Huwezi kuamini nikikujulisha kikamilifu kuhusu mabadiliko ambayo yametokea katika jumuiya hii kama matokeo ya kuhamia kwenu hapa, mkianzisha shule, na kufanya mikutano hii midogo." {9T 237.1}

Kwa hiyo ndugu zetu walipotishwa na mateso na kutupwa katika mashaka kuhusiana na wafanye nini, ushauri uleule ulitolewa kama ulivyotolewa katika kujibu swali linalohusu michezo. Nilisema: "Tumieni Jumapili katika kufanya kazi ya umishionari kwa ajili ya Mungu. Walimu, nendeni na wanafunzi wenu. Wachukueni waingie msituni [hizi ndizo tulizoziita wilaya zisizo na makazi mengi msituni, ambapo nyumba ziko umbali wa maili moja au mbili], na kuwatembelea watu majumbani mwao. Wajulishe kuwa unavutiwa na wokovu wa nafsi zao." Walifanya hivyo, na, kama matokeo, wakafaidika sana wenyewe na kuweza kuwasaidia wengine pia. Baraka ya Mungu ikatulia juu yao walipochunguza Maandiko kwa bidi katika ili kujifunza jinsi ya kuwasilisha Kweli za Neno kwa njia ambayo Kweli hizi zingepokelewa kwa upendeleo. Agosti 20, 1903. - {9T 237.2}

Wakati fulani wale waliokuwa wasimamizi wa shule yetu huko Avondale waliniuliza, wakisema: "Tutafanye nini? maofisa wa sheria wameagizwa kuwakamata wale wanaofanya kazi siku ya Jumapili." Niliwajibu hivi: "Itakuwa ni rahisi sana kuuepuka ugumu huo. Itoeni Jumapili kwa Bwana kama siku ya kufanya kazi ya kimishionari. Wachukueni wanafunzi wakafanye mikutano katika sehemu mbalimbali, na kufanya kazi ya umishenari wa njia ya uganga. Watakutana na watu katika majumba yao na hapo watata nafasi nzuri ya kuuwasilisha ukweli. Kutumia siku ya Jumapili kwa njia hii ni jambo linalokubalika mbele za Bwana." {9T 238.1}

Tunapaswa kufanya yote tuwezayo ili kuondoa ubaguzi uliomo katika akili za wengi dhidi ya kazi yetu na dhidi ya Sabato ya Biblia. - {9T 238.2}

Wafundishe watu kupatana katika mambo yote na sheria za nchi yao wakati wawezapo kufanya hivyo bila kuwa kinyume na sheria ya Mungu. - {9T 238.3}

Wakati fulani mioyo ya watesi inaweza kuathiriwa na hisia za mbingu kama ilivyokuwa moyo wa mtesi mtume Paulo kabla ya kuongoka kwake. {9T 238.4}

## SURA YA 29

## MANENO YA TAHADHARI

Kristo aliwaambia wanafunzi Wake: “Tazama, mimi nawatuma kama kondoo kati ya mbwa-mwitu; kuweni wenye hekima kama nyoka, na wapole kama hua.” Mathayo 10:16. Mashambulizi ya Shetani dhidi ya watetezi wa Ukweli yatazidi kuwa machungu na ya kudhamiriwa hadi mwisho wa wakati. Kama katika siku za Kristo makuhani wakuu na watawala waliwachochea watu dhidi yake, ndivyo leo viongozi wa kidini watachochea uchungu na chuki dhidi ya Ukweli kwa wakati huu. Wananchi wataongozwa kwa vitendo vya unyanyasaji na upinzani ambavyo hawangefikiria kamwe kama hawangejazwa na uadui wa wale wanaodai kuwa Wakristo kinyume na Ukweli. {9T 239.1}

Watetezi wa Ukweli watafuata njia gani? Wana Neno la Mungu lisilobadilika, la milele, na wanapaswa kufichua Ukweli kwamba wana ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu. Maneno yao hayapaswi kuwa magumu na mkali. Katika uwasilishaji wao wa Ukweli lazima wadhihirishe upendo na upole na utu wa Kristo. Hebu Ukweli ufanye kazi ya kukata; Neno la Mungu ni kama upanga mkali, ukatao kuwili, nalo litakata njia yake ndani ya moyo. Wale wanaojua kuwa wanao Ukweli hawapaswi, kwa kutumia ukali na mkali maneno, kumpa Shetani nafasi moja ya kuwasilisha roho yao vibaya. {9T 239.2}

Kama watu lazima tusimame kama alivyofanya Mkombozi wa ulimwengu. Wakati wa pambano na Shetani kuhusiana na mwili wa Musa, Kristo hakuthubutu kuleta mashitaka dhidi yake. Alikuwa na kila uchochezi fanya hivi, na Shetani alikatishwa tamaa kwa sababu hangeweza kuamsha roho ya kulipiza kisasi ndani ya Kristo. Shetani alikuwa tayari kutafsiri vibaya kila kitu kilichofanywa na Yesu; na Mwokozi hangempa nafasi, si ya kufanana na udhuru. Hangegeuka kutoka kwa njia Yake iliyonyooka ya ukweli ili kufuata mambo ya Shetani ya kutangatanga, kupinda na kugeukageuka na ya kuhatarisha. {9T 239.3}

Tunasoma katika unabii wa Zekaria kwamba wakati Shetani pamoja na sinagogi lake lote waliposimama ili kuyapinga maombi ya Yoshua kuhani mkuu, na kumpinga Kristo, ambaye alikuwa karibu kuonyesha upendeleo kwa Yoshua: "Bwana akamwambia Shetani, Bwana na akukemee, Ewe Shetani; naam, Bwana uliyechagua Yerusalemu na akumeee; je! hiki si kinga kilichotolewa motoni? {9T 24.1}

Njia ya Kristo katika kushughulika hata na adui wa roho inapaswa kuwa kielelezo kwetu katika kuchangamana kwetu kote na wengine ili isilete mashtaka ya matusi dhidi ya yoyote; hatupaswi kutumia ukali kwa wale ambao wana shauku ya kuijua njia sahihi kama sisi wenyewe tulivyo. {9T 240.2}

Wale ambao wameelimishwa katika Kweli kwa kanuni na mfano wanapaswa kufanya juhudi kubwa kwa wengine ambao hawana ujuzi wa Maandiko isipokuwa kwa njia ya tafsiri zilizotolewa na watumishi na washiriki wa kanisa, na ambao wamepokea mapokeo na hekaya kama ukweli wa Biblia. Hushangazwa na uwasilishaji wa Ukweli, ni kama ufunuo mpya kwao, na hawawezi kustahimili kuwa na Ukweli wote, katika tabia yake ya kuvutia zaidi, iliyowasilishwa kwao mwanzoni. Yote ni mpya na ya mageni, na kinyume kabisa na yale waliyoyasikia kutoka kwa watumshi wao; na wameelekea kuamini yale watumishi waliyowaambia--kwamba Waadventista Wa Sabato ni makafiri na hawaiamini Biblia. Hebu na ile Kweli iwasilishwe kama ilivyo katika Yesu, mstari kwa mstari, kanuni juu ya kanuni, huku kidogo na huku kidogo. {9T 240.3}

Hebu wale wanaoandika kwa karatasi zetu wasifanye misukumo isiyo ya fadhili na ambayo hakika litaleta madhara na kwamba itafunga njia na kutuzuia kufanya kazi ambayo tunapaswa kufanya ili kufikia matabaka yote, Wakatoliki wakiwemo. Ni kazi yetu kusema ukweli kwa upendo na sio kwa kuuchanganya na mambo ambayo hayajatakaswa ya moyo wa asili na kusema mambo ambayo yana ladha ya roho ile ile inayomilikiwa na adui zetu. Misukumo yote mikali itarudi juu yetu kwa kipimo maradufu wakati nguvu iko kwenye mikono ya wale wanaoweza kuitumia kwa ajili kudhuru. Mara kwa mara ujumbe umetolewa kwangu kwamba hatupaswi kusema Neno moja, kuchapisha sentensi moja, hasa kwa njia ya haiba, isipokuwa ni muhimu sana katika kuutetea ukweli, ambao utawachochea adui zetu dhidi yetu na kuamsha tamaa yao kuyeyuka. Kazi yetu itafungwa hivi karibuni, na hivi karibuni wakati wa taabu, ambayo haujawahi kuwepo, utatujia, ambayo hatuujui ila kidogo tu. {9T 240.4}.

Bwana anataka watenda kazi Wake wamwakilishe Yeye, Mtendakazi Mkuu wa Umisionari. Udhihirisho wa harara siku zote huleta madhara. Sifa muhimu kwa maisha ya Kikristo lazima zijifunzwe kila siku katika shule ya Kristo. Yeye mwenye kutojali na kughafilika katika kutamka maneno au kuandika maneno ya kuchapishwa kutumwa kutangazwa ulimwenguni, kutuma matamshi ambayo hayawezi kurudishwa tena, ndivyo hujinyima kustahili kukabidhiwa kazi takatifu ambayo inawahusu wafuasi wa Kristo kwa wakati huu. Wale wanaojizoeza kutoa misukumo mikali wanatengeneza mazoea ambayo yataimarika kwa kurudia-rudia na itabidi yatubiwe. {9T 241.1}

Tunapaswa kuchunguza kwa uangalifu njia zetu na roho zetu, na kuona ni kwa namna gani tunafanya kazi tuliyopewa na Mungu, ambayo inahusisha hatima ya roho. Wajibu wa juu kabisa uko juu yetu. Shetani imesimama tayari, amekasirika sana kuhamasisha mawakala wote wa kishetani, ili awafanye waungane na watu

waovu na kuleta juu ya waaminio Ukweli mateso makali na ya haraka. Kila neno lisilo la busara linalotamkwa kupitia kwa ndugu zetu litakuwa hazina juu na mkuu wa giza. {9T 241.2}

Ningependa kuuliza: Je! ni kwa jinsi gani akili za kibinadamu zenye kikomo zinathubutu kuongea maneno ya hovyo na ya kijasiri yatayoziamsha nguvu za kuzimu dhidi ya watakatifu wa Mungu, wakati Malaika Mkuu Mikaeli hakuthubutu kuleta mashtaka dhidi ya Shetani ya kutukana, bali akasema: “Bwana na akukemee”? Yuda 9. {9T 242.1}.

Haitawezekana kwetu kuepuka magumu na mateso. Yesu alisema: “Ole ni wa ulimwengu kwa sababu ya mambo ya kukosesha! maana hayana budi kuja mambo ya kukosesha; lakini ole wake mtu yule aliletaye jambo la kukosesha! “Mathayo 18:7. Lakini kwa sababu machukizo yatakuja, ni lazima tuwe waangalifu tusichochee mambo tabia ya asili ya wale wasiopenda Ukweli, kwa maneno yasiyo ya hekima na udhihirisho wa roho isiyo na fadhili. {9T 242.2}

Ukweli wa thamani lazima uwasilishwe kwa nguvu yake ya asili. Makosa ya udanganyifu ambayo yameenea, na yanayoongoza ulimwengu kuwa mateka, yanapaswa kufunuliwa. Kila juhudi inafanywa ili kunasa watu wenye mawazo ya hila, ili wawageuze kutoka kwenye kweli na kuzigeukia hadithi za uongo na kuwatayarisha kudanganywa, kwa udanganyifu mkuu. Lakini wakati nafsi hizi zilizodanganyika zinageuka kutoka kwenye Ukweli na kwenda kwenye upotofu, msiseme nazo neno moja la kukemea. Tafuta kuwaonyesha hawa watu maskini, waliodanganyika hatari yao na kuwafunulia jinsi gani Mwenendo wao kuelekea Yesu Kristo ulivyo wa huzuni; lakini yote yafanyike kwa huruma. Kwa namna ya kazi ifaayo baadhi ya nafsi zilizonaswa na Shetani zinaweza kurejeshwa kutoka katika nguvu yake. Lakini usiwalaumu na kuwahukumu. Kukejeli msimamo unaoshikiliwa na wale walio katika makosa haitawafumbua macho yao yaliyopofuka wala kuwavuta kwenye Ukweli. {9T 242.3}

Wanadamu wanapopoteza mwelekeo wa kielelezo cha Kristo na kutoiga namna Yake ya kufundisha, hujikuta wakijitosheleza na kwenda kukutana na shetani wakiwa na na silaha zake. Adui anajua vizuri jinsi ya kugeuza silaha zake kwa wale wanaozitumia. Yesu alizungumza maneno ya ukweli tupu, safi na haki. {9T 243.1}

Iwapo kuna watu walihitaji kutembea kwa unyenyekevu mbele za Mungu, ni kanisa Lake, wateule Wake katika kizazi hiki. Sote tunahitaji kuombolezea ubutu wa uwezo wetu wa kiakili, kushindwa kuthamini upendeleo na fursa zetu. Hatuna la kujivunia. Tunamhuzunisha Bwana Yesu Kristo kwa ukali wetu, kwa misukumo

yetu isiyo kama ya Kristo. Tunahitaji kuwa wakamilifu ndani Yake. {9T 243.2}

Ni kweli tumeamriwa "piga kelele usiache, usiache, paza sauti yako kama tarumbeta: uwahubiri watu Wangu kosa lao, na nyumba ya Yakobo dhambi zao." Isaya 58:1. Ujumbe huu lazima uweze kutolewa; lakini ingawa ni lazima utolewe, tunapaswa kuwa waangalifu tusiwalazimishe na kuwakusanya watu na kuwahukumu wale ambao hawana nuru tuliyo nayo sisi. Hatupaswi kwenda katika njia yetu kufanya misukumo migumu kwa Wakatoliki. Miongoni mwa Wakatoliki kuna wengi ambao ni Wakristo waangalifu na ambao hutembea katika nuru yote inayowaangazia, na Mungu atafanya kazi kwa niaba yao. Wale ambao wamekuwa na upendeleo mkubwa na fursa, na ambao wameshindwa kuendeleza nguvu zao za kimwili, kiakili, na kimaadili, lakini ambao wameishi ili kujifurahisha wenyewe na wamekataa kubeba wajibu wao, wako katika hatari kubwa zaidi na kuwa katika hukumu kubwa mbele za Mungu kuliko wale walio katika upotofu juu ya mambo ya mafundisho, lakini ambao wanatafuta kuishi ili kuwatendea wengine mema. Usiwashutumu wengine; wala usiwahukumu. {9T 243.3}

Tukiruhusu mawazo ya ubinafsi, mawazo yasiyo ya kweli, na visingizio vya uwongo vitulete katika hali ya upotovu wa akili na moyo, ili tusijue njia na mapenzi ya Mungu, tutakuwa na hatia zaidi kuliko mwenye dhambi aliye wazi. Tunahitaji kuwa waangalifu sana ili tusiwahukumu wale ambao, mbele ya Mungu, wana hatia kidogo kuliko sisi wenyewe. - {9T 243.4}

Hebu kila mtu akumbuke kwamba sisi hatupaswi kukaribisha mateso. Hatupaswi kutumia ukali na maneno ya kuumiza. Yaweke mbali ya kila nakala iliyoandikwa, yaondoe nje ya kila anwani iliyotolewa. Hebu Neno la Mungu liweze kukata, na kukemea; hebu watu wenye kikomo wajifiche na wakae ndani ya Yesu Kristo. Hebu roho ya Kristo ionekane. Hebu wote walindwe katika maneno yao, wasije wakawaweka wale wasio wa imani yetu katika upinzani wa mauti dhidi yetu na kumpa Shetani nafasi ya kutumia maneno ambayo hatujashauriwa kuifunga njia yetu. - {9T 244.1}

Kutakuwa na wakati wa taabu ambao haujawahi kutokea tangu kuwepo kwa taifa. Kazi yetu ni kujifunnza kuondoa katika mijadala yetu yote kila kitu ambacho kina ladha ya kulipiza kisasi na ukaidi na kuwa kinyume dhidi ya makanisa na watu binafsi, kwa sababu hii siyo njia na mbinu ya Kristo. - {9T 244.2}

Ukweli kwamba watu wa Mungu, ambao wanaujua Ukweli, wameshindwa kutekeleza wajibu wao kulingana na nuru iliyotolewa katika Neno la Mungu hutufanya sisi kuwa waangalifu zaidi, ili tusiwakwaze wasioamini. kabla hawajasikia sababu za imani yetu kuhusu Sabato na Jumapili. {9T 244.3}

## SEHEMU YA 8—MASHAURI KWA WAKATI

Tazama, Naja upesi; Shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako.” Ufunuo 3:11.

# SURA YA 30
# UWAKILI MWAMINIFU

*[Makala Hii Ilisomwa Mbele Ya Wajumbe Kwenye Mkutano Kwenye Jimbo La San Jose (California)., Januari, 1907.]*

Kristo ametununua kwa bei ya damu Yake mwenyewe. Amelipa gharama ukombozi wetu, na ikiwa tutaishikilia hazina, itkuwaa yetu kwa karama ya bure ya Mungu. {9T 245.1}

"Wawiwa nini na Bwana wangu?" Luka 16:5. Ni ngumu kusema. Yote tuliyo nayo hutoka kwa Mungu. Anaweka mkono Wake juu ya mali zetu, akisema: “Mimi Ndiye mmiliki halali wa ulimwengu wote; hizi ni mali Zangu. Niwekeeni wakfu zaka na dhabihu. Unapoleta mali hizi maalum kama Ishara ya uaminifu wako na kujisalimisha kwako kwa enzi Yangu, baraka yangu itakuzidishia mali yako. nawe utakuwa nayo tele." {9T 245.2}

Mungu anaijaribu kila nafsi inayodai kumwamini. Wote wamekabidhiwa vipaji. Bwana amewapa watu mali Zake wazitumie. Amewafanya mawakili Wake, na ameweka katika umiliki wao fedha, nyumba na mashamba. Haya yote yanapaswa kuhesabiwa kuwa ni mali ya Bwana na kutumika kuendeleza kazi Yake, kujenga ufalme Wake ulimwenguni. Katika kutumia mali ya Bwana, tunapaswa kumtafuta Yeye kwa ajili ya hekima Yake, ili tusitumie dhamana Yake takatifu kujitukuza wenyewe au kujiingiza katika misukumo ya kujitukuza nafsi. Kiasi kinachokabidhiwa kinatofautiana, lakini wale walio na karama ndogo zaidi hawapaswi kuhisi hivyo kwa sababu talanta yao ya mali ni ndogo, kwamba hawawezi kufanya chochote nayo. {9T 245.3}

Kila Mkristo ni wakili wa Mungu, aliyekabidhiwa mali yake. Kumbuka maneno:
"hapo tena inapohityajiwa katika mawakili ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu.” 1Wakorintho 4:2. Hebu na tuwe na hakika kuwa hatumwibii Mungu katika nodi au nukta zozote, kwani mengi yanahusika katika swala hili. {9T 246.1}
Vitu vyote ni vya Mungu. Wanadamu wanaweza kupuuza madai Yake. Huku akiwa amejaza baraka Zake kwao, wanaweza kutumia karama Zake kwa ajili ya kujiridhisha nafsi; lakini wataitwa kutoa hesabu kwa uwakili wao. {9T 246.2}

Wakili hujitambulisha mwenyewe na bwana wake. Hukubali majukumu ya uwakili, na ni lazima kuchukua nafasi ya bwana wake, akifanya kama bwana wake ambavyo angefanya. Nia ya bwana wake inakuwa yake. Nafasi ya wakili ni ya heshima kwa sababu bwana wake anamwamini. Ikiwa kwa njia yoyote anatenda

kwa ubinafsi na kugeuza faida iliyopatikana kwa kufanya biashara na mali ya bwana wake kwa faida yake mwenyewe, amepotosha imani iliyowekwa ndani yake. {9T 246.3}

Msaada wa Injili

Bwana amefanya utangazaji wa injili utegemee kazi na karama za hiari ya watu Wake wote. Yule anayetangaza ujumbe wa rehema kwa wanadamu walioanguka ana kazi nyingine pia—ya kuweka mbele za watu wajibu wa kuendeleza kazi ya Mungu kwa mali yao. Ni lazima awafundishe kwamba sehemu ya mapato yao ni ya Mungu na inapaswa kutolewa kwa utakatifu kwa kazi Yake. Somo hili linapaswa kuwasilishwa kwa maaandiko na mfano; anapaswa kujihadhari asije akafanya kwa tabia yake mwenyewe kupunguza nguvu ya mafundisho yake. {9T 246.4}

Kile ambacho kimetengwa kwa mujibu wa Maandiko kama ni mali ya Bwana huwa ni mapato ya injili na si yetu tena. Si bora zaidi ya kufuru kwa mtu kuchukua kutoka katika hazina ya Mungu ili kujitumikia mwenyewe au kutumikia wengine katika mambo yao ya kiulimwengu. Wengine wamekuwa na makosa katika kugeuza kutoka kwa madhabahu ya Mungu kile ambacho kimewekwa wakfu hasa Kwake. Wote wanapaswa kuzingatia suala hili katika nuru ya Kweli. Mtu yeyote, akiwa katika shida, asichukue pesa zilizowekwa wakfu kwa makusudi ya dini na kuitumia kwa faida yake, akijituliza dhamiri yake kwa kusema kwamba atalipa kwa wakati fulani ujao. Afadhali kupunguza matumizi ili kuendana na mapato, kujibana mahitaji, na kuishi kulingana na uwezo kuliko kutumia pesa za Bwana kwa madhumuni ya kilimwengu. {9T 246.5}

## Matumizi ya Zaka

Mungu ametoa mwongozo maalum kuhusu matumizi ya zaka. Hataki kwamba kazi Yake iwe kilema kwa kukosa mali. Ili pasiwe na kazi ya kubahatisha na isiyo na makosa, ameufanya wajibu wetu katika jambo hili kuwa wazi sana. Sehemu ambayo Mungu amejiwekea Mwenyewe haipaswi kuelekezwa kwa makusudi mengine yoyote zaidi ya yale aliyoyabainisha. Mtu yeyote asijisikie yuko huru kuhifadhi zaka yake, kuitumia kulingana na uamuzi wao wenyewe. Hawapaswi kuitumia kwa ajili yao wenyewe wakati wa dharura, wala kuitumia wanavyoona inafaa, hata katika kile wanachoweza kukiona kuwa kazi ya Bwana. {9T 247.1}

Mtumishi anapaswa, kwa kanuni na mfano, kuwafundisha watu kuiona zaka kuwa takatifu. Asihisi kwamba anaweza kuihifadhi na kuitumia kulingana na uamuzi wake mwenyewe kwa sababu yeye ni mtumishi. Sio yake. Hana uhuru wa kujitolea chochote anachofikiri ni haki yake. Hatakiwi kutoa ushawishi wake kwa mipango

yoyote ya kukengeusha kutoka kwenye matumizi halali ya zaka yao na matoleo yaliyowekwa wakfu kwa Mungu. Inapaswa kuwekwa kwa Mungu hazina iliofanyika takatifu kwa ajili ya utumishi Wake kama alivyoweka. {9T 247.2}

Mungu anatamani mawakili Wake wote wawe sawa katika kufuata mipango ya kimbingu. Hawapaswi kutibua mipango ya Bwana kwa kufanya baadhi ya misaada au kutoa zawadi au sadaka wakati au jinsi mawakala wa kibinadamu, watakavyoona inafaa. Ni sera mbaya sana kwa watu kutafuta kuboresha mpango wa Mungu, na kuvumbua mavumbuzi, wakiweka wastani wa misukumo yao mizuri juu ya tukio hili na lile, na kuyamaliza kinyume na matakwa ya Mungu. Mungu anawaita wote kutoa ushawishi wao kwa ajili ya mipango Yake Mwenyewe. Ameufanya mpango Wake ujulikane, na wote ambao wangeshirikiana Naye lazima watekeleze mpango huu badala ya kuthubutu kujaribu kuuboresha. {9T 248.1}

Bwana akamwagiza Musa, kwa ajili ya Israeli, akisema, Nawe waamuru wana wa Israeli wakuletee mafuta ya zeituni ya kupondwa kwa ajili ya nuru, ili kuifanya ile taa kuwaka daima.” Kutoka 27:20. Hii ilipaswa kuwa sadaka ya daima, ili nyumba ya Mungu ijazwe inavyopaswa kwa ajili ya utumishi Wake. Watu wake leo wanapaswa kukumbuka kuwa nyumba ya ibada ni mali ya Bwana na kwamba inapaswa kutunzwa kwa uangalifu. Lakini fedha za kazi hii hazipaswi kutoka katika zaka. {9T 248.2}

Ujumbe ulio wazi sana, wa uhakika nimepewa kwa ajili ya watu wetu. Nimeamriwa kuwaambia kwamba wanafanya makosa katika kutumia zaka kwa vitu mbalimbali ambavyo, ingawa ni vyema kwa vyenyewe, siyo kitu ambacho Bwana amesema kwamba zaka inapaswa kutumika kwacho. Wale wanaotumia zaka hivi huondoka kutoka kaatika mpango wa Bwana. Mungu atahukumu kwa mambo haya. {9T 248.3}

Sababu moja ambayo zaka inaweza kutumika kwa madhumuni ya shule. Bado wengine wanafikiri kwamba watangazaji wa Neno na wainjilisti wanapaswa kuungwa mkono kutoka katika zaka. Lakini kosa kubwa hufanyika wakati zaka inatolewa kutoka kwa kitu ambacho inapaswa kutumika – kuwasaidia watumishi. Siku hizi kunapaswa kuwe watendakazi wenye sifa mia moja shambani ambapo sasa kuna mmoja tu. {9T 248.4}

### Wajibu Mzito

Zaka ni takatifu, iliyohifadhiwa na Mungu kwa ajili Yake Mwenyewe. Inapaswa kuletwa katika hazina Yake ili itumike kuwategemeza watenda kazi wa injili katika

kazi zao. Kwa muda mrefu Bwana ameibiwa kwa sababu wapo wale ambao hawatambui kwamba zaka ni sehemu ya Mungu iliyohifadhiwa. {9T 249.1}

Wengine hawajatosheka na wamesema: "Sitatoa tena zaka yangu; kwa maana sina imani na jinsi mambo yanavyosimamiwa katika kiini cha kazi." Lakini je!, utamwibia Mungu kwa sababu unafikiri usimamizi wa kazi sio sawa? Weka malalamiko yako, kwa usahili na kwa uwazi, katika roho sahihi, kwa nama zinazofaa. Peleka maombi yako ili mambo yarekebishwe na kuwekwa sawa; lakini usijiondoe katika kazi ya Mungu, na kujionesha usivyo mwaminifu, kwa sababu wengine hawatendi sawa. {9T 249.2}

Soma kwa makini sura ya tatu ya Malaki na uone kile Mungu anachosema kuhusu zaka. Ikiwa makanisa yetu yatachukua msimamo wao juu ya neno la Bwana na kuwa waaminifu katika kulipa zaka zao katika hazina Yake, watendakazi wengi zaidi watahimizwa kuchukua kazi ya utumishi. Watu wengi zaidi wangejitoa kwenye huduma ikiwa wasingeambiwa kuhusu hazina iliyopungua. Kunapaswa kuwa na mali tele katika hazina ya Bwana, na kungekuwa na zaka kama mioyo na mikono yenye ubinafsi haingezuia au kuitumia ili kusaidia kazi zingine. {9T 249.3}

Rasilimali za Mungu zilizohifadhiwa hazipaswi kutumiwa kwa njia isiyo na mpangilio kama hiyo. Zaka ni ya Bwana, na wale ambao wanaiingilia wataadhibiwa kwa kupoteza hazina yao ya mbinguni isipokuwa wametubu. Hebu kazi isizuiliwe kwa sababu zaka imeelekezwa kwenye mikondo mbali mbali tofauti na ile ambayo Bwana hutaka ipelekwe. Maandalizi yanapaswa kufanywa kwa ajili ya aina hizi nyingine za kazi. Zinapaswa kutegemezwa, lakini si kutoka katika zaka. Mungu hajabadilika; zaka bado itatumika kwa ajili ya kusaidia utumishi. Ufunguzi wa maeneo mapya unahitaji ufanisi zaidi wa utumishi kuliko tulionao sasa, na hivyo lazima kuwe na mali kwenye hazina. {9T 249.4}

Wale wanaokwenda kama wahudumu wana jukumu zito linalowahusu jambo ambalo ni la ajabu kupuuzwa. Wengine hufurahia kuhubiri, lakini hawatoi kazi yao binafsi kwa makanisa. Kuna haja kubwa ya kufundishwa kuhusu wajibu kwa Mungu, hasa kuhusu kulipa zaka kwa uaminifu. Wahudumu wetu wangehuzunika kwa huzuni ikiwa hawangelipwa mara moja kwa kazi yao; lakini je, watafikiri kwamba lazima kuwe na chakula katika hazina ya Mungu ambayo inaweza kuwategemeza watendakazi? Ikiwa wakishindwa kutimiza wajibu wao wote katika kuwaelimisha watu kuwa waaminifu katika kumtolea Mungu iliyo yake, kutakuwa na uhaba wa mali katika hazina ili kuendeleza kazi ya Bwana. {9T 250.1}

Mwangalizi wa kundi la Mungu anapaswa kutimiza wajibu wake kwa uaminifu. Ikiwa anachukua nafasi ambayo kwa sababu haimpendezi, atamwachia mtu

mwingine afanye, yeye si mfanyakazi mwaminifu. Na asome katika Malaki maneno ya Bwana akiwashtaki watu kwa wizi kwa Mungu kwa kumnyima zaka. Mungu mwenye nguvu anatangaza: "Mmelaaniwa kwa laana." Malaki 3:9. Wakati mtu anayehudumu kwa Neno na mafundisho anaona watu wanafuata njia ambayo italeta laana hii juu yao, ni kwa vipi atapuuza wajibu wake wa kuwapa maagizo na onyo? Kila mshiriki wa kanisa anapaswa kufundishwa kuwa mwaminifu katika kulipa zaka kwa uaminifu. {9T 250.2}

“Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba Yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa majeshi, mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha au la.” Mstari wa 10. - {9T 251.1}

Ninaomba kwamba ndugu zangu watambue kwamba ujumbe wa malaika wa tatu una maana kubwa kwetu na kwamba kushika Sabato ya Kweli ni ishara inayowatofautisha wale wanaomtumikia Mungu na wale wasiomtumikia Yeye. Hebu wale ambao wamekuwa na usingizi na wasiojali, waamke. Tumeitwa kuwa watakatifu, na tunapaswa kuepuka kwa uangalifu kutoa mvuto ambao una maana ndogo iwapo tutabaki au hautabaki na sifa za kipekee za imani yetu. Juu yetu kuna wajibu wa thamani wa kuchukua msimamo thabiti zaidi wa Ukweli na haki kuliko tulivyochukua hapo awali. Mstari wa kuweka mipaka kati ya wale ambao wanazishika amri za Mungu na wasiozishika unapaswa kuwekwa kwa uwazi usio na shaka. Tunapaswa kumheshimu Mungu kwa uangalifu, tukitumia kwa bidii kila njia ya kutuweka katika uhusiano wa agano naye Yeye, ili tupokee baraka Zake—baraka muhimu sana kwa watu ambao wanapaswa kupimwa kwa ukali sana. Kutoa hisia kwamba imani yetu, dini yetu, haina nguvu inayotawala maishani mwetu ni jambo kubwa sana kumvunjia Mungu heshima. Hivyo tunageuka kutoka katika amri zake, ambazo ni maisha yetu, tukikana kwamba Yeye ni Mungu wetu na sisi tu watu Wake. {9T 251.2}

“BWANA, Mungu wako, Ndiye Mungu, Mungu mwaminifu, ashikaye agano Lake na rehema Zake kwao wampendao na kuzishika amri Zake hata vizazi elfu; naye huwalipa wamchukiao mbele ya uso wao, kuwaangamiza; hatakuwa mlegevu Kwake Yeye amchukiaye, atamlipa mbele ya uso Wake." Kumbukumbu la Torati 7:9, 10. {9T 251.3}

Tutakuwa wapi kabla ya vizazi elfu vilivyotajwa katika andiko hili kumalizika? Hatima yetu itakuwa imeamuliwa milele. Ama tutakuwa tumetangazwa kuwa tunastahili makazi katika ufalme wa milele wa Mungu au tutakuwa tumepokea hukumu ya kifo cha milele. Wale ambao wamekuwa wa kweli na waaminifu kwa agano lao na Mungu; wale ambao, wakiikumbuka Kalvari, wamesimama imara juu

ya mwamba upande wa Kweli, wanaojitahidi daima kumheshimu Mungu, watasikia pongezi: “Vema,mtumwa mwema na mwaminifu.” Lakini wale ambao wamemtolea Mungu utumishi wa moyo nusu tu, wakiruhusu maisha yao yafanane na njia na mazoea ya ulimwengu, watasikia maneno ya huzuni: "Ondokeni Kwangu; siwajui ninyi." {9T 252.1}

## SURA YA 31
## FAIDA

"Mheshimu Bwana kwa mali yako, na kwa malimbuko ya mazao yako yote; ndipo ghala zako zitakapojazwa kwa wingi, na mashinikizo yako yatafurika divai mpya." Mithali 3:9, 10. {9T 253.1}

"Kuna atawanyaye, lakini huongezewa zaidi; kuna azuiaye isivyo haki, lakini huelekea uhitaji. Nafsi ya mtu mkarimu itawandishwa, anyweshaye atanyweshwa mwenyewe." Mithali 11:24, 25. {9T 253.2}

"Muungwana huwaza mambo ya kiungwana, naye hushika sana mambo ya kiungwana." Isaya 32:8. {9T 253.3}

Hekima ya Kimbingu imeweka, katika mpango wa wokovu, sheria ya kutenda na kurejesha, kufanya kazi ya faida, katika nyanja zake zote, hubariki mara dufu. Anayetoa kwa wahitaji huwabariki wengine na ndivyo hujibariki kwa kiwango kikubwa zaidi. {9T 253.4}

### Utukufu wa Injili

Ili mwanadamu asipoteze matokeo yaliyobarikiwa ya ukarimu, Mkombozi wetu aliunda mpango wa kumweka kama mfanyakazi pamoja Naye. Mungu angeweza kufikia lengo Lake katika kuokoa wenye dhambi bila msaada wa mwanadamu, lakini alijua kwamba mwanadamu hangeweza kuwa na furaha bila kuchukua sehemu katika kazi hii kubwa. Kwa mlolongo wa mambo ambayo yangehitaji kujitoa kwake, humpa mwanadamu njia bora ya kutenda wema, na humfanya kuwa na mazoea ya kutoa kuwasaidia maskini na kuendeleza kazi Yake. Kwa ajili ya mahitaji Yake, ulimwengu ulioharibiwa unachota kutoka kwetu talanta za mali na za mvuto, ili kuwasilisha kwa wanaume na wanawake Ukweli, ambao wao wanaangamia wakiuhitaji. Na tunapotii wito huu, kwa kazi na kwa matendo ya ukarimu, tunafananishwa na sura Yake Yeye ambaye kwa ajili yetu alifanyika maskini. Katika kutoa tunabariki wengine na hivyo kujikusanyia utajiri wa kweli. {9T 253.5}

Ni utukufu wa injili kwamba ujengwe juu ya kanuni ya kurejesha katika jamii iliyoanguka sura ya Mungu kwa udhihirisho wa mara kwa mara wa wema. Kazi hii ilianzia katika nyua za mbinguni. Hapo Mungu aliwapa wanadamu ushahidi usio na shaka wa upendo ambao aliwachukulia nao. Bwana "aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee; bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16. Karama ya Kristo inaufunua moyo wa Baba. Inashuhudia kwamba, kwa kuuchukua ukombozi wetu, hatazuilia chochote, hata kama ni kizuri kiasi gani, ambacho ni muhimu katika kuikamilisha kazi Yake. {9T 254.1}

Roho ya ukarimu ni roho ya mbinguni. Upendo wa Kristo wa kujitoa unafunuliwa juu ya msalaba. Ili mtu apate kuokolewa, alitoa vyote alivyokuwa navyo kisha akajitoa Mwenyewe. Msalaba wa Kristo unavutia wema wa kila mfuasi wa Mwokozi aliyebarikiwa. Kanuni iliyoonyeshwa hapo ni kutoa, na kutoa. Hili, linapofanywa kwa wema na matendo mema, ni tunda la Kweli la maisha ya Kikristo. Kanuni ya walimwengu ni kupokea na, Kupokea tu, na kwa hivyo wanatarajia kupata furaha; lakini ilifanyika katika kuyabeba yote, matunda yake ni taabu na kifo. {9T 254.2}

Nuru ya injili inayoangaza kutoka katika msalaba wa Kristo inakemea ubinafsi na kuhimiza ukarimu na wema. Haipaswi kuwa na hoja ya kulalamila kuwa kuna ongezeko la wito wa kutoa. Mungu katika majaliwa Yake anawaita watu Wake kutoka katika nyanja zao zilizo na mipaka ya utendaji, kuingia katika shughuli kuu. Jitihada zisizo na kikomo zinahitajika wakati huu ambapo giza la maadili linaufunika ulimwengu. Wengi wa watu wa Mungu wako katika hatari ya kunaswa na mambo ya dunia na uchoyo. Wanapaswa kuelewa kwamba ni rehema Yake ndiyo inazidisha mahitaji ya mali zao. Vitu vinavyoita ukarimu katika vitendo lazima viwekwe mbele yao, au la hawawezi kuiga tabia ya Yule aliye Kielelezo kikuu. {9T 254.3}

## Baraka za Uwakili

Katika kuwaagiza wanafunzi Wake kwenda “ulimwenguni mwote, na kuihubiri Injili kwa kila kiumbe,” Kristo aliwapa wanadamu kazi ya kueneza ujuzi wa neema yake. Lakini wakati wengine huenda kuhubiri, huwaita wengine kujibu madai yake juu ya matoleo ambayo kwayo wanaweza kuunga mkono kazi katika nchi. Ameweka mali mikononi mwa wanadamu, ili karama Zake takatifu ziweze kutiririka kupitia njia za kibinadamu katika kufanya kazi alizotuteua katika kuwaokoa wenzetu. Hii ni moja ya njia za Mungu kumwinua mwanadamu. Ni kazi ambayo mwanadamu anaihitaji, kwani itachochea huruma ya ndani kabisa ya moyo wake na kutia katika utendaji uwezo wa juu wa akili. {9T 255.1}

Kila kitu kizuri cha dunia kiliwekwa hapa kwa mkono wa ukarimu wa Mungu kama onyesho la upendo wake kwa mwanadamu. Masikini ni Wake, na matendo ya dini ni Yake. Dhahabu na fedha ni za Bwana, Naye angeweza kuzinyesha kutoka mbinguni kama angechagua. Lakini badala ya haya amemfanya mwanadamu kuwa wakili wake, akimkabidhi mali, si ya kujilimbikizia, bali ya kutumika katika kuwanufaisha wengine. Hivyo humfanya mwanadamu kuwa mfereji wa kusambaza baraka Zake duniani. Mungu alipanga mfumo wa ukarimu ili mwanadamu awe kama Muumba Wake, mkarimu na asiye na ubinafsi katika tabia, na hatimaye awe mshiriki pamoja na Kristo wa thawabu tukufu ya milele.{9T 255.2}

## Kukutano karibu na Msalaba

Upendo ulioonyeshwa pale Kalvari unapaswa kuhuishwa, kuimarishwa, na kuenezwa miongoni mwa makanisa yetu. Je! hatutafanya yote tuwezayo ili kutoa uwezo kwa kanuni ambazo Kristo alizileta hapa duniani? Hatuendelei kujitahidi kuanzisha na kutoa ufanisi kwenye shughuli za ukarimu ambazo sasa zinahitajika bila kuchelewa? Unaposimama mbele ya msalaba na kumwona Mkuu wa mbinguni akifa kwa ajili yako, unaweza kuzuia moyo wako, ukisema: "Hapana; sina chochote cha kutoa"? {9T 256.1}

Watu wamwaminio wa Kristo wanapaswa kuudumisha upendo Wake. Upendo huu unapasqa kuwavuta pamoja karibu na msalaba. Ni kuwaondolea ubinafsi wote na kuwafungamanisha na Mungu na wao kwa wao. {9T 256.2}

Kutana karibu na msalaba wa Kalvari kwa kujitoa na kujizuia. Mungu atakubariki unapofanya kwa ubora wako. Unapokaribia kiti cha neema, unapojikuta umefungwa kwenye kiti hiki cha enzi kwa mnyororo wa dhahabu kushuka kutoka mbinguni hadi duniani ili kuwavuta watu kutoka kwenye shimo la dhambi, moyo wako utatoka na kupenda kwa ajili ndugu na dada zako ambao hawana Mungu na hawana tumaini katika ulimwengu. {9T 256.3}

## SURA YA 32
## ROHO YA KUJITEGEMEA

*[Makala Ilisomwa Mbele Ya Wajumbe Wa Mkutano Mkuu Wa Kanisa-Gc, Washington, D. C., Mei 30, 1909.]*

Kabla ya kuondoka Australia, na tangu nije katika nchi hii, nimeagizwa kuwa kuna kubwa kazi ya kufanywa Marekani. Wale waliokuwa kazini hapo mwanzo wanapita. Wachache tu miongoni mwa waanzilishi wa kazi sasa wamebaki kati yetu. Mizigo mingi mizito iliyobebwa na watu wenye uzoefu wa muda mrefu hapo awali sasa inawaangukia vijana. {9T 257.1}

Uhamisho huu wa majukumu kwa watendakazi ambao uzoefu wao ni mdogo unakabiliwa na hatari fulani ambazo tunapaswa kujilinda nazo. Ulimwengu umejaa ushundani wa ukuu. Roho ya kujiondoa kutoka kwa watendakazi wenzetu, roho ya kutokuwa na mipango, iko kwenye hewa tunayoipumua. Na kwa baadhi, juhudi zote za kuweka utaratibu zinachukuliwa kuwa hatari--kama kizuizi cha uhuru wa binafsi, na hivyo kuogopwa kama upapa. Nafsi hizi zilizodanganywa huona kuwa ni fadhila kujivunia uhuru wao wa kufikiri na kutenda kwa kujitegemea. Wanatangaza kwamba hawatakubali neno la mtu yeyote, kwamba hawamtegemei mtu yeyote. Nimeagizwa kwamba ni jitihada maalum za Shetani kuwaongoza wanadamu kuhisi kwamba Mungu anapendezwa na wao kuchagua njia yao wenyewe bila ya ushauri wa ndugu zao. {9T 257.2}

Hapa ndipo kuna hatari kubwa kwa usitawi wa kazi yetu. Lazima tuingie kwa busara, kwa utulivu, kupatana na maamuzi ya washauri wanaomcha Mungu; kwani katika njia hii pekee ndiko kuna usalama wetu na nguvu. Vinginevyo Mungu hawezi kufanya kazi nasi na kwa sisi na kwa ajili yetu. {9T 257.3}

Loo, jinsi Shetani angefurahi kiasi gani kama angeweza kufaulu katika jitihada zake za kuingia miongoni mwa watu hawa na kuitawanya/kuikoroga kazi katika wakati ambapo mfumo kamili ni muhimu na utakuwa nguvu kubwa ya kuweka nje maasi ya uongo na kukanusha madai ambayo hayajaidhinishwa na Neno la Mungu! Tunatakiwaa kushikilia kazi kwa usawa, kwamba hakutakuwa na

kuvunjwa kwa mfumo wa umoja na utaratibu ambao umejengwa kwa kazi ya busara, na makini. Ruhusa haipaswi kutolewa kwa vitu visivyo na utaratibu ambavyo vinatamani kudhibiti kazi kwa wakati huu. {9T 257.4}

Wengine wameendeleza wazo kwamba, tunapokaribia mwisho wa wakati, kila mtoto wa Mungu atachukua hatua bila ya mfumo wowote wa kidini. Lakini nimeagizwa na Bwana kwamba katika kazi hii hakuna kitu kama kila mtu kuwa huru. Nyota zote za mbinguni ziko chini ya sheria, kila moja ikivuta nyingine kufanya mapenzi ya Mungu, zikitoa utii wao wa pamoja kwa sheria inayotawala tendo lao. Na, ili kazi ya Bwana iendelee kwa uhai na uthabiti, ni lazima watu wake wajiunge pamoja. {9T 258.1}

Mienendo yenye kufanya na kuacha, kufanya na kuacha, yenye kufaa ya baadhi ya wanaodai kuwa Wakristo inawakilishwa vyema na kazi ya farasi wenye nguvu lakini wasio na mafunzo. Wakati mmoja anavuta mbele, mwingine anarudi nyuma, na kwa sauti ya bwana wao mmoja anavuta mbele na mwingine anasimama palepale. Kama watu hawatenda kwa umoja katika kazi hii kubwa na kuu kwa wakati huu, kutakuwa na mkanganyiko. Sio ishara nzuri wakati watu wanapokataa kuungana na ndugu zao na kupendelea kutenda peke yao. Hebu watendakazi wazingatie ujasiri wa ndugu ambao wako huru kuonyesha kila utengano kutoka kwenye kanuni sahihi. Ikiwa watu wanavaa nira ya Kristo, hawataweza kujitenga; watavuta pamoja na Kristo. {9T 258.2}

Wafanyakazi wengine huvuta kwa uwezo wote ambao Mungu amewapa, lakini bado hawajajifunza kuwa hawapaswi kuvuta peke yao. Badala ya kujitenga, hebu wapate kupatana na watenda kazi wenzao. Isipokuwa wamefanya hivi, shughuli zao zitafanya kazi kwenye wakati mbaya na kwa njia mbaya. Mara nyingi watafanya kazi kinyume na kile ambacho Mungu angefanya, na hivyo kazi yao ni mbaya zaidi kuliko upotevu. {9T 258.3}

## Umoja katika Utofauti

Kwa upande mwingine, viongozi miongoni mwa watu wa Mungu wanapaswa kujilinda na hatari ya kushutumu mbinu za watenda kazi binafsi ambao wanaongozwa na Bwana kufanya kazi maalum ambayo ni wachache wanaofaa kuifanya. Ndugu wenye wajibu wasiwe wepesi wa kukosoa mienendo ambayo haiendani kikamilifu na mbinu zao za kazi. Wasifikirie kwamba kila mpango unapaswa kuakisi utu wao wenyewe. Hebu wasiogope kuamini mbinu za wengine; kwa kuizuia imani yao kwa ndugu mtendakazi ambaye, kwa unyenyekevu na bidii iliyojiweka wakfu, anafanya kazi maalum kwa njia iliyowekwa na Mungu, ndivyo wanavyofanya kurudisha nyuma maendeleo ya kazi ya Bwana. {9T 259.1}

Mungu anaweza na atawatumia wale ambao hawajapata elimu kamili katika shule za wanadamu. Kulitia shaka Uwezo Wake wa kufanya hivi ni kudhihirisha kutokuamini; ni kuwekea mipaka uwezo mkuu wa Yule ambaye Kwake hakuna kisichowezekana. Oh, kwa sababu ya hili kutozingatiwa, tahadhari ya kutaomini! LInaacha nguvu nyingi sana za kanisa bila kutumika; inafunga njia ili Roho

Mtakatifu asiweze kuwatumia wanadamu; inawaweka katika kando wale walio tayari na wanaoambatana kufanya kazi katika namna ya Kristo; inakatisha tamaa ya kuingia kazini wengi ambao wangekuwa watenda kazi wazuri pamoja na Mungu kama wangepewa nafasi sawa. {9T 259.2}

Kwa nabii gurudumu ndani ya gurudumu, kuonekana kwa viumbe hai vilivyounganishwa nayo, vyote vilionekana vigumu na visiyoelezeka. Lakini Mkono wa hekima Isiyo na kikomo unaonekana kati ya magurudumu, na utaratibu mkamilifu ni matokeo ya kazi yake. Kila gurudumu, likiongozwa na mkono wa Mungu, hufanya kazi kwa upatanifu mkamilifu na kila gurudumu lingine. Nimeonyeshwa kuwa vyombo vya binadamu vinawajibika kutafuta sana nguvu na kujaribu kudhibiti kazi vyenyewe. Wanamwacha Bwana Mungu, Mtendakazi Mwenye Nguvu, kupita kiasi nje ya mbinu na mipango yao, na wala wasimtegemee Yeye kwa kila kitu kuhusiana na maendeleo ya kazi. Hakuna mtu anayepaswa kufikiria kwa muda kuwa ana uwezo wa kusimamia mambo ambayo ni ya mkuu, MIMI NIKO. Mungu katika majaliwa yake anatayarisha njia ili kazi ifanywe na mawakala wa kibinadamu. Kisha basi kila mtu asimame kwenye nafasi yake ya wajibu, kutenda sehemu yake kwa wakati huu na kujua ya kwamba Mungu Ndiye mkufunzi wake. {9T 259.3}

### Halmashauri kuu ya Kanisa (General Conference)

Mara nyingi nimeagizwa na Bwana kwamba uamuzi wa mtu yeyote usikabidhiwe kwa uamuzi wa mtu mwingine yeyote. Kamwe akili ya mtu mmoja au akili ya watu wachache isichukuliwe kuwa ya kutosha katika hekima na uwezo wa kudhibiti kazi na kusema ni mipango gani itafuatwa. Lakini wakati, katika Konferensi Kuu, hukumu ya ndugu waliokusanyika kutoka sehemu zote za fildi imetezingatiwa, uhuru wa kibinafsi na uamuzi wa kibinafsi haupaswi kudumishwa kwa ukaidi, bali kujisalimisha. Kamwe mtendakazi hapaswi kuzingatia kama fadhila kudumisha nafasi yake ya uhuru, kinyume na uamuzi wa mfumo wote kwa jumla. {9T 260.1}

Wakati fulani, wakati kikundi kidogo cha watu waliokabidhiwa usimamizi wa jumla wa kazi, katika jina la Konferensi Kuu, kilitaka kutekeleza bila busara mipango na kuzuia kazi ya Mungu, nilisema kwamba nisingeweza tena kuzingatia sauti ya Konferensi kuu, inayowakilishwa na watu hawa wachache, kama sauti ya Mungu. Lakini hii si kusema kwamba maamuzi wa Konferensi Kuu inayoundwa na kusanyiko la watu walioteuliwa ipasavyo, wawakilishi kutoka sehemu zote za fildi hayapaswi kuheshimiwa. Mungu amewapa wito (amewawekea mikono) kwamba wawakilishi wa kanisa lake kutoka sehemu zote za dunia, wanapokusanyika katika Konferensi Kuu, watakuwa na mamlaka. Kosa ambalo baadhi wako katika hatari ya kulifanya ni katika kutoa akili na maamuzi ya mtu mmoja, au ya kikundi kidogo cha watu, kuwa kipimo kamili cha mamlaka na kushawishi kwamba Mungu ameweka katika kanisa Lake katika maamuzi na sauti ya konferensi Kuu

iliyokusanyika kupanga kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya kazi Yake. {9T 260.2}

Wakati nguvu hii, ambayo Mungu ameiweka katika kanisa, imeidhinishwa kabisa kwa mtu mmoja, naye anathibitishwa kuwa na mamlaka ya kuwa mwamuzi kwa akili zingine, hapo utaratibu wa Kweli wa Biblia umepindishwa. Juhudi za Shetani juu ya akili ya mtu kama huyo zingekuwa za hila zaidi na wakati fulani karibu kumshinda nguvu kwani adui angetumaini kwamba kupitia akili yake angeweza kuathiri wengine wengi. Hebu tuipe mamlaka iliyo juu iliyopangwa katika kanisa ambacho tuna mwelekeo wa kumpa mtu mmoja au kikundi kidogo watu. {9T 261.1}

## SURA YA 33
## MGAWANYIKO WA MAJUKUMU

Soma mbele ya wajumbe wa almashauri kuu, Washington DC Mei 30, 1909

Mungu angekuwa na watu wenye kuelewa watu. Wajumbe huenda halmashauri kuu kupanga mabo na kuchagua watu. Hawa watu hupimwa na kuhakikishwa. Hawa watu huaminika. Kuchagua wawakilishi wa kuhudhuria halmashauri ni jambo muhimu. Watu hawa wataweka mipango yatakayo fuatwa kwa maendeleo ya kazi. Hata hivyo watu hawa wanapaswa kuwa watu wenye uelewa, wenye kufikiri na kuleta matokeo yanayotokana na athari. (9T 262.1)

Wakaja ikapita kesho yake, huyo Musa hukaa na kuhukumu watu, na watu wakasimama na Musa tangu asubuhi mpaka jioni. Na Mkwewe Musa alipoyaona yote aliyowafanyia watu, akasema, Ni jambo gani hili uwatendealo hao watu? Kwani wewe kuketi hapo peke yako, na watu wote kusimama kwako tangu asubuhi hata jioni? Musa akamwambia mkwewe, Ni kwa sababu watu hunijilia mimi wapate kumwuliza Mungu, wakiwa na neno, hunijilia; nami naamua kati ya mtu na mwenziwe, nami nawaeleza amri za Mungu na sheria Zake. Na mkwewe Musa akamwambia, Jambo hili ufanyalo si jema. Huna budi kudhoofika wewe na hawa watu walio pamoja nawe pia; maana jambo hili ni zito mno kwako; huwezi wewe kulitenda peke yako. Sikiliza sasa neno langu, nitakupa ushauri na Mungu na awe pamoja nawe; uwe wewe kwa ajili ya watu mbele za Mungu, nawe umletee Mungu maneno yao; nawe utawafundisha zile amri na sheria, nawe utawaonyesha njia ambayo inawapasa kuiendea, na kazi ambayo inawapasa kuifanya. Zaidi ya hayo utajipatia katika watu hawa watu walio na uwezo, wenye kumcha Mungu, watu wa Kweli, wenye kuchukia mapato ya udhalimu; ukawaweka juu yao, wawe wakuu wa maelfu, na wakuu wa mamia, na wakuu wa hamsini, na wakuu wa makumi; nao wawaamue watu hawa siku zote kisha kila neno lililo kubwa watakuletea wewe, lakini kila neno dogo wataliamua wenyewe; basi kwako wewe mwenyewe utapata nafasi zaidi, nao watauchukua huo mzigo pamoja nawe. {9T 262.2}

Kwamba utafanya jambo hili, na Mungu akikuagiza hivyo, basi utaweza kusimama wewe, na watu hawa wote nao watakwenda mahali pao kwa Amani. {9T 263.1}

Basi Musa akasikiliza neno la baba mkwe wake akafanya yote aliyokuwa amemwambia. Na Musa akawachagua watu wenye uwezo katika Israeli yote, akawaweka wawe vichwa juu ya watu, wakuu wa maelfu, na wakuu wa mamia, na wakuu wa hamsini, na wakuu wa makumi. Nao wakawaamua watu siku zote; mashauri magumu wakamletea Musa, lakini kila neno dogo wakaliamua wenyewe. Kutoka 18:13-26. {9T 263.2}

Katika sura ya kwanza ya Matendo, pia, mwongozo hutolewa kuhusu mwanaume kubeba majukumu ndani ya kanisa. Uasi wa Yuda na kuondoka kwa uwazi mbele ya mitume, ililazimu wachague mwingine wa kuziba nafasi yake. Haya alisema Petro. {9T 263.3}

"Basi katika watu waliofuatana nasi wakati wote Bwana Yesu alipokuwa akiingia na kutoka kwetu, kuanza tangu ubatizo wa Yohana hata siku ile alipochukuliwa kwetu kwenda juu, inapasa mmoja wao awe shahidi wa kufufuka Kwake pamoja nasi. Wakaweka wawili Yusufu, aitwaye Barsaba, aliye na jina la pili Yusto, na Mathiya. Kisha wakaomba wakasema, Wewe Bwana ujuaye mioyo ya watu wote, tuonyeshe ni nani uliyemchagua kati ya hawa wawili, ashike mahali katika huduma hii na utume huu, alioukosa Yuda, aende pake mahali pake mwenyewe. Wakapiga kura, kura ikamwangukia Mathiya; naye akahesabiwa kuwa pamoja na mitume kumi na mmoja. Matendo 1:21-26. {9T 263.4}

Kupitia maandiko haya tunajifunza kuwa Bwana anao watu aliowaandaa kwa nafasi maalum. Mungu huwafundisha watu Wake kusogea kwa makini na kuwapa hekima watu ambao hawatakana watakatifu waaminifu. Kama siku za Kristo waumini waliitaji kuongozwa na watu wenye wajibu katika nafasi zao, sisi tunaoishi katika kipindi hiki tunahitaji kusonga mbele kwa uangalifu zaidi. Tunapaswa kuwakilisha kila jambo mbele za Mungu, Naye husikiliza maombi yetu tunayomwomba. {9T 264.1}

Bwana Mungu huchagua wanaume wenye uzoefu kubeba majukumu kwaajili ya kazi Yake. Watu hawa wanapaswa kuwa na mvuto maalum. Ikiwa nguvu yote iliyotolewa kwa hawa watu, hii ni wito wao. Wote waliochaguliwa kubeba mizigo katika kazi ya Mungu hawapaswi kuwa na harara au kuwa wabinafsi. Hawapaswi kuwa mfano au mvuto wa uovu. Bwana hakuwapa wanaume na wanawake uhuru wa kushauri wazo la kawaida katika kazi Yake litakaloondoa utakatifu uliowazunguka. Kazi ya Mungu ni kuinua zaidi utakatifu kwa watu Wake. Kwa njia zote tunapaswa kukuza na kuinua tabia za Kweli. Wote waliowekwa kuangalia kazi ya Mungu katika taasisi zetu walitengeneza hali ya kumwinua Mungu na nia yake. Kiujumla afya ya kazi hutegemea uaminifu wa watu waliochaguliwa kuwa walinzi wa kubeba matakwa ya Mungu ndani ya makanisa. {9T 264.2}

Watu ni lazima wawekwe kueneza uzoefu, sio kwa ajili ya vitu binafsi, bali kwa vitu vya Mungu, katika kueneza uelewa wa tabia ya Kristo. Kadiri wanavyo mfahamu Yesu zaidi, ndivyo wanavyokuwa waaminifu kumwakilisha Yesu zaidi kwa ulimwengu. Wanapaswa kuisikiliza sauti Yake na kuwa makini katika Neno Lake. {9T 265.1}

### Onyo

Kisha akaanza kuikemea miji ile ambamo ndani yake ilifanyika miujiza Yake iliyo mingi, kwa sababu haikutubu. Ole wako, Korazini! Ole wako, Bethsaida! Kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwenu ingalifanyika katika Tiro na Sidoni, wangalitubu zamani kwa kuvaa magunia na majivu. Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi Tiro na Sidoni kustahimili adhabu zao siku ya hukumu kuliko ninyi. Nawe Kapernaumu, je! Utakuzwa mpaka mbinguni? Utashushwa mpaka kuzimu; kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwako ingalifanyika katika Sodoma, ungalikuwapo mji huo hata leo. Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi nchi ya Sodoma kustahimili adhabu yake siku ya hukumu kuliko wewe {9T 265.2}

Nawe Kapernaumu uliyejiinua hata mbinguni, utashushwa chini hata kuzimu, kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwako ingalifanyika katika Sodoma, ungalikuwapo mji huo hata leo. Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi nchi ya Sodoma kustahimili adhabu yake siku ya hukumu kuliko wewe. {9T 265.3}

Wakati huo Yesu alijibu akasema, Ninakushukuru Ee! Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa sababu mambo haya umewaficha wenye hekima na akili ukawafunulia watoto wachanga. Kwa kuwa ndivyo ipendezavyo mbele Zako. Akasema nimekabidhiwa vyote na Baba Yangu wala hakuna amjuaye Mwana ila Baba, wala hakuna amjuaye Baba ila Mwana. Na yeyote ambaye Mwana apenda kumfunulia. {9T 265.4}

Njooni Kwangu msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha. Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu, kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu, kwa maana nira Yangu ni laini na mzigo Wangu ni mwepesi. Mathayo 11:20-30. {9T 265.5}

Ni vyema na salama kuwa mpole na mnyenyekevu na mwenye huruma, lakini wakati huo huo ukiwa imara kama mwamba ukifundisha habari za Kristo. Maneno Yake ni maagizo kamili ambayo yanhitaji utiifu kamili. Hata Neno moja lisipotezwe maana. Ukweli utadumu milele. Hatuwezi kuchukua tumaini letu kuwa sehemu ya uongo au kujifanya/feki. Wote wanaofanya hivyo watajikuta wamepoteza uzima wa milele. Sasa tunapaswa kunyoosha mapito yetu, tusije

kuwa vipofu na kupindisha njia. Wakati kipofu anageuka na kutoka kwenye njia salama, nani awajibishwe, ila wale waliowapoteza. Hao maneno ya uzima hayawezi kuwasaidia kupata uzima wa milele, kwa kazi ya udanganyifu asili yake ni baba wa uongo. {9T 266.1}

Nina maneno kwa wale wanaosema kuwa wapo salama kupata elimu ndani ya Battle Creek. Bwana amefungia nje taasisi zetu kubwa mbili imara ndani Battle Creek, na ametoa onyo baada ya onyo, kama Kristo alivyowapa onyo Bethsaida na Kaperanaumu. Kuna umuhimu wa kuwa na bidii ya kusikiliza na kutazama kila Neno linayotoka katika kinywa cha Mungu. Hatuwezi kuishi bila dhambi tukiwa tumetoka kwenye Maneno ya Kristo. Mwokozi wetu anataka tutubu kila kosa. Wale watakaonyenyekeza mioyo yao na kuungama dhambi zao watasamehewa. Makosa yao watasamehewa. Lakini mtu anayedhani kuwa kuungama dhambi zake ni kuonyesha udhaifu, hawezi kupata msamaha, hawezi kumwona Kristo kama Mkombozi, naye ataendelea mbele katika makosa yake, akitekeleza tamaa zake na kuongeza dhambi baada ya dhambi. Nini kitakachokutwa siku ile vitabu vitakapofunguliwa na kila mtu kuhukumiwa sawasawa na kile kilichoandikwa katika vitabu hivyo? {9T 266.2}

Sura ya tano ya kitabu cha Ufunuo kinapaswa kujifunzwa kwa ukaribu. Ni jambo kubwa muhimu kwa wale wanaotenda kazi ya Mungu katika siku hizi za mwisho. Kuna baadhi ambao hudanganyika. Hawawezi kutambua nini kinachoujia ulimwengu. Wale ambao huruhusu akili zao kufungwa kutazama dhambi, inahusiana na jambo gani, wamedanganywa kwa jinsi ya kutisha. Isipokuwa wafanye uamuzi wa kudharimia watajikuta wamepunguka wakati wakisubiri tangazo la Mungu la hukumu kwa watoto wa mwana wa Adamu. Wamekosa juu ya sheria na kuvunja agano la milele, nao watapokea kadiri ya kazi zao. {9T 267.1}.

‘’Nami nikaona, alipoifungua muhuri wa sita, palikuwa na tetemeko kuu la nchi, jua likawa jeusi kama gunia la singa, mwezi wote ukawa kama damu, na nyota zikaanguka juu ya nchi kama vile mtini upukutishavyo mapooza yake, utikiswapo na upepo mwingi. Mbingu zikaondolewa kama ukurasa ulivyokunjwa, na kila mlima na kisiwa kikahamishwa toka mahali pake. Na wafalme wa dunia na wakuu na majemadari na matajiri na wenye nguvu na kila mtumwa na mwungwana wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima, wakiiambia milima na miamba, Tuangukieni tusitirini mbele za uso Wake Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi na hasira ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku iliyo kuu ya hasira yao imekuja naye ni nani awezaye kusimama? Ufunuo 6:12-17. {9T 267.2}

Baada ya hayo nikaona, na tazama mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa na kabila na jamaa na lugha wamesimama

mbele ya kile kiti cha enzi na mbele za Mwana Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao. Wakilia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi na Mwana Kondoo….. Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana Kondoo. Kwa hiyo wapo mbele ya kiti cha enzi cha Mungu nao watamtumikia mchana na usiku katika hekalu Lake, na Yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema Yake juu yao. Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga wala hari iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana-Kondoo aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga Naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao. Ufunuo 7:9-17. {9T 267.3}

Katika maandiko haya makundi mawili huletwa kama mtazamo. Kundi moja huruhusu kudanganywa na kujiweka upande wa wale wanaopambana na Kristo. Hawa kutoelezewa ujumbe uliotumwa kwao na badala yake kujivalia wenyewe vazi la haki. Dhambi sio dhambi mbele ya macho yao. Wanafundisha uongo kuwa ni Kweli na kupitia kwao roho nyingi huongozwa kwenye udanganyifu. {9T 268.1}

Tunahitaji kuchukua tahadhari sisi wenyewe. Onyo limekiwisha kutolewa. Tunaweza kutazama ukamilifu wa utabiri uliotolewa na Kristo na kuandikwa katika sura ya ishirini na moja ya kitabu cha Luka? Ni wangapi wanaojifunza Maneno ya Kristo? Ni wangapi hujidanganya na kudanganya roho zao wenyewe huku wakikosa mibaraka ambayo wengine hutegemea kama nguvu zao wakiiamini na kuitii? Bado wanaendeleza majaribio ya fursa ya kung'ang'ania tumaini iliyowekwa kabla hatujapata injili. Acha tutubu na kufanywa wafuasi, na tunaposhikilia dhambi zilizofungiwa nje. Mbingu na nchi zitapita lakini Maneno Yangu hayatapita kamwe. Basi jiangalieni, mioyo yenu isije ikalemewa na ulafi, na ulevi na masumbufu ya maisha haya, siku ile ikawajia ghafula kama mtego unasavyo, kwa kuwa ndivyo itakavyowajilia watu wote wakaao juu ya uso wa dunia nzima. Basi kesheni ninyi kila wakati mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayotokea na kusimama mbele za Mwana wa Adamu. Luka 21:33-36. {9T 268.2}

Maonyo yaliyotolewa na Kristo je! Yapitwe bila kushugulikiwa? Tunahitajika kufanya bidii ya kazi ya maungamo sasa, wakati sauti ya neema ya huruma husikika? {9T 269.1}

“Kesheni basi kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu. Lakini fahamuni neno hili kama mwenye nyumba angalijua ile zamu mwivi atakayokuja, angalikesha wala asingaliiacha nyumba yake kuvunjwa. Kwasababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari, kwa kuwa katika saa msiyoidhani Mwana wa Adamu Yuaja.

Ni nani basi yule mtumwa mwaminifu mwenye akili, ambaye bwana wake alimweka juu ya nyumba yake, awape watu chakula kwa wakati wake? Heri mtumwa yule ambaye ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo. Amin, nawaambieni, atamweka juu ya vitu vyake vyote. Lakini mtumwa yule mbaya akisema moyoni mwake, Bwana wangu anakawia; akaanza kuwapiga wajoli wake na kula na kunywa pamoja na walevi; bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani, na saa asiyojua, atamkata vipande viwili, na kumwekea fungu lake pamoja na wanafiki, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. Mathayo 24:42-51. {9T 269.2}

## SURA YA 34
## KATIKA UNYENYEKEVU NA IMANI

*[Soma Kwenye Los Angeles, California, Mkutano Wa Makambi, Mwezi August 15-31, 1907, Na Baada Ya Hapo Kuchapwa Na Jehovah Is Our King (Yehova Ni Mfalme Wetu)]*

Maagizo maalum nilipewa kwaajili ya watu wa Mungu, kuwa nyakati za hatari zinakuja juu yetu. Katika dunia iliyojaa uharibifu na kuongezeka kwa vurugu. Nguvu ya watu ndani ya kanisa hutegemea alivyopanda, wale ambao wamechaguliwa kuchukua nafasi ya kutumaini katika haki kutawala. {9T 270.1}

Watu ambao Bwana amewaita katika nafasi muhimu ya kupalilia unyenyekevu na kumtegemea Yeye. Hawatafuti kukumbatia sana mamlaka, kwa kuwa Mungu hakuwaita katika kazi ya kuongoza bali ya kupanga na kushauri kama washiriki na watenda kazi wenzao. Mahitaji na maagizo ya Mungu yanaweza kufanywa na kila mfanyakazi. {9T 270.2}

### Mshauri wa Busara

Kwa sababu ya umuhimu wa kazi huko California ya kusini na shida mfadhaiko ambao umewazunguka, lazima wachaguliwe watu wasiopungua watano wenye hekima na uzoefu wa kushauriana na marais wa majimbo au jimbo kuu (union conferences) kulingana na mipango na sera. Bwana hafurahishwi na wale ambao huonyesha kungoza hata wale ambao wamewazidi uzoefu wao wenyewe. Kwa sababu hii ya hatua baadhi wamefunuliwa kuwa hawakufaa kujaza nafasi muhimu walizochukua. Mwanadamu yeyote ambaye hujisambazia upana wa uwiano na kutafuta kudhibiti wafuasi wake, hujihakikishia kuwa ni watu hatari waliopewa

majukumu ya kidini. {9T 270.3}

Hakuna wa kung'ang'ania wazo lake isipokuwa pesa mkononi mwake, hakuna ulazima wa kuondoa wito uliofanywa maana ya kuweka. Ikiwa uzoefu wetu wa mara kwa mara huko nyuma hufuata inatufuata, tungekuwa tuna poteza vitu muhimu, pale tunapopata manunuzi ya shule ya Fernando, manunuzi ya mali ya sanitarium huko Paradise, Glendale, na Roma Linda. {9T 270.4}

### Songa mbele

Kusita kuchukua hatua ya kusonga mbele katika wito wa kuwekeza mali mpaka tukiwa na pesa mkononi ya kukamilisha kazi tuliyoifikiria, sio kutumia hekima mara zote. Katika kufanikisha kazi Yake Bwana haweki wazi mara zote kila mipango mbele ya watumishi Wake. Wakati mwingine Bwana huwajaribu watu Wake kwa kuwafanya wasonge mbele kwa imani. Mara nyingi huwaleta kwenye shida na mitihani. Akiwaagiza kusonga mbele wakati miguu yao huonekana kugusa maji ya bahari nyekundu.  Ni wakati kama huo maombi ya watumishi Wake hupanda juu kwa Kristo kwa bidii ya imani, ambayo huifungua njia mbele yao na kuwaleta nje katika eneo pana. {9T 271.1}

Bwana anahitaji watu Wake katika siku hizi waamini ya kwamba Yeye atatenda makuu kwa ajili yao kama alivyowafanyia wana Israeli katika safari yao ya kutoka Misri kwenda Kaanani. Tunapaswa kuwa na imani iliyoelimishwa ambayo haitasitasita kufuata maelekezo ya Kristo katika uzoefu mgumu. ''Nenda mbele'' ni agizo la Mungu kwa watu Wake. {9T 271.2}

Imani na utii wenye uchangamfu vyahitajika ili kuwezesha mipango ya Bwana iweze kutimia. Wakati akionyesha umuhimu wa kuanzisha kazi katika maeneo ushawishi utapatikana, watu wanapaswa kutembea na kufanya kazi kwa imani. Kwa mazungumzo ya uchaji Mungu, unyenyekevu wao, maombi yao, na bidii ndivyo jitihada, wajitahidi kuwaleta watu kufahamu kazi njema ya Bwana aliyoimarisha ndani yao. Ilikuwa ni mpango wa Bwana kuwa kituo cha tiba cha Loma Linda kiwe mali ya watu wetu, na Bwana akalileta hilo, wakati ile mito ya shida ikifurika katika kingo zake. {9T 271.3}

Kufanya kazi kwa masilahi ya binafsi kwa kupata faida binafsi ni jambo moja. Katika hili, watu wanaweza kufuata uamuzi wao wenyewe. Lakini kuendeleza kazi ya Bwana duniani ni jambo lingine kabisa. Anapoweka mpango kwamba mali fulani ihifadhiwe kwa ajili ya kuendeleza kusudi Lake na ujenzi wa kazi Yake, iwe ya sanitarium (tiba ya asilia) au kazi ya shule, au kwa tawi lingine lolote, atafanya hiyo kazi  iwezekane ikiwa wale walio na uzoefu wataonyesha imani na

usadikisho wao katika makusudi Yake, na itasonga mbele mara moja ili kupata manufaa aliyoyaelekeza. Wakati sisi hatutafuti kupora mali kutoka kwa mtu yeyote, lakini wakati jambo la faida linapotokea, tunapaswa kuwa wepesi machoni kuiona faida, ili tufanye mipango kwa ajili ya kuiinua kazi. Na wakati tufanyapo hivi tunapaswa kutumia juhudi zote ili kupata matoleo ya hiari kutoka kwa watu wa Mungu kwa ajili ya kusaidia haya maeneo ya miradi/ujenzi mpya. {9T 272.1}

Mara nyingi Bwana huona kwamba watenda kazi Wake wana mashaka juu ya kile wanachopaswa kufanya. Katika nyakati kama hizo, ikiwa wataweka tumaini lao Kwake, atawafunulia hao mapenzi Yake. Kazi ya Mungu sasa ni inapaswa kusonga mbele kwa kasi, na kama Watu wake wataitikia wito Wake, atawafanya wenye mali watoe mali zao na hivyo kufanya kazi Yake iweze kukamilishwa duniani. "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana." Waebrania 11:1. Imani katika Neno la Mungu litawaweka watu Wake katika kumilki mali ambayo itawawezesha kufanya kazi kubwa katika miji mikubwa inayongojea ujumbe wa Kweli. {9T 272.2}

Ubaridi na kutojali, kunakofanywa na kutokuamini ambako baadhi ya watendakazi hufanya kazi yao ni kosa kubwa kwa Roho wa Mungu. Mtume Paulo asema hivi: “Yatendeni mambo yote pasipo manung’uniko na mashindano, mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila kati ya kizazi chenye ukaidi kilichopotoka, ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu. Mkishika Neno la uzima; nipate kuona Fahari katika siku ya Kristo, ya kuwa sikupiga mbio bure, wala sikujitaabisha bure. Naam, hata mkimiminwa juu ya dhabihu na ibada ya imani yenu, nafurahi, tena nafurahi pamoja nanyi nyote." Wafilipi 2:14-17. {9T 273.1}

Inatupasa kuhimizana sisi kwa sisi imani hiyo hai ambayo Kristo ameifanya iwezekane kwa kila mtu anayeamini kuwa nayo. Kazi inapaswa kuendelezwa mbele kama Bwana atayarishavyo njia. Anapowaleta watu Wake katika sehemu zenye shida, basi ni fursa yao kukusanyika pamoja kwa ajili ya maombi, wakikumbuka mambo hayo yote yanatoka kwa Mungu. Wale ambao bado hawajashiriki katika uzoefu wa kujaribiwa unaoikabili kazi katika siku hizi za mwisho hivi karibuni watalazimika kupitia matukio ambayo yatajaribu vikali imani yao kwa Mungu. Ni wakati watu Wake hawaoni njia ya kusonga mbele, wakati Bahari ya Shamu iko mbele yao na jeshi linalowafuatia nyuma, kwamba Mungu anawaambia: "Songeni mbele." Anafanya hivyo ili kujaribu imani yao. Wakati uzoefu kama huo unapokuja kwako, songa mbele, ukimtumaini Kristo. Tembea hatua kwa hatua katika njia anayoiwekea alama/nyayo. Majaribu yatakuja, lakini songa mbele. Hii itakupa uzoefu ambao utaimarisha imani yako kwa Mungu na kukufanya ufae kwa ajili ya huduma ya Kweli.{9T 273.2}

## Mfano wa Kristo

Uzoefu wa kina na mpana zaidi katika mambo ya kidini unakuja kwa watu wa Mungu. Kristo Ndiye kielelezo chetu. Kama kwa njia ya kuishi kwa imani iliyo hai na utii uliotakaswa kwa Neno la Mungu tunadhihirisha upendo na neema ya Kristo, ikiwa sisi tutaonesha kwamba tunayo dhana ya Kweli ya uongozi wa Mungu katika kazi, tutapeleka kwa ulimwengu nguvu inayoshawishi. Cheo cha juu hakitupi thamani mbele za Mungu. Mwanadamu anapimwa kwa kujiweka wakfu na uaminifu katika kufanya mapenzi ya Mungu. Ikiwa watu wa Mungu waliosalia watafanya hivyo wakitembea mbele Zake kwa unyenyekevu na imani, atatekeleza kupitia kwao kusudi Lake la milele, akiwawezesha wafanye kazi kwa upatanifu katika kuupa ulimwengu Ukweli kama ulivyo katika Yesu. Atatumia wote -- wanaume, wanawake, na watoto—katika kufanya nuru iangaze kwa ulimwengu na kuita watu watakao kuwa waaminifu kwa amri Zake. Kupitia imani ambayo watu Wake wanaiishi ndani Yake, Mungu ataujulisha ulimwengu kwamba Yeye Ndiye Mungu wa Kweli, Mungu wa Israeli. {9T 274.1}

"Lakini mwenendo wenu uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo," mtume Paulo ahimiza, "ili nikija na kuwaona ninyi, au nisipokuwapo, niyasikie mambo yenu, kama mnasimama katika roho moja; kwa moyo mmoja mkishundania imani ya Injili; Wala hamwogopi adui zenu, katika neno lo lote; kwao hao ni ishara madhubuti ya kupotea, bali kwenu ninyi ni ishara ya wokovu, huo utokao kwa Mungu. Maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili Yake." {9T 274.2}

"Basi ikiwako faraja yo yote katika Kristo, yakiwako matulizo yoyote ya mapenzi, ukiwako ushirika wo wote wa Roho, ikiwako huruma yoyote na rehema, ijalizeni furaha yangu, ili mwe na nia moja, wenye mapenzi mamoja,wenye roho moja, mkinia mamoja. Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake.
{9T 274.3}

"Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine .Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; Ambaye Yeye mwanzo alikuwa Yu Mungu, Naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza, akawa mtii, hata, mauti ya msalaba. Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, na akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa Jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni;na vya

duniani, na vilivyo chini ya nchi; na kila ulimi ukiri kwamba YESU KRISTO ni BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba. Basi, wapenzi wangu, kama vile mlivyotii siku zote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana Ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema." Wafilipi 1:27-29; 2:1-13. {9T 275.1}

Nimeagizwa kuwasilisha maneno haya kwa watu wetu wa Kusini mwa California. Wanahitajika katika kila mahali ambapo kanisa linaanzishwa, kwajili ya uzoefu mgeni ambao umekuwa ukija katika safu zetu. {9T 275.2}

Ni wakati sasa wanadamu kunyenyekeza mioyo yao mbele za Mungu na kujifunza kufanya kazi katika njia Zake. Hebu hao ambao wametafuta kuwatawala wafanyakazi wenzao wajifunze ili kujua wao wako katika roho ya namna gani. Wanapaswa kumtafuta Bwana kwa kufunga na kuomba, na kwa unyenyekevu wa nafsi. {9T 275.3}

Kristo katika maisha Yake ya hapa duniani alitoa mfano ambao wote wanaweza kuufuata kwa usalama. Analithamini kundi Lake, na hataki mamlaka yoyote yawekwe juu yao ambayo yatawawekea mipaka ya uhuru katika utumishi Wake. Hajawahi kumweka mwanadamu kama mtawala juu ya urithi wake. Dini ya Kweli ya Biblia itaongoza kujitawala, si kumtawala mtu mwingine. Kama watu tunahitaji ujazo mkubwa zaidi wa Roho Mtakatifu, ili tuweze kuubeba ujumbe adhima/mzito ambao Mungu ametupa, bila kujiinua. {9T 275.4}

Ndugu, yashikeni maneno yenu ya kukaripia kwa ajili ya nafsi zenu. Lifundisheni kundi la Mungu kumtazama Kristo, sio kumkosea mwanadamu. Kila nafsi inayokuwa mwalimu wa Ukweli lazima ichukue maishani mwake matunda ya utakatifu. Akimtazama Kristo na kumfuata, atawasilisha kwa roho zilizo chini ya usimamizi wake mfano wa jinsi Mkristo aliye hai na anayejifunza atapaswa kuwa. Hebu Mungu akufundishe njia Yake. Mwulize Yeye kila siku ili kuyajua mapenzi yake. Atatoa ushauri usio na makosa kwa wote wanaomtafuta kwa moyo wa Kweli. Tembeeni kwa kustahili wito mlioitiwa, mkimsifu Mungu katika mazungumzo yenu ya kila siku na katika sala zenu. Hivyo, kwa kulishikilia Neno la uzima, mtazivuta roho zingine kuwa wafuasi wa Kristo. {9T 276.1}

## SURA YA 35
## KWA WAFANYAKAZI WA KUSINI MWA CALIFORNIA

*[Ilichapishwa Kwanza Katika Shuhuda Maalum, Sehemu B, Namba. 10, Yehova Ni Mfalme Wetu.]*

Asubuhi hii siwezi kupumzika. Akili yangu ina wasiwasi juu ya hali ya Kusini mwa California. Mungu amamempa kila mtu kazi Yake, lakini kuna wengine ambao kwa maombi hawafikirii wajibu wao binafsi. {9T 277.1}

Wakati mfanyakazi anapochaguliwa kwa ajili ya ofisi, ofisi hiyo yenyewe haileti kwake uwezo ambao hakuwa nao hapo awali. Cheo cha juu hakimpi mhusika fadhila za Kikristo. Mtu ambaye anadhania kwamba akili yake binafsi ina uwezo wa kupanga na kubuni katika ngazi zote za kazi anaonesha ukosefu mkubwa wa hekima. Hakuna akili ya mtu mmoja inayoweza kubeba majukumu mengi na mbalimbali ya konferensi yanayojumuisha maelfu ya watu na matawi mengi ya kazi. {9T 277.2}

Lakini hatari kubwa kuliko hii imefunuliwa kwangu katika hisia ambayo imekuwa ikiongezeka miongoni wafanyakazi wetu kwamba watumishi na watendakazi wengine katika kazi wategemee mawazo ya viongozi fulani kuwaongoza wafanyakazi kufafanua majukumu yao. Akili na uamuzi wa mtu mmoja havipaswi kuchukuliwa kuwa vinaweza kudhibiti na kuunda konferensi. Mtu binafsi na kanisa wana wajibu wao binafasi. Mungu amempa kila mtu kipaji au vipaji vya kutumia

na kuendeleza. Katika kutumia vipaji hivi huongeza uwezo wake wa kutumika. Mungu amempa kila mtu akili, na karama hii anataka wafanyakazi kuitumia na kuiboresha. Mwenyekiti wa Jimbo lazima asifikirie kuwa uamuzi wake binafsi unapaswa kudhibiti uamuzi wa wote. {9T 277.3}

Katika konferensi kusiwepo na mapendekezo yanayopaswa kuharakishwa bila muda kuchukuliwa na ndugu kuyapima kwa umakini katika pande zote za hoja. Kwa sababu rais wa konferensi alipendekeza mipango fulani, wakati fulani imekuwa ikizingatiwa kuwa si lazima kushauriana na Bwana juu ya mambo hayo. Kwa hivyo mapendekezo yamekubaliwa ambayo hayakuwa kwa manufaa ya kiroho ya waumini na ambayo yalihusishwa, zaidi sana yakionekana katika tafakari ya kwanza kuwa ya kawaida. Mienendo kama hii haiko katika mpango wa Mungu. Mambo mengi sana, mengi yamechukuliwa na kuamuriwa kwa kura, ambayo yamehusisha zaidi ya ilivyotarajiwa na zaidi ya wale waliopiga kura wangekuwa tayari kuidhinisha kama wangechukua muda kufikiria swala kutoka katika pande zote. {9T 278.1}

Hatuwezi kwa wakati huu kumudu kuwa wazembe au wapuuzi katika kazi ya Mungu. Ni lazima tumtafute Bwana kwa bidii kila siku ikiwa tungelikuwa tayari kwa uzoefu unaotujia. Mioyo yetu inapaswa kutakaswa kutoka katika kila hisia ya kujiinua,na kanuni hai za Ukweli zinapaswa kupandwa ndani nafsi. Vijana na wazee na watu wa makamo wanapaswa sasa kutekeleza fadhila na wema wa tabia ya Kristo. Wanapaswa kila siku kuwa wanafanya maendeleo ya kiroho, ili wawe vyombo vya heshima katika huduma ya Bwana. {9T 278.2}

"Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, alipokwisha, mmoja wa wanafunzi wake alimwambia, Bwana, tufundishe sisi kusali, kama vile Yohana alivyowafundisha wanafunzi Wake.” Luka 11:1. Ombi Kristo alilowapa wanafunzi Wake katika kujibu ombi hili halifanywi kwa lugha ya makelele, bali linaeleza kwa Maneno rahisi mahitaji ya nafsi. Ni fupi na linahusika moja kwa moja na mahitaji ya kila siku. {9T 278.3}

Kila nafsi ina fursa ya kusema/kuleta kwa Bwana mahitaji yake maalum na kutoa shukrani zake binafsi kwa ajili ya baraka ambazo Yeye hupokea kila siku. Lakini zile sala nyingi ndefu na zisizo na roho, zisizo na imani, ambazo hutolewa kwa Mungu, badala ya kuwa furaha Kwake, huwa ni mzigo. Tunahitaji sana! mioyo safi, iliyoongoka. Tunahitaji kuimarishwa imani yetu. “Ombeni, nanyi mtapewa,” Mwokozi aliahidi; "tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa.” Mathayo 7:7 Tunapaswa kujifunza kuliamini katika Neno hili na kuleta nuru na neema ya Kristo katika kazi zetu zote. Tunahitaji kumshikilia Kristo na kubaki kumshikilia Yeye mpaka tujue kwamba nguvu ya neema Yake ibadilishayo inadhihirika ndani

yetu. Ni lazima tuwe na imani katika Kristo kama tungeakisi tabia ya kimbingu. {9T 278.4}

Kristo aliuvisha Uungu Wake kwa ubinadamu na kuishi maisha ya sala na kujinyima, na ya mapambano ya kila siku na majaribu, ili awasaidie wale ambao leo wanashambuliwa na majaribu. Yeye Ndiye ufanisi wetu na nguvu. Anatamani kwamba, kupitia kwa ugawaji wa neema Yake, wanadamu wawe washirika wa asili ya kimbingu na hivyo kuepuka uharibifu uliomo duniani utokanao na tamaa. Neno la Mungu katika Agano la Kale na Jipya, likisomwa kwa uaminifu na kupokelewa maishani, litatoa hekima ya kiroho na uzima. Neno hili linapaswa kuthaminiwa kitakatifu. Imani katika Neno la Mungu na katika uweza wa Kristo kwa kubadilisha maisha utamwezesha muumini kufanya kazi zake na kuishi maisha ya furaha katika Bwana. {9T 279;1}

Tena na tena nimeagizwa kuwaambia watu wetu: Hebu imani na tumaini lenu liwe kwa Mungu. Usimtegemee binadamu ambaye anayekosea, kuufafanua wajibu wako. Ni fursa yako kusema: "Nitalihubiri jina Lako kwa ndugu zangu, katikati ya kusanyiko nitakusifu. Ninyi mnaomcha Bwana, msifuni; Enyi nyote mlio wazao wa Yakobo, mtukuzeni, mcheni, Enyi nyote mlio wazao wa Israeli. Maana hakulidharau teso la mteswa, wala hakuchukizwa nalo, wala hakumficha uso wake , bali alipomlilia, akamsikia. Kwako zinatoka sifa zangu:. . . nitaziondoa nadhiri zangu mbele yao wamchao. Wapole watakula na kushiba; wamtafutao Bwana watamsifu mioyo yenu na iishi milele." Zaburi 22:22-26. {9T 279.2}

Maandiko haya yanafaa kwa uhakika. Kila mshiriki wa kanisa anapaswa kuelewa kwamba Mungu Ndiye pekee ambaye Kwake tunatafuta ufahamu na wajibu wa mtu binafsi. Ni sawa ndugu washauriane pamoja; lakini watu wanapopanga kile ambacho ndugu zao watafanya, hebu waone kwamba wamemchagua Bwana kama mshauri wao. Wale ambao watamtafuta Yeye unyenyekevu watapata neema Yake inatosha. Lakini wakati mtu mmoja anaporuhusu mwingine aingie kati yake na wajibu ambao Mungu amemwonyesha, akimpa mwanadamu ujasiri wake na kumkubali kama kiongozi, ndipo anatoka kwenye jukwaa la Kweli hadi kwenye jukwaa la uongo na hatari. Mtu kama huyo, badala ya kukua na kuendelea, atapoteza hali yake ya kiroho. {9T 280.1}

Hakuna uwezo kwa mtu yeyote kurekebisha tabia yenye kasoro. Tumaini letu binafsi na imani lazima viwe ndani ya Yule ambaye ni zaidi ya binadamu. Tunahitaji kukumbuka kwamba msaada umewekwa kwa Yule Mwenye uweza. Bwana ametoa msaada unaohitajika kwa kila nafsi itakayoukubali.  Sanitarium, California, Oktoba 3, 1907. {9T 280.2.1}

## SURA YA 36
## "MIMI NI MTOTO MDOGO TU"

*[Ilichapishwa Kwanza Katika Ushuhuda Maalum, Sehemu B, Namba. 10, Yehova Ni Mfalme Wetu.]*

Mwanzoni mwa utawala wake Sulemani aliomba hivi: “Ee Bwana, Mungu wangu, umenitawaza niwe mfalme mimi mtumishi wako badala ya Daudi baba yangu; na mimi ni mtoto mdogo tu, sijui jinsi inipasavyo kutoka wala kuingia,” 1Fal 3:7. {9T 281.1}

Sulemani alikuwa amemrithi Daudi baba yake kwenye kiti cha enzi cha Israeli. Mungu alimheshimu sana, na, kama tujuavyo, katika miaka ya baadaye akawa mfalme mkuu zaidi, tajiri zaidi, na mwenye hekima zaidi aliyepata kukaa juu ya kiti cha enzi cha ufalme wa kidunia. Mwanzoni katika utawala wake Sulemani alivutwa na Roho Mtakatifu kwa uadilifu wake kwa majukumu mazito aliyopewa, na, ingawa alikuwa tajiri wa vipaji na uwezo, alitambua kwamba bila msaada wa Mungu alikuwa mnyonge kama mtoto mdogo kuzitekeleza. Sulemani hakuwahi kuwa tajiri sana au mwenye hekima sana au mkuu kama wakati alipokiri kwa Bwana: "Mimi ni mtoto mdogo tu, sijui jinsi inipasavyo kutoka wala kuingia." {9T 281.2}

Ilikuwa katika ndoto, ambapo Bwana alimtokea, akisema, "Omba utakalo nikupe" (mstari wa 5) Sulemani, hivyo alionesha hisia yake ya kutokuwa na uwezo na uhitaji wake wa msaada wa Bwana. Aliendelea: “Mtumwa wako yuko katikati ya watu wako uliowachagua, watu wengi wasioweza kuhesabiwa, wala kufahamiwa idadi yao,kwa kuwa ni wengi. Kwa hiyo nipe mimi mtumwa wako moyo wa adili niwakuhukumu watu wako, na kupambanua mema na mabaya; maana ni nani awezaye kuwahukumu hawa watu wako walio wengi? {9T 281.3}

"Neno hili likawa jema machoni pa Bwana, ya kuwa Sulemani ameomba neno hili. Mungu akamwambia,Kwa kuwa umeomba neno hili, wala hukujitakia maisha ya siku nyingi; wala hukutaka utajiri kwa nafsi yako, wala hukutaka roho za adui zako; bali umejitakia akili za kujua hukumu;basi, tazama, nimefanya kama ulivyosema; tazama, nimekupa moyo wa hekima na wa akili; hata kabla yako hapakuwa na, wala baada yako hatainuka mtu kama wewe. Na mambo yale usiyoyaomba nimekupa, mali na fahari, hata hapatakuwa na na mtu katika wafalme kama wewe siku zako zote.” Sasa masharti: “Nawe ukienda katika njia Zangu, na kushika mausia Yangu. na amri Zangu, kama Daudi baba yako alivyokwenda,basi nitakapozifanya siku zako kuwa nyingi. {9T 281.4}

“Sulemani akaamka, na kumbe, ni ndoto, akaenda Yerusalemu, akasimama mbele ya sanduku la agano la BWANA, akatoa sadaka za kuteketezwa, na sadaka za amani, na akafawanyia karamu watumishi wake wote." Aya 8-15. {9T 282.1}

Wote walio na nafasi za kuwajibika wanahitaji kujifunza somo linalofundishwa katika ombi la unyenyekevu wa Sulemani. Wanapaswa kukumbuka kuwa uongozi hautabadilisha tabia au kumfanya mwanadamu asiwe na makosa. Kadri mtu anavyochukua uongozi wa juu, ndivyo anabeba jukumu kubwa zaidi, mvuto wake anaoonesha unakuwa mpana na ndivyo zaidi anakuwa na haja ya kuhisi utegemezi wake juu ya hekima na nguvu za Mungu na kukuza tabia bora na takatifu zaidi. Wale wanaokubali nafasi ya wajibu katika kazi ya Mungu wanapaswa kukumbuka daima kwamba pamoja na wito wa kazi hii Mungu ,pia, amewaita waenende kwa uangalifu mbele zake na mbele ya wanadamu wenzao. Badala ya kuzingatia wajibu wao wa kuelekeza na kuamrisha, wanapaswa kutambua kwamba wanapaswa wao wenyewe kuwa wanafunzi. Mtendakazi mwaminifu anaposhindwa kujifunza somo hili, kuachiliwa kwake kutoka katika maajukumu kwa haraka ndiyo itakuwa bora kwake na kwa ajili ya kazi ya Mungu. Cheo kamwe hakitoi utakatifu na ubora wa tabia. Anayemheshimu Mungu na azishikaye amri Zake, mwenyewe anaheshimiwa. {9T 282.2}

Swali ambalo kila mmoja anapaswa kujiuliza kwa unyenyekevu wote ni: "Je, ninastahili nafasi hii? Je! nimejifunza kuishika njia ya Bwana ili kutenda haki na

hukumu?” Mfano wa Mwokozi duniani tumepewa ili tusienende kwa nguvu zetu wenyewe, bali kila mtu ajihesabu nafsi yake, kama Sulemani alieleza, "mimi ni mtoto mdogo tu." {9T 283.1}

**"Wafuasi wa Mungu, kama Watoto Wapendwa"**

Kila nafsi iliyoongoka kweli inaweza kusema: "Mimi ni mtoto mdogo; lakini mimi ni mtoto wa Mungu." Ilikuwa kwa gharama isiyo na kikomo mpango huo ulifanywa ili familia ya kibinadamu irudishwe kuwa wana pamoja na Mungu. Hapo mwanzo, Mungu aliumba mtu kwa sura Yake. Wazazi wetu wa kwanza walisikiliza sauti ya mjaribu na kujisalimisha kwa nguvu za Shetani. Lakini mwanadamu hakuachwa kwa matokeo ya uovu aliouchagua. Ahadi ya Mkombozi ilitolewa. "Nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke," Mungu akamwambia nyoka, "na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino." Mwanzo 3:15. Kabla hawajasikia kuhusu mwiba na michongoma, ya huzuni na taabu ambayo lazima iwe sehemu yao, au mavumbi ambayo lazima warudiye, walisikiliza Maneno ambayo hayangeweza kushindwa kuwapa matumaini. Yote yaliyokuwa yamepotea kwa kujisalimisha kwa Shetani yangeweza kupatikana tena kupitia Kristo. {9T 283.2}

Mwana wa Mungu alitolewa ili kuukomboa ubinadamu. Katika mateso yasiyo na kipimo, kutokuwa na dhambi kwa wadhambi, gharama ililipwa ambayo ilikuwa ya kukomboa jamii ya kibinadamu kutoka kwenye nguvu ya mharibifu na kuwarudisha tena katika sura ya Mungu. Wale wanaokubali wokovu unaoletwa kwao katika Kristo watajinyenyekeza mbele za Mungu kama watoto Wake wadogo. {9T 283.3}

Mungu anataka watoto Wake wamwulize yale mambo yatakayomwezesha kuidhihirisha neema yake kupitia kwao kwa ulimwengu. Anawataka watafute ushauri wake, watambue uwezo wake. Kristo anaweka madai ya upendo juu ya wote ambao amewapa uhai Wake; wanapaswa kutii mapenzi Yake ikiwa watashiriki furaha aliyoweka tayari kwa wote wanaoakisi tabia Yake hapa. Ni vizuri kwetu kuuhisi udhaifu wetu, kwa maana ndipo tutaweza tafuta nguvu na hekima ambayo Baba hufurahia kuwapa watoto Wake kwa ajili ya pambano lao la kila siku dhidi ya nguvu za uovu. - {9T 284.1}

Ingawa elimu, mafunzo, na ushauri wa wale walio na uzoefu ni muhimu, watendakazi wanapaswa wafundishwe kwamba wasitegemee kabisa uamuzi wa mtu ye yote. Kama watumishi huru wa Mungu, wote wanapaswa kuomba hekima Yake. Wakati mwanafunzi anapotegemea kabisa mawazo ya mwingine, akiikubali mipango Yake na asiende mbali zaidi, huona tu kupitia macho ya mtu huyo na,

haendi mbali, huona tu kupitia katika macho ya mtu huyo, na Zaidi huwa mwangwi wa mwingine. {9T 284.2}

## SURA YA 37
## THAWABU YA JUHUDI ZA DHATI

"Kazi ya mtu aliyoijenga juu yake ikika/ikidumu, atapata thawabu.." 1 Wakorintho 3:14. Utukufu utakuwa thawabu iliyotolewa wakati watendakazi waaminifu watakapokusanyika karibu na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo. Wakati Yohana alipouona utukufu wa Mungu katika hali yake kufa, akaanguka kama mfu; hakuweza kuvumilia kuuona. Lakini watoto wa Mungu watakapokuwa wamevaa kutokufa, "watamwona Yeye kama alivyo." 1 Yohana 3:2. Watasimama mbele ya kiti cha enzi, wakiwa wamekubaliwa katika Mpendwa. Dhambi zao zote zimefutwa, makosa yao yote yameondolewa. Sasa wanaweza kuutazama utukufu usiohafifishwa, na usiofichika wa kiti cha enzi cha Mungu. Wamekuwa washirika pamoja na Kristo katika mateso Yake, wamekuwa watendakazi pamoja Naye katika mpango wa ukombozi, na wanashiriki Naye katika furaha ya kuona roho zikiokolewa katika ufalme wa Mungu, huko humsifu Mungu milele zote. {9T 285.1}

Ndugu yangu, dada yangu, nawasihi mjiandae kwaajili ujio wa Kristo katika mawingu ya mbinguni. Siku kwa siku utupilieni mbali upendo wa ulimwengu kutoka mioyoni mwenu. Jueni kwa uzoefu, ni nini maana ya kuwa na ushirika na Kristo. Jitayarisheni kwa ajili ya hukumu, ambayo Kristo atakapokuja, ili

kuadhimishwa na wote wanaoamini, muweze kuwa miongoni mwa watakao kutana naye kwa amani. Siku hiyo wale waliokombolewa watang'aa katika utukufu wa Baba na wa Mwana. Malaika, wakivigusa vinubi vyao vya dhahabu, watamkaribisha Mfalme na nyara Zake za ushindi --wale ambao wameoshwa na kufanywa weupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Wimbo wa ushindi utarindima na kupenyeza, na utaijaza mbingu yote. Kristo ameshinda. Anaingia katika nyua za mbinguni, akifuatana na watu waliokombolewa, mashahidi wa utume Wake wa mateso na kujitoa sadaka, hivi vinaonyesha kwamba kazi Yake haikuwa bure. {9T 285.2}

Kufufuka na kupaa kwa Bwana wetu ni ushahidi wa hakika wa ushindi wa watakatifu wa Mungu juu ya kifo na kaburi, na hutangaza ahadi kwamba mbingu iko wazi kwa wale wanaofua nguo zao za tabia na kufanywa weupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Yesu alipaa kwa Baba kama mwakilishi wa jamii ya wanadamu, na Mungu atawaleta wale wanaoakisi sura Yake kutazama kwa macho yao haya yote, na kushiriki pamoja Naye utukufu Wake. {9T 286.1}

Kuna nyumba na makazi kwa wasafiri wa duniani. Kuna mavazi ya wenye haki, yenye taji za utukufu na mtende ya ushindi. Yote ambayo yametutatanisha na kutukanganya katika majaliwa ya Mungu yatafanywa wazi katika ulimwengu ujao. Mambo magumu kueleweka, mafumbo na vitendawili, hapo yatapata ufafanuzi. Siri za neema zitafunuliwa mbele yetu. Pale ambapo akili zetu zenye ukomo ziliona mkanganyiko tu na ahadi zilizovunjika, tutaona upatanifu kamili na mzuri. Tutajua kwamba upendo usio na kikomo uliyasimamia mambo ambayo yalionekana kutujaribu zaidi. Tutakapotambua utunzaji laini/mwororo wa Yeye ambaye hufanya vitu vyote kufanya kazi pamoja kwa ajili ya wema wetu Warumi 8:28, tutafurahi kwa furaha isiyoneneka na iliyojaa utukufu. {9T 286.2}

Maumivu hayawezi kuwepo katika angahewa ya mbinguni. Katika makazi za waliokombolewa hakutakuwa na machozi, wala misafara ya mazishi, wala beji za maombolezo. “Wala hapatakuwa na mwenyeji au mkazi atakayesema, Mimi ni mgonjwa; watu wakaao humo watasamehewa uovu wao.” Isaya 33:24. Wimbi moja la furaha na utajiri litabubujika na kutawanyika kadri umilele udumuvyo na kusonga mbele. {9T 286.3}

Bado tuko katikati ya vivuli na misukosuko ya shughuli za kidunia. Hebu na tuzingatie kwa umakini zaidi baraka za baada ya hapa. Hebu imani yetu ipenye katika kila wingu la giza na kumtazama Yeye aliyekufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Yeye Ameifungua milango ya paradiso kwa wote wanaompokea na kumwamini Yeye. Kwa hao, Yeye huwapa uwezo wa kufanyika wana na binti za Mungu. Hebu mateso yanayotuumiza sana yawe masomo elekezi, yanayotufundisha kusonga mbele kuelekea alama ya tuzo ya mwito wetu mkuu katika Kristo. Hebu na tutiwe moyo na wazo kwamba Bwana Yu karibu kuja. Hebu tumaini hili litufurahishe mioyo yetu. "Bado kitambo kidogo, na Yeye ajaye atakuja,

na wala hatakawia." Waebrania 10:37. Wana heri hao watumishi, wamebarikiwa hao watendakazi, ambao wakati atakapokuja Bwana wao, atawakuta wakikesha. {9T 286.4}

Tuna furaha ya ajabu kuwa safarini kuelekea nyumbani. Yeye aliyetupenda hata akafa kwa ajili yetu ametujengea mji. Yerusalemu Mpya ni mahali petu pa pumziko. Hakutakuwa na huzuni katika mji wa Mungu. Hakuna kilio na mayowe ya huzuni, hapana maombolezo ya matumaini yaliyovunjika-vunjika na mapenzi yaliyozikwa, hivi havitasikika milele tena. Hivi karibuni mavazi yenye uzito wa huzuni yatabadilishwa kuwa vazi arusi. Hivi karibuni tutashuhudia kutawazwa kwa Mfalme wetu. Wale ambao maisha yao yamefichwa pamoja na Kristo, wale ambao wamepigana vile vita vizuri vya imani katika dunia hii; watang'aa kwa utukufu wa Mkombozi katika ufalme wa Mungu. {9T 287.1}

Haitachukua muda mrefu hadi tutakapomwona Yeye ambaye ndani Yake matumaini yetu ya uzima wa milele yamejikita na kukaa humo. Na katika uwepo Wake, majaribu na mateso yote ya maisha haya yatakuwa kama sifuri tu. “Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu. Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu, mpate ile ahadi. Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, na Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia.” Mistari 35-37. Tazameni juu, tazameni juu, na imani yenu iendelee kuongezeka daima. Hebu Imani hii iwaongoze katika njia nyembamba, na ngumu iongozayo katika malango ya mji wa Mungu, ili kuingia katika ng'ambo iliyo kuu, iliyo pana, isiyo na mipaka ya utukufu usio na kifani, kwa ajili ya waliokombolewa. “Kwa hiyo, ndugu, vumilieni, hata kuja Kwake Bwana. Tazama, mkulima hungoja kuvuna matunda ya ardhi yaliyo ya thamani, huvumilia kwa ajili yake hata yatakapopata mvua ya kwanza na ya mwisho. Nanyi vumilieni; thibitisheni mioyo yenu, kwa maana kuja Kwake Bwana kunakaribia." Yakobo 5:7, 8. {9T 287.2}